# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Tano – Tarehe 9 Aprili, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge walipiga makofi kumshangilia Spika kwa kurejea Bungeni)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Katibu tuendelee.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli, niivunje tu Kanuni yako na mimi niseme tunafurahi kukuona. Karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Taarifa za Matoleo ya Magazeti pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikoa cha Mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

(i) Toleo Na. 05 la tarehe 02 Februari, 2018;
(ii) Toleo Na. 06 la tarehe 09 Februari, 2018
(iii) Toleo Maalum Na. 03 la tarehe 13 Februari, 2018;
(iv) Toleo Na. 07 la tarehe 16 Februari, 2018;
(v) Toleo Na. 08 la tarehe 23 Februari, 2018;
(vi) Toleo Na. 09 la tarehe 02 Machi, 2018;
(vii) Toleo Na. 10 la tarehe 09 Machi, 2018;
(viii) Toleo Na. 11 la tarehe 16 Machi, 2018; na
(ix) Toleo Na. 12 la tarehe 23 Machi, 2018.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba nakala za magazeti haya zimeshasambazwa na zimetolewa pia kwa mfumo wa nakala tete.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tunakushukuru sana. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 34

**Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa – Mkoa wa Simiyu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Mkoa wa Simiyu ambao ni mkoa mpya hauna Hospitali ya Rufaa, hivyo wagonjwa wanalazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilometa 140 kufuata huduma hiyo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Shinyanga na Mwanza; mwaka 2015/2016 Mkoa wa Simiyu ulipokea fedha kidogo ya kuanzisha jengo la *OPD*.

(a) Je, Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa?

(b) Je, ni lini Serikali imepanga kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukukaribisha tena katika Bunge letu tukufu. Tumefurahi sana kukuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, Wizara inapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kutambua jitihada ambazo Serikali imefanya katika kuendeleza mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu, ukiwa ni mmoja wa mikoa mipya ulioanzishwa mwaka 2012. Kutokana na uhitaji wa huduma za afya ngazi ya rufaa katika ngazi ya mkoa, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu iliandaa na kupeleka andiko Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa kwa kuzingatia mahitaji ya kitabibu kwa ajili ya kuingizwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, niongeze hapa tu kwamba, pamoja na andiko hili hospitali hii sasa kwa agizo la Mheshimiwa Rais, zimeletwa tena katika Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikitoa fedha na hadi sasa jumla ya shilingi 2,087,268,672 zimeshatolewa. Kati ya fedha hizo, shilingi 299,896,185 zilitumika kununua ardhi yenye ukubwa wa ekari 121. Shilingi milioni 595,650,815 zilitumika katika ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* na utawala katika awamu ya

kwanza na shilingi 1,191,721,672 zilitumika kuendeleza ujenzi wa jengo la *OPD* katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga fedha zaidi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za tiba katika Hospitali za Rufaa za mikoa ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Simiyu. Hii inaenda sambamba vilevile na kupatiwa ahadi ya fedha ya shilingi bilioni 10 ambayo zilitolewa na Mheshimiwa Rais alipotembelea Mkoa wa Simiyu tarehe 11 Januari, 2017.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, Mheshimiwa Rais alipotembelea Mkoa wa Simiyu mapema Januari, 2017 baada ya kuona maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa, kwanza hakuridhishwa na bajeti iliyotengwa ya shilingi bilioni 38 ya kujenga Hospitali ya Mkoa. Hivyo, akasema hospitali hiyo ijengwe kwa shilingi bilioni 10 na kwamba akatoa ahadi zitolewe shilingi bilioni 10 ili mwaka 2019 aje kuzindua hospitali hiyo. Mpaka sasa ni jengo la *OPD* tu ndilo lililokamilika na 2017 mpaka leo hakuna fedha yoyote iliyoletwa na Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah, swali sasa.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, naomba *commitment* ya Serikali kuhusiana na ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, swali langu dogo la pili; tunayo Hospitali Teule ya Somanda, hospitali hiyo ina changamoto. Madaktari wanaohitajika ni 22, waliopo ni wanane, lakini hao wanane hawana *examination room,* hamna Mganga wa Usingizi wala hakuna *casuality room*.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha hospitali hiyo teule ya mkoa ili wananchi wa Mkoa wa Simiyu wasihangaike kwenda Mkoani Mwanza?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Leah Komanya; na nimpongeze kwa kufuatilia afya na maendeleo ya wananchi wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba, Mheshimiwa Rais mwishoni mwa mwaka 2017 alikabidhi hospitali zote za rufaa za mikoa ambazo zilikuwa zinasimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuja katika Wizara ya Afya. Na sisi ndani ya Wizara ya Afya tumeshajipanga kuhakikisha kwamba hospitali hizi tunazihudumia na kuzisimamia kikamilifu ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti kama nilivyosema katika jibu langu la awali.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema tu kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais ni *commitment,* nasi ndani ya Wizara tutaendelea kuisimamia kuhakikisha kwamba fedha hizo zinapatikana kwa malengo ambayo yamekusudiwa, baada ya kufanya tathmini ya kina kuangalia mahitaji halisi ya Hospitali hii ya Simiyu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, swali lake la pili lilikuwa ni kuhusiana na watumishi. Katika mwaka wa fedha uliopita, Serikali iliajiri watumishi 3,152 ambao tuliwagawa katika mikoa mbalimbali. Tunatambua bado tuna changamoto kubwa sana ya watumishi na tunatarajia kwamba Serikali itatoa kibali hivi karibuni na Mkoa wa Simiyu utazingatiwa katika mahitaji yake.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali hili limechukua muda mwingi. Naomba tuendelee na swali la Mheshimiwa Abdallah Ali Mtolea, Mbunge wa Temeke kwa Wizara hiyo hiyo ya Afya.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kabla ya kuuliza naomba nifanye marekebisho machache kwenye hii *Order Paper* maana yake imeandikwa kwamba namuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,

TAMISEMI lakini swali nalielekeza Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto.

Baada ya marekebisho hayo naomba swali hili la Wanatemeke sasa lipate majibu ya Serikali.

Na. 35

**Serikali Kuihudumia Hospitali ya Temeke**

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA** aliuliza:-

Serikali iliipandisha hadhi Hospitali ya Temeke kuwa Hospitali ya Mkoa ambayo sasa inastahili kuhudumiwa na Wizara badala ya Halmashauri ili huduma inayotolewa hapo ifanane na hadhi ya Hospitali ya Mkoa.

Je, ni lini Serikali itaanza kuihudumia hospitali hiyo kwa kiwango kinachostahili ili kuipunguzia mzigo Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, Serikali iliipandisha hadhi Serikali ya Temeke kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Hospitali hiyo ni moja ya hospitali tatu katika Mkoa wa Dar es Salaam zilizopandishwa hadhi kuwa Hospitali za Rufaa za Mkoa ikiwa ni pamoja na Hospitali za Mwananyamala na Ilala. Lengo ni kuhakikisha kuwa huduma za afya za kibingwa zinawafikia wananchi na kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, katika mwendelezo wa kuboresha huduma za kibingwa kwa wananchi, tarehe 25 Novemba, 2017 Hospitali ya Temeke ni miongoni mwa hospitali 23 za

Rufaa za Mikoa ambazo zilikabidhiwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutoka TAMISEMI wakati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua Hospitali ya Mafunzo ya Mloganzila. Wizara yangu imekabidhiwa hospitali hizi kutoka TAMISEMI tarehe 15 Machi, 2018.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha hospitali hii inatoa huduma kulingana na hadhi iliyopewa, Serikali imeweka vipaumbele vya kuboresha utoaji wa huduma ikiwa ni pamoja na:-

(i) Vipaumbele vya kuongeza madaktari bingwa wanane katika fani za magonjwa ya akinamama, upasuaji, mifupa, mama na watoto na magonjwa ya ndani. Hospitali ya Temeke kwa sasa ina wataalam hao.

(ii) Kuhakikisha upatokanaji wa dawa na vifaatiba.

(iii) Kuhakikisha mipango ya hospitali inawekwa wakiasaidiana na Wizara katika kukarabati vyumba vya upasuaji, maabara na vyumba vya wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha hospitali hii ili kukidhi mahitaji ya wananchi kulingana na uwezo uliopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sipingani na mpango huu wa Serikali katika kuzichukua moja kwa moja hospitali hizi, hasa ukizingatia Halmashauri zetu sasa hivi zina hali mbaya kichumi kutokana na vyanzo mbalimbali kuondolewa. Nataka kujua sasa, mfumo wa utumishi baada ya kuzichukua hizi hospitali utakuweje kwa maana za mamlaka za kinidhamu kwa

watumishi waliokuwa wakifanya kazi kwenye hizi hospitali? Hilo moja.

Mheshimiwa Spika, la pili, wakati Wizara inapanga namna gani ya kuzihudumia hizi hospitali, huwa inaangalia idadi ya watu katika eneo husika, mfano kwa Hospitali ya Temeke mnaangalia idadi ya watu katika Wilaya ya Temeke, lakini ukweli ni kwamba Hospitali ya Temeke haihudumii tu watu wa Temeke, inahudumia na maeneo jirani kwa sababu ya jiografia yake ilivyo, maeneo kama ya Kigamboni, Mkuranga na sehemu nyingine kama Kibiti na Rufiji.

Je, Wizara mmelizingatiaje hili, ili kuhakikisha sasa huduma mtakazozitoa katika Hospitali ya Temeke zitaenda sambamba na idadi kubwa ya watu wanaopata huduma katika eneo hilo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, sisi ndani ya Wizara baada ya kukabidhiwa hospitali hizi tumefanya tathmini ya kina kuangalia mahitaji ya miundombinu ya kiutumishi ya hospitali hii. Niseme tu kwamba kuna maboresho makubwa ambayo tumeyafanya ndani ya Wizara kwanza; kwanza, kuanzisha *section* maalum ambayo itakuwa inasimamia Hospitali za Rufaa na za Mikoa katika Idara ya Tiba.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Idara Kuu ya Utumishi tumefanya mabadiliko, tutakuwa na Mkurugenzi Msaidizi ambaye naye atakuwa anasimamia Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tumefanya maboresho vilevile katika Hospitali za Rufaa za Mikoa baada ya kuitwa Waganga Wafawidhi. Matarajio yetu ni kwamba sasa wasimamizi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa watakuwa wanaitwa Wakurugenzi kamili na watapata hadhi hiyo na taratibu zote hizo tumeshazikamilisha.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Nidhamu bado yako chini ya Mabaraza ya Taaluma ambayo nayo yako chini ya Ofisi ya Mganga Mkuu. Kwa hiyo, Mamlaka za Nidhamu zitaendelea kufanya kazi kwa mujibu ule ule, hata pale wakati zikiwa TAMISEMI, mamlaka ya nidhamu yalikuwa bado chini ya Wizara ya Afya chini ya mabaraza, chini ya Mganga Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mtolea, ni kweli Wilaya ya Temeke ina watu takribani milioni 1.6 na Hospitali ya Temeke imekuwa ikiwahudumia wananchi wengi pamoja na Wilaya nyingine za jirani. Serikali inatambua hilo, tutazingatia hilo, lakini sambamba na hilo tunaboresha mnyororo wa utoaji huduma kwa maana ya kuboresha vituo vya afya, kujenga Hospitali za Wilaya na zahanati ili sasa ule mnyororo wa rufaa uweze kuwa kamili na kuhakikisha kwamba Hospitali ya Rufaa ya Mkoa inafanya kazi ya rufaa ya mkoa.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano. Swali linaulizwa na Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi.

Na. 36

**Ujenzi wa Daraja Kati ya Lugezi na Kisorya**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Uwepo wa mawasiliano ya uhakika kati ya Visiwa vya Ukerewe na Mkoa wa Mara ni muhimu kwa uchumi wa wananchi wa Ukerewe na hatua kadhaa zimeshachukuliwa kuhakikisha daraja kati ya Lugezi na Kisorya linajengwa.

Je, ni hatua ipi inachukuliwa na Serikali kuhakikisha daraja hilo linajengwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali, naomba uniruhusu nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kumshukuru Mungu kwa kukurejesha na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha mawasiliano kati ya visiwa vya Ukerewe na mikoa mingine, imefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara yote ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya – Nansio (Ukerewe) yenye urefu wa kilometa 118.

Aidha, usanifu umejumuisha madaraja mawili ya Lugezi yenye urefu wa mita 600 na mita 450 yanayounganisha Kisorya na Nansio pamoja na maandalizi ya nyaraka za zabuni. Kazi ya usanifu imekamilika na ujenzi kwa kiwango cha lami kati ya Bulamba hadi Kisorya katika barabara hii unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hiyo, pamoja na madaraja mawili kati ya Kisorya na Nansio ili kuunganisha Kisiwa cha Ukerewe na Mikoa ya Mara, Simiyu na Mwanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara nyingi za mikoa sasa zimeshajengwa na kuna tatizo kubwa sana la barabara Wilayani na vijijini; na *TARURA* wamepewa jukumu la kujenga barabara hizi, lakini pesa wanazozipata bado hazitoshi. Serikali sasa haioni sababu za msingi za kubadili

*formula* ya ugawaji wa pesa kati ya *TANROADS* na *TARURA* ili kuongeza *percentage* ya pesa zinazoenda *TARURA*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kati ya Lugezi na Kisorya kuna kivuko ambacho ni mbadala wa daraja, lakini katika kivuko kile kuna tatizo kubwa la utozaji wa nauli, hususan mizigo ambayo inaleta kero sana kwa wananchi kwa mizigo iliyo chini ya kilo 20. Inategemea busara ya mtozaji kama kilo moja atatoza kiasi gani? Kilo mbili kiasi gani?

Sasa Serikali haioni sababu kuweka kiwango maalum, kwa mfano, chini ya kilo 20 wananchi wasitozwe tozo zozote za nauli ya mizigo ili kuondoa migogoro ambayo imekuwa inajitokeza mara kwa mara kati ya vivuko vya Kisorya na Lugenzi na Bugorora na Ukara? Nashukuru.

**SPIKA:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, majibu kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunaendelea na ujenzi wa barabara na kipaumbele kilikuwa kwenye barabara kuu. Barabara kuu zina urefu wa zaidi ya kilometa 8,000 na kwa sasa hivi tumeshavuka nusu ya urefu huo. Kwa maana hiyo, sasa ni fursa ambayo itawezesha Serikali kuelekeza fedha nyingi kwa ajili ya kutengeneza barabara ambazo zinaunganisha mikoa na hatimaye pia kwenda kuunganisha barabara ambazo ziko chini ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba utambue hivyo, pamoja na wapiga kura wa Ukerewe kwamba tumejipanga vizuri. Mara baada ya kukamilisha sehemu kubwa ya barabara kuu, nguvu kubwa ya Serikali itaelekezwa katika eneo la barabara ambazo ziko kwenye Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kwamba tunachukua hatua gani kwa ajili ya gharama ya kivuko hiki cha MV Ujenzi?

Mheshimiwa Spika, ninatambua, nasi upande wa Serikali tumelichukua hili, lakini tumeshaanza kufanya utafiti wa kuhakikisha kwamba suala la bei hii ya vivuko tunaliangalia kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, iko hoja kwamba gharama ya ubebaji wa mizigo iko chini kwenye baadhi ya maeneo, lakini yako maeneo yanaonesha kwamba gharama ni kubwa. Kwa maana hiyo sasa, tunafanya utafiti ili tuweze kuja na bei ambayo itakuwa rafiki kwa watumiaji wa vivuko hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Ukerewe tuvute subira. Nawaomba na wenzetu wa upande wa *TEMESA* waharakishe hili zoezi la kufanya utafiti ili tuweze kuchukua hatua ambayo itafanya usafiri huu uwe rafiki kwa watumiaji wa vivuko. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Hapana, Mheshimiwa Chegeni. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwanza nafurahi kukuona ukiwa mzima wa afya na tunakupongeza sana kwamba Bunge hili lilikuwa limeku-*miss,* sasa tunafurahi kukuona kwenye kiti chako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na makofi hayo na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, muuliza swali Mheshimiwa Mkundi amezungumzia suala la Ukerewe. Ukerewe inaunganishwa na barabara inayotoka Nyanguge kupita Busega mpaka pale Ndabaga. Barabara kuu ni mbovu kabisa, hata daraja la Mto Simiyu pale Magu halikidhi mahitaji ya usafirishaji katika mikoa hiyo. Je, Serikali inatoa

*commitment* gani ya kuweza kukarabati barabara hii kutoka Nyanguge - Magu - Busega mpaka pale Ndabaga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa sababu barabara hii tumekuwa tukizungumza kwa maana ya kuifanyia maboresho.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kabla *commitment* haijatolewa, lakini niseme tuko *committed* kwa sababu ule usanifu umefanyika na kwa maana hiyo, hata katika bajeti inayokuja, Mheshimiwa Mbunge tumetenga fedha kwa ajili ya kuboresha eneo hili.

Mheshimiwa Spika, niahidi tu kwamba baada ya Bunge nitatembelea eneo hili. Sijapata fursa ya kutembelea maeneo haya ili Mheshimiwa Mbunge tuweze kushauriana vizuri, na mimi nijionee mwenyewe namna gani tunaweza kusukuma kwa haraka ili barabara hii iweze kupitika.

**SPIKA:** Tunahamisha kwenye Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 37

**Kurejeshwa Viwanda Vilivyogeuzwa kuwa Maghala**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Katika Jiji la Dar es Salaam kuna Viwanda vingi ambavyo vimebadilishwa matumizi yake na kugeuzwa kuwa maghala ya kuhifadhia vifaa mbalimbali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvirejesha viwanda hivyo kwenye matumizi yake ya awali?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya Mashirika ya Umma 341 yaliyobinafsishwa hadi mwaka 2007 viwanda vilikuwa 156. Madhumuni ya ubinafsishaji wa viwanda yalikuwa ni pamoja na kutoa ajira, kuzalisha bidhaa zinazokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa na kuongeza mchango wa viwanda katika uchumi wa Taifa. Ufufuaji wowote wa viwanda ambao unaleta matokeo hayo ni sahihi kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Dar es Salaam, ni kweli kuna baadhi ya viwanda vilivyobadili matumizi ya awali na kuanza shughuli nyingine za kiuchumi. Baadhi yake ni vile vilivyouzwa kwa utaratibu wa ufilisi na mali moja moja na hivyo kutokuwa na mikataba ya mauzo inavyowalazimisha wamiliki kuendeleza shughuli za viwanda za awali.

Mheshimiwa Spika, Viwanda hivyo ni pamoja na *TANITA One* ambacho kwa sasa kinatumika kama maghala; *Tanzania Publishing House Limited Investment* ambacho kwa sasa ni duka la vitabu, *Tractors Manufacturing Company Limited* ambapo kwa sasa kuna jengo la biashara la *Quality Centre, Light Source Manufacturing* ambapo *TATA Holding)* pamoja na *Tanganyika Packers Ltd* ya Kawe *(Kawe Meat Plant)* ambapo eneo lilinunuliwa na *National Housing* kwa ajili ya ujenzi wa makazi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhamasisha na kuwezesha viwanda visivyofanya kazi, vifanye kazi. Mpaka sasa uhamasishaji huu umewezesha viwanda 18 vikiwemo vya Dar es Salaam kama vile kiwanda cha *UFI* kilichokuwa kinatengeneza zana za kilimo, kilibadilishwa na kuwa *Tanzania Steel Pipe Limited* na kuanza

kutengeza mabomba ya maji na vingine vinaendelea kufanyiwa ukarabati na vingine tayari vinafanya kazi.

Hivyo, chini ya Kamati Maalum yenye wataalam toka sekta mbalimbali, tunafuatilia utendaji wa kiwanda kimoja hadi kingine mpaka vyote viweze kufanya kazi kwa tija.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ambayo yamenitosheleza, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri wazi kuwa kuna baadhi ya viwanda viliuzwa na kubadilishwa matumizi; na kwa kuwa sera ya Tanzania ni kutaka tupate Tanzania ya viwanda; je, Serikali inatoa tamko gani sasa kwa hao wanunuzi na wafilisi wa hivyo viwanda wasibadilishe matumizi na badala yake waendeleze viwanda kama Serikali yetu inavyotaka?

Swali la pili, kwa kuwa wanawake wa Dar es Salaam, Lindi na Mtwara walikuwa wanapata ajira kubwa sana katika viwanda vya kubangua korosho vya *TANITA*, leo hii viwanda hivyo vimewekwa kuwa maghala na maeneo ya kuweka matakataka tu mengine; hususan wanawake wa Mbagala, Kongowe, Temeke, Kurasini, Tandika, wote walio wengi walikuwa wanapata ajira katika kiwanda cha *TANITA* cha Mbagala; je, Serikali ina mpango gani wa kuvifufua viwanda vya *TANITA* vya kubangua korosho ili wanawake walio wengi waweze kupata ajira katika viwanda hivyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili kutoka kwa Mheshimiwa Mariam Kisangi. Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusiana na viwanda ambayo vimebadilisha matumizi, niseme tu kama ambavyo nimesema awali. Lengo la Taifa ni kuhakikisha kwamba viwanda

vinatoa ajira. Kwa hiyo, tusingependa kusema moja kwa moja kwamba ni marufuku kubadilisha matumizi kwa sababu inawezekana biashara iliyokuwepo wakati huo, kulingana na mtaji na mashine zilizopo yawezekana haiendani na wakati wa sasa. Tunachotaka ni kwamba viwanda hivyo viendelee kufanya kazi hata kwa kuangalia bidhaa nyingine ambazo zinaweza zikazalishwa hapo na kuendelea kutoa ajira.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna wale ambao wakati viwanda vinabinafsishwa, waliandika maandika na wakapewa masharti maalum ya kuendeleza viwanda hivyo. Wengine hawajatekeleza kabisa masharti hayo na matokeo yake, viwanda hivyo vimehujumiwa na vingine vimekuwa hata mashine zake hazipo. Tunawaambia ole wao, tutapitia kimoja hadi kimoja na wale ambao wataonekana kwamba hawajakidhi matakwa ya mikataba, naamini Serikali itachukua hatua kali inayostahili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwanda ambacho ni cha *TANITA,* niseme tu kwamba sambamba na maelezo uliyoeleza Mheshimiwa Mbunge pia sisi tutatembelea lakini la msingi kama ambavyo nimesema awali tungehitaji kuona kwamba viwanda vyetu vinafanya kazi yenye tija na kuweza kutoa ajira kwa watu wengi zaidi ikiwemo akina mama.

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda tuendelee na Wizara ya Fedha na Mipango. Swali linalizwa na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji.

Na. 38

**Kuhusu Hisa za Serikali katika Kiwanda cha Sukari cha Kagera**

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina hisa kiasi gani katika Kiwanda cha Sukari cha Kagera?

(b) Je, kiasi cha fedha kilichokopwa na mwekezaji kwa *guarantee* ya Serikali kimeshalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haimiliki hisa katika Kiwanda cha Sukari cha Kagera na Serikali kupitia *PSRC* ilibinafsisha kiwanda hicho kwa Kampuni ya *Kagera Saw Mills Limited* kwa kuuza hiza zake zote mnamo mwaka 2001.

(b) Mheshimiwa Spika, mwekezaji alikopa kiasi cha dola za Kimarekani milioni 65 kwa kutumia *guarantee* ya Serikali mwaka 2004 ikiwa ni *guarantee* ya miaka 12. Hadi sasa zaidi ya dola za Kimarekani milioni 56.88 zimesharejeshwa sawa na asilimia 87.5 ya mkopo wote. Aidha, marejesho ya sehemu ya mkopo uliobaki wa dola za Kimarekani milioni 8.12 yatafikia ukomo wake mwezi Julai, 2019.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Swali langu la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri, nataka kufahamu; je, Serikali iliafiki mwekezaji huyu kukopa na kwenda kuwekeza kiwanda kikubwa nchini Congo wakati hapa nchini bado kuna uhaba mkubwa wa sukari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili la nyongeza ni kwamba majuzi Kiwanda cha Sukari cha Mahonda kimefungwa kutokana na uhaba wa miwa. Hali hii itapelekea Zanzibar kukosa sukari. Naomba kufahamu; je, Serikali ni lini sasa itatekeleza ujenzi wa Kiwanda cha Sukari kule Rufiji kwa kutumia bonde la Mto Rufiji katika ardhi iliyotengwa katika

Kata ya Muhoro, Chumbi, Mkongo pamoja na Kata ya Mbwara ili kuweza kuwatosheleza Watanzania kwa upatikanaji wa sukari ya kutosha?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri, Fedha na Mipango Dkt. Ashatu Kijaji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha *Kagera Sugar* mpaka leo kimeshawekeza zaidi ya dola za Kimarekani milioni 250 na kiasi kilichokopwa kwa *guarantee* ya Serikali ni dola za Kimarekani milioni 65; kwa hiyo kusema wamewekeza dola milioni 250, halafu wamekopa milioni 65 na kupeleka Congo, naona siyo jambo la kawaida. Na mimi nimefika mwenyewe Kiwanda cha *Kagera Sugar* nimejionea uwekezaji mkubwa uliowekezwa.

Mheshimiwa Spika, ni imani ya Serikali na tunatambua hivyo kwamba pesa yote iliyokopwa kupitia *guarantee* ya Serikali hii dola za Kimarekani milioni 65 imewekezwa yote ndani ya Taifa letu na ni moja ya viwanda vinavyofanya vizuri sana ndani ya Taifa letu, kimeajiri Watanzania wengi, kinatoa huduma za afya bure katika ukanda wote unaozunguka Kiwanda cha *Kagera Sugar,* kinatoa huduma za elimu bure kwa watoto wote wa wafanyakazi ndani ya *Kagera Sugar* na ndani ya wananchi wanaozunguka kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kuwapa moyo Kiwanda cha *Kagera Sugar* kwamba wanafanya vizuri waendelee kuwekeza kwa ajili ya manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kuliarifu Bunge lako Tukufu, Serikali ipo kwenye mchakato wa kuendelea kukiwezesha Kiwanda cha *Kagera Sugar* ili kiendelee kuwa cha mfano ndani ya Taifa letu, kiwanda kinachomilikiwa na Watanzania halisi wenye uchungu na Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, napenda kusema kuwa Serikali ilifanya jambo jema kurejesha bonde lile lilokuwa linamilikiwa na *RUBADA.* Sasa hivi Serikali ya Magufuli, Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali ya viwanda,

tunafahamu na ndiyo maana juzi tuliwaambia ndugu zetu wa Zanzibar, Zanzibar kuna upungufu wa sukari, miwa haitoshi. Leo kiwanda kimefungwa kwa sababu miwa haitoshi kwa ajili ya Kiwanda cha Mahonda; na Serikali yetu iko tayari kabisa Mheshimiwa Mchengerwa kwenda kuwawezesha wananchi wa Rufiji kuwekeza kwenye mashamba yale tuweze kupata *outgrowers* wengi na kiwanda kitawekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Khatib, nini tena? Miwa haitoshi! Swali la nyongeza Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza na mimi nitoe shukrani kwa Mwenyezi Mungu kukujalia wewe kurudi hapa katika hali ya afya na uzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyoyo zetu zimefurahika na nafsi zetu zimeburudika kukuona tena katika kiti chako. Karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri; Tanzania kila mwaka tunakuwa na upungufu wa sukari kutokana na uzalishaji mdogo wa viwanda, lakini zipo taarifa za uhakika kwamba Kiwanda cha *Kagera Sugar* kimekuwa kikisafirisha sukari kupeleka Uganda kila mwaka.

Je, ni kwa nini sukari haitoshi katika soko la nchi yetu na Kiwanda cha *Kagera Sugar* kinaruhusiwa kuuza Uganda lakini Zanzibar haitoshi kwa Zanzibar, lakini hairuhusiwi kuleta Tanzania Bara? Kwa nini?

**SPIKA:** Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Dkt. Tizeba, tafadhali, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi niungane na wengine kukupongeza na kukutakia afya njema sana na karibu tena katika Bunge letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ni kwamba suala la sukari na biashara yake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki linayo *protocol* maalum. *Protocol* hiyo inaelekeza kwamba bidhaa hii haiwezi kuhama kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine bila makubaliano kwanza kupitia katika Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Ndiyo maana hata sukari ikizalishwa namna gani Kenya au Uganda au Tanzania haiwezi kwa kirahisi tu kuvuka mipaka wa Tanzania kwenda au kutoka nje ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kadri tulivyo na kumbukumbu, Serikali hii hajawahi kumpa kibali *Kagera Sugar* kupeleka sukari nje ya nchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Swali linalofuata ambalo linaelekezwa Wizara ya Mambo Ndani ya Nchi. Nalo litaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Bububu, Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma.

Na. 39

**Ukarabati wa Kituo cha Polisi Bububu**

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA** aliuliza:-

Kituo cha Polisi Bububu ni kikongwe sana na pia kimechakaa sana na kinahitaji ukarabati mkubwa.

Je, ni lini kituo hicho kitafanyiwa ukarabati?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, na mimi naomba niungane na Waheshimiwa wengine kumshukuru Mwenyezi Mungu kukujalia kuungana na sisi leo ukiwa mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Bububu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uchakavu wa vituo vya polisi vikongwe nchini kikiwemo Kituo cha Polisi cha Bububu. Jeshi la Polisi lina mpango wa kuvikarabati vituo hivyo kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, ukarabati wa vituo hivyo vya Polisi kikiwemo Kituo cha Polisi Bububu utafanyika ili kuboresha mazingira ya kazi kwa askari wetu ili kuwawezesha kutoa huduma bora kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Safi sana. Jibu fupi, linatosheleza na zuri. Mheshimiwa Mwantakaje, watakaje tena? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini kidogo hayaniridhishi, kwa sababu yeye mwenyewe Naibu Waziri amekwenda kujionea kituo hicho cha Bububu, alikitembelea.

Je, kituo kile kwa sababu hakina *computer,* hakina *photocopy machine* na mpaka hivi sasa hivi wanaenda kutoa *photocopy* nje ya kituo. Ni lini Serikali itachukua hatua ya kukipatia *computer* na *photocopy machine?*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu huko nyuma niliulizwa suala la gari ya polisi, kwa sababu kituo changu kipo barabarani na kina uhalifu mwingi katika Jimbo langu la Bububu.

Je, ni lini Serikali itatupatia gari hilo la Polisi ili kupunguzia wananchi usumbufu? Kwa sababu sasa hivi wakiomba gari binafsi wanachukua ili kwenda kusaidia kufanya doria?

Naiomba Serikali ijitahidi ili kituo changu kipate gari ya doria ili kupunguza usumbufu kwa wananchi. Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi. Bububu kule kuna upungufu.

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa

Mwantakaje kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba mazingira ya askari wetu hasa katika Kituo cha Polisi Bububu katika Jimbo lake yanakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulifanya ziara ya pamoja kwenye kituo hiki na kuna mambo mengi tuliyarekebisha, lakini nimhakikishie, kama tumeweza kurekebisha mambo makubwa ambayo mwenyewe anafahamu, sidhani kama hili la *photocopy* na *computer* litatushinda. Nimwombe tu avute subira, tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, upande wa suala la pili kuhusiana na gari, kwa sasa bado hatuna magari, lakini tunatarajia kupata magari. Kwa hiyo, tutaangalia ukubwa wa changamoto zilizopo nchi nzima, kwa sababu upungufu haupo Bububu peke yake, yako maeneo mbalimbali nchini. Kwa hiyo, kadri ya idadi ya magari itakapopatikana, tutaangalia uwezekano vilevile wa kukipatia Kituo cha Polisi cha Bububu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ruth Mollel nimekuona. Swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali aliloulizia Mheshimiwa aliyezungumza sasa hivi, halina tofauti kabisa na Gereza la Keko ambalo miundombinu yake ni mibaya na pia kuna msongamano mkubwa sana wa wafungwa na wengi wao zaidi ya nusu ni mahabusu na hivyo hivyo kwenye Gereza la Segerea.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba *justice* inakuwa *dispense,* mapema watu watoke na magereza yawe na wafungwa ambao ndio wangestahili kukaa pale na hiyo miundombinu iliyokuwepo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tunakiri juu ya tatizo la msongamano, kwani ukiangalia takribani Magereza yote kwa ujumla nchini ukiachia mbali la Keko na mengine, mpaka leo tunavyozungumza, tuna takriban wafungwa wanaokadiriwa kufika mpaka 40,000 na wakati *capacity* ya Magereza yetu haizidi 30,000. Kwa hiyo, utakuta tuna idadi ya wafungwa kama 10,000 hivi ambao wamezidi kiwango magerezani.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo, ndiyo maana Serikali inachukua jitihada mbalimbali kupunguza msongamano huu ikiwemo kupitia zile sheria nne tulizozipitisha hapa Bungeni za kuwapatia kifungo cha nje wafungwa kwa utaratibu wa *parole,* lakini pia utaratibu wa *community services* za *EML*, lakini pia kwa kupitia msamaha wa Rais. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake alizochukua za kupunguza idadi ya wafungwa mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, pia moja ya jitihada ambazo Serikali inachukua, ni kuhakikisha kwamba tunatenga bajeti ya kutosha kadri ya hali ya fedha inavyoruhusu kupanua Magereza yetu yaweze kuwa na ukubwa zaidi na kuongeza magereza mengine nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizo ndizo jitihada ambazo tunachukua na tunaamini kabisa kadri tunavyokwenda hivi, sasa hivi uchumi wetu wa nchi, unakwenda vizuri, naamini miaka ya mbele tatizo la msongamano litapungua kama siyo kuisha kabisa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mwuliza swali alikuwa anauliza kuhusu ukarabati wa kituo, lakini kwa kuwa Wilaya ya Kilolo ni ya siku nyingi sana na haijawahi kujengewa Makao Makuu ya *OCD* yalipo Makao Makuu ya Wilaya toka imeanzishwa, na kufanya *OCD* kukaa mbali na *DC*. *(Makofi)*

Je, ni lini sasa Serikali itaona umuhimu wa kujenga Makao Makuu ya Polisi yalipo Makao Makuu ya Wilaya ya Kilolo?

**SPIKA:** Jibu la swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, *Engineer* Hamad Masauni, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni sahihi kabisa, Kilolo hatuna Kituo cha Polisi cha Wilaya na hii ni moja ya vituo 65 vya wilaya nchini ambavyo hatunavyo na ambavyo vipo katika mpango wa Serikali wa kuvijenga. Kwa hiyo, Kilolo ni kimojawapo.

Mheshimiwa Spika, wakati jitihada hizi za Serikali za kuweza kuona jinsi gani tunafanya kujenga vituo 65 zinaendelea, basi nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya ziara katika Mkoa wa Iringa hivi karibuni ili tushirikiane tuangalie namna gani nyingine ambayo tunaweza tukafanya ili kuweza kuunga mkono jitihada za Serikali za kujenga kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tuendelee. Bado tuko Wizara ya Mambo ya Ndani hiyo hiyo, swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini. Mheshimiwa Mwalongo tafadhali.

Na. 40

**Huduma kwa Wafungwa**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inatumia pesa kiasi gani kuhudumia mfungwa mmoja kwa siku kwa huduma ya chakula tu?

(b) Vitendo kama kulala chini, kulala bila blanketi au shuka, kulala bila neti vimekuwa vya kawaida kabisa katika Magereza yetu nchini; je, hii nayo ni sehemu ya adhabu ambayo wafungwa wanapewa kwa mujibu wa sheria?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza katika kutekeleza jukumu lake la kuwapokea na kuwahifadhi wahalifu kisheria, pia hutoa huduma ya chakula kwa wahalifu kupitia bajeti inayotengwa na Serikali kila mwaka wa fedha. Gharama ya chakula kwa mfungwa mmoja kwa siku ni wastani wa shilingi 1,342.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za wafungwa na mahabusu Magerezani kwa kununua vifaa mbalimbali vya malazi ikiwemo magodoro, shuka, mablanketi na madawa ya kuua wadudu kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha. Kwa msingi huo inapotokea ukosefu wa huduma hizo, inakuwa siyo sehemu ya adhabu kwa wafungwa bali hutokea kutokana na idadi kubwa ya wafungwa gerezani.

**SPIKA:** Nani ametoka Magereza juzi juzi? Mheshimiwa Mchungaji. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, sijapewa swali la nyongeza.

**SPIKA:** Ooh, mwenye swali lake, Mheshimiwa Mwalongo tafadhali, ahsante. Mchungaji utafuata.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kipengele kimoja tu cha swali na kipengele kinachofuata

hajakisoma. Kwa kuwa nimepewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza nafikiri atakisoma atakaporudi kwenye jukwaa.

Mheshimiwa Spika, Gereza la Njombe lina msongamano mkubwa sana na katika msongamano huu wako akina mama wenye watoto wadogo mle ndani ya Gereza.

Je, Serikali sasa iko tayari kuwapa chakula maalum watoto wale ili kutokuwaathiri makuzi yao na kuwafanya wakue wakiwa na afya bora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Gereza la Njombe, yuko Mahabusu anaitwa Erick Mgoba. Mahabusu huyu amepelewa Hospitali ya Rufaa kwa kushirikiana na Gereza la Njombe ili apatiwe matibabu. Alivyofika Hospitali ya Rufaa Mbeya akatakiwa kulipa shilingi 300,000 ili atibiwe na akarudishwa Njombe bila kutibiwa na afya yake ni mbaya.

Je, Serikali iko tayari kumtibu mahabusu huyu ili kuokoa maisha yake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mbali ya upungufu wa fedha ambazo tunatumia kwa kumlisha chakula mfungwa, ambayo nimezungumza katika jibu langu la msingi kwamba ni shilingi 1,342; lakini tunahakikisha kwamba chakula ambacho anakula mfungwa ni chakula chenye kiwango cha kutosha. Tunapima hivyo kulingana na *calories* ambayo nadhani ni 2,200 na kitu kwa kila mfungwa; 2,200 kwa mfungwa mwanaume na 2,500 kwa wafungwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la watoto na wafungwa wa kike na wa kiume kwa ujumla, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wanapata chakula chenye ubora na chenye kiwango cha kuridhisha, juu ya upungufu

wa fedha, lakini kiwango tunahakikisha kwamba kinakuwa kwa maana ya lishe, inakuwa ni lishe ambayo iko sawa kabisa kitabibu.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusiana na matibabu ya mfungwa ambaye amemzungumza amesema kama tuko tayari, naomba baada ya Bunge hili mimi na yeye tukutane tuone jinsi gani tunalishughulikia hili jambo. Ni lazima tuhakikishe kwamba mfungwa huyu anapata matibabu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilishakutaja Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Na mimi nikupongeze kwa kurudi salama, tuliku-*miss* pia.

Mheshimiwa Spika, elimu ya kisasa ya sheria sasa hivi ina-*encourage* kupunguza misongamano kwenye Magereza, wanapokwenda kwenye Mahakama wahakikishe wanapunguza misongamano na kuwapeleka watu Magerezani bila sababu.

Mheshimiwa Spika, kama swali la msingi ambavyo limeulizwa ukienda kwenye Magereza yetu, kuna msongamano mkubwa sana. Kwa mfano, Gereza la Segerea ambalo nili-*happen* kulitembelea juzi, *capacity* yake ni mahabusu 700, lakini sasa hivi lina mahabusu na wafungwa 2,400. Wanalazimika watu kulala upande mmoja mmoja kwa zamu baada ya muda tena inapigwa *alarm,* halafu wageukie upande mwingine. Huu ni ukiukwaji kabisa wa haki za binadamu. Kuna watoto wengi ambao wako *under age* wamekaa pale, wengine wanatakiwa waende shuleni. Hii tuna-*cripple* Taifa la baadae, wala hatuwasaidii wale watoto ambao wako Magerezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu; kwa kuwa hii *modern law* inafundisha kupunguza mahabusu kwa kadri iwezekanavyo wasiende Magerezani; ni kwa nini Serikali imekuwa ikipeleka wanasheria kutetea kesi za Serikali ambao

wamekuwa wakilazimisha wale ambao wanaweza wakapata *bail* waende kukaa mahabusu, kama ambavyo kesi zetu sisi zilikuwa zina *bail,* lakini Mawakili wa Serikali wakawa wanalazimisha twende kule tukaongeze msongamano?

**SPIKA:** Hilo swali sidhani kama ni la Mambo ya Ndani ya Nchi na Profesa Kabudi ametoka hapa sasa hivi, alikuwepo, sijui, *okay*, Mheshimiwa tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, mahabusu kuwekwa ndani kwa muda mrefu siyo suala tu la kwamba Serikali haitaki kesi ziishe mapema, lakini kuna sababu nyingi za msingi za baadhi ya watuhumiwa kutoachiwa.

Mheshimiwa Spika, moja, mara nyingine ni kwa sababu ya usalama wao. Kwa mfano, kama ni watu ambao wametenda makosa ambao unahisi kwamba wakienda nje wanaweza wakapata matatizo, mara nyingi Serikali inajaribu kuwalinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya pili, kuna watuhumiwa ambao wakitoka nje wanaweza vilevile kwenda kuharibu ushahidi. Kwa hiyo, Serikali inaangalia hivyo vitu vyote. Siyo suala la kwamba hutaki kesi iishe, lakini yawezekana unapowaachia kurudi, wanaenda kusababisha kesi ichelewe kwa sababu wataharibu ushahidi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko nilikuona ulisimama. Uzoefu upande wa pili huko kwenye watoto. *(Kicheko)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli kabisa kwamba msongamano kwenye Magereza yetu Tanzania, Tarime na hata Segerea nilipoenda ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza ambalo nauliza hapa, Mheshimiwa Waziri wakati anatoa takwimu za gharama kwa wafungwa, amesema ni shilingi 1,200 kwa

chakula. Nilipokuwa Segerea kwenye swali langu ninaloenda kuuliza, kule kuna wamama wamefungwa wanadaiwa shilingi 150,000 mathalani, lakini amefungwa miezi sita. Kwa gharama ambazo amezitoa Mheshimiwa Naibu Waziri unakuta zinavuka pale tena mpaka shilingi 270,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mama ambaye amefungwa miezi sita, anaumwa ugonjwa wa *fibroid* ana-*over breed*, kila siku jioni *ambulance* inampeleka Amana.

Je, ni kwa nini Serikali isitumie busara ya zaidi kwa hawa akina mama ambao wengine wana watoto wachanga ambao unakuta wanafungwa kwa kesi za shilingi 100,000 au 200,000 wasiweze kuzi-*waive* uki-*compare* na gharama ambazo wanaenda kuhudumia kwenye ile jamii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole Nasha bado amesimama, endelea tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, suala la kwamba fedha ambayo wanadaiwa ni kidogo, ni suala la kisheria. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge anafikiri sheria ile imepitwa na wakati na haitendi haki, ni rahisi yeye kuleta hoja Bunge hili libadilishe sheria kwa sababu sheria ndiyo zinasema hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana na kwa kweli Wabunge wanawake mko wengi hapa, mambo kama hayo kama yapo kweli, basi ni vizuri mkaungana kuangalia mateso ya akina mama wa aina hiyo. *(Makofi)*

Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Ooh, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani nyongeza ya majibu tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nipongeze kwa majibu mazuri yaliyotolewa. Nataka tu kumuomba Mheshimiwa Mwalongo kwa ile hoja ya jambo mahususi alilolileta kwamba baada ya Bunge, basi tuonane

ili nilipate vizuri kwa sababu jambo lake alilolileta lile ni mahususi ili tuweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambazo tumezipata, niweke tu kumbukumbu sawa, siyo kila Magereza yana msongamano. Tuna baadhi ya Magereza ambako katika mikoa ile kiwango cha uhalifu ni kidogo, hata msongamano Magerezani ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilienda Mkoa wa Lindi, Gereza lilikuwa na uwezo mkubwa kuliko kiwango cha wahalifu. Hivyo hivyo, nilienda kwa Mheshimiwa Shangazi kule, kiwango cha Gereza la kule ni kikubwa kuliko wahalifu walioko mle.

Kwa hiyo, nitoe rai kwa Watanzania na jamii nzima ya Watanzania kuepuka kufanya uhalifu kwa kweli, kwa sababu sisi kama Serikali hatupendi watu kuwa magerezani, lakini tunawapeleka kwa sababu ya uhalifu wanaoufanya.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi tukaacha wahalifu wakawa nje na kama watu watafanya uhalifu, ni kwamba wataenda magerezani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi ,tafadhali.

Na. 41

**Timu ya Tathmini Kukagua Miradi ya Maji - Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kutuma timu ya tathmini ya kukagua Miradi ya Maji ya Kwediboma, Kwekivu, Sange, Chamtui na Mafuleta ili kuona kama vigezo na viwango vya ujenzi wa miradi hii mikubwa vimezingatia thamani ya fedha *(value for money audit)?*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya maji nchini ikiwemo maeneo ya vijijini ili kuweza kuwapatia wananchi huduma ya maji safi, salama kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2020. Ili miradi ya maji iweze kutekelezwa kwa ufanisi, Serikali hufanya ufuatiliaji na tathmini ili kupima matokeo ya mradi uliokamilika na unaoendelea kulingana na vigezo vitano (kufaa, kutekelezeka, ufanisi, athari na uendelevu) katika mpangilio unaoeleweka ili kusaidia kuboresha miradi mingine inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ombi la Mheshimiwa Mbunge, naomba nimshukuru kwanza kwa kuona umuhimu wa kufuatilia miradi ya maji iliyoko jimboni kwake. Hivyo namhakikishia kuwa nitatuma timu ya wataalam kwa ajili ya kwenda kufanya ukaguzi wa ujenzi wa miradi hiyo ili kuona kama vigezo na viwango vya ujenzi wa miradi hiyo mikubwa vimezingatiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali moja au mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba dhamira ya Serikali ni kuwahudumia wananchi na kuwapelekea huduma iliyo imara, lakini swali la msingi ilikuwa ni kueleza changamoto ya miradi hii.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kufanya ziara kupitia miradi yote ambayo nimeitaja hapo juu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi. Mheshimiwa Naibu Waziri, uko tayari kufanya ziara?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwenda kwao haogopi kiza na Kilindi ni nyumbani, nipo tayari kwenda Kilindi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swali fupi la nyongeza, nilikuona.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na wenzangu kukupa pole na kushukuru na kufurahi kukuona leo Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia, Mohamed Kigua, kwamba kwa kweli miradi ya maji ina matatizo mengi na ni vizuri kwa kweli tathmini ikafanywa. Wilaya yangu ya Hanang ina visima vilivyochimbwa vina mwaka mmoja hakuna kuendeleza maji yakapatikana na watu wanatoa machozi pale, na mimi naomba na tathmini hiyo au Tume nayo iende kule Hanang kuona tatizo ni nini ili tuweze kusahisha wananchi wapate maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukukaribisha. Karibu sana kwenye Bunge, tangu ulivyotuacha, tunaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la mama yangu Mheshimiwa Mary Nagu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuhusu changamoto za miradi, Wizara yangu tayari imeunda timu ya wahandisi ambayo imeshaanza kazi, ambayo itakuwa inapitia maeneo yote ya changamoto. Ni wataalam wazuri, wataainisha changamoto zote ili tuweze kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu miradi ambayo tumeshapata vyanzo vya maji kama kwa Mheshimiwa Mary Nagu kule Katesh, katika Programu ya Utekelezaji wa Miradi

ya Maji kwanza tunatafuta chanzo, tukishapata chanzo ndiyo tunatafuta sasa fedha kwa ajili ya kuweka mtandao wa mabomba.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mary Nagu kwamba bajeti inayokuja tutaweka fedha za kutosha ili tuweze sasa kuyachukua maji na kuyapeleka kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Bado tuko Wizara hiyo hiyo Waheshimiwa. Naomba tuendelee na swali la Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar, Mbunge wa Newala Vijijini na kwa niaba yake nimwombe Mheshimiwa Abdallah Chikota.

Na. 42

**Mradi wa Maji wa Makondeko**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA (K.n.y. MHE. AJALI R. AKBAR)** aliuliza:-

Je, nini hatma ya Mradi wa Maji wa Makondeko?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeandaa mpango madhubuti katika kuhakikisha inaboresha huduma ya maji kwa wananchi wanaohudumiwa na Mradi wa Maji wa Kitaifa wa Makonde. Katika kufikia lengo hilo, Wizara inatekeleza mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kazi za muda mfupi, Wizara imefanya ununuzi wa mabomba ya urefu wa kilometa 24 kwa ajili ya kukarabati baadhi ya maeneo yaliyochakaa sana yenye kipenyo cha inchi mbili hadi sita,

kwa maeneo ya Makote hadi Nanguruwe, Nanda hadi Kitangali, Chihangu hadi Mnyambe, Ghana Juu hadi Lukokoda na Mahuta hadi Nanywila. Aidha, ununuzi wa pampu kumi umefanyika ambazo zitafungwa katika vyanzo vitano vya kuzalisha na kusambaza maji. Matayarisho ya ulazaji wa mabomba na ufungaji wa pampu yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda wa kati Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo *(CRIDIF)* kutoka Afrika ya Kusini wametekeleza ukarabati wa visima sita ambavyo vimeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita miloni 6.72 hadi lita milioni 11.88 kwa siku katika chanzo cha Mitema.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa *CRIDIF* wanaendelea na upembuzi yakinifu kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili ambayo itahusu ununuzi na ujenzi wa bomba kuu kutoka chanzo cha Mitema kwenda Nanda la urefu wa kilometa 8.56 lenye kipenyo cha inchi 12; ujenzi wa mtandao wa usambazaji kutoka Nanda kwenda Kijiji cha Mtopwa na ukarabati na ujenzi wa matanki ya maji katika Vijiji vya Mtopwa, Nanywila na Mtavala.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa muda mrefu, Serikali imepanga kutumia kiasi cha dola za Kimarekani milioni 84 kutoka mkopo wa masharti nafuu wa Serikali ya India ambazo zitatumika kufanya ukarabati wa mradi mzima. Kwa sasa majadiliano kwa ajili ya kusaini mkataba wa kifedha yanaendeea kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya India.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chikota, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kila tunapouliza kuhusu ukarabati mkubwa wa Mradi wa Makonde tunaambiwa kwamba kuna dola za Kimarekani milioni 84 ambazo ni za mkopo kutoka

Serikali ya India, lakini kila siku tunaambiwa majadiliano yanaendelea. Sasa nilitaka nipate *commitment* ya Serikali, majadiliano hayo yataisha lini na mkataba utasainiwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mradi huu wa Makonde unahusisha Halmashauri nne; Newala Vijijini, Newala Mjini, Tandahimba na Nanyamba, lakini majibu ya Naibu Waziri yanazungumzia Halmashauri tatu tu. Sasa nilitaka nipate maelezo ya Serikali kuhusu mpango wa Serikali kutoa maji Mitema na kupeleka Halmashauri ya Mji wa Nanyamba.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Chikota kwa namna ya kipekee anavyowatetea wananchi wake, lakini kikubwa ni kuhusu suala la fedha za India.

Sisi kama Wizara ya Maji, kwa kuwa huu ni mpango mkubwa na mpango wowote mkubwa wenye mafanikio makubwa lazima uchukue muda. Sisi kama Wizara tunafuata taratibu lakini tunaamini utekelezaji wa mradi huu utaondoa kabisa tatizo la maji. Kwa hiyo, sisi kama Wizara ya Maji tutafanya jitihada za haraka ili jambo hili liweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la chanzo cha Maji cha Mto Mitemba, sisi kama Wizara tumeshapokea andiko kuhusu suala zima la kutumia chanzo cha Mitemba ambacho kitaweza kutatua tatizo la maji kwa Halmashauri tatu, kwa maana ya Halmashauri ya Tandahimba, Newala na Nanyamba pamoja na maeneo ya jirani. Kwa kuwa andiko lile tumelipata, tunalifanyia kazi katika kuhakikisha tunalitekeleza kwa wakati kama ilivyopangwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa twende swali la mwisho kwa siku ya leo. Mtaona muda wetu ulivyo; kwa

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, tafadhali.

Na. 43

**Kufungwa kwa Mnada wa Magena - Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Mnada wa Magena uliopo Halmashauri ya Mji wa Tarime una miundombinu yote licha ya kufungwa na Serikali bila sababu maalum na kusababisha adha kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo pamoja na upotevu wa ushuru. Mwaka 2016 aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi alitembelea mnada huo na kuagiza mnada ufunguliwe.

Je, ni kwa nini mnada huu wa Magena haujafunguliwa mpaka sasa ili kutoa fursa za ajira na kuokoa mapato yanayopotea?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, na mimi naomba uniruhusu kwanza kukukaribisha kama vile walivyokukaribisha Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika Bunge letu tukufu.

Mheshimiwa Spika, niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnada wa Magena ulikuwa kati ya minada 10 ya mipakani uliokuwa chini ya Wizara ya Kilimo na Mifugo mwaka 1995. Mnada huo ulikamilika kujengwa mwaka 1995 na kufunguliwa mwaka 1996 ambapo ulifanya kazi kwa takriban mwaka mmoja, ambapo ng'ombe 104,000 waliuzwa na jumla ya shilingi milioni 260 zilikusanywa kama maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza, ikiwemo wizi wa mifugo na sababu

za kiusalama, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mara, tarehe 14 Mei, 1997 iliagiza mnada huo ufungwe na kuwapatia wafugaji mnada mbadala wa Mpakani. Kutokana na hali hiyo, uongozi wa Mkoa wa Mara uliiomba Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ya wakati huu ifute mnada wa Magena na *Kirumi Check Point* iteuliwe kuwa mnada wa mpakani kwa kuwa tayari kuna kizuizi cha Mto Mara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilikubali ombi la uongozi wa Mkoa wa Mara na hivyo ikaanza kujenga mnada eneo la Kirumi sehemu ambayo kuna kizuizi cha asili cha Mto Mara na ujenzi huu umekamilika kwa asilimia 80 na unatarajiwa kufunguliwa mwaka huu wa 2017/2018. Kwa kuwa kazi ya Kituo cha Polisi inaendelea na kazi ya kuweka umeme katika eneo lile imekamilika.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Mnada wa Kirumi yameanza kuonekana ambapo Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Mara, kuanzia mwezi Julai, 2016 hadi Februari, 2018 imekusanya jumla ya shilingi 221,270,000 kutokana na vibali na faini mbalimbali za ng'ombe 9,842, mbuzi na kondoo 4,886 kutoka Mikoa ya Rukwa, Kagera, Simiyu, Shinyanga, Mara na Mwanza waliokuwa wakisafirishwa kwenda Kenya bila ya vibali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Kwanza kabisa nioneshe masikitiko yangu na kwa namna gani Serikali haiwezi kuweka kumbukumbu. Mwaka 2016 niliuliza swali hili na majibu walinipa haya haya licha ya kwamba aliyekuwa Waziri alikuja Tarime na akajionea hali halisi na akatoa agizo kwamba ule mnada ufunguliwe, lakini leo mnaleta majibu ya kumbukumbu za mwaka 1997. Maswali yangu mawili ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wafanyabiashara wa ng'ombe wanapeleka ng'ombe nchini Kenya kwa mnada

ambao upo mpakani wa Mabera kupelekea upotevu mkubwa wa mapato ambayo yangekuja Tanzania kupitia *multiplier effect,* Wakenya wangekuja kununua zile ng'ombe Tanzania kwa sababu wanategemea ng'ombe za kutoka Tanzania kuliko ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali hamkutaka kutumia rejea ya muhtasari ya kikao cha mwaka 2016 ambapo tulikaa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Tarime, Waziri na watendaji wa Wizara husika pamoja na mimi Mbunge na baadaye tukaongea na wananchi? Kwa nini hamkutumia ule muhtasari ili mweze kufuata maamuzi yaliyofikiwa kuweza kufungua Mnada wa Magena?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wafanyabiashara wa ng'ombe ambao wanapeleka Kenya wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa sana kwenye kuvusha ng'ombe hizi. Kwa kuwa mnada ambao wameuweka rejea wa *check point* ya Kirumi hautoi suluhishi, kwa sababu wakinunua ule mnada siyo wa mpakani wanapokuja kuvusha ng'ombe kwenda Kenya wanasumbuliwa sana.

Ni kwa nini sasa Waziri (maana yake inaonekana hamtunzi kumbukumbu) husika usije tena kwenye Mnada wa Magena uweze kujionea uhalisia na maamuzi yale ili sasa uweze kuruhusu mnada huu kufunguliwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko na kwa hakika Mheshimiwa Esther Matiko anashiriki kikamilifu katika kumuunga mkono Mheshimiwa Rais juu ya ulinzi wa rasilimali za nchi yetu na ndiyo maana anasisitiza sana kuhakikisha rasilimali za mifugo zinaweza kudhibitiwa pale ili ziweze kuinufaisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anatusisitiza kwa nini tusitumie Mnada wa Magena sawa na muhtasari wa

mwaka 2016 ilipokaa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya kule Mara na Wizara yetu; na swali la pili, kwa nini Mheshimiwa Waziri asiende Magena?

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie kwamba hivi sasa Wizara yetu imeunda tume maalum ambayo inapitia maeneo yote katika nchi yetu kufanya tathmini ya minada tuliyonayo ya awali zaidi ya 480 na minada ya upili na mipakani ili kuweza kujiridhisha na maombi yaliyoletwa. Nataka nimwambie kwamba moja ya eneo ambalo tutalifanyia kazi baada ya tathmini hii inayokwenda kukamilishwa na Wizara na wataalam wetu, ni hili alilolileta hapa Mheshimiwa Esther Matiko.

Mheshimiwa Spika, kwa kumhakikishia ni kwamba tutafika Magena pia. Mimi kama Naibu Waziri na Waziri wangu tutakubaliana, tutakwenda Magena kujiridhisha na hiki anachokisema. Kwa faida ya nchi yetu, tukiona kwamba jambo hili lina faida nasi, tutalitekeleza sawa na ushauri wake. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona muda hauko upande wetu na tuna mambo mengi mezani siku ya leo. Tuendelee na mipangilio mingine.

Kwanza kabla sijatangaza wageni tulionao leo, nichukue nafasi hii Waheshimiwa Wabunge kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunirudisha salama. Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa dua na sala zenu na niwashukuru sana wote walioniombea, Watanzania wengi sana walikuwa wakituma habari; na kipekee wapiga kura wangu wa Kongwa, nasema wote kwa ujumla wenu ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mwanadamu sio jiwe, lazima kupita katika mapito na kila mwanadamu ana mapito anayoweza kupitia

kutegemeana na tunaoamini alivyopangiwa. Kwa hiyo, ukiupata msalaba, unaubeba kwa amani. Niendelee tu kumwomba Mwenyezi Mungu kwamba msalaba wangu na mimi usiwe mzito sana, uwe wa kadiri tu. *(Makofi)*

Vinginevyo nashukuru tumerudi tupo pamoja na niwashukuru sana wasaidizi wangu hapa mezani, Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia; Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Najma; Katibu wa Bunge na timu yake, wamefanya kazi kubwa sana wakati ambao sikuwepo kwa kushirikiana nanyi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaomba tuendeleze gurudumu letu na tuna kipindi kirefu cha Bunge la Bajeti, kwa hiyo bila ushirikiano mkubwa wa karibu, kazi yetu itakuwa ngumu. Nawashukuru sana wote kabisa. *(Makofi)*

Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu tulikuwa tukiwasiliana na alikuwa akinitia moyo sana nilipokuwa kitandani kule. Baadhi yenu labda hamjawahi kulazwa hospitali mkiwa mnaumwa sana, halafu *somehow* upo kama peke yako kidogo, halafu ukaona jinsi ambavyo mawazo yanavyokuja, yanavyozunguka na wakati mwingine dalili zinataka kuonyesha kama kesho kunaweza kusikuche hivi; ina raha yake na taabu yake kidogo. Siwaombei mpitie katika mambo hayo, nawaombea msipate machungu hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni tulionao leo ni wageni wawili wa Mheshimiwa Oscar Mukasa ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Maendeleo ya Jamii Hombolo Mkoani Dodoma, karibuni sana wanafunzi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara

ambao ni wapiga kura wake kutoka Mvomero Mkoani Morogoro. Karibuni sana wana Mvomero, karibuni Bungeni.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Ally Saleh ambao ni familia yake kutoka Zanzibar wakiongozwa na mke wake Bi. Mwanahamis Maulid. Ahsante sana, karibuni sana Dodoma. Dodoma ni njema, ni shwari kama Zanzibar vile. *(Makofi)*

Wageni wengine ambao wametembelea Bunge ni wageni watano ambao ni wakazi wa Nkuhungu, mkoani Dodoma. Karibuni sana wana Nkuhungu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu napenda tuwape pole Wabunge wa Mkoa wa Lindi na wananchi wa Lindi kwa ujumla kutokana na msiba uliotokea leo asubuhi wa Mzee Mtopa aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Lindi kwa miaka mingi. Nimepata taarifa hizo, napenda kusema poleni sana Wana-Lindi. Huyu Mzee alikuwa mmoja wa viongozi mahiri kabisa katika siasa za nchi yetu. Katibu.

**MHE. GOODLUCK MLINGA:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**SPIKA:** Haya Katibu nitajie majina.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Kauli za Mawaziri.

**SPIKA:** Nitajie majina ya wenye miongozo.

**NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Pudenciana, Mheshimiwa Komu na Mheshimiwa Mlinga.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaanza na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ambayo inajulikana, sina sababu ya kuisoma.

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma tulipewa taarifa humu Bungeni ambayo tuliona ni njema, kwamba Wabunge hawatakuwa wanavaa vitambulisho badala yake unakuwa nacho kwenye *bag* ikitokea kuna mahali kuna sintofahamu unaweza ukatoa kwa maana ya kujieleza zaidi kwa watu ambao labda kuna walinzi wageni, tangu tumeanza Bunge hili limejirudia na hatujapata maelezo, tukiuliza kama Wabunge hatuambiwi ni kwa nini hili zoezi, badala ya kwenda mbele, ku-*advance,* tuliomba hatua ya kuvaa vitambulisho kama watoto wa shule imeshapitwa na wakati, sasa ije hoja ya hata kutovua mikanda na viatu, kuwe na teknoljia ya kisasa sana, lakini kwa namna ilivyo ni kwamba tunarudi nyuma zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako na ni muhimu katika hili kama kunakuwa na mabadiliko makubwa kama haya basi Wabunge tunajulishwa, wewe unaambiwa tu kitambulisho kiko wapi, huelewi kinachoendelea. Nadhani kwamba hili jambo ni muhimu na kwa sababu bahati nzuri umerudi, upo, tupate maelezo. Ni kwa nini badala ya kwenda mbele kiulinzi tunarudi nyuma na ni kwa nini hatukupata taarifa, ni sababu gani za msingi, labda huenda hivi vitambulisho vimezuia nini au vinaongeza nini. Ni hayo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 67(8) ambayo sitaisoma kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Spika, leo wakati swali namba 40 likiwa linajibiwa kumetokea mkanganyiko humu Bungeni, kwa sababu Naibu Waziri amesema Magereza yetu yamezidiwa na wafungwa kwa kiasi cha wafungwa 10,000 lakini baadae

Mheshimiwa Waziri akasema siyo kweli kwamba katika Magereza yetu yote Magereza yameelemewa. Sasa kwa sababu ya kuweka rekodi sawasawa, tunaomba mwongozo wako ili tujue ni nani yuko sahihi kati ya Waziri na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili kama Waziri yuko sahihi, Serikali ikiri vilevile kwamba...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri amesema siyo Magereza yote, yapo baadhi ya Magereza na akatoa mifano ya Gereza la Lindi na Gereza lingine ambalo lina wafungwa wachache kwa hiyo, hakuna *contradiction* hapo. *(Makofi)*

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo sehemu ya pili ya sababu ya kuomba mwongozo wako, kwamba kama ni kweli kwamba kuna baadhi ya magereza ambapo *capacity* haijawa *utilized accordingly,* nafikiri Serikali inapaswa ikiri kwamba kwenye hiyo Wizara kuna upungufu mkubwa sana wa ufanisi, kwa sababu kama mateso yalivyoelezwa kwenye maswali ya nyongeza, hivyo ndivyo hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kungekuwepo na kila sababu ya...

**SPIKA:** Mheshimiwa Komu nakuomba ushauri wako huo uweke, itakapokuja Wizara ya Mambo ya Ndani utachangia tu huo ushauri vizuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba mwongozo wako kuhusiana na mambo yanayoendelea kutokea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, tumeanza Bunge hili muda mrefu na tukiwa tukitumia hizi mashine za kukaguliwa. Mashine hizi nafikiri mwanzoni tulikuwa tunaweza kupita vizuri, lakini kwa

sasa inaonekana tunaanza kuvua nguo, maana yake unapoambiwa uvue viatu, mwili wa binadamu una vivutio mbalimbali. Sasa unaona mtu anaanza kuvua mkanda unaanza kushtuka, utasema sasa huyu vipi, anaanza kujiandaa ama vipi, anapoanza kufunga mkanda lazima afunue shati, sasa utaona maumbile ya ndani na tuko hapa zaidi ya mwezi mzima, kwa hiyo, kidogo inaniletea taabu. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, leo pia nimepita pale, baada ya kupita kote nilikopita mashine hazikupiga kelele, nimefika hapa mashine imepiga kelele nikasema viatu, nikavua, nikawaambia jamani lakini kuvuanavuana vitu siyo vizuri, tengenezeni mashine zenu. Baadae nikapita tena, mashine ikalia, wakasema mkague, sasa katika kukagua tunashikanashikana, mtu anakushika, kwa kweli haipendezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitegemea..., Waheshimiwa Wabunge siyo jambo la kuchekesha, mimi nilitegemea angekuwa mashine ya kupitisha juu ya mwili lakini katumia mikono yake kunipapasa. Sasa tuelewane jamani, wengine tunatoka Katavi huko mbali, tumeacha familia zetu, mambo ya kuanza kupapasana asubuhi unaweza ukamharibia mtu uelekeo wa kuingia Bungeni na kuanza kusikiliza. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, pamoja na marekebisho ya hizo mashine, kwa sababu hizo mashine hazijirekebishiki *automatically,* ni wao wanazirekebisha, basi ziweze kutambua vitu. Huwezi kuanza kumshikashika mtu mpaka kiunoni, kuna vitu vya ndani vinavyopiga kelele pale. *(Kichecko)*

Mheshimiwa Spika, isifike mahali tukaanza kutiana hanjamu bila sababu za msingi. Kwa hiyo, ninaomba hizo mashine wazirekebishe zitusome, zisome baadhi ya vitu na siyo kukaa tunavuana mikanda, viatu, kuna vidole vina kazi zake, sasa mambo ya kukaa tunavuanavuana nguo siyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo pia kuhusu viti. Hivi viti bado havijatengenezwa vinatuumiza migongo.

Mheshimiwa Spika, mimi yangu ni hayo tu. ahsante. *(Makofi/ Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Bado Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, bado Mlinga.

**SPIKA:** Najua kwamba Mheshimiwa Mlinga bado, lakini kwa jinsi hoja hii ilivyopigiwa makofi mengi ndiyo maana nikasimama kidogo, inaonekana hili jambo linawakera wengi humu ndani ya mjengo. Suala alilolisema Mheshimiwa Waitara la kuvaa vitambulisho na hili la kwenye milango yetu ya kuangalia mambo ya usalama. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge amesikia, naomba tuyafanyie kazi haya malalamiko, tuzungumze na wenzetu tuone namna bora zaidi ya kufanya mambo kisomi na kwa nia bora zaidi. *(Makofi)*

Kwa kweli, kupapasana papasana hakufai hata kidogo, hizo kwanza ni njia za kizamani kweli za kufanya kazi. Kama watu hawajakaa sawasawa, lakini waache kabisa hiyo habari ya kupapasa Wabunge wangu, haiwezekani hata kidogo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mengine tutayaweka sawa, mengine tutazungumza kwenye Kamati ya Uongozi ili tuweze kwenda tu vizuri bila tatizo lolote. Kwa sababu bahati nzuri baadhi ya mageti Mbunge akifika wakiaangalia jina lake na picha yake inaonekana pale kwamba ni Mbunge huyo ameingia. Kwa hiyo tutazungumza, unaweza ukawawekea hivyo vitambulisho wageni wote na wafanyakazi, lakini Wabunge wasivae kwa sababu tayari umeshaona picha yake. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Baba!

**SPIKA:** Tutayaweka sawa na tutaambiana wakati ukifika. Tunaendelea na Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wangu unahusu kudhalilishwa kwa Bunge. Gazeti la Raia Mwema, Toleo Namba 556 la tarehe Tisa na 10 Aprili, 2018, limeandika kwa maandishi makubwa Bunge linajipendekeza?

Mheshimiwa Spika, gazeti hilo limeweka picha ya Mbunge Mstaafu, Baba yetu, Marehemu Samuel Sitta, Mheshimiwa Anne Makinda na picha yako wewe, kwa maelezo yake ndani mwandishi amejaribu kutengeneza taswira ya ushiriki wa Bunge katika ufunguzi wa miradi mbalimbali ya Mheshimiwa Rais tunaposhiriki kana kwamba tunajipendekeza.

Mheshimiwa Spika, mwandishi ameshindwa kuelewa kuwa kazi ya Bunge ni pamoja na kuisimamia na kuishauri Serikali, hivyo ninaomba mwongozo; kwanza gazeti hili limelidharau Bunge; pili, gazeti hili limelidhalilisha Bunge kwa wananchi ambao ndio tegemeo lao kwa ajili ya kuisimamia Serikali; tatu, gazeti hili linataka kutuchonganisha kati yetu Wabunge na Mheshimiwa Rais; mwisho, gazeti hili linataka kutuchonganisha sasa kwa wananchi kuwa tumewatelekeza matokeo yake tumeikumbatia Serikali.

Kwa hiyo, mwongozo wangu nataka ama wahariri wa magazeti haya wachukuliwe hatua na mwisho wahariri wa magazeti yote ambayo tunayategemea katika Taifa letu tuwaite tuwape semina waelewe umuhimu wa Bunge kwa Serikali ni nini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mlinga, nashukuru sana. Hilo nitalitolea maelezo katika siku zijazo, tulichukue ili Katibu na timu yake waweze kupata hilo gazeti, walipitie na tupate ushauri unaohitajika kuhusiana na jambo hilo. Nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**KAULI ZA MAWAZIRI**

**SPIKA:** Kauli za Mawaziri Waheshimiwa Wabunge ni kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Ningeomba Waheshimiwa Wabunge mbaki mmsikilize vizuri, nadhani anajaribu kuja kutoa maelezo kuhusu jambo ambalo mmelilalamikia sana humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Kepteni Mkuchika, karibu tafadhali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niungane na Wabunge wenzangu kukukaribisha nyumbani, tunazidi kukuombea afya yako izidi kuimarika ili tuliokuchagua kuwa Spika, uendelee kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa kauli za Serikali kuhusu watumishi walioondolewa kwenye Mfumo wa Malipo ya Mishahara kwa kukosa sifa ya cheti cha kufaulu mtihani wa elimu ya kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kupitishwa na kuanza kutumika kwa Sera ya Menejimenti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la mwaka 1999, pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma *(The Public Service Act)* Na. 08 ya mwaka 2002, Serikali iliweka sharti kwamba kiwango cha chini cha kuwezesha mtumishi kuajiriwa katika utumishi wa umma ni kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne.

Aidha, kwa nyakati mbalimbali, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Serikali kupitia TAMISEMI, ilitoa nyaraka kadhaa za kufafanua utekelezaji wa uamuzi huo kama ifuatavyo:-

(a) Nyaraka mpya za kada mbalimbali za maendeleo ya utumishi wa umma za mwaka 2002 ambazo zilihuisha utumishi wa umma ili kuendana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la mwaka 1999 na Sheria ya Utumishi wa Umma *(Public Service Act)* Na. 08 ya mwaka 2002.

(b) Waraka wa Utumishi *(Establishment Circular)* Na. 01 wa mwaka 2004 kuhusu utekelezaji wa miundo ya maendeleo ya utumishi ya mwaka 2002 ambao ulieleza kwamba Watumishi wa Umma ambao walikuwa katika ajira kabla ya tarehe 20 Mei, hawatalazimika kujipatia sifa ya kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne ili waendelee na ajira katika utumishi wa umma.

Nataka kurudia tena hapa, watumishi wa umma ambao walikuwa katika ajira kabla ya tarehe 20 Mei, 2004, hawatalazimika kujipatia sifa ya kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne ili waendelee na ajira katika utumishi wa umma. *(Makofi)*

(c) Katibu Mkuu - Utumishi, barua yake ya tarehe 10 Aprili, 2006 ambayo pamoja na mambo mengine ilibainisha kwamba ajira zote mpya hazina budi kufanyika kwa kuzingatia miundo ya maendeleo ya utumishi iliyokuwa ikitumika wakati huo, mwaka 2006 ambayo moja ya vigezo vikuu ilikuwa kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne kama sifa ya msingi.

(d) Barua ya Katibu Mkuu - TAMISEMI ya tarehe 13 Julai, 2005 kuhusu utekelezaji wa ajira za mkataba wa miaka mitatu, mitatu kwa watendaji wa vijiji na mitaa. Barua hii iliwatambua watendaji wa vijiji 3,940 waliokuwa na sifa na ambao hawakuwa na sifa yaani wenye kiwango cha elimu ya msingi (darasa la saba) waliokuwa kwenye ajira ya mkataba kabla ya tarehe 20 Mei, 2004.

(e) Barua ya Katibu Mkuu - Utumishi ya tarehe 30 Juni, 2011 ambayo ilieleza kwamba baada ya Katibu Mkuu Kiongozi kupokea maombi kutoka kwenye Mamlaka za

Serikali za Mitaa zilizokosa Watumishi wenye sifa za miundo ikiwa ni pamoja na sifa ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne, Katibu Mkuu Kiongozi ambaye ni Mkuu wa Utumishi wa Umma aliridhia ajira za watumishi wa kada mbalimbali wapatao 1,370 waajiriwe ili shughuli za Serikali zisiathirike katika Halmashauri husika.

(f) Barua ya Katibu Mkuu Utumishi ya tarehe 10 Julai, 2017 kuhusu ufafanuzi wa sifa ya kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne na cha sita katika ajira kwenye utumishi wa umma. Barua hii pamoja na mambo mengine ilisisitiza kwamba watumishi wa Umma ambao walikuwa katika ajira kabla ya tarehe 20 Mei, 2004 hawatalazimika kujipatia sifa ya kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne ili waendelee na ajira katika utumishi wa umma, isipokuwa wale walioajiriwa baada ya tarehe 20 Mei, 2004 ambao miundo yao ya utumishi iliwataka kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne na ambao hadi mwezi Julai, 2017 hawakuwa wamewasilisha vyeti vyao kuhakikiwa, mishahara yao isimamishwe kuanzia mwezi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama utakavyoona, utekelezaji wa ajira katika utumishi wa umma tangu kuanza kutumika kwa miundo mipya umekuwa na tafsiri tofauti na ndiyo sababu barua nyingi za kutoa ufafanuzi zilitolewa kuanzia mwaka 2002 baada ya Serikali kubaini kwamba baadhi ya mamlaka za ajira zilikuwa zikiajiri watumishi wasiokuwa na sifa stahiki katika baadhi ya kada.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo, Serikali ilitoa maelekezo kupitia barua ya Katibu Mkuu - Utumishi tarehe 10 Julai, 2017 ikiwataka waajiri kusimamisha mishahara ya watumishi walioajiriwa baada ya tarehe 20 Mei, 2004 wakiwa hawana sifa ya kufaulu mtihani wa elimu ya kidato cha nne hadi watakapowasilisha vyeti vyao. Katika zoezi hili jumla ya watumishi 7,384, Watendaji wa Vijiji 3,817, Watendaji wa Mitaa 51, Watendaji wa Kata 253, madereva wa magari 330, kada za afya 1,060 na kada nyinginezo walisimamishwa mishahara na waajiri wao. Hata hivyo, idadi hii ya watu 7,000 ilichanganya sasa watumishi ambao hawakuwa na sifa,

watumishi waliokuwepo kabla ya tarehe 20 Mei, 2004 pamoja na wale waliolegezewa masharti ya muundo wa Mkuu wa Utumishi wa Umma (Katibu Mkuu Kiongozi) kupitia barua iliyopitia kwa Katibu Mkuu - Utumishi ya tarehe 30 Juni, 2011.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelekezo hayo sahihi ya Serikali yaliyotolewa mara kwa mara, kumejitokeza malalamiko ya kutozingatiwa kwa maelekezo hayo wakati wa utekelezaji. Malalamiko haya yamepokelewa na ofisi yangu kutoka kwa watumishi walioathirika pamoja na Vyama vya Wafanyakazi. Aidha, Serikali imepokea ushauri na maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano huu wa Bunge unaoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali imeamua na inaagiza kama ifuatavyo:-

(a) Watumishi wote ambao walikuwa na ajira ya kudumu au ajira za mikataba kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa au ajira za muda *(employment on temporary terms)* ambao walikuwa kazini kabla ya tarehe 20 Mei, 2004 ulipoanza kutumika Waraka wa Utumishi *(Establishment Circular)* Na. 01 wa mwaka 2004 warejeshwe kazini mara moja. *(Makofi)*

Narudia tena sehemu hiyo, warejeshwe kazini mara moja, walipwe mishahara yao kwa kipindi chote ambacho walikuwa wameondolewa kazini, waendelee na ajira hadi watakapostaafu kwa umri kila mmoja. *(Makofi)*

(b) Watumshi wa umma 1,370 walioregezewa masharti ya sifa za muundo kupitia barua ya Katibu Mkuu - Utumishi ya tarehe 30 Juni, 2011 warejeshwe kazini mara moja, walipwe mishahara yao kwa kipindi chote ambacho walikuwa wameondolewa kazini na waendelee na ajira zao hadi watakapostaafu kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwamuzi huu uliotajwa hapo juu hautawahusu watumishi wa makundi yafuatayo:-

(1) Watumishi waliowasilisha vyeti vya kugushi katika kumbukumbu za ajira zao hata kama walikuwepo kabla ya 2004.

(2) Watumishi waliokuwepo katika ajira kabla 20 Mei, 2004 ambao katika kumbukumbu zao rasmi kama vile taarifa binafsi (*personal records)*, fomu za tathmini ya utendaji *(OPRAS)* na kadhalika. Wale ambao walijaza taarifa za uwongo kwamba wanayo elimu ya kidato cha nne lakini wakashindwa kuthibitisha kwa kuwasilisha vielelezo vya sifa hizo kwa mujibu wa miundo yao ya utumishi.

(3) Watumishi wote walioajiriwa baada ya tarehe 20 Mei, 2004 wakiwa hawana sifa ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne, kwa kuwa waliipatia ajira kinyume cha maelekezo ya Serikali.

(4) Watendaji Wakuu na Wakuu wa Idara za Utawala na Utumishi wote walioshiriki kuwaajiri watumishi wasiokuwa na sifa ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne katika utumishi wa umma baada ya tarehe 20 Mei, 2004 watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria kanuni na taratibu.

(5) Watendaji Wakuu na Maafisa wote wanaosimamia zoezi hili ambao kwa namna yoyote ile watashiriki kuhujumu zoezi hili kwa kuondoa au kuharibu muindombinu kuharibu kumbukumbu za watumishi ili haki isitendeke watachukuliwa hatua za kinidhamu na kijinai kama ikibidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Mkuchika tunakushukuru sana.

Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na uchangiaji kama ilivyo ada atakayeanza hapa ni Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye na Mheshimiwa Ngeleja ajiandae. Mheshimiwa Gimbi.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuweka mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii, pia nimpe pole Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mwenyekiti wangu na viongozi wengine waandamizi wanaopitia changamoto zinazoendelea katika Taifa hili. Naamini kabisa kwamba nguvu ya umma iko siku itashinda dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kumrudisha Mheshimiwa Spika wetu na kwa uhai ambao anao kwa sasa Mungu aendelee kumjalia na kumpa afya njema ili aweze kuliongoza Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja naomba niende kwenye Mkoa wangu wa Simiyu nikianza na changamoto ambazo zinaendelea katika Wilaya ya Itilima tarehe 30 Machi, kuna watu ambao wanaishi kandokando ya hifadhi waliuawa na tembo ambao wanazunguka kwenye mashamba ya wananchi. Naomba nitoe masikitiko yangu kwamba Serikali imekuwa ikikaa mbali sana na hawa wananchi ambao wanapata madhara haya na nisikitike kwamba hata kwenye misiba ya haya majanga yanayotokea

Serikali haifiki. Mfano ninao kwa hawa wananchi waliofariki tarehe 30 katika kijiji cha Nyantugutu na kijiji cha Longalombogo, hata Mkuu wa Wilaya hakufika kwenye huo msiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana tunapozungumza kwamba kuna kifuta machozi kwa hawa wananchi mfuko wa maafa ambao uko kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu uhakikishe kwamba hawa watu wanapopata madhara kama haya na familia zao Serikali iweze kufumbua macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili naomba nijielekeze kwenye mradi wa maji wa kutoka Ziwa Victoria kwenda Mkoa wa Simiyu.

Waheshimiwa Wabunge walionitangulia kuchangia Mheshimiwa Raphael Chegeni na Mheshimiwa Mashimba Ndaki wamegusia sana kuhusu suala la huu mradi. Mradi huu umekuwa ni kizungumkuti katika Mkoa wetu na nasikitika kwamba naamini kabisa toka uhuru au toka dunia iumbwe wananchi wa Mkoa wa Simiyu hawajawahi kuonja maji ya Ziwa Victoria licha ya kwamba kuna wengine wanaoga kwenye Ziwa Victoria lakini hawajawahi kunywa maji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ieleweke kabisa kwamba mnamuaibisha Mheshimiwia Rais, tunapozungumza kwamba Mheshimiwa Rais anatoka maeneo hayo ya Kanda ya Ziwa Victoria halafu kwenye maeneno yake hakuna maji ni jambo ambalo tunasikitika sana. Kwa hiyo, ninaomba sana mradi huu uharakishwe kwenye bajeti hii ya Serikali muone umuhimu wa kuhakikisha kwamba mradi huo unawafikia, kwani kuwafikia mradi huu haitoshi tu kwamba watanufaika kunywa maji hayo, inatosha pia kuchochea maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji katika mkoa huu. Kwa hiyo, niombe sana Serikali ione umuhimu wa kupeleka mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bado narudi kule kuhusu barabara ya kutoka Bariadi kupitia Makao Meatu kwenda Karatu, Arusha; Serikali ihakikishe kwamba ule ujenzi

unakamilishwa kwa wakati muafaka ili kuweza kuchochea maendeleo kwenye Mkoa wetu wa Simiyu kwa lengo la kupeleka maendeleo kwa kasi licha ya kuwa kwamba Mkuu wa Mkoa anapambana kadri Mungu ambavyo anamjaalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia sana kuhusu suala la kilimo, naomba nijikite kwenye suala la zao la pamba, kwenye zao la pamba lazima tukubaliane kwamba wananchi wamehamasika sana kulima zao la pamba sasa isitoshe tu kuhamasika kulima zao hili la pamba. Naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu itoe bei elekezi mapema ili wananchi hawa wajue kabisa kwamba mwaka 2018 watauza kwa bei ya shilingi ngapi katika zao lao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwa nini watoe bei elekezi kuna watu kwa sasa wanapita kwenye mashamba ya wakulima na kuwalaghai wananchi kwa bei ambazo wanaziona wao bila kujua kwamba wananchi hawa kuna muda itafika watauza kwa bei stahiki na watapata faida watanufaika na zao lao. Kwa hiyo, ninaomba mtoe kauli ya Serikali kwamba mwaka huu 2018 bei ya pamba ni kiasi gani lakini pia itoe kauli kwa wananchi ambao wanapita kwenye mashamba kwa ajili ya kuwalaghai wananchi hawa na matokeo yake wanashindwa kunufaika na pamba hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo nataka nichangie ni kuhusu Wilaya ya Itilima, Mheshimiwa Leah Komanya alisimama akauliza kuhusu swali la Hospitali ya Rufaa; mimi naomba nitoe masikitiko kwamba pamoja na kwamba Mheshimiwa mwenzangu anadai kwamba tupate Hospitali ya Rufaa, Mkoa wa Simiyu una Wilaya kama mbili mpya lakini nasikitika kwamba Wilaya hizi hazina hata Hospitali ya Wilaya, hazina Mahakama za Wilaya, hazina Vituo vya Polisi hususani Wilaya ya Itilima ambayo ni miongoni mwa Wilaya kubwa. Wilaya ina kata 22, ina vijiji 102, ina vitongoji 446, imegawanyika katika tarafa nne lakini cha kusikitisha Wilaya ya Itilima haina Hospitali ya Wilaya, haina Mahakama ya Wilaya na tatu, haina Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi kilichopo kiko nje na Makao Makuu ya Wilaya kwa maana ya kata jirani na hata tarafa jirani. Kwa hiyo, ninaomba sana kwamba angalau kwenye bajeti ya 2018/2019 basi Serikali ione umuhimu angalau kutupatia kimojawapo kati hivi ambavyo nimevitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia kwa umakini sana ni suala la viwanda. Ukisoma kwenye mpango wa bajeti wa mwaka 2018/2019 katika ukurasa wa 12, kifungu cha (8), Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mpango ametueleza kwamba mpaka sasa Serikali ina viwanda 3,600. Pia ukisoma kwenye ripoti ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda ametueleza kwamba tuna viwanda 3,060 ukisoma kwenye ripoti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye anasema tuna viwanda 3,306. Sasa wapo watu wanahoji kwamba tunataka kujua viwanda vidogo ni vingapi na viwanda vikubwa ni vingapi, mimi nomba muhoji kwamba hii ni Serikali moja lakini kila mtu ana takwimu za kwake. Kwa hiyo, ni namna gani ambavyo huhitaji kuhoji maswali mengi unahitaji kupata majibu kupitia *document* na *data* zao ambazo wanazitoa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeongoza Taifa hili kwa miaka miwili na zaidi lakini naomba niseme kwamba kwa lugha nyepesi ni kwamba tumefanikiwa kuwa na hivi viwanda ambavyo tayari vina takwimu hizi ambazo ninyi mnaweza mkajumlisha mkaona kwamba Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mpango ame-*miss* vingapi na Mheshimiwa Waziri Mkuu ame-*miss* vingapi.

Mheshimiwa Spika, turudi kwenye historia ya Mwalimu Nyerere, Mwalimu Nyerere alitawala miaka 24 kwa taarifa ya Dkt. Neville Reuben katika Kigoda cha Mwalimu 2016 amesema kwamba Mwalimu Nyerere alifanikiwa kuwa na viwanda 414 kwa kipindi cha miaka 24 aliyotawala.

Ndugu zangu mnaweza mkaona kwamba hawa ndugu zangu wao wametawala miaka miwili na zaidi wako hapo kwenye hivi viwanda.

Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge wanahoji kwamba viwanda vidogo ni vingapi na vikubwa vingapi! Waheshimiwa Wabunge nataka niwaambie mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Mazingira, hivi viwanda mnavyovihoji mimi Mjumbe sijawahi kuviona. Sijawahi kuviona kwa sababu hata kwenye ziara ya Kamati ilifaninkiwa kwenda kutembelea *SIDO* kwenye karakana za *SIDO* ambazo hata mashine zake zilizoko kule hata watumishi majina yake walishasahau zinaitwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni namna gani Kamati haishirikishwi ipasavyo kwenye jambo la kufika kwenye hivi viwanda ingawa hivi viwanda ukimsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda anavijua kwa ufasaha mkubwa, hali kadhalika tumeona namna ambavyo Mheshimiwa Rais kuna maeneo anasema viwanda hivi vipo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kwa heshima kabisa, ikizingatiwa kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba taarifa zinazotolewa kuhusu viwanda na tumekuwa tukitoa ufafanuzi mara kwa mara, mpaka kufikia mwaka 2014 kutokea kwenye sensa ya mwaka 2012 na 2014 ikahakikiwa taarifa rasmi zilisema kwamba, Tanzania kwa ujumla wake kwa viwanda vidogo sana, vidogo, vya kati na vikubwa tulikuwa na viwanda 53,243 na kwa kipindi hiki cha Awamu ya Tano taarifa inasema kwamba tuna viwanda 3,306 tumekuwa tukiwafahamisha kila wakati, lakini ni ngumu ngumu sana kukubaliana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusu suala la

kutembelea viwanda tunaomba pia hilo ulitoe kama mwongozo wako, kwa sababu Wizara tunadaiwa kuwatembeza Waheshimiwa Wabunge kwenye kila kiwanda wakati nafahamu kwa uzoefu wangu kwamba Kamati inapotembelea kama ni kiwanda au kama eneo lolote wanalohitaji kutembelea ni pamoja na jinsi ambavyo ratiba inakuwa imepangwa kupitia Ofisi yako.

Kwa hiyo, naomba hayo yawekwe vizuri ili tusiwe ikawa inatoa migongano ya mara kwa mara kati ya Wizara na Kamati. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dotto ulishamaliza muda wako na hii ni taarifa tu ya ujumla, kwa hiyo, haina haja sana ya wewe kuweza kuulizwa kama unaikubali au huikubali lakini taarifa ya ujumla ni taarifa ya Serikali kwamba takwimu ziko hivi.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Kamati nilitaka kusema tu kitu kimoja, safari za Kamati hizi ambazo mlienda mara ya mwisho Kamati zote madhumuni yake yalikuwa ni kwamba muende mkaangalie utekelezaji wa kazi za Serikali kwa bajeti mliyoipitisha mwaka wa fedha huu ambao tunaumalizia hivi sasa, hata mwakani itakuwa hivyo pale mwishoni ni kufuatilia utendaji wa shughuli za Serikali. Kwa hiyo, isingekuwa rahisi kwenda kutembelea viwanda binafsi vya watu huko katika ratiba hii.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tuelewane tu kidogo, vinginevyo baadae inatakiwa ninyi wenyewe kama Kamati mjipangie wakati, kwa sababu mna bajeti yenu mna Mwenyekiti wa Kamati, mna Makamu mna Makatibu, mna bajeti yenu, vipaumbele mnaviweka ninyi wenyewe. Kwa hiyo, haisaidii sana kuja kulalamika hapa Bungeni wakati kumbe mpira mnao ninyi wenyewe. Katika ile ziara ambayo inawekwa kwa jili ya kukagua shughuli za Serikali msichanganye na haya mambo tena ya binafsi, haiende hivyo. Ahsante sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, tunakukaribisha tena nyumbani namshukuru Mungu aliye kukurudisha salama, karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa uamuzi ambao umewasilishwa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Utumishi Baba yangu Mzee Mkuchika. Nadhani mmefanya jambo jema kuona hali halisi na kuchukua hatua. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi waliouchukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipopiga kura mwaka 2015 Mikoa ya Lindi na Mtwara, moja ya sababu tuliamini sana kwamba uchumi wa gesi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara ni ukombozi mkubwa na uko salama mikononi mwa Rais Magufuli na Serikali ya Awamu ya Tano. Tulipopiga kura ndiyo ulikuwa mkataba wetu siyo, kwa maneno lakini iliwekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 76 na 77 inaanzia ukurasa wa 75, eneo kubwa sana limezungumzwa uchumi wa gesi, suala la gesi na imeandikwa mafuta na gesi asilia. Kwa hiyo, kura nyingi alizozipata Magufuli ni kwa sababu ya makubaliano haya yaliyoko kwenye hii Ilani ya Uchaguzi kwamba atakwenda kuyaendeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa *summary,* moja ilikuwa ni kuendela miundombinu ambayo ita-*facilitate* huu uchumi wa gesi wa Lindi na Mtwara. Pili, ilikuwa ni kuwandaa wananchi wanufaike na kufaidika kwa gesi na mafuta kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Lipo jambo *specific* la ujenzi wa mradi wa *LNG plant* kwa Mikoa ya Lindi, kwa hiyo hili limo kweye ilani ya uchaguzi. Pili, kwenye mpango wa miaka mitano na mpango ambao umekuwa ukiwasilishwa hapa mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana nilipoangalia hotuba ya Waziri Mkuu kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho hakuna neno gesi kabisa. Inaonekana ukienda hata *site* kwenyewe, shughuli mbalimblai zinazoendana na

gesi kwa Lindi na Mtwara ni kama vile zimeanza kufungwa na zimesimama kabisa.

Swali langu la kwanza, hivi ni bahati mbaya hotuba ya Waziri Mkuu imeshindwa kuliona jambo hili kuwa ni kubwa na ikaamua kuliacha au Serikali imeamua kuachana nalo? Kwa sababu naona jitihada kubwa zinaanza kwenda kwenye *Stieglers* (umeme wa maji) mimi sina matatizo nalo inawezekana ndiyo maamuzi lakini *Stieglers* kwenye Ilani haimo. Ilani tumezungumza nishati ya gesi tena kwa sehemu kubwa sana na hii ndiyo ilikuwa imani ya wananchi wa Lindi na Mtwara kwa Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zilikuwepo jitihada zilifanywa na Mzee Mwinyi mpaka tukapata Songosongo, jitihada zikafanywa na Mzee Mkapa, Awamu ya Nne ikaja kwenye jitihada hizi za huu uchumi ambao tulianza kupata matumaini nao.

Mheshimiwa Spika, wakati jitihada zinafanyika watu watakumbuka, kuna watu walipoteza maisha Lindi na Mtwara, kuna watu walipata majeraha na vilema Lindi na Mtwara, kuna mali za watu lakini tukaamini kuna neema kesho. Kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na bahati mbaya tulimkabidhi Mheshimiwa Magufuli tukaamini liko salama, alipotupa Mheshimiwa Majaliwa tukaamini tuko salama zaidi, kwa sababu Waziri Mkuu ametoka kwetu. Sasa ni bahati mbaya sana kwamba humu ndani hakuna kabisa, maana yake ni kwamba hili jambo pengine limeanza kuachwa sasa twende kwenye *Stieglers*. Je, hatusaliti Ilani ya Uchaguzi ya CCM? Je, hatuwasaliti wananchi wa Lindi na Mtwara waliotupa kura na kutuamini kwamba gesi yao na uchumi wao uko salama? Hili ni bomu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa mchakato hali ya kisiasa, hali ya kijamii Lindi na Mtwara kulikuwa na taabu, sasa imetulia tukiamini neema ipo, kiuchumi baada ya harakati za gesi na mafuta Kusini watu walianza kuja kuwekeza uchumi wa Lindi na Mtwara ukaanza kukua, watu wakaanza kuwekeza. Hali ilivyo sasa hivi watu wameanza

kuondoka, uchumi wa Lindi na Mtwara unadorora, hali yetu ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa unyenyekevu sana asikubali suala la gesi lifie mikononi mwake akiwa Waziri Mkuu wa Tanzani, siyo sawa. Nimeuliza maswali hapa mara moja, mara mbili Serikai imeendelea kusisitiza, mchakato unaendelea lakini huo mchakato ambao hauwi *reflected* kwenye hotuba nzima ya Waziri Mkuu, mimi nadhani tuambieni ukweli, kama limeshindikana hili hebu tujue ukweli, tusiwasaliti wananchi wa Lindi na Mtwara siyo sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ukiacha gesi na mafuta, Lindi na Mtwara ni korosho. Mwaka jana kuna jitihada zimefanyika mambo yameenda vizuri, lakini Serikali ikafanya uamuzi, ikachukua kazi iliyokuwa inafanywa na Mfuko wa Pembejeo na Waziri anajua, wakasema ipelekwe kwenye Bodi ya Korosho na pembejeo hasa *sulphur* itagawanywa bure. Kulikuwa na mapungufu yalitokea lakini tukafumba macho kwa sababu ndiyo mara ya kwanza tukasema fanyeni uchunguzi, mlikokosea mrekebishe. Hali inavyoenda sasa hivi mwaka huu hali itakuwa mbaya kuliko tunavyodhani, kwa sababu mpaka mwezi huu wa nne wakulima hawajui chochote. Mheshimiwa Waziri, Jimbo langu mwezi huu watu wanaanza kupuliza dawa leo hawajaambiwa chochote.

Mheshimiwa Spika, wakati mnachukua mfuko ulikuwa na zaidi ya shilingi bilioni 49, walikuwa na uwezo wangeendelea nao, mkatuaminisha na tukawaamini, lakini hali inavyoendelea mbaya sana, kwa hiyo, tumaini peke yake lililokuwa limebaki Kusini ilikuwa korosho. Mnajua mbaazi imekwenda kutoka shilingi 200 mpaka shilingi 100, kuna wakulima wameacha mbaazi shambani wamesema bora zifie huko, sasa na korosho mnatupeleka huko, siyo sawa jamani! Ukiacha Lindi na Mtwara twende wapi, tuishi vipi sasa? Hili ni kutusaliti. Tulipotoa kura tuliwekeza tukaamini mtatusaidia, mkiendelea kufanya hivi mnatusaliti Mheshimiwa Waziri Mkuu na siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama imeshindikana rudisheni kwenye mfuko wa pembejeo tulikuwa tunakwenda vizuri. Kuna dhana ya kudhani kila mtu mwizi, siyo sawa, Mfuko wa Pembejeo ulienda vizuri sana. Mmebeba tumewaachieni bado mnakwenda vibaya kuliko hata mlivyochukua, hapa ni kutunyonga na siyo sawa sawa mtakuwa mnatusaliti sana watu wa Lindi na Mtwara *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anajua kuna watu bado wanadia mpaka leo malipo ya korosho. Kuna wakati fulani tulizungumza hapa, Ushirika ndiyo mkono wenu wa kusaidia kushirikiana na wakulima kuhakikisha wanapata soko, bei na mfumo mzima wa mazao yao. Hali ilivyo kule tumeweka watu, bahati mbaya elimu yao ndogo, sasa kuna mahali walikuja watu wamepata hasara ya zaidi shilingi milioni 400 na hawajui imepatikanaje, kwa nini? Wako watu wamechaguliwa uwezo hawana, sasa kwa nini tusibadilishe mfumo kwenye wale wa kuchanguliwa haya tusijali elimu yao, lakini tupate watu wa kusimamia, haya ni mabilioni ya hela yanasimamiwa na darasa la saba anashindwa kupiga hesabu, anakuja analia anatakiwa akamatwe, apelekwe Mahakamani, ukimuuliza umepotezaje hajui! Sasa kama tunashindwa hata hili la kuimarisha ushirika kwa sababau mapesa yapo, kwa nini tusiajiri watu wenye uwezo, waliosoma wakasimamia hela zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda mpaka leo *loss* ni kubwa matokeo yake ni nini? Wakulima wanaambiwa wakubaliane wachangie *loss* inayopatikana, lakini hii *loss* inasababishwa na nani? Inasababishwa na wakubwa kwenye mabenki na wakubwa kwenye Ushirika ngazi ya juu, siyo hawa wa chini, hawa wa chini hawajui chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu kwa Serikali, la kwanza, tupitie upya mfumo wa ushirika. Pamoja na kuchaguana demokrasia safi, lakini ni vizuri tupate watu wa kuajiriwa wenye elimu ya utunzaji wa mahesabu wakashirikiane kusaidia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape tunakushukuru sana muda haupo upande wako.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa William Ngeleja atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Saddiq. Mheshimiwa Ngeleja.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, na mimi ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla kukukaribisha hapa Bungeni kwa mara nyingine. Ni faraja kukuona unaongoza tena jahazi lako hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuipongeza Serikali kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini kwa nafasi hii tunawapongeza sana wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, watendaji kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Tunafahamu kabisa kwamba mjadala huu unajenga mustakabali wa Taifa kwahivyo kwa yale mazuri yanayofanywa ni vema kuyasemea.

Moja, nikukupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa unayoifanya wewe kama msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali. Umefanya ziara nyingi sana mikoani na maelekezo yako yamesaidia sana kuongeza kasi ya utekelezaji na kurekebisha kasoro ambazo zilikuwepo za kiutendaji. Sengerema tutakukumbuka sana kwa ziara uliyofanya ndani ya mwezi mmoja na nusu uliopita.

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa kwamba Serikali inawasikiliza Wabunge na jamii kwa ujumla ni taarifa iliyotolewa sasa hivi na Mheshimiwa Mkuchika, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais. Hongereni sana Serikali kwa kusikiliza mawazo ya wawakilishi wa wananchi, wafanyakazi,

watumishi wetu wa darasa la saba wamekuwa na kilio cha muda mrefu na hivi ndivyo ambavyo inatakiwa Taifa tuendelee kulijenga kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, heshima ya Serikali ni pamoja na namna ambavyo inatayarisha nyaraka zake na kuzitunza. Hapa nazungumzia Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo ya Bunge lako Tukufu mara kadhaa tumetembelea Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na kwa miaka mingi amekuwa na changamoto nyingi sana, lakini niseme kuanzia mwaka jana Serikali imechukua hatua kubwa na kwa hili kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tunampongeza sana Mheshimiwa Jenista Mhagama kama Waziri mhusika kwa hatua za kurekebisha *management* pale.

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba kwa Serikali ni kukamilisha *management* pale. Mkurugenzi Mtendaji au *CEO* wa pale sasa hivi anakaimu, lakini amefanya kazi kubwa sana kwa kipindi ambacho amekuwa akikaimu. Naomba Serikali ikamilishe uteuzi, mpate Mtendaji Mkuu ili shughuli ziendelee vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia pia kwa wale ambao tumeguswa na hii programu ya *MIVARF. MIVARF* ni programu ambayo inaratibiwa na Serikali kuhusu miundombinu ya masoko lakini uongezaji thamani wa mazao na huduma za kifedha vijijini. Kwa wale tunaoguswa ni programu maalum sana na nzuri sana. Tunashukuru sana kwa wale ambao wamekuwa wakiunga mkono na kujua kwamba kuna taasisi mbalimbali za kimataifa, hii kwa kweli ime-*compliment* juhudi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sengerema tuna mradi mkubwa wa umwagiliaji wa maji, uliibuliwa miaka mitano iliyopita, gharama yake ni bilioni 2.5, Serikali ilishaleta milioni 700 lakini *1.8 billions* hatujapata. Tumeanza kuzungumza na wafadhili wa *MIVARF* wako tayari kutusaidia na ndiyo maana tunasema hii awamu ya pili ambayo Serikali inaendelea na mazungumzo tunaiomba sana ikamilishwe haraka kwa

sababu inakuja kuisaidia Serikali mahali ambapo ina upungufu wa fedha programu hii itasaidia kukamilisha miradi iliyokwama ikiwemo mradi wa Sengerema wa Katunguru *Irrigation Scheme.*

Mheshimiwa Spika, ukisoma ukurasa wa 45 kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inazungumzia habari ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini *(TARURA)*. Tumeanzisha Wakala na tumeukabidhi majukumu ya kufanyia matengenezo barabara za mtandao wa vijijini, madaraja yake na makalvati mbalimbali. Kuna barabara tumeipa Wakala huu jukumu la kutengeneza kilometa 108,946.2

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa taarifa iliyotolewa na Mheshimwa Waziri Mkuu ya utekelezaji kwa mwaka huu wa fedha ni kilometa 4,183 tu ndizo ambazo zimetengenezwa ni kwa sababu ndicho kiwango cha fedha tulichokitenga.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba kulishauri Bunge lako tukufu ni kwamba kwa hatua tuliyonayo hii, tukienda kwa *speed* hiyo kwa huo mtandao wa kilometa zaidi ya 100,000 itatuchukua miaka 26 kuweza kurekebisha barabara zetu za vijijini, leo tunafahamu kwamba zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania na hasa uchumi wao unategemea vijijini. Ushauri kwa Bunge lako tukufu na kwa Serikali ni kwamba, ule mgawanyo wa fedha za Serikali kutoka kwenye Mfuko wa Barabara ambao sasa hivi unasimamia kwa asilimia 70 barabara kuu na za mikoa na asilimia 30 kwa barabara za vijijini, tuurekebishe ili tuuwezeshe Wakala huu ufanyekazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba twende 50 kwa 50 na ninasema hilo nikitambua kwamba tuna umuhimu wa kutengeneza barabara za vijijini na mijini, lakini ukilinganisha uwiano wa uwezekano wa kupata mikopo na Serikali imethibitisha hivi karibuni kwamba tunakopesheka. Kwa wale wanaoweza kutukopesha kwa masharti nafuu wataweza kutukopesha kirahisi kwa barabara za mijini ama zinazounganisha mikoa ama barabara kuu, lakini siyo rahisi

sana kupata mkopo kwa barabara za vijijini. Tufanye kama tulivyofanya kwenye Umeme Vijijini *(REA)* tumetumia fedha ya ndani na leo tunajisifu kwa sababu ya hatua tuliyofikia ya kutenga bajeti mahsusi kutoka kwenye vyanzo vyetu. Ninaomba tuurekebishe mgawanyo uwe *fifty/fifty* vinginevyo uwe 45 kwa 55 ili tupate fedha nyingi za kurekebisha barabara zetu za vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine sambamba na hilo ambalo wenzangu wamelizungumza, Wakala huu bado unaeleaelea uwajibike sasa, taratibu na kanuni zirekebishwe, uwajibike kwenye Halmashauri husika na hasa za kule kwenye Wilaya zetu kwa sababu hao ndiyo watakaoshirikiana nao kubaini barabara zipi mbovu na hata mipango wanayoipanga ya kwenda kutekeleza hizo barabara, tukifanya hivyo tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 56 unazungumzia afya, nizungumzie eneo moja tu la huduma za tiba za kibingwa. Taarifa za Serikali kama kumbukumbu yangu iko sahihi na Waheshimiwa Wabunge wengine ni kwamba ugonjwa wa saratani katika Hospitali ya *Ocean Road* tumekuwa tukitaarifiwa zaidi ya asilimia 60 ya wagonjwa wanaofikishwa pale kwa matibabu wanatoka Kanda ya Ziwa. Ombi langu ni moja tu, Kanda ya Ziwa tuna Hospitali ya Rufaa Bugando tunaomba ipewe kipaumbele, washirikiane na *Bugando Hospital.*

Mheshimiwa Spika, najua Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu yupo hapa wamekuwa wakishirikiana vizuri sana, tunaomba waongeze kuna kifaa ambacho kinahitajika ili watekeleze vizuri utaratibu wa kuwasaidia Watanzania wenye magonjwa ya saratani na kwa sababu ni eneo ambalo linahusu wagonjwa wengi, nadhani mkiwasaidia tutafika mbali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nape amezungumzia uwekezaji katika sekta ya gesi, nalizungumza suala hili ikiwa ni eneo ambalo ninalifahamu kidogo. Nimekuwa nikiskia Serikali inasema mkakati uliopo ni kwamba inapofika mwaka

2020 tuwe tumeshafikisha megawati 5000 na mwaka 2025 tufikishe megawati 10,000. Kiufupi tu ni kwamba kwa vyanzo vilivyopo ikiwemo cha maji cha *Stieglers Gorge* havizidi megawati 5000 sasa nataka kujiuliza tunatokaje kuanzia hapo mwaka 2021 kwenda kwenye mwaka 2025 kama hatufanyi mipango ya kuendeleza gesi sasa hivi ikiwemo na huu mradi mkubwa wa kuchakata gesi wa *LNG* ambao amezungumza Mheshimiwa Nape. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania kama walivyo binadamu wengine wanahitaji kuishi kwa matumaini kwa kupewa mipango ya Serikali. Tunapowataarifu Watanzania kwamba mipango imefikia lengo fulani, tunawajenga kisaikolojia lakini tunawandaa pia kupokea fursa zinazokuja na uwekezaji wa namna hiyo. Kwa hivyo, ninachosisitiza ni kwamba, kwa sababu bomba la gesi tulilo nalo sasa hivi linatumika kwa asilimia sita tu kwa taarifa ambazo zimekuwa zikisikika, asilimia 94 haijatumika, tuendeleze miradi hii, tuhakikishe kwamba gesi pia tusiiache pembeni, kwa sababu mipango yake ya uwekezaji katika gesi inachukua muda mrefu sana siyo suala la miaka miwili/mitatu; kwa hiyo, tusipoanza mapema maana yake ni kwamba tunajiweka katika mazingira magumu mno kufikia lengo ambalo tumelikusudia *megawatts* 10,000 za umeme mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali izingatie suala hili, tulifanyie kazi, wafunguke pia kwenye upande wa sekta ya gesi. Lakini tunafikaje huko?

Mheshimiwa Spika, sisi wenyewe hatuwezi kuifadhili miradi hii, njia pekee iliyopo na juzi Mheshimiwa Rais amefungua ukurasa mpya wa mahusiano na sekta binafsi, tuipe kipaumbele sekta binafsi itusaidie, isaidiane na Serikali katika kuendeleza miradi hii, vinginevyo kama tulivyo kwa fedha zetu, tunajenga *SGR,* tunanunua ndege zetu wenyewe, tunajenga *Stieglers Gorge* kwa fedha zetu, hatujakamilisha miundombinu ya elimu, bado tuna changamoto katika afya, tunataka fedha nyingi kwa ajili ya *TARURA*, tunahitaji kuboresha huduma za maji, sisi wenyewe kama tulivyo, kama

Serikali hatuwezi kufanya hivi na ni nchi chache sana duniani zilizofanikiwa kwa kutegemea vyanzo vyake vyenyewe bila kuishirikisha sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba tuipe sekta binafsi kadri itakavyowezekana ushirikiano mkubwa ili waweze kutusaidia kutufikisha kwenye malengo ambayo tunakusudia.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kwenye maji. Mwaka jana tuliongeza shilingi 50 kutoka kwenye lita ya mafuta, naomba tena mwaka huu tuongeze shilingi 50 nyingine ili tuongeze kasi ya kufikisha huduma za maji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa na fursa hii, nawatakia kila la kheri. Naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa William Ngeleja. Nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Suleiman Saddiq, utafuatiwa na Mheshimiwa Bungara kama hayupo Mheshimiwa Devotha Minja atafuatia. Mheshimiwa Suleiman Saddiq.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo. Niungane na Wabunge wenzangu kukukaribisha tena Bungeni karibu sana Bungeni tumefarijika sana kukuona ukiwa na afya njema na unang'ara kweli kwenye Kiti chako, Mwenyezi Mungu akufanyie wepesi zaidi, *Inshallah. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo na mimi niweze kuzungumza mawili matatu ya maendeleo kwa nchi yetu na Wilaya yetu ya Mvomero.

Naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayofanya katika nchi yetu, kwa kazi ambayo italeta manufaa makubwa leo na kesho na kesho kutwa tunampongeza sana na tunasema wananchi wa Mvomero tuko naye bega kwa bega.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi ambayo anafanya hususani kusimamia masuala mbalimbali ya pamba, kilimo na maendeleo kwa ujumla na naomba niwapongeze na wenzake wote na timu yao yote.

Mheshimiwa Spika, bila ya kupoteza muda naomba nizungumzie suala la Wilaya ya Mvomero, uvamizi wa ardhi katika Wilaya ya Mvomero uliofanywa na Manispaa ya Morogoro, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Maliasili na Waziri wa Ardhi kwa pamoja wanisikilize kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Morogoro imevamia eneo la Wilaya ya Mvomero na wameanzisha mitaa miwili ndani ya Wilaya ya Mvomero, mtaa wa kwanza unaitwa *CCT Forest* na mtaa wa pili unaitwa Maili Kumi na Nane.

Mheshimiwa Spika, Mitaa hii ipo ndani ya Wilaya ya Mvomero wapiga kura wa Mjini wanapiga kura katika Wilaya ya Mvomero na maeneo hayo yalianzishwa kwa mujibu wa utaratibu na sheria za nchi yetu. *GN. No.* 204 ya mwaka 1953 ilianzisha msitu wa kuni ambao uko ndani ya Wilaya ya Mvomero. *GN No*. 366 ya mwaka 2002 ilianzisha Wilaya ya Mvomero na *GN* Na. 242 ya mwaka 1991 ilianzisha Manispaa ya Morogoro hizi *GN* zote zipo kisheria na zipo pale kila mmoja inaeleza mipaka na maeneo jinsi yalivyo. Nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimuombe Waziri wa TAMISEMI mara watakapofanya majumuisho naomba tamko la Serikali eneo hili sasa litambulike kama eneo halali la Wilaya ya Mvomero na wavamizi wote waondoke wananchi waliopo maeneo yale tutawatambua kama wananchi wa Mvomero hatuna ugomvi nao. Kwa hiyo, naomba suala hili lifanyiwe kazi na Serikali na tupate majibu ya haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni eneo la *NARCO - National Ranch* zile kubwa ambazo ziligawiwa kuna eneo ambalo walipewa wenzetu ambao hadi leo maeneo yale hawajaendeleza kuna kampuni mbili moja inaitwa Katenda *group* na moja inaitwa Elisa Mollel walipewa heka 5000. Eneo

lile walipewa mwaka 2002 hadi leo maeneo yale hawajayaendeleza, leo kuna kaya zaidi ya 430 zinaishi eneo lile, naomba Waziri muhusika aunde timu yake waje wakague eneo lile watukabidhi Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, tuweze kuliendeleza, tuweze kuwaleta wawekezaji eneo limekaa bure limekuwa pori yamebaki majoka, yamebaki mapori ambayo hayana faida yoyote kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda unavyoenda haraka naomba haya maeneo yote ya *NARCO* yaliyopo ndani ya Wilaya ya Mvomero Mheshimiwa Waziri alikuja akazungumza naomba sasa aje na timu yake tukae na timu ya Mvomero tuweze kuona ni namna gani maeneo yale yataendelezwa na yataleta faida.

Mheshimiwa Spika, Mvomero tumepata wawekezaji wengi maeneo ya barabarani yote ni mapori hayaendelezwi, namuomba Waziri wa Maliasili akumbuke ombi la Wilaya ya Mvomero tuliloandika barua na kupeleka ofisini kwake tunahitaji heka 10,000 za barabarani tuwape wawekezaji waweze kujenga viwanda, waweze kuleta mashamba bora ya kisasa tuweze, kusonga mbele. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Maliasili aweze kukumbuka barua yetu ya Mvomero.

Mheshimiwa Spika, pia tuna mgogoro wa hifadhi na Mikumi *National Park* na kijiji cha Doma na Kata ya Doma, namuomba Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Maliasili, Waziri wa Ardhi watuletee timu tuweze kukaa nao chini *Mikumi National Park* wameingia kwenye eneo la Mvomero, wameingia kwenye mashamba ya wakulima na sasa hivi wameweka na *beacon,* suala hili naomba tamko litolewe na ikiwezekana timu ya Mawaziri tukutane tuweze kuona tunafanyaje.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe tamko kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, mapato ya ndani asilimia 40 na ile 20 asilimia 60 mapato ya ndani yale yaende kwenye miradi ya wananchi, fedha za mapato ya ndani zinatumika kulipa madeni ya Halmashauri, fedha za mapato ya ndani

zinatumika katika mipango ya Wilaya ambayo sio maendeleo na miradi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamejenga zahanati wanahitaji bati, wananchi wanahitaji pampu ya kisima fedha hizi zinakwenda kwenye sherehe za Nane Nane, fedha hizi zinakwenda kwenye mambo mengine, naomba tamko la Waziri Mkuu fedha za mapato ya ndani kwa mujibu wa kanuni na sheria zirudi kwenye miradi ya wananchi na bahati nzuri Waziri Mkuu nimeonana nae na baadaye tutaonana nitamkabidhi na baadhi ya *documents* ili tamko litolewe wananchi wa Mvomero wapate maendeleo kutokana na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo moja kubwa katika Wilaya ya Mvomero, Wilaya ya Mvomero kijiografia unatoka mpakani na Handeni unarudi mpaka Morogoro Mjini unaanza safari unaacha Manispaa unakwenda Mzumbe, unakwenda mpaka Mgeta, unakwenda mpaka Kikeo, unasafiri masaa zaidi ya 10 kutoka kwenye Kata moja kwenda kwenye Kata nyingine tulipeleka ombi tunaomba Jimbo la Mvomero ligawanywe ili tuwe na Majimbo mawili ya uchaguzi. Suala hili tumelifikisha kwenye vikao mbalimbali bado tutaleta na *documents* zetu tunaomba Serikali inapofanya marekebisho ya Majimbo ya Uchaguzi watuangalie Mvomero namna gani jiografia yetu ilivyokuwa ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho naomba kuipongeza Serikali, ninampongeze Waziri wa Utumishi kwa kauli yake ya leo Bungeni kuhusu ajira za watumishi hii ndiyo Serikali sikivu ya CCM, Waziri wa Utumishi nakupongeza, naipongeza Serikali kwa maamuzi haya mazuri ambayo yana tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, bila ya kupoteza muda nasema naunga mkono hoja. Ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Suleiman Saddiq tunakushukuru. Mheshimiwa Bungara hayupo, Mheshimiwa

Devotha Minja, Mheshimiwa Bungara upo kuna watu wameniambia haupo.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, nilitoka kidogo.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimefurahi sana kwa kuwa umerudi salama kutoka katika matibabu, tunakuombea Mwenyezi Mungu afya yako izidi kuimarika na *Inshallah* itaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nitazungumzia sana habari za siasa na hususan hali ya kisisasa katika nchi yetu. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye utangulizi pale, misingi ya Katiba na kwa kuwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeamua rasmi kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, undugu na amani. Kwa hiyo, Katiba yetu inazungumzia uhuru na haki ndiyo jambo la kwanza ili nchi yetu tuwe na mapenzi, kupendana, undugu na amani, lakini kama nchi yetu haitokuwa na uhuru na haki undugu na amani hautokuwepo katika nchi yetu, ndiyo msingi kwa Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nia yetu ni nchi yetu na jamii yetu ijengwe kwa msingi huo, kwa hiyo kwa msingi hiyo yaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia ambayo Serikali yake huamini Bunge lenye wajumbe waliochaguliwa na Mahakama iliyowakilisha kwa nchi pia yenye Mahakama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ukurasa wa saba inasema, nchi yetu inaendelea kuwa na amani na utulivu ili hali mimi kwa utafiti wangu naona hizi habari siyo za kweli kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina matatizo sana, kama hatukubali kama nchi ina matatizo naomba tutegemee

kwamba nchi yetu huko mbele tunakokwenda hali itakuwa mbaya sana. Mimi mwenyewe nilimuandikia barua Waziri wa Mambo ya Ndani, kuna gari Noah ilifika Kilwa tarehe 29 Novemba, ikampigia simu kijana mmoja anaitwa Abdallah Said Ngaranga wakamwambia njoo uchukue mzigo wako hapa Kilwa Masoko, Mheshimiwa Abdallah Ngaranga alifuatana na Mheshimiwa mmoja anaitwa Hamisi Mtori, kufika pale Kilwa Masoko ile gari ya aina ya Noah nyeusi wakamuita yule kijana njoo ndani uchukue mzigo, alipoingia ndani yule kijana, kijana wa pili akawa yuko nje alivyoingia ndani wakamuita na yule wa pili, yule wa pili kaona hata Noah hii nyeusi siielewi akakimbia na askari mmoja akamkimbiza yule kijana akaingia katika makapa akapiga risasi yule askari, lakini jamaa hakusimama, akaondoka akafika Kivinje.

Mheshimiwa Spika, nikaitwa mimi kwamba mtu wetu mmoja katekwa, kwa bahati nzuri nikapiga simu Polisi Masoko nikaambiwa kwamba kweli yule kijana amekamatwa yuko polisi hapa. Usiku huo wakakamatwa vijana tisa, nikaenda polisi siku ya pili nikaambiwa kweli vijana walikamatwa walikuwepo hapa, lakini hatuwezi kuwaandikia kwa sababu walikuwa wamepitia tu. Nikaandika barua kwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, katika vijana hao 11 wakarudishwa tisa na mpaka sasa hivi wako Kilwa, lakini wawili hawajarudishwa mpaka leo. Mmoja anaitwa Ndugu Ally Mohamed Shali na mwingine anaitwa Ndugu Yussuf Kipuka mpaka leo hawajarudishwa, lakini tuna uhakika walichukuliwa, walikuja kituo cha Polisi Kilwa Masoko mpaka leo hawajarudishwa na wazazi wao hawajulikani wapi walipo.

Mheshimiwa Spika, hii ni ukweli kabisa ninataka leo Waziri atupatie vijana wetu wawili hawa, ushahidi upo tarehe 21 Julai, askari hao hao walikwenda Kijiji kimoja cha Chumo wakaenda msikitini usiku saa saba, wakapiga risasi msikitini mle, wakawachukua watu 10 msikitini. Tumekwenda asubuhi damu zimetapakaa ndani ya msikiti, katika watu hao

wakarudi wote 10, katika 10 waliorudi mmoja kafa, mmoja hana jicho, mmoja wakamwambia wewe unafuga ndefu wamemchoma ndevu zake, wamemnyoa ndevu kwa kumchoma moto, watu hawa wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mnatuambia kwamba nchi hii ina amani na utulivu mimi sielewi? Watu hawa wapo na huyo mtu mmoja amekufa tumemzika na majina yao nitakutajia. Samahani kidogo nimeandika aliyefariki anaitwa Ismail Bwela, aliyetoka jicho anaitwa Mbaraka Masaburi, aliyechomwa ndevu anaitwa Muharam Yalife, wapo! Wamepigwa risasi msikitini, mmoja amekufa na Serikali haijasema chochote mpaka leo na wamerudishwa wako Kilwa pale.

Mheshimiwa Spika, unaposema nchi hii ina amani na utulivu sielewi! Ninawaunga mkono waraka uliotolewa na Maaskofu. Nawaunga mkono Maaskofu mlichokisema ni sawasawa na maneno ya Maaskofu ni maneno ya Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii nchi imeharibika leo waislamu lazima wasiseme, tumetengenezewa jambo tunaitwa magaidi, kwa hiyo Mashekhe wote wa kiislam wakitaka kutetea haki zao kuhusu waislam wenzao tunaambiwa aah!Ninyi magaidi mnawatetea magaidi na ndiyo maana waislam hawawezi kusema sasa hivi, watasema vipi wakati wao wanaambiwa ni magaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza Maaskofu sasa hivi matumaini kwa Watanzania ni sehemu mbili tu Mahakama na Maaskofu, lakini waislamu hatuwezi kusema! Akipigwa muislam akisema unaambiwa unatetea magaidi eeh! Waislam wote tumerudi nyuma, tunaomba sana.....

Mheshimiwa Spika, nitunzie muda wangu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bungara utulie, Mheshimiwa Sanga nimekuona taarifa.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji wa sasa hivi, Mheshimiwa Mbunge kwani wale askari zaidi ya kumi waliouwawa na wananchi wengine kule Kibiti, wale siyo binadamu mbona wale hawazungumzii?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa nimeipokea. Wewe tulia nitamjibu mwenyewe huyu.

Katika watu wanaolaani kwamba wale watu wamepigwa kwa makosa wale askari pamoja na mimi, lakini siwezi kuacha kusema watu wengine wakionewa haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, polisi wakionewa nitasema, wananchi wakionewa watasema! Nia yetu hapa tunataka amani na utulivu ndiyo hoja, sijasema kwamba waliopigwa risasi polisi sijasema hivyo, nimesema polisi wameiniga msikitini wamewapiga watu risasi sasa mkatae kwamba hamkupiga watu risasi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Rufiji hiyo ilikuwa watu wanapigwa risasi wanauawa, mkatengeneza mazingira kwamba wale wanaopigwa ni wa CCM na mkahalalisha Viongozi wetu wa *CUF* wamekamatwa na mpaka sasa hivi hawajulikani walipo, nitawatajia watu sita waliokamatwa katika *operation* mpaka sasa hatujui walipo, nataka tujue wako wapi. Mtu wa kwanza....

**SPIKA:** Mheshimiwa Bungara, muda haupo upande wako, tunakushukuru sana.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, basi nitakuletea majina ya hao watu sita waliokamatwa tunataka tujue wako wapi, ni wa Rufiji nitakuletea majina. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Minja atafuatiwa na Mheshimiwa Kiza Mayeye. Mheshimiwa Devotha Minja endelea.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja.

Mheshimiwa Spika, nimepitia vizuri kitabu cha hotuba hii ya Waziri Mkuu. Nilitegemea ningeona mambo mengi humu; nilitegemea Waziri Mkuu angetueleza hali halisi ya siasa ya nchi hii kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, kwa yale ambayo yanaendelea katika nchi hii, ukandamizaji wa demokrasia unaoendelea katika Taifa hili, kuendelea kunyimwa kwa vyama vya siasa kufanya haki yake ya msingi ya kufanya mikutano; tunaelewa, kazi ya chama chochote cha siasa katika Taifa hili ni kuendelea kutafuta wanachama wapya na kupima afya yake, lakini hivi sasa hali ya siasa iliyoko Tanzania haifananishwi na nchi yoyote ambayo iko katika nchi za Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, kwa nini nasema hali ya siasa si nzuri? Ni kwa sababu ya uonezi wa waziwazi na ukandamizaji wa waziwazi. Mfano mzuri tunaouzungumzia hapa ni baadhi ya viongozi wetu wa chama ambao waliwekwa mahabusu wakala Pasaka mahabusu, akiwemo Mwenyekiti wetu wa Kambi ya Upinzani ilhali Mahakama ya Kisutu ilishatoa dhamana, kwa kisingizio kwamba gari ya kupeleka mahabusu ni mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nje ya Mahakama ya Kisutu ukiangalia wakati tunapewa taarifa hizo zilikuwepo *defender* zaidi ya 30, magari ya washawasha yalikuwemo katika eneo la Kisutu. Unajiuliza, ni magari hayo hayo ya Polisi yameharibika, yameshindwa kuwaleta watuhumiwa Mahakamani, lakini magari hayo hayo yanazunguka Kisutu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ifike mahali tuseme ukweli kwamba Taifa hili tunataka kulipeleka wapi. Mwanzoni niliposikia kwamba upo mkakati kwamba tukiingia madarakani tutahakikisha tumeumaliza upinzani. Nilijua

kuumaliza upinzani maana yake ni kufanyia kazi hoja za msingi za upinzani, ni kuhakikisha malalamiko ya upinzani wanayoyatoa dhidi ya wananchi kwa Serikali yanafanyiwa kazi, ndiyo namna ya kuiua upinzani, lakini namna ya kuua upinzani sio hivyo, ndiyo hivi tunavyoviona sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna matamko yanayoendelea. Mimi juzi nimemsikiliza Rais akiwa Arusha. Anawaambia Askari wa Jeshi la Polisi fanyeni mtakavyo, nipo nyuma yenu, nawa-*support.* Tunajua kazi ya Jeshi la Polisi na amewapongeza kwa jinsi walivyoshughulikia watu kwenye maandamano. Ukiangalia maadamano yale, watu walivyoumizwa wakiwa kama majambazi, watu wameishia kupigwa risasi, wengine wamekufa; sasa kauli za namna hii zinaipeleka wapi Taifa hili? Kwa maneno mepesi ni kwamba ukiwaambia unawa-*support* kwa maana hiyo waendelee na kazi hiyo ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza wachangiaji wa wiki iliyopita. Kuna mchangiaji mmoja alisema wapinzani wanalalamika, bilioni sita za uchaguzi *it's peanuts!* Bilioni sita kwa nchi maskini kama hii ambayo inaishi chini ya dola moja; bilioni sita tunaona ni sawa kwenye uchaguzi?

Mheshimiwa Spika, nilishangaa kwa sababu unaposema hizi bilioni sita za uchaguzi unazungumzia zile za Tume. Hivi umehesabu gharama nyingine ambazo zinaendana na uchaguzi? Umehesabu nauli za wananchi ambao wanatoka maeneo hayo kwa siku 30 wanapanda daladala wanaenda kwenye uchaguzi? Umehesabu Wabunge ambao wanatoka maeneo yao wanaweka mafuta wanakwenda kwenye uchaguzi? Umehesabu gharama...

**MHE. ABDALLAH M. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**T A A R I F A**

**SPIKA:** Ndiyo taarifa tafadhali, Mheshimiwa nakukubalia.

**MHE. ABDALLAH M. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninampa taarifa mzungumzaji ya kwamba hoja ya gharama ilipokuwa ikizungumzwa ilikuwa ikilinganisha gharama za uchaguzi mdogo uliozungumzwa na wazungumzaji hapa na ikilinganishwa na gharama ya kura ya maoni ambayo tunataka Katiba mpya na tukasema je, kama gharama ya uchaguzi ni jambo la kikatiba tunaiona ni nyingi, inakuwaje tunapodai twende kwenye Katiba mpya ilhali tukijua Katiba mpya tutakuwa na kura za maoni? Huo ndiyo msingi wa hoja! Msingi wa hoja haukuwa kwamba bilioni sita si kitu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Devotha, hiyo ni Taarifa kutoka kwa Mbunge mpya kabisa hapa Bungeni Mheshimiwa Mtulia. Endelea kuchangia *(Makofi)*

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, hivi bilioni sita, Mwananyama watu wanalala chini, bilioni sita ingefanya kazi yake, hiyo bilioni sita anayoiona ni ndogo. Bilioni sita hiyo anayoiona ni ndogo ingefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kule kwa Manjunju ambako maji yanafurika kila wakati zingesaidia kuleta *plan* watu wakae vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziko gharama nyingine zinazotokana na chaguzi hizi. Unapozungumzia hiyo bilioni sita peke yake hujaweka gharama nyingine, misafara mikubwa kuliko hata ya Waziri Mkuu ya Mkuu wa Mkoa, hujaweka misafara ya magari ya washawasha, hujaweka misafara yanayobeba mbwa kwa ajili ya chaguzi. Vile vile hujaweka gharama za watu waliokufa/waliopoteza maisha ambao wamezikwa kwa gharama za Serikali akiwemo yule binti Akwilina.

Mheshimiwa Spika, hujaweka gharama za Katibu wetu wa CHADEMA Hananasif ambaye naye alifariki, zile zote ni gharama. Kwa hiyo, tusiione bilioni sita tu tukaiona, tukifanya tathmini tunaweza tukaona *in reality* unaweza ukaogopa kuingia kwenye uchaguzi. Nafikiri kungekuwa kuna namna tu mtu akatoka huko, akaingia huku, tukaendelea! *(Makofi)*

## TAARIFA

**SPIKA**: Mheshimiwa Devota upokee taarifa, Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika kwanza namtukuza Mungu kwa ajili ya afya yako, lakini naomba nimpe taarifa rafiki yangu, pacha wangu Devotha, kuhusiana na gharama unazozisema, nataka nikupe taarifa kwamba Jimbo la Singida Kaskazini wananchi wale wali-*suffer* lakini sasa hivi pamoja na gharama zilizotumika wamepata Mbunge na sasa hivi mahitaji yale waliyokuwa wanayahitaji Mbunge wao anawawakilisha vyema humu ndani na wanashirikiana naye.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo zile fedha ambazo wewe unasema kwamba ni gharama zimeokoa maisha ya wananchi wa Singida Jimbo la Kaskazini kwa kupata Mbunge anayeweza kwenda kujua matatizo ya wananchi walioko kule kuliko wangebaki na hizo hela unazozisema kama zisinhgetumika wananchi wale wange-*suffer.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema uchaguzi uliofanyika sasa hivi hizo hela ni *peanuts* kuliko matatizo ya wananchi na faida ambayo wanaipata sasa hivi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Devota, umeyachokoza mwenyewe. *(Kicheko)*

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa ajili ya muda niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona Waheshimiwa Wabunge wamechangia sana kuhusu ununuzi wa ndege. Hakuna mtu ambaye anasema ununuzi wa ndege ni mbaya, lakini tunachokilalamikia na kukisema siku zote ni gharama za ununuzi wa ndege. Taifa kama hili kununua ndege tatu *cash* kwa hali ambayo tunayo.

Mheshimiwa Spika, mataifa yaliyoendelea yote hivi sasa yanaanza ku-*withdraw* kuingia kwenye biashara za ndege kwa sababu biashara ya ndege *returns* zake si za karibu hivyo. Ni hasara ku-*run* ndege. Sasa sisi kwa Taifa maskini kama hili tunaenda kununua kwa *cash,* tungejifunza hata kwa wenzetu *Precision* na *Fastjet* ndege zao wamenunuaje. Ukiangalia zote hizo watu wamenunua kwa mikopo, watu wananunua hisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, ukiangalia hata huo unafuu wa ndege tunaoambiwa kwamba zimenunuliwa kwa kodi zetu, ukiangalia leo *ATCL* kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma unazungumzia karibu, lakini saba lakini ukipanda *Fastjet* kwenda Dar es Salaam – Mbeya na kurudi ni 230,000. Sasa unafuu uko wapi? Tunaweza tukasema kweli tunaunga mkono ununuzi wa ndege?

**MHE. JANETH Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**T A A R I F A**

**SPIKA:** Taarifa, ruksa Mheshimiwa, endelea na taarifa.

**MHE. JANETH Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami naomba nitoe taarifa kwa mzungumzaji wa sasa hivi. Hili suala la ndege limezungumziwa sana humu ndani na wenzetu hawa. Ndege zimenunuliwa si kwa ajili ya *passengers* peke yake. Sasa hivi sisi tunataka kukuza utalii na utalii unatuingia pesa nyingi sana za kigeni na utalii wetu sisi umekuwa ukitegemea ndege za wenzetu. Tunataka sasa hivi kuwa na utalii unaokuja moja kwa moja Tanzania kwa kutumia ndege zetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kama tunanunua kwa *cash* tunapunguza gharama ya riba. Kwa hiyo, hiyo ni sahihi kabisa na kama hela ipo inanunuliwa ndege kwa ajili ya kufanya utalii wetu uwe bora zaidi. Kwa hiyo hakuna kitu cha ajabu, mambo ya kusema wenzetu, *Precision,* si wenzetu na Serikali. *Precision* ni kampuni binafsi na inakufa.

**SPIKA:** Jamani, muda wa Devota si umeisha mezani huko? Devota, Taarifa hiyo. Bado dakika moja eh?

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, hivi ndege tulizonazo hizi zinatoka nje ya nchi? Hata hivyo, ningeweza nikaelewa kama tumenunua ndege ambayo inatoka hapa inakwenda Marekani, inaleta watalii, wanakuja moja kwa moja hapa. Hivi niulize hata hiyo ndege kutoka Canada mpaka kufika Tanzania ilichukua siku ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee…

**SPIKA:** Wanakwambia inakuja *Dreamliner* itafanya hiyo Marekani – Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kuhusu suala la Serikali kujinasibu kwamba inakwenda kupambana na ufisadi.

Mheshimiwa Spika, pale Manispaa ya Morogoro iko barabara ambayo imejengwa kutoka Kichangani kwenda Tubuyu ina kilometa nne. Kilometa moja tu imejengwa kwa shilingi bilioni 3.4. Barabara hiyo haina mito, haina kona, haina makorongo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili Mheshimiwa Devota. Ahsante sana. Mheshimiwa Kiza Mayeye atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii . Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukurudisha salama na afya yako inaendelea kuimarika, hakika neno la Bwana lihimidiwe siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri kwa sababu inaeleweka. Nimeisoma na nimeielewa vizuri. Sasa naomba nianze kuchangia katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zote ambazo zinafanywa na Serikali yetu, lakini bado katika suala zima la afya, changamoto ni kubwa, wauguzi wamekuwa ni changamoto kubwa. Katika maeneo ambayo natokea, Mkoa wa Kigoma hospitali nyingi hazina wauguzi. Hata hivyo, pamoja na kwamba hazina wauguzi hata miundombinu ya hospitali hizo bado ni changamoto. Waganga wanaishi katika mazingira magumu, nyumba za Waganga hakuna. Niiombe sana Serikali ijitahidi kuzingatia hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndani ya Mkoa wangu wa Kigoma tuna Hospitali ya Mkoa ambayo inaitwa Maweni. Hii ni hospitali kubwa ambayo inahudumia wananchi wengi na ukizingatia Kigoma tuko mpakani ambako tunapokea wakimbizi kutoka Burundi na Congo bado wanakwenda wanatibiwa mahali pale. Niiombe sana Serikali ituletee ma-*specialist* ndani ya Mkoa wetu wa Kigoma katika hospitali hii ya mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa uchunguzi ambao nimeufanya, mpaka sasa tuna-*specialists* watatu. *Specialist* wa akinamama, wa upasuaji na watoto. Niiombe sana Serikali mtuongezee ma-*specialist* katika hospitali yetu ya mkoa. Kwa sababu leo unapoweka *specialist* mmoja katika upasuaji naye ni mwanadamu ana dharura, kesho asipokuwepo kazini maana yake unawaambia watu wa Kigoma hamtakiwi kufanyiwa upasuaji. Niiombe sana Serikali ituletee wauguzi, ituletee waganga katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, nimetembelea katika vijiji mbalimbali ndani ya Wilaya yangu ya Kigoma Vijijini. Nimekwenda Vijiji vya Kiziba, Mwamgongo na Bugamba, kuna changamoto kubwa. Usafiri wanaoutumia ni kupita na boti ndani ya maji. Tuangalie katika maisha ya kawaida

mama huyu mjamzito anahitaji *operation* ya haraka, lakini hakuna boti ya haraka ya kuweza kumtoa Bugamba au Mwamgongo kumpekea hospitali ya Maweni. Niiombe sana Serikali iwaangalie watu wa pale angalau tupate boti ambayo litawasaidia wananchi wa maeneo haya kuwasafirisha kwenda katika hospitali ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, niiombe tena Serikali; natokea katika Wilaya ya Kigoma Vijijini, lakini mpaka sasa hatuna hospitali ya Rufaa; tuna vituo viwili vya afya ambavyo ni; Bitale, Nyamasovu ambacho ni cha *mission* na kingine kinajengwa Mwamgongo ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya amekifungua mwezi uliokwisha. Niombe sana Serikali mtuangalie Wilaya ya Kigoma Vijijini tuweze kupata hospitali hii ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala zima la vifaa. Hospitali ya Mkoa wa Kigoma na maeneo mengine yote ya Tanzania, hospitali hizi zinakabiliwa na kukosa vifaa. Leo unapokwenda katika hospitali ya Mkoa wa Kigoma hakuna *CT-Scan machine* inalazimu mtu apewe rufaa kutoka Kigoma kwenda Bugando, kutoka Kigoma kwenda Muhimbili; hali hii inasababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi. Niiombe Serikali tupate vifaa hivyo katika hospitali zetu na tuweze kuwasaidia wananchi wetu wapate huduma ndani ya mikoa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee suala zima la barabara. Maeneo mengi ndani ya nchi yetu barabara bado ni changamoto kubwa. Nirudi kule kule katika Mkoa wangu wa Kigoma tuna barabara ambayo inatoka Mwandiga – Bubango – Chankele inakwenda Kagunga ambayo tunasema ni Kagunga *Road.*

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali itusaidie barabara hii iingie katika Mpango, iwekwe kiwango cha lami iweze kuwasaidia wananchi hawa ambao maisha ya yamekuwa ni kupita katika maji, wanahatarisha maisha yao na wao waweze kutumia usafiri wa barabara. Kwa hiyo niiombe sana Serikali, barabara hii muweze kuisaidia tuipate.

Itatusaidia sana na wananchi hawa na wataweza kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine pasipokuwa na wasiwasi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la *TARURA.* Wananchi wengi hawana uelewa kuhusu *TARURA.* Natokea katika Kijiji cha Mwandiga, wengi hawaelewi *TARURA* wanafanya kazi gani na hata mimi nilikuwa nashangaa, kwa nini barabara hizi za mitaa hazifanyiwi kazi, nikajua ni *TANROADS* lakini nikaambiwa sasa zimekwenda kwa *TARURA.* Niiombe sana Serikali iwasaidie *TARURA* bajeti ipatikane, barabara hizi zitengenezwe.

Mheshimiwa Spika, vile vile nishauri *TARURA* washirikiane na watu kama Waheshimiwa Madiwani ili waweze kuwapa vipaumbele wajue ni barabara gani wanatakiwa wazianze, ni barabara gani za vipaumbele wazifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana Serikali ifanyie kazi hilo. Pia niongelee barabara ya kutoka Kidahu – Nyakanazi. Hii barabara ni *potential,* ni barabara muhimu sana. Kwa taarifa nilizonazo mkandarasi yuko pale lakini barabara hii inasuasua. Nimeipita nilikuwa nikitembea katika Vijiji vya Pamila, nimepita barabara ile, unakuta hapa pamechimbwa, hapa pamechimbwa, inaonekana mkandarasi yuko *slow.* Niiombe sana Serikali itusaidie barabara ile imalizike kwa wakati na kazi ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee tena katika uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Katika ukurasa wa 14 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema kwamba kuna pesa ambazo zimetengwa katika *SACCOS* lakini pia katika vikundi vya akina mama zaidi ya bilioni 3.4 katika Halmashauri 53. Ningeomba ufafanuzi; hizi halmashauri ambazo hizi pesa zimekwenda ni zipi? Kwa sababu leo katika Halmashauri yangu ya Kigoma Vijijini kuna vikundi vya akinamama, kuna vikundi vya walemavu, kuna vikundi vya vijana lakini bado hawajapatiwa pesa hizo. Niombe kufahamu, halmashauri

hii haijapata na kama pesa zimefika zimetumikaje au wanapewa akinamama wa mjini tu na sio akinamama vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niiombe sana Serikali iwaangalie akinamama, vijana na walemavu, kwa sababu naamini ukimwezesha mama umeikomboa jamii; na vijana wa Kitanzania wanataka ajira, ajira imekuwa ni changamoto. Tuwawezeshe mitaji waweze kufanya kazi ili wasikae vijiweni ambako matokeo yake ni kuvuta bangi na kuingia katika biashara ya kujiuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine niongelee suala zima la reli. Nimefurahishwa sana na Serikali kwamba, inakwenda kuanzisha huu mradi wa *standard gauge.* Ni mradi mzuri, tuuunge mkono, lakini ningeomba sana usiishie katika Mkoa wa Tabora, ufike mpaka Kigoma, tunahitaji *standard gauge* ndani ya Kigoma. Kwa sababu, naamini kabisa ikifika Kigoma tutakuza uchumi wa nchi, tutakuza uchumi wa Kigoma. Leo Kigoma tayari tumepata bandari kavu ya Katosho, naamini kama *standard gauge* itafika Kigoma, Wakongo, Warundi, magari ambayo watayaleta katika bandari ile ya Kigoma watatumia reli hii ya *standard gauge. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, Kigoma na sisi tupate hii *standard gauge* ningeomba sana hii *metre gauge,* reli hii ya kati, Serikali iboreshe miundombinu. Changamoto ni kubwa, asilimia 90 ya wananchi wa Kigoma tunategemea usafiri wa reli ya kati. Wengi hawana uwezo wa kupanda ndege, wengi hawana uwezo wa kupanda mabasi haya kwa Sh.60,000/= wanakimbilia huku kwenye treni ya Sh.18,000/= lakini miundombinu ni mibovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Kigoma unaambiwa terni itaondoka saa 2.00 asubuhi, lakini unakuja kuondoka saa 8.00 usiku. Wale walioko pale abiria ni akinamama, watoto, kuna wagonjwa, kuna wajawazito. Wengine wametoka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiza Mayeye. Mheshimiwa Joseph Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Rita Kabati.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa naomba niungene na wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Watanzania kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kukurejesha salama na kuendelea na majukumu yako ya kulijenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kutumia nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna ambavyo wametupa kipaumbele wananchi wa Madaba. Wizara ya Afya, Maji, Elimu, Miundombinu, Umeme na TAMISEMI hawajakauka katika Jimbo la Madaba. Kwa kweli, katika maeneo hayo tumepiga hatua kubwa sana na wananchi wa Madaba hawataridhi kama nitaanza hotuba yangu bila kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Wizara hizo pamoja na watumishi wote wa Wizara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, sitawatendea haki Mashujaa wa Vita ya Majimaji ambao tunawakumbuka tarehe 27 Februari, kila mwaka kwa sababu nisiposema baadhi ya maneno yamepotoshwa ndani ya Bunge lako Tukufu. Wiki iliyopita Mheshimiwa Ngombale aliilalamikia Serikali kana kwamba makumbusho tunayoyafanya Majimaji ni upendeleo.

Mheshimiwa Spika, tutatafuta nafasi ya kulifafanua, lakini kwa kifupi tu ni kwamba, historia ya makumbusho ya Majimaji sisi wenyewe wakazi wa Mkoa wa Ruvuma tulianza kuchukua hatua kuwakumbuka mashujaa wale na Serikali imekuja kushirikiana na sisi karibu miaka 90 baadaye. Sheria na miongozo ya Serikali ipo, nimshauri tu Mheshimiwa Mbunge

afuatilie hatua mbalimbali za kufikia huko na sisi Wanaruvuma tunaunga mkono sana jitihada za Watanzania wenzetu waliopigana vita kulinda heshima ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye hotuba yangu. Hotuba yangu nitaiweka kwenye eneo moja tu kubwa muhimu, juu ya namna gani Serikali ya Tanzania, Serikali ya Uchumi wa Viwanda inahitaji sana ushiriki kamili wa Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki kifupi Wizara hizi mbili, Wizara ya Viwanda na Wizara hii ya Nishati, wamepiga hatua kubwa sana, hatua ambayo Waheshimiwa Wabunge hatuwezi kuibeza. Upande wa viwanda na biashara idadi ya viwanda imeongezeka kutoka 454 ambayo ilikuwa mwaka 2015 na sasa tuna viwanda vipya tu katika kipindi hiki cha miaka mitatu, viwanda 3,306.

Mheshimiwa Spika, katika hili nitaweka nukta kidogo. Kuna watu wanaibeza Serikali wakisema kwamba, viwanda hivi 3,306 si viwanda vyenye hadhi ni mashine za kusaga, sijui mafundi cherehani. Watu wafanye kazi ya kutafuta takwimu. Idadi ya ajira katika kipindi hiki kifupi, kwenye sekta binafsi, sekta ambayo inatokana na viwanda, ilifika 137,054; ukigawanya kwa idadi ya viwanda unapata wastani wa kila kiwanda kimeajiri watu wasiopungua 40. Sasa watu 40,000 si kiwanda? Watu wafanye kazi ya kutafuta takwimu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kuhusu viwanda tumepiga hatua; mwaka 2015 sekta hii ilikuwa inakua kwa asilimia 7.9 na sasa inakua kwa asilimia 9.8. Huu ni ukuaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sekta ya umeme nayo imepiga hatua ambazo hatuwezi kuzibeza. Moja, sekta hii imejiwekea malengo ya mwaka 2020 ya kuwa na *megawatts* 4,915 na 2025 *megawatts* 10,000. Kwa kipindi hiki kifupi kuanzia mwaka 2015 wakati Serikali ya Awamu ya Nne inamaliza kipindi chake cha madaraka, ilimaliza wakati Watanzania tuna umeme

wa *megawatts* 1,308 tu; leo tuna *megawatts* zaidi ya 2,500. Katika kipindi hiki kifupi katika sekta ya umeme, umeme umeongezeka kwa asilimia 52, hili si jambo la kubeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara hii inayoshughulika na umeme imeweka mikakati madhubuti ya kufikia malengo ya kuwa na umeme wa *megawatts* 4,915. Ipo miradi mipya ambayo imeanzwa ikiwepo *Stieglers Gorge,* lakini unaona kwenye *Kinyerezi I* na *Kinyerezi II* tunaona kuna *Kinyerezi I Extension* ambayo itazalisha umeme wa *megawatts* karibu 250, lakini kuna *Kinyerezi III* ambayo itazalisha umeme *megawatts* 600. Hiyo ni mikakati mizuri itakayotupeleka kwenye malengo yetu ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naona kuna watu wemesema jimboni kwangu. Nichukue nafasi hii, kwa vile nimekumbushwa niishukuru sana Wizara ya Nishati. Leo katika historia ya Madaba, mwaka huu uliokwisha tarehe 25 Desemba, 2017 wananchi wa Madaba wameanza kupata umeme, tangu kupata uhuru. Hili ni jambo la historia na ni jambo la kujivunia sana, naomba niishukuru Wizara katika kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, sipendi kusema kwamba, kila penye mafanikio hapakosi fitina, lakini nataka niseme kila panye mafanikio hapakosi changamoto. Malengo ya *megawatts* 4,915 tuliyojiwekea kwa mwaka 2020 na malengo ya *megawatts* 10,000 tuliyojiwekea ukilinganisha na Tanzania ya uchumi tunaoutaka ni kiwango kidogo sana cha umeme.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano kadhaa. Zipo nchi kadhaa ambazo zimepiga hatua ambayo sisi sasa tunaelekea, lakini huko nyuma zilifanana sana na sisi kiuchumi na kimikakati.

Mwaka 1970 nchi ya Afrika Kusini ilikuwa na umeme wa *megawatts* 14,000 sisi leo tuna megawatts 2,500 na tunakwenda kutengeneza Tanzania ya viwanda kwa

mkakati wa kuwa na *megawatts* 4,915. Umeme huu hautoshi kabisa na haya malengo ni ya chini sana, hayatatupa Tanzania ya viwanda tunayoitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo mifano mingi. Mexico mwaka 1994 walikuwa na *megawatts* 35,000; lakini leo Afrika Kusini wanaongelea *megawatts* 44,000 wakati nchi nyingine kama za Korea Kusini wanaongelea *megawatts* 84,000 sisi tumejiwekea malengo ya *megawatts* 4,000. Pamoja na kupiga hatua kubwa katika hilo, lazima tukiri kwamba, mkakati wetu lazima tuubadilishe na lazima tutengeneze vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niishauri Serikali kwenye eneo hili. Natambua mikakati mikubwa ambayo Serikali imejiwekea kwenye umeme, tuna mikakati hiyo ambayo nilikwishaitaja. Hata hivyo, kadri ya utafiti wa Benki ya Maendeleo ya Afrika vyanzo vya umeme wa Tanzania vinavyotokana na maji haviwezi kutupatia umeme unaozidi *megawatts* 4,000. Tunataka tutafute *megawatts* 10,000 na tunataka tufike *megawatts* zaidi ya 40,000 ili kupata Tanzania ya viwanda. Hiki kiwango ni kidogo, ni lazima Serikali iangalie vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba zilizotangulia tumeongelea kuhusu umeme wa gesi, nadhani kwa bahati mbaya Mheshimiwa Waziri Mkuu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhagama, muda hauko upande wako.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nilishakutaja Mheshimiwa Rita Kabati, atafuata Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nianze na dua la kukuombea, naomba Mwenyezi Mungu akujalie, akupe afya njema na wote wanaokutakia mabaya washindwe kwa Jina la Yesu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na pongezi kubwa kabisa za kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha hotuba yake; na nimpongeze Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Ikupa.

Mheshimiwa Spika, pia niwaambie wenzetu mwenye macho haambiwi ona, hivi kazi zote ambazo Mheshimiwa Rais, ambazo Serikali hii imezifanya, miradi mingi imefunguliwa, kila siku Mheshimiwa Waziri Mkuu anakwenda huku na huku, kweli hamuioni jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe tu niseme kwamba, ukisoma ukurasa wa 10 unaonesha kabisa wananchi wameanza kuelewa sera za Chama cha Mapinduzi, wamehama wengi sana. Katika uchaguzi tu kati ya 59; 58 tumeshinda CCM na Wabunge wote majimbo yote tumeshinda na niwapongeze hata Wabunge ambao wamehama upande ule wakaja upande huu wa kwetu; hongereni sana kwa kuja huku wala hamjakosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, niwapongeze Mawaziri wote waliopo katika Serikali hii bila kuwasahau wanawake wenzetu; hamjatuangusha wanawake, mmefanya kazi vizuri sana tu. Kila siku tunawaona mnahangaika huko na huko kwa kweli mko vizuri, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na kuchangia kuhusu uwezeshaji kwa vijana. Niendelee tu kuipongeza Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kwamba, walikuja Iringa wakafungua yale mafunzo ya vijana katika Chuo cha Don Bosco, Mheshimiwa Jenista nakushukuru sana. Vijana wengi sana wameitikia mwitikio mkubwa sana katika kile chuo mpaka kumetokea changamoto kubwa vijana wengi wanakosa sehemu za kusoma kwa sababu zile nafasi ni

chache. Tungetamani hata kila wilaya yale mafunzo yaendeshwe ili vijana wengi waweze kupata yale mafunzo. Pia, kuna changamoto kwamba, vijana wale miezi sita sasa hawajapata posho, labda hilo liangaliwe ili waweze kupata wasisome kwa shida sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile tulikuwa tunaomba pengine iwepo *connection* kati ya wakuu wa wilaya pamoja na chuo ili kuratibu maana imekuwa malalamiko yanatufuata sisi Wabunge tunashindwa sasa twende wapi. Tunaomba pia, hilo liangaliwe. Pia, uwepo utaratibu mzuri kuhakikisha kwamba, wale wanaohitimu yale mafunzo angalau pia halmashauri zao ziweze kuwapatia asilimia tano ile ya mikopo.  Pia kama kuna kazi basi wapewe za kutengeneza madawati, chaki na kadhalika ili ile mikopo iwe rahisi kuweza kurejeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Jenista, niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Mavunde wamefanya kazi nzuri sana kufuatilia mikataba ya wafanyakazi katika viwanda, katika makampuni yale ya wawekezaji. Sasa niombe, sasa hivi waelekee kwenye hizi sekta ambazo si rasmi; kwa mfano wafanyakazi wa ndani wanafanya kazi kwenye mazingira ambayo bado ni magumu sana.

Mheshimiwa Spika, najua wengine waajiri wao mko humu ndani, lakini mtanisamehe lazima niwasemee, wengi wametoka kwenye Mkoa wetu wa Iringa, bado malalamiko yao ni makubwa sana hawatendewi haki. Vile vile kuna wafanyakazi ambao wanafanya kazi kwenye migahawa nao bado mikataba yao si mizuri. Hawa wenzetu wanaofanya kazi kwenye baa nao wanafanya kazi kwenye mazingira magumu ingawa ile bia yenyewe inatuletea faida kubwa sana katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nisisahau kabisa naomba niwasemee wenzetu waandishi wa habari, wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana tunaonekana kwenye TV, wanatuandika kwenye magazeti, lakini nao pia mikataba

yao si mizuri sana kwa sababu utakuta bado wengine hawana hata bima hizi za afya, hawana bima za maisha, wanahatarisha hata maisha yao. Vile vile tunatakiwa tuwasaidie ili wafanye kazi kwenye mazingira mazuri waendelee kujenga Taifa letu kwa kuandika vizuri. Mishahara yao pia, bado haieleweki, kila mwajiri anamwekea vyovyote anavyotaka; kwa hiyo, niombe kabisa pia, waangaliwe.

Mheshimiwa Spika, niendelee katika sekta ya afya. Niendelee kuipongeza Serikali kwa sababu, wamepunguza changamoto ya upatikanaji wa dawa kwenye hospitali na vituo vya afya, lakini kuna changamoto kwenye Hospitali yetu ya Mkoa wa Iringa. Kwamba eneo lile ni dogo sana na lina mwingiliano na magereza. Tulishawahi kusema na Waziri wa Mambo ya Ndani analijua na Naibu Waziri wa Afya naye si muda mrefu alikuwa kule ameona.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo inasababisha Madaktari wetu Bingwa wanakaa nje ya hospitali, kwa hiyo inakuwa shida sana kuwahudumia wagonjwa wanapopata shida usiku. Vile vile tuna changamoto ya Daktari Bingwa wa Watoto, hakuna kabisa kwenye hospitali yetu ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, vile vile upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi sekta ya afya, karibu asilimia 60 ni tatizo katika mkoa mzima; na Hospitali ya Wilaya ya Mufindi yenyewe inaongoza kwa sababu asilmia 40 hakuna wafanyakazi. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie kuziba zile nyufa za wafanyakazi ambao waliondolewa ili wagonjwa waweze kutendewa haki.

Mheshimiwa Spika, niipongeze pia Serikali kwa mgawo wa *4.5 billion* katika wilaya zetu kujenga hospitali za wilaya katika mkoa wetu; Wilaya ya Kilolo, Wilaya ya Mufindi, *Iringa DC.* Japokuwa katika hospitali ya manispaa hatujatengewa kitu chochote na kuna changamoto kubwa ya jengo la vipimo hakuna kabisa na kuna mashine za *X-Ray, CT-Scan, Ultrasound,* hakuna kabisa. Vilevile wodi za kulaza

wagonjwa wengine pia, hakuna na tulikuwa tunategemea kwamba, ile hospitali ingepunguza msongamano wa wagonjwa wa hospitali ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, najua kwamba, Mheshimiwa jafo alishapita na kuona hizi changamoto, kwa hiyo niombe kwa kweli zifanyiwe kazi. Mashine hizi zitakazopatikana zitasaidia hata gharama ndogondogo za kuiendesha ile hospitali. Vile vile huduma ya wazee dawa ni ghali sana, zipo nje ya mfumo, kwa hiyo huduma zile ambazo ziko nje ya mfumo wa bima yao wanapata shida kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kukaa na wafanyabiashara na kusikiliza changamoto zao. Ni kweli tozo katika viwanda zimekuwa nyingi sana, ningeomba kwa kweli waziangalie ili tuendelee kuhamasika na huu uchumi wa viwanda, ili viwanda vingi viweze kufunguliwa.

Mheshimiwa Spika, nichukulie tu mfano mdogo kwenye sekta ya maziwa. Unaona *TFDA* ile *yogurt* wana-*charge flavor* dola 3,000, lakini hii ingechajiwa tu labda kwa zao lenyewe la maziwa bila kuangalia kila *flavour* kwa sababu mtu akiwa na *flavour* 10 anachajiwa *(charge)* dola 3,000. Kwa hiyo, naona hii pia, Waziri wa Mifugo aliangalie.

Mheshimiwa Spika, vilevile *OSHA.* Hii *OSHA* wanapima afya za wafanyakazi unalipia Sh.80,000, Manispaa nao wanapima afya za wafanyakazi wanalipia tena; sasa hii ingewekwa kwenye sekta moja, ili zote zichajiwe *(charge)* kwa pamoja. Hii inawakatisha sana watu wanaofanya kazi katika sekta hii ya maziwa.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi kuna watendaji wengine hawaitakii mema hii nchi yetu, kwa sababu kwa mfano tarehe tatu mwezi wa nne walikamata gari la maziwa la *ASAS* pale Iringa. Lile gari lilivyokamatwa limekamatwa kuanzia saa 12.00 limekuja kuachiwa saa 6.00 wamechajiwa *(charge)* 1,000,000/= kwa kosa ambalo kwa kweli, ukilisikiliza wala si kosa.

Mheshimiwa Spika, sasa hapohapo ukatokea uharibifu wa *packets* 3,000 takriban 3,500,000/=. Sasa hii inaleta matatizo sana kwa wenzetu ambao tunatagemea kwamba, wangetusaidia hata uajiri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Rita Kabati.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii, kwa yale ambayo sijachangia nitachangia kwenye Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana! ahsante sana! Mheshimiwa Livingstone Lusinde ndiye anayefuata na atafuatiwa Mheshimiwa Kemilembe Lwota. Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, na mimi naungana na Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamemshukuru Mungu kwa ajili ya afya yako tunaendelea kukuombea. Inawezekana hata sisi wenyewe tuna matatizo lakini bado hatujapimwa sawasawa. Kwa hiyo, kwa kweli tunakuombea Mheshimiwa Spika uendelee kuimarika ili uweze kuwatumikia wananchi wako wa Jimbo la Kongwa lakini na sisi Wabunge wenzako.

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu za pili zinakwenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wanaomsaidia kazi. Hotuba ni nzuri, wameiwasilisha vizuri lakini imegusa maeneo mengi muhimu. Isipokuwa kuna baadhi ya maeneo Waheshimiwa Wabunge tutawakumbusha ili nanyi muweze kuongeza nguvu kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mungu sana kwa sisi wakazi wa Mkoa wa Dodoma kutupatia mvua za kutosha mwaka huu ingawa baadhi wa maeneo zimeleta majanga

makubwa sana, kama uharibifu wa barabara inayotoka Dodoma Mjini kwenda Ilangali. Pale daraja limesombwa kwa hiyo, tuna uhakika kwamba Serikali watafuatilia kulitengeneza haraka ili kuweza kuwanusuru wananchi wa ukanda ule wa Tarafa ile ya Mpwayungu ili mazao yao ya biashara yaweze kufika kwa wakati hapa Dodoma ambapo kwa kweli ndiko kwenye soko kubwa tunalolitegemea.

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa mengi nami naomba nitoe mchango wangu kidogo katika baadhi ya masuala ambayo yamezunguzwa mahali hapa.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa, kuna mambo ambayo yamefanyika kwa miaka miwili na nusu unaweza kusema ni miujiza. Kwa sababu matukio makubwa na ya kutisha tumeyaona yakifunguliwa na haya yote yakikamilika, reli ikakamilika, umeme wa maji ukakamilika, barabara zetu zimekamilika nina hakika kabisa kwamba yatachagiza maendeleo kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na tunamwomba Mungu aendelee kumlinda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa ndege; nataka niwakumbeshe baadhi ya watu wanaweza kuwa aidha wadogo au wamesahau. Uamuzi wa kulifufua shirika la ndege sio mara ya kwanza, baada ya iliyokuwa Jumuiya ya *East Africa* kufa na ndege nyingi kubakishwa nchini Kenya na sisi tukapata moja. Mwalimu Nyerere mwaka 1977 alifufua shirika lile kwa kununua ndege zinazokadiriwa kufikia kama nne au tano kwa wale watu wazima kama mimi mnaweza kukumbuka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Rais anachokifanya sasa anafufua shirika la ndege, ni kama vile una debe moja la mbegu unajiuliza ukaange ule au uende ukapande zizae ili waweze kutumia wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wengine wamezungumza kwa dharau sana. Mtu anasema eti watu

wanaenda kupiga picha kwenye ndege, watu wanashangilia ndege. Hapa wako Wabunge hapa wako humu ndani kwa sababu wameletwa na ndege. Wengine *helicopter* zilipokuwa zikikusanya watu ndiyo wakachaguliwa kuingia humu ndani ya Bunge wamesahau.

Mheshimiwa Spika, kuna chama hapa hakina ofisi ya mkoa, hakina ofisi ya wilaya, kimepata ruzuku zaidi ya mabilioni ya pesa, lakini huwa wanakodia ndege wakati wa uchaguzi ili Wabunge wao waweze kushinda. Wamesahau wanaingia humu ndani kutukana ndege maskini wa Mungu. Hivi kama kweli isingekuwa *helicopter* zinawasaidia, si tungeona mmejenga hata ofisi ya Mkoa?

Mheshimiwa Spika, tumeona *NCCR* Mageuzi mahali pengine wana ofisi, tuwameona *CUF* wana ofisi ya kueleweka lakini kuna chama kina kaofisi *squatter* pale Kinondoni wanapiga kelele kila siku hapa.

Mheshimiwa Spika, unashindwa kuwaelewa kabisa kwa nini msioneshe hayo maendeleo kwenye chama chenu kwa ruzuku mlizopewa? Mbona mnakodia *helicopter* hizo hizo? Kwa hiyo, kununua ndege Mheshimiwa Rais mimi naona ni jambo jema kwa sababu tutapanda sisi, watapanda Watanzania na lile shirika litaleta maendeleo makubwa*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dharau kwenye viwanda vidogo si njema. Tunadharau mafundi cherehani, hivi hapa Waheshimiwa Wabunge bila mafundi cherehani si tungekuwa uchi tu hapa. Wengi tunashona tunashona nguo huko. Leo nataka niwaambie kiko kiwanda ambacho kinatusaidia sana juzi tu ndiyo nimekiona. Kiwanda cha Saloon jamani kumbe Wabunge tunalindwa sana na saloon. Kuna Mbunge mmoja amekosa kwenda Saloon siku tatu, sura yake imebadilika kabisa, wala siyo yeye.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunataka tuwashukuru sana hata watu wa *saloon;* akinadada wa *saloon*, akinababa wa *saloon* kumbe mnatuweka vizuri mpaka

tunaonekana watu wa maana mbele za watu. Kwa hiyo hivi ni viwanda vidogo ambavyo Watanzania vinatuletea maendeleo lakini na sisi vinatuletea heshima fulani. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane, Waheshimiwa Wabunge wameongea vizuri sana hapa kuhusu gharama za uchaguzi, hili nataka niwaunge mkono. Kuna gharama kubwa sana kurudia chaguzi ndogo, lakini ambao wanaweza kutusaidia kwa kweli wanaweza kutusaidia Wapinzani, kwa sababu Serikali imeshaundwa Wabunge wengi wa CCM una uhakika Mbunge wa Upinzani hata akishinda haendi kubadili Serikali. Kwa nini mnaweka wagombea msiweke ili kunusuru mapesa hayo yaende kwenye maendeleo. Hakuna sababu maana hata ukishinda kiti kimoja, kilo moja ya sukari haiwezi kwenda kukolea kwenye pipa la maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hakuna sababu ya vyama vya upinzani kuweka wagombea kwenye uchaguzi mdogo, maana tayari umeshafahamika aliyeshinda kafahamika kuna sababu gani za kuweka mgombea kwenda kupoteza hela za nchi. Kwa hiyo ni vema wakatuunga mkono, kuanzia sasa hivi kukitokea uchaguzi mdogo hakuna sababu ya wao kuweka mgombea na sisi tutapita bila kupingwa, hakutakuwa na gharama pesa zote zitaenda kwenye maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge wamezungumza sana leo hapa, wamezungumza kwa uchungu mkubwa sana. Mbunge mmoja wa CHADEMA amezungumza sana kuhusu Rais kutoka Kanda ya Ziwa na kwamba ni aibu sana Kanda ya Ziwa kukosa maji. Akasimama ndugu yangu Nape akasema Waziri Mkuu anatoka Kusini ni aibu kukosa maendeleo. Sasa najiuliza tuna Waziri Mkuu wa Kusini, tuna Rais wa Kanda ya Ziwa? Tuna Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jamani. Hatuna Rais wa Kanda, tuna Waziri Mkuu wa Jamhuri Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tusiwafanye viongozi wetu wakawa viongozi wa Kanda haiwezekani na mtakuwa hamtutendei haki. Hivi na sisi ambao Spika unatoka Dodoma mbona unawaruhusu wao kusema, kwa nini usituruhusu sisi wa Dodoma tuseme sana ili shida zetu zisikilizwe. Haitawezekana!

Mheshimiwa Spika, hili jambo lazima tujue Viongozi wakishakuwa wa Kitaifa, wanaongoza Taifa la Tanzania na sio sehemu walikotoka. Kwa hiyo kama Rais anahakikisha kwamba kwao hakuna maji lakini wengine wamepata huyo ndio Rais bora analitazama Taifa, hatazami upande wake. Kama Mheshimiwa Waziri Mkuu anaelekea sehemu zingine za Tanzania anazunguka kuhakikisha maendeleo yanapatikana huyo ndio Waziri Mkuu bora.

Mheshimiwa Spika, sikutegemea kwamba tuanze kuwagawa viongozi wetu kwa namna ya wanakotoka haiwezekani. Tusimame katikati tuishauri Serikali mambo ya msingi yafanyike ili nchi nzima ipate maendeleo. Nchi hii ni kubwa ndugu zangu, nchi hii changanya Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi ndipo unaweza ukaikaribia ukubwa wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, huwezi ukapeleka maendeleo kwa haraka na maeneo yote yakaridhika ndugu zangu, twendeni taratibu. Twendeni taratibu, twendeni awamu kwa awamu. Sehemu zingine ukipeleka sehemu zingine wanasubiria, sehemu zingine ukipeleka sehemu zingine wanasubiria, tutafika tu mahali na nchi nzima itapata maendeleo. Kwa hiyo nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge tuvute subira, viongozi wanahitaji kuungwa mkono.

Mheshimiwa Spika, watu wanazungumzia habari ya usalama...

**MHE. JOSEPH K. MUSKUMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ni Mheshimiwa Musukuma eeh.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo,

**SPIKA:** Haya, ruksa

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nataka tu nimpe taarifa mzungumzaji kwamba amezungumza suala la Nape alivyokuwa akichangia, ,nasema kwamba hata Mbunge aliyemwachia jimbo alikuwa ni Waziri wa Mambo ya Nje, Wafadhili wote alikuwa anazungumza nao hakuwapeleka Mtama alituletea na sisi Geita, ni hiyo tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa yako Mheshimiwa Musukuma. Bahati mbaya tu mwenyewe hayupo maana na mimi nilitaka asikie lakini atakusikia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba sana sisi kama Taifa kama nchi, viongozi wetu wagawanye rasilimali za nchi kwa usawa maeneo yote. Hata yale ambayo haya vivutio vikubwa vinavyokusanya hela nayo wayatazame. Kwa mfano tunaelewa sisi Dodoma hapa tuna zao la zabibu. Zao la zabibu hili likifunguliwa viwanda vya kutosha tutanufaika, watu wetu watapata pesa, watalima, watauza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifugo, sisi tumepata kiwanda kizuri kabisa cha kuandaa ngozi pale katika Kijiji cha Idipu, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu umeme upelekwe kwenye kile kiwanda. Kile kiwanda hakiishi kwa wakati kwa sababu umeme wenye nguvu kubwa haujafika pale kiwandani.

Mheshimiwa Spika, umeme ukiweza kufika na sisi ni wafugaji, tuna ng'ombe wengi wanachinjwa kwenye minada, ngozi nyingi zinapelekwa pale, wananchi wa jimbo la Mtera nao watapata maendeleo makubwa. Tutanufaika na hii hoja ya uanzishwaji wa viwanda maana kiwanda tayari kinajengwa.

Mheshimiwa Spika, naomba tuitazame Tanzania katika yale maeneo ambayo yamesahaulika kwa muda mrefu tuyatupie macho. Maana kuna mwingine ana maji ana barabara nzuri akija hapa kupiga porojo ni sawa, lakini kuna wengine vitu vyote vitatu hawana, tuangalie kimoja wapate. Watu ambao wanaishi kijijini; tunapoteza akinamama wengi sana wakati wa kujifungua, kwa sababu unaweza kukuta wakati wa kujifungua njia imefunga, maji yamekata barabara, gari haliwezi kufika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kupata *ambulance,* lakini kuna mahali *ambulance* hazipiti kwa sababu barabara ni mbovu. Tumeondoa barabara kutoka Halmashauri tumezipeleka *TARURA,* lakini ukitazama uwezo wa *TARURA* na bajeti yao bado ndogo bado hai-*reflect* maendeleo ya barabara za vijiji. Kwa hiyo, tunaomba waongezewe pesa, ziwe nyingi ili waweze kutengeneza zile barabara kwa kiwango kinachotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwatazame sana! Watu tumejenga sekondari za Kata, tumejenga mashule vijijini, lakini bado namna ya kuwachagiza wananchi wa vijijini ni umeme ufike kwa wakati. Kuna baadhi ya maeneo hayana umeme Tarafa nzima ya Mkwayungu haina umeme. Tukiwapelekea umeme watu wa Mkwayungu baadhi ya mambo yao mengi watafanyia kule, watakamua alizeti zao kule, hawana haja ya kuzileta Dodoma Mjini. Dodoma Mjini wataleta mafuta. Kwa hiyo viwanda vidogo vitaanzishwa Mkwayungu.

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana tunaposimama hapa na sisi lengo letu ni kuwaunga mkono na kuwatia moyo Waheshimiwa Mawaziri. Ukilitazama Baraza hili ni dogo kuliko lililopita, lakini Mawaziri wake wanafika kila kona ya Tanzania, lazima tuwapongeze na kuwatia moyo. Hawa ni binadamu usiku kucha wanasafiri wanafika kwenye majimbo yetu wanaongea na wananchi, lazima na sisi tuwaunge mkono.

Kwamba Waheshimiwa Mawaziri tunatambua kazi kubwa mnayoifanya sisi kama Wabunge wenzenu tunawaungeni mkono, endeleeni kuchapa kazi ili Taifa hili liweze kusogea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wamezungumza hapa kuhusu amani. Amani na utulivu ipo lakini ipo kwa sababu na wahalifu nao wapo. Tuwaombe Serikali waendelee kuwasaka wahalifu kwenye kila nyanja ya uhalifu unavyotokea. Tusiichafue Serikali kwa sababu ya kosa moja.

Mheshimiwa Spika, ikitokea kiongozi mmoja wa dini amekengeuka pengine amezini Mungu aepushe mbali hatuwezi kulaumu dini nzima, haiwezekani. Tunamlaumu huyo huyo kwa kufanya hilo kosa. Kwa hiyo lazima tukubaliane, kwamba uhalifu upo lakini tuitake Serikali kupambana na uhalifu kama inavyofanya siku zote.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kemilembe Lwota, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, halafu tutaenda Zanzibar Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuzungumza asubuhi hii ya leo. Vile vile niungane na Wabunge wenzangu wote na Watanzania kwa ujumla kwa kukukaribisha tena kwenye Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Timu yake yote kwa hotuba zao nzuri ambazo wametuletea; vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara ambayo alifanya katika Mkoa wetu wa Mwanza, ziara ambayo imekuwa na mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sitatenda haki kama nitasimama kuchangia hapa leo nisiongelee masuala ya uvuvi ambayo yanaendelea kwenye Mkoa wetu wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla wake. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la unyanyasaji wa wavuvi wa Kanda ya Ziwa. Nia ya Serikali ni njema kabisa wote tunafahamu ya kukomesha uvuvi haramu, lakini kinachofanyika sasa hivi ni kinyume na ni mambo ambayo hayapo kabisa hata kwenye sheria zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Mawaziri, kazi kweli nzuri wanafanya na kubwa lakini kuna watu ambao wapo huko *site,* kuna *task force* imeundwa. Hii *task force* kinachoendelea huko mikoani mwetu, naongelea Mkoa wa Mwanza ni hatari kubwa kabisa kabisa. Nia ya Mheshimiwa Rais wetu ni njema ya kuwaokoa na kuwasaidia wanyonge lakini kinachofanyika ni kuendelea kuwakandamiza na kuwaumiza na kufanya uvuvi usiwepo kabisa kwenye mkoa wetu.

Naomba niweze kukupa mifano ambayo inaendelea kwenye Mkoa wetu wa Mwanza. Ni kweli nyavu zimechomwa ambazo zilikuwa zinajulikana nyavu haramu sawa tumekubali. Hata hivyo, mpaka sasa hivi tunavyoongea hizo nyavu halali ambazo zinatakiwa ziwepo hakuna nyavu. Nyavu zimekuwa kama madawa ya kulevya. Sasa hivi nyavu zinauzwa kwa magendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa watu ambao wako huko *site,* hiyo *task force* ambayo naiongelea, wanashika watu, wanawanyanyasa watu, wanakuwa na maskari wanatoza faini ambazo hazipo kwenye sheria wala kanuni wala taratibu yoyote ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mifano; kuna baadhi ya wavuvi ambao wameshikwa na Mheshimiwa Waziri nimshukuru kwa sababu ni msikivu tumeongea naye na anasaidia baadhi ya mambo. Mtu anakamatwa kwenye gari ya samaki anaambiwa hauna koleo la plastiki. Faini ya koleo hili la plastiki ni shilingi milioni tano; na *consistency*

haipo. Mmoja atashikwa leo ataambiwa faini milioni tano, mwingine atashikwa kesho anaambiwa ni shilingi milioni mbili, mwingine anashikwa kesho kutwa anaambiwa faini milioni kumi, tunakwenda wapi kama Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunajua ugumu wa ajira uliopo. Watu hawa ni watu ambao wengine niseme ni watu wa chini kweli wanaofanya kazi za uvuvi. Watu hawa wameamua kujiajiri lakini ajira imekuwa ya matatizo. Tumeongea sana humu ndani lakini hiyo *operation* bado inaendelea na inaendelea kwa nguvu na inaumiza wananchi wetu kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali, kuna haja na umuhimu wa kukaa na kuangalia haya mambo yanayoendelea huko, mambo yanayoendelea ni mabaya ni mabaya, ni mabaya na unyanyasaji wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea suala ya madawa ya kulevya. Niipongeze sana Serikali, imeleta juzi hapa sheria ambayo tumeipitisha ambayo imesaidia kudhibiti na kupunguza madawa ya kulevya kwa kiasi kikubwa sana kwa upande wa Bara. Hata hivyo kwenye hii hotuba ya Kamati ya UKIMWI pia tumeiona kiwango kikubwa sana cha kudhibiti kwa upande wa Bara sasa hivi na kazi kubwa sana inafanyika na watu hawa wa Mamlaka ya Dawa za Kulevya. Hata hivyo kinachoendelea kwa upande wa ndugu zetu upande wa Zanzibar, wafanyabiashara hawa wengi wamehamia upande wa Zanzibar kwa sababu ya sheria kali ambazo zilizowekwa kwa upande wa Bara.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, naiomba sasa Serikali ifike mahali ikae na ndugu zetu wa Zanzibar, waweke sheria ambazo zitakuwa ngumu kwa pande zote mbili ili kama tumeamua kudhibiti na kukabiliana na madawa ya kulevya iwe kwa pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea kuhusu suala la UKIMWI. Asilimia100 za fedha za maendeleo ya fedha za UKIMWI zinatoka nje, sisi kama nchi hatujatenga fedha yoyote

ya masuala ya UKIMWI. Kuna haja sasa kama Serikali ifike mahali tuanze kutenga fedha za ndani ili tuweze kuwasaidia Watanzania hao wengi na hili ni janga la kila mmoja wetu. Nadhani kama hatujaguswa binafsi tutakuwa tumeguswa kwa ndugu zetu na familia zetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna haja kama Serikali kujipanga na kutenga fedha za ndani ili tuweze kuendelea kudhibiti na kupunguza maambukizi mapya ambayo yanazidi kuongezeka kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali pia kwa kuanzisha huu mfuko wa UKIMWI. Tumeanzisha huu Mfuko na tukatenga fedha bilioni 5.5 kwa mwaka wa fedha 2016/2017, lakini mpaka dakika hii tunayoongea hakuna fedha yoyote ambayo imekwenda. Sasa hawa watu watafanyaje kazi bila kuwa na fedha. Kwa hiyo naona kuna shida na kuna umuhimu sana wa kuliangalia hili ili tuweze kusaidia Watanzania wengi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee tena kidogo kuhusu suala la elimu. *Research* nyingi ambazo zimefanyika, zinaonyesha kuna uhusiano mkubwa sana kati ya sayansi na maendeleo. Leo hii tunavyoongea, si maneno yangu hata ni juzi tu Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamini Wiliam Mkapa amesema elimu yetu inaporomoka; na huu ni ukweli usiopingika. Tunahitaji mjadala mkubwa kama Taifa, tuweze kukaa na kutengeneza mfumo wa elimu.

Mheshimiwa Spika, nia na madhumuni ya nchi yetu ni kutengeneza Tanzania ya viwanda. Hata hivyo, hatuwezi kupata viwanda bila kuwa na wataalam, bila kuwa na Watanzania wenye uelewa mzuri wa kuweza kutimiza azma hii nzuri ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimniwa Spika, hali ya Walimu wetu sasa hivi ni mbaya, *motivation* ni zero. Wanafanya kazi kwa kwa sababu hawana *options* nyingine, lakini kiuhalisia wanaenda hawana wanachokifanya kwa sababu maslahi hayapo, maslahi yao bado ni duni, wana madai yao ambayo hayajalipwa kwa

muda mrefu. Kwa hiyo ifike mahali sasa kama nchi tutengeneze mfumo mzuri ili kuweza kuwa-*motivate* hawa watu kwa vile hawa ndio wanaotufundishia watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa nia yake nzuri kabisa ya kuifanya elimu bure, ni kweli elimu bure imepatikana na leo hii tunavyoongea watoto wengi sana wameenda kwenye shule zetu. Hata hivyo wingi wa watoto hao pia umekuwa ni tatizo. Chumba kimoja kinakuwa na watoto zaidi ya mia mbili. Katika hali ya kawaida watoto hawa hawawezi kuelewa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, tuna upungufu mkubwa wa madarasa, tuna upungufu mkubwa wa Walimu wa *primary*, tuna upungufu mkubwa wa Walimu wa sayansi. Kwa hiyo Waziri wa Elimu atakapokuja kutujibu hapa atueleze kuna mkakati gani wa Serikali wa kuweza kuyabadilisha haya mambo ili tuweze kuwa na elimu bora.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia uwanja wetu wa ndege wa Mkoa wa Mwanza. Wote mnafahamu Mwanza ndilo Jiji la pili kutoka Dar es Salaam, lakini uwanja wetu wa ndege sehemu yetu ya kusubiria abiria kwa kweli inasikitisha, siyo hadhi ya Mkoa wa Mwanza. Naomba tuje tupate mkakati wa Serikali ni lini sasa uwanja huu utarekebishwa na tutatengenezewa kiwanja ambacho kitakuwa na hadhi ya Jiji la pili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna lingine nataka kuzungumzia kuhusu masuala ya nishati ya mkaa. Wote tunafahamu zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania wanatumia mkaa majumbani kwao...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kemilembe

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kemilembe. Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Niungane na Waheshimiwa wa Bungeni na Watanzania wote kumshukuru Mungu kwa kukupa afya njema, tunaomba aendelee kukutetea na kukupigania katika majukumu yako.

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana hiyo kauli ya Serikali ambayo imetolewa leo hapa Bungeni asubuhi kwa ajili ya kuwarejesha watumishi wa umma ambao waliondolewa kinyama kwenye kazi zao, kwa kweli nashukuru sana, tumerudisha imani na matumaini kwa wale watendaji.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi Serikali ilikuja na mkakati kuhakikisha kwamba watoto wote wa Kitanzania wanakaa kwenye madawati na ikawezekana. Hata hivyo, hivi tunavyoongea watoto wengi wa Tanzania kutokana na idadi kuwa wengi, wengi wao wanakaa nje, jua linawapiga, mvua yao, jua lao.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali, kwa mpango ule ule iliyokuja nao 2016/2017 watoto wakaweza kukaa kwenye madawati wote, tunaomba Serikali ije na mkakati maalum kuhakikisha watoto wote wanakaa kwenye madarasa. Katika wilaya zote hakuna sehemu ambapo madarasa yanatosha na kiukweli mtoto anayesoma nje hata ufaulu unakuwa ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la vyakula mashuleni. Kutokana na tamko lililotolewa na Serikali kwamba elimu ni bure wazazi na walezi wameona kwamba hata jukumu la vyakula shuleni ni jukumu la Serikali, kwa hiyo watoto wengi sasa hivi hawali shuleni na mtoto ambaye ana njaa hafundishiki. Tunaiomba Serikali itoe ufafanuzi mzuri kwenye shule namna gani wazazi wahakikishe watoto wanakula shuleni.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba tumepanda kielimu kwa maeneo mengi *particularly* kwenye Wilaya yangu ya Kaliua tumepanda vizuri sana na najua tumechangiwa na Walimu lakini pia watoto kula mashuleni na *speed* ya viongozi kufanya kazi; lakini sasa hivi wameacha kula tumeona *trend* yao imeanza kushuka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba Serikali itoe ufafanuzi mzuri namna gani watoto waanze kula shuleni tukizingatia wengi wao wanatoka nyumbani hawajala mpaka jioni wana njaa, kwa hiyo hawawezi kufaulu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la mifugo. Nchi yetu ni nchi ya pili kuwa na mifugo mingi Afrika, lakini ukiangalia pato la Taifa ambalo linaletwa na sekta ya mifugo bado ni dogo sana. Tatizo ni kwamba pamoja na kuwa tunaongoza kwa kuwa na mifugo mingi, lakini mifugo yetu haina tija kwa sababu hakuna maeneo yanayopangwa popote kwenye mikoa wala wilaya kwa ajili ya malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengine mifugo inaonekana kama ni changamoto, wanaonekana wanazurura na kila siku wanakamatwa na wanapigwa risasi huko kwenye hifadhi. Hatujaweza kama Watanzania kutumia rasilimali ya mifugo kama uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali lazima kwenye bajeti hii tuje na mpango mkakati namna gani kila mkoa na wilaya ambao wanaendeleza mifugo watenge maeneo kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, hakuna malisho, wakati wa mvua nyingi malisho yanajaa, ikiondoka mvua mifugo yote inateketea, kwa hiyo Mfugaji anafuga wakati wa mvua wakati wa ukame mifugo yote imepotea. Tunaiomba Serikali ije na mpango wakati wa mvua tuwe na utaratibu wa kuvuna majani tutengeneze *hay*, tutengeneze *silage* tutunze vyakula ili tufuge kwa tija.

Mheshimiwa Spika, lingine tuwe na viwanda. Tulikuwa na viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo. Tulikuwa na *Tanganyika Packers* leo hamna. Ni kweli sasa hivi tunajitahidi kuwa na machinjio ya kisasa, lakini hatuna viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri kwenye mifugo kila kitu ni mali. Kwato, ngozi, nyama, mifupa, kila kitu ni mali. Tukiweza kutumia vizuri sekta ya mifugo tutaweza kuhakikisha kwamba inaingiza pato zuri kwa Taifa letu na tukaweza kufanya wafugaji wakawa ni watu ambao wana tija siyo huku wananyanyaswa kila siku kwa sababu Serikali haijaweza kuweka mfumo mzuri wa mifugo kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Mfuko wa Wanawake na uwezeshaji wa wanawake wa vijana. Tumeiona hapa Serikali imetenga fedha milioni mia saba themanini na tatu kwa ajili ya vijana ambapo vijana 840 kutoka halmashauri mbalimbali wamenufaika. Vijana 840 ni kijiji kimoja au viwili. Leo tuna vijana wangapi Tanzania, tuna wilaya ngapi, tuna kata ngapi, tuna vijiji vingapi? Kuja na vijana 840 mimi nashangaa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, fedha zinazotengwa kwenye halmashauri ni kidogo sana. Leo Kaliua tumetenga zaidi ya milioni mia mbili hamsini, vijana wenyewe wamekuja na vikundi hamsini, hatukuweza kuwapa wote tumewapa vikundi 15. Wanawake wamekuja na vikundi 56 tumewapa vikundi 30 na wanaomba milioni kumi unawapa milioni mbili, haitoshi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatenga lakini kwa kweli kama hatujajizatiti vizuri Serikali hatuwezi kusaidia vijana wakaweza kujiajiri, hatuwezi kusaidia wanawake wakaweza kujiajiri kwa sababu fedha tunayotenga ni kidogo. Halmashauri zetu tunafahamu uwezo wake, hawana uwezo wa kuweza kusaidia vikundi vyote vinavyoundwa. Kwa hiyo naiomba Serikali, lazima itenge fedha ya kutosha ili wanawake wawezeshwe, vijana wawezeshwe ili nchi yetu

iondokane na kundi kubwa ambalo linakosa ajira na waweze kuendeleza familia zao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la kilimo; nazungumzia kidogo kwa sababu nitazungumzia kwenye sekta ijayo. Tuna shida kubwa Taifa letu, hatujaweza kuwa na mizani ya kisasa kwenye manunuzi ya mazao, tumelia Bungeni na mimi binafsi nimeongea sana hapa. Leo bado wakulima wanakwenda kulaliwa kule vijijini, wakulima wanakwenda kununuliwa mazao yao bila mizani ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, vile vile leo lumbesa inaendelea, pia kuna ndoo za *Mozambique,* mkulima analima kwa shida, anavuna kwa shida hata kwenda kuuza anaibiwa. Naiomba Serikali kwa nini tunashindwa kusimamia mizani ya kisasa kwa ajili ya kununua mazao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali inaruhusu lumbesa mpaka hivi leo dunia ya leo, kwa nini Serikali inaruhusu *Mozambique* ndoo moja inachukua mpaka galoni saba, kwa nini inaruhusu? Hatuwezi kuwa na nchi ya viwanda bila kuwa na kilimo chenye tija. Pia tunahitaji wakulima wanufaike na wanachokilima, tunaiomba Serikali ije na mpango, ituambie kwa nini tumekubali wakulima waendelee kuibiwa wakati wakulima hao hao tunawategemea waendeleze Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni maji; katika Wilaya ya Kaliua bado hatuna mpango mkakati wa kupata maji. Mpango wa Ziwa Victoria kutoa maji kutoka Mto Malagarasi ni mpango wa muda mrefu. Leo ni mwaka wa tano bado mpango huu uko kwenye upembuzi yakinifu. Naiomba Serikali kwenye mpango wa mwaka huu ituletee mpango wa muda mfupi kuwatua wanawake wa Kaliua ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, leo mvua zinanyesha ukienda Kaliua akinamama angalau wanatulia, watoto wanaenda shule, njoo mwezi Agosti ni hatari. Kwa hiyo naiomba sana

Serikali ije na mpango huu mwaka huu tuhakikishe kwamba tunapata maji wanawake wa Kaliua, watoto waende shule kwa wakati na tuondokane na shida.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Maji Victoria haufiki Kaliua wala Urambo, kwa hiyo mpango pekee wa kuwapatia wana Kaliua maji ni kutoka Mto Malagarasi lakini mpango huu unaenda taratibu sana na fedha inayopangwa pale ni ndogo haitoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni afya; Kaliua tunaishukuru Serikali imetutengea fedha kwa ajili ya hospitali yetu ambayo tunategemea kujenga Kaliua, lakini pia Kaliua mpango wetu wa mwaka huu ni kuwa na vituo vya afya, tumeongeza vituo vya afya vinne, viwili Ulyankulu, viwili Kaliua, Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, wananchi sasa hivi wanacheka kwa *speed* kubwa Mheshimiwa Rais alivyofika Kaliua alitoa milioni kumi kwa ajili ya kituo cha Kaliua Usinge ambapo wengi wao wanatibiwa kule Nguruka.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iongeze nguvu kwenye kituo cha Usinge ili wananchi ambao wanatibiwa Nguruka waweze kutibiwa pale kwenye kituo cha Usinge iongeze nguvu ya Rais. Mfuko wa Jimbo tumeongeza, wananchi wanachanga sana kila siku, Rais ameweka nguvu tunaomba na Serikali pia itusaidie mwaka huu tuhakikishe kwamba kituo kile kinakamilika ili wananchi wa Kaliua waweze kupata huduma za afya kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie hata hapa Dodoma. Benjamin Mkapa wanafanya kazi nzuri sana ya kuokoa wananchi na pia Wabunge wenyewe, lakini Madaktari hakuna. Hivi sasa ninavyoongea kuna Mbunge amelazwa pale...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sakaya nakushukuru sana muda wako umeisha. Sasa Mheshimiwa Saada Mkuya atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho mchana wa leo, tafadhali Mheshimiwa Saada.

**MHE. SAADA S. MKUYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kupata hii nafasi. Kwanza lazima tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kukupa afya njema na tumekuwa pamoja leo hapa, kwa kweli kama haupo huwa tuna-*miss* kule kutokukuwepo kwako, kwa hivyo lazima tunamshukuru Mwenyezi Mungu *Alhamdulillah rabbil-aalamina,* Mwenyezi Mungu aendelee kukupa afya njema.

Mheshimiwa Spika, la pili vile vile nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini vile vile pamoja Mawaziri Dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na Manaibu wake wanafanya kazi nzuri sana sana na wanahitaji pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina hoja nyingi, ni chache. Kwanza nashukuru kwamba hotuba yetu hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imelizingatia vile vile suala la Muungano, lakini kwa uchache wake imeeleza sana ni kwa jinsi gani hizi *activity* za kutafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali za Muungano wetu. Tunashukuru kwa ku-*note* hiyo, lakini nadhani itakuwa busara zaidi tukiendelea mbele ku-*note* vile vile *achievement* ambazo zimepatikana katika Muungano wetu huu ambao kesho kutwa tu tunatimiza miaka 54. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wazee wetu walipokuwa wanaunga, Mzee wetu Karume pamoja na Mwalimu Nyerere waliungana wakijua wanaungana na kila mmoja alikuwa anajua wanaungana katika *context* ipi. Wakati tunaungana Zanzibar ilikuwa ndogo hata leo wakazi wake nadhani kwa takwimu labda tunaweza kuwa tumefika kama milioni moja na laki tano ni kidogo ukilinganisha na wakati huo ilipokuwa Tanganyika hata leo Tanzania zaidi ya watu milioni hamsini,

lakini ilikubalika kwa *spirit* ya kuwa Muungano wetu utakuwa na *mutual benefit* katika maeneo ambayo tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na mambo mengi ambayo yalikuwa yamezungumzwa hapa na nakuomba sana Mheshimiwa Spika, hili ni Bunge ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ikiwa Zanzibar haimo hili haliwezi kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Neno la Jamhuri ama jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatokana na uwepo wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita kulitoka mijadala mingi sana hapa na mjadala ambao unazungumzwa na anayezungumza ni mwana CCM anavyoi-*portray* Zanzibar *as if* Zanzibar hakuna mamlaka. Sasa naomba leo kupitia Bunge lako Tukufu tunaomba hizi *statements* za kuidogosha *statements* za kuidhalilisha Zanzibar ziishe. Lazima tu-*recognize* Zanzibar ina Serikali inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein, Zanzibar kuna chombo cha kutunga sheria ambacho ni Baraza la Wawakilishi, lakini Zanzibar kuna Mahakama.

Mheshimiwa Spika, unapozungumza kwamba Zanzibar ama Kiwanda cha Mahonda ambacho kinazalisha sukari isiingie kwa sababu si sukari inayozalishwa Mahonda nadhani kuna *mis-conception* kubwa sana hapa. Nitaomba sana Waheshimiwa Wabunge tunaposimama ni lazima tuwe tuna takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana *theory* zote katika dunia hii za uchumi, *theory* zote zinasisitiza kuhusu masuala ya *production*, kwa sababu ndiyo yanayojenga *long term growth*. Sasa vile vile kwa upande wa Zanzibar ilipokuja sera ama ilipokuja hoja ya viwanda; uchumi wa viwanda ni uchumi wa viwanda kwa Tanzania nzima; na Zanzibar nayo ikajitutumua ikasema na sisi tuna kiwanda.

Mheshimiwa Spika, sasa kupitia Bunge lako vile vile naomba Waheshimiwa Mawaziri namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tunamshukuru kwa ziara yake aliyoifanya, lakini

nadhani itakuwa busara zaidi akifanya *special visit* kwa ajili ya ku-*visit* kile Kiwanda cha Sukari Mahonda. Hatukatai walanguzi wapo na walanguzi si peke yao wanatoka Zanzibar hao wanaokwepa kodi wako kila sehemu na *Alhamdulillah* Serikali zote mbili zinajitahidi katika kupambana nao.

Mheshimiwa Spika, nami naungana na Waheshimiwa wenzangu kwamba hawa watu wasiachiwe, lakini ukianza kuitengeneza Zanzibar *as if* wale ambao wanakwepa kodi, wale ambao wanakuja na majahazi, wale wanaotembea ni kwamba ndio Zanzibar na ndiyo *character* ya Wazanzibari, nadhani hili siyo sahihi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi biashara zipo tunafanya, mimi nadhani katika Muungano wetu hakukuwa na kikwazo hiki cha *Inter-trade* tunafanya biashara. Kule Zanzibar kuna viwanda vya maji, lakini vile vile vina-*compete* na viwanda utakuta Kilimanjaro ipo Zanzibar imejaa. Kwa hiyo sisi hatuku-*withdraw* ipo.

Mheshimiwa Spika, utakuta maji mengi ambayo yanazalishwa Dasani yote yapo na biashara inakwenda, *why this so special to* sukari? Bidhaa zipo mbalimbali na nadhani *statement* zinapotoka namna kama hizi, hawa ni watu ambao hawautakii mema huu Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu Muungano wetu tunauhitaji sote, wazee wetu walipoungana wameungana kwa *spirit* ya umoja, lazima sisi tuwe wamoja. Leo unaposimama ukaizungumza Zanzibar huwezi kusimama ukaizungumza Kenya au Burundi namna kama ile. Unapomzungumza ndugu yako kwa maneno ambayo si ya kweli huwezi hata kumwambia mtu mwingine yuko mbali; hili siyo sahihi wenzangu.

Mheshimiwa Spika, ubaya wa mambo tunaozungumza wengine wengi ni wana CCM ambao hata Zanzibar chama kinachoongoza ni Chama cha Mapinduzi.

Tuna Serikali ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi. Sasa unapoongea, sasa hivi nimemsikia kuna Mheshimiwa anasema wafanyabiashara kwa sababu ya sheria kali wamehamia Zanzibar, *do you know* Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, tukizungumza Zanzibar maana yake ni kwamba sisi Waheshimiwa tumekwenda asubuhi jioni tumerudi. Kuna sheria zake, sheria zipo na Serikali inajitahidi, changamoto hazikosi na ziko kila sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lililopita tumeambiwa, kuna Mheshimiwa alisimama hapa anasema Zanzibar haijawahi kukamata hata kilo moja ya *Cocaine*, lilizungumzwa ndani ya Bunge hili. Ukiniambia hivyo unadharau mamlaka, unadharau Serikali, unadharau jitihada ambazo zinafanyika. Hawa watu kila siku wanakamatwa na hizi juhudi zinafanyika katika pande mbili zote.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa Mawaziri wanakutana, Mawaziri hawa wanazungumza na wanakuwa wana jitihada zao wenyewe wanazungumza. Sawa changamoto zinatokea tunakubali, lakini si katika *context* hii ambayo inazungumzwa, lazima tuheshimu.

Mheshimiwa Spika, *trust me,* Zanzibar ikiwa inazungumzwa kiasi kama hiki sisi Wabunge ambao tunatoka Zanzibar tunajiona humu ndani kama *second class MP's which is not fair*. Sisi ni Wabunge kama Wabunge wengine, unapoizungumza Zanzibar na sisi tunapata uchungu kwa sababu kinachozungumzwa si sahihi.

Mheshimiwa Spika, tunawaomba haya mambo ya kukaa ukaanza kudharau mamlaka nyingine ambayo zimo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunaomba sana, tunapata tabu sana kule nyumbani, wanatushangaa sana wenzetu, *what are you doing there?* Kwa sababu kinachozungumzwa kinakuwa hakina *fact*.

Mheshimiwa Spika, tunaomba jamani tuheshimiane, tuwe vizuri kwa sababu tuna *spirit* moja katika chombo cha

dola ambacho tunakutana na tuna-*converge* hasa kwenye *context* ya Muungano ni Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakuwa wamoja sote tunasimama kwa pamoja tofauti zetu za kiitikadi zipo, lakini *when it comes to United Republic of Tanzania* hiki ndicho chombo ambacho kina-*portrait*.

Mheshimiwa Spika, sasa...

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa taarifa, Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Naomba kumpa taarifa Mheshimiwa anayezungumza. Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI ndiye aliyezungumza kwamba dawa za kulevya zimedhibitiwa Bara, lakini Zanzibar bado hazijadhibitiwa sawa sawa. Kwa hiyo tunataka akiwa anazungumza mzungumzaji atambue kwamba tunajadili Taarifa ya Kamati.

**SPIKA:** Ni taarifa tu hiyo, Mheshimiwa Saada.

**MHE. SAADA S. MKUYA:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana ndugu yangu, nilichokizungumza hapa kilichokuwa kimezungumzwa Bunge lililopita Zanzibar hakujawahi kukamatwa hata kilo moja ya unga. Kwa hivyo ninapozungumza vilevile awe ananisikiliza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *context* hii ya ujenzi wa viwanda inasaidia sana katika ujenzi ...

**MHE. KHATIB S. HAJI:** Mheshimiwa Spika taarifa.

**SPIKA:** Taarifa kutoka upande gani? Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB S. HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeongea kwamba pamoja na taarifa zilizopo kwamba Zanzibar haijawahi kukamata

madawa ya kulevya, napenda nimpe taarifa kwamba kuna washtakiwa ambao kesi zao hazijaisha *container* la madawa ya kulevya kutoka Bara lilikamatwa katika Bandari ya Zanzibar hadi leo kesi bado iko Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mkuya apokee taarifa hii.

**MHE. SAADA S. MKUYA:** Mheshimiwa Spika, naipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na hayo hizi ni katika changamoto za maendeleo ya nchi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saada ahsante sana, muda. *(Makofi)*

**MHE. SAADA S. MKUYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nawashukuruni sana, jioni uchangiaji wetu utaendelea majina yale ambayo ninayo kutoka CHADEMA wote mtachangia na CCM pia wote, *CUF* tumeshapunguza karibu wote, lakini tutaangalia kama kutakuwa na nafasi kidogo.

Tangazo ni moja tu hapa linatoka kwa Mheshimiwa Kuchauka, anaomba Wabunge wote wa kutoka Mkoa wa Mtwara mkutane pale Jengo la Utawala kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Kuchauka anawaomba Wabunge wa Mkoa wa Mtwara mkutane pale Jengo la Utawala kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Baada ya hayo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni. Ahsanteni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Azzan Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Tukae. Tunaendelea na majadiliano na tunaanza na Mheshimiwa Kiteto Koshuma ajiandae Mheshimiwa Ignas Malocha, nafikiri mmekubaliana dakika tano, tano.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa muda ni mchache nitakuwa na mambo machache sana ya kuchangia siku ya leo, lakini namshukuru Mungu kwa kuweza kunipa afya njema ili niweze kuendelea kutoa michango yangu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, naomba nianze kwa kuchangia suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi. Katika ukurasa wa 14 wa hotuba ya Waziri Mkuu ameelezea ni namna gani Serikali imejitahidi kutoa mikopo ile ya asilimia 10 ya Halmashauri kwa akinamama, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo machache sana ya kuongelea juu ya suala hii la hii asilimia 10 ambayo inatolewa katika Halmashauri. Halmashauri nyingi sana hapa nchini hazitoi hii asilimia 10 kwa akinamama, vijana pamoja pamoja na watu wenye ulemavu ipasavyo. Hata hivyo, hatujaona Serikali ikichukua hatua yoyote juu ya Halmashauri zile ambazo hazitoi vizuri au hazitengi hii asilimia 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika ukurasa wa 14 wa hotuba ya Waziri Mkuu ameeleza pale kwamba, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.4 kwa vikundi 5,169 katika Halmashauri 153. Swali la kujiuliza hapa katika taarifa hii, tuna Halmashauri takribani 183, Halmashauri ambazo zimetoa mikopo ni 153, je, hizo Halmashauri zingine ambazo hazijatoa mkopo zimechukuliwa hatua gani mpaka kufikia leo hii? Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge hili wamekuwa

wakizungumza sana kwamba Halmashauri ambazo hazitoi mikopo zipewe adhabu au kuchukuliwa hatua za kinidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati tunajadili bajeti tuliona Halmashauri ya Ukerewe pamoja na Halmashauri ya Magu katika Mkoa wa Mwanza, kwa masikitiko makubwa sana Halmashauri hizo hazikutenga kabisa fedha, lakini hatujaona hatua yoyote ile ikichukuliwa. Kwa maana hiyo watu hawa wamekuwa wakiona kwamba hizo pesa wana hiari ya kutoa au kutokutoa na inaonekana kwamba ni sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa stahili hii hatuwezi kuona maendeleo yakiwepo katika Mkoa wa Mwanza. Ukiangalia wanawake wa Mkoa wa Mwanza wanajitahidi sana kujishughulisha na shughuli mbalimbali na wanatarajia kabisa kwamba Halmashauri ziweze kuwasaidia kuwapa hii pesa ya mkopo ili waweze kufanya shughuli zao ndogo ndogo, lakini sasa Wakurugenzi wamekuwa wakifanya sijui niseme ni ukaidi au vipi mpaka hawatoi pesa hizo. Hivyo, naitaka Serikali iweze kuwachukua hatua Wakurugenzi wote ambao hawatengi pesa hizi za asilimia kumi kwa vijana, wanawake pamoja na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, naomba nitoe ushauri mdogo. Fedha hizi ambazo zimekuwa zikitolewa zinatolewa kidogo. Unakuta Halmashauri *let's say* inatoa shilingi milioni 200 kwa vikundi vingi, unakuta mwisho wa siku vikundi vinapewa shilingi laki mbili mbili, mwisho wa siku hii pesa ambayo wanapewa inakuwa haileti tija katika kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoshauri ni jambo moja. Kwa kuwa sasa hivi Serikali ya Awamu ya Tano imekuja na sera ya viwanda basi tuiunge mkono kwamba hizi pesa badala ya hawa akinamama kupewa *cash in hand* wakakopeshwa na mwisho wake wanashindwa kuzilipa

waweze kupatiwa kwa *style* ya kwamba wanapewa labda mashine kwa ajili ya kuweza kutumia kutengeneza vitu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Mkoa wangu wa Mwanza akinamama wengi wanajishughulisha na suala la kusindika bidhaa mbalimbali ambazo zinatumika majumbani kama vile viungo vya pilau, karanga, nyanya, *tomato paste* na *pineapple* ambayo inakuja kuwa *pineapple sauce.* Kwa hiyo, kuna vitu vingi sana ambavyo wanajishughulisha navyo. Kwa maana hiyo naomba Serikali iwasaidie akinamama hawa badala ya kuwapa pesa basi waweze kuwasaidia mashine ambazo zinaweza zikasaidia kuweza kuleta tija katika utengenezaji wa bidhaa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala zuri ambalo linaweza likafanyika. Katika Mkoa wa Mwanza akinamama nimebahatika kukaa nao kikao na wanahitaji wao vifungashio ili waweze kufungasha hizi bidhaa ndogo ndogo ambazo wanatengeneza. Kwa hiyo, naishauri Serikali Tanzania nzima na Halmashauri zote, fedha hizi badala ya kuwapatia *cash* kwa mkopo wawasaidie kwamba hawa akinamama ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, unga mkono hoja.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Malocha ajiandae Mheshimiwa Augustino Masele.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa niungane na wenzangu kushukuru Serikali kwa kauli ambayo imetoa

asubuhi ya kuwarejesha Watendaji wetu wa Vijiji wa darasa la saba. Ilikuwa ni huzuni kubwa sasa imekuwa furaha, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hotuba ya Waziri Mkuu katika kipengele kinachohusiana na kilimo. Ukiangalia ukurasa wa 27 katika hotuba ya Waziri Mkuu ameelezea kwa kifupi juu ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na biashara. Katika maelezo yake ameelezea ufanisi mkubwa uliokuwa umetokea katika msimu wa 2016/2017 na 2017/2018 kwamba wananchi walizalisha chakula yapata tani milioni 15.9 na mahitaji ya chakula yalikuwa ni milioni 13.3, kwa maana ya ziada ilikuwa ni tani milioni 2.6 na ziada nyingine ambayo ilinunuliwa na *NFRA* ni tani 26. Ukifanya hesabu unakuta karibu tani milioni 5.5 haikununuliwa na kiwango hicho ndiyo kilibaki kwa wananchi wamehangaika nacho na hawakujua wauze wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linahuzunisha sana katika nchi yetu. Wakulima wa mahindi wamepata shida sana katika jambo hili, wanazalisha kwa jitihada zao na kwa nguvu kubwa lakini wanakosa wapi wauze mazao hayo. Hadi sasa kilio hicho bado kinaendelea, wananchi wana hali mbaya sana hasa Mkoa wangu wa Rukwa ukienda karibu Wilaya zote, ukienda kwenye magulio yale utafikiri watu wana msiba kwa sababu mazao yao wamekosa kwa kuuza na maendeleo yamesimama. Kama mtu alianza nyumba 2015 imesimama vilevile haiendelei. Sasa tunajiuliza hii hali itaendelea mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ya kitabu hiki cha Waziri Mkuu hakuna mahali ambapo wameeleza ni namna gani watatatua tatizo hili. Kwa hiyo, wameacha wakulima kwenye *dilemma,* sasa sijui wakulima wa mahindi waache kulima au ni kitu gani kinatokea. Hali hii ni mbaya sana, uchumi umesimama na wananchi wamefilisika, je, Serikali inakubali hali hii iendelee na hata huu uchumi wa viwanda tunaouzungumzia, vitakuwa na faida gani kama mwananchi hana uchumi wa kununua bidhaa ndani ya kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nizungumzie jambo labda Waziri wa Kilimo atakuja kutuelezea ni namna gani mwaka huu amepanga mipango mizuri ya kuwezesha wananchi kuuza mahindi yao ikiwa ni pamoja na kufungua mipaka. Kwa sababu kuacha hali hii kuendelea sioni sababu ya wananchi kuendelea kulima mahindi, watasimama na ndiyo maana hata unaona hata mwaka huu uzalishaji umepungua wameshindwa kununua mbolea kwa sababu hawana pesa, wamelima kienyeji, wamepanda mbegu ambayo sio bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizunguka katika Wilaya zetu zote za Mkoa wa Rukwa mazao yapo chini sana hayajastawi, hii ni kutokana na wananchi kukosa fedha za kununulia pembejeo kwa sababu mahindi waliyozalisha hayajanunuliwa na mengine yameoza. Kwa hiyo, jambo hili ni la kuangaliwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka nizungumzie suala la *TARURA.* Kwanza tunapoingeza Serikali, tuna imani chombo hiki kimeanza kufanya kazi nzuri. Tunachoomba chombo hiki kinapaswa kipewe fedha za kutosha, kisipopewa fedha za kutosha itakuwa ni sawa na Halmashauri zetu zilivyokuwa zinahangaika na barabara hizi zinashindwa kutengenezwa kwa sababu zilikuwa zilikuwa zinapewa fedha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa pesa hizi angalieni Halmashauri ambazo barabara zake zina changamoto. Kwa mfano ukichukulia Halmashauri yangu ya Wilaya ya Sumbawanga jiografia yake ni mbaya na barabara ni mbaya, hazipitiki muda mwingi kwa sababu jiografia yake imekaa utata, barabara zinaunganishwa na milima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia barabara ya Mawezunzi – Msia, Miangalua - Chombe – Kipeta, ukija huku Miangalua kuelekea Laela ukizunguka kule Kwakifuti barabara ni mbaya, daraja la Kaengesa limeshabomoka ambalo lilijengwa na Wamishionari sasa hivi halipo, linahitaji pesa nyingi. Barabara ya Kaengesa – Myunga

inahitaji pesa nyingi, kivuko cha pale Laela kwenda kwenye hospitali kinahitaji pesa nyingi. Kwa hiyo, tunaomba *TARURA* waweze kuwezeshwa kupata pesa nyingi ili waweze kumudu kutengeneza barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeona Serikali inafanya jitihada ya kutengeneza *standard gauge,* tunashukuru...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masele ajiandae Mheshimiwa Hamad Bobali.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi ili kusudi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Waziri Mkuu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nipende tu kuwapa pole wananchi wangu wa Kata za Ngemo na Ushirika waliopata tatizo la kuharibikiwa nyumba zao kutokana na tetemeko lililotokea tarehe 25 Machi, 2018. Kwa maana hiyo, nipende tu kuishauri na kuiomba Serikali iendelee na utaratibu ule uliotajwa katika ukurasa wa 69 katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inayohusiana na uratibu wa maafa, kwa maana ya kwamba mabadiliko ya tabianchi katika nchi yetu yamekuwa yakileta madhara kwa maana ya kwamba mpaka sasa tumejikuta mambo ambayo yalikuwa hayapatikani katika nchi yetu sasa yameanza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona tetemeko la ardhi lilitokea Kagera na sasa katika Wilaya ya Mbogwe tumepata tatizo hilo tarehe 25 usiku na kwa maana hiyo inaonesha kwamba huenda majanga kama haya yakaendelea kutokea. Kwa hiyo, naishauri Serikali iendelee kujiimarisha zaidi ili kwamba mambo haya yatakavyojitokeza katika kiwango ambacho siyo cha kawaida tuweze kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu sasa kwa kuanza kuipongeza kwanza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Pombe Joseph Magufuli akisaidiwa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Suluhu Hassan pamoja na Waziri wetu Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Serikali hii inafanya kazi nzuri, tuwe wakweli na tuache habari ya ushabiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za Serikali hii ni zile ambazo zimekuwa zikipigiwa kelele ndani ya Bunge hili, tumeiomba sana Serikali ijenge reli kwa kiwango cha *Standard Gauge,* kazi hii imefanywa, upanuzi wa Bandari ya Dar es salaam Serikali inaendelea kufanya. Tumezungumzia habari ya Shirika la Ndege, watu wote humu tumekuwa tukipiga kelele, Serikali imesikia na ndege hizo imeanza kuzileta, lakini sasa naona tena watu wanaanza kugeuka kuwa vinyonga. Tunayoyazungumza humu yanapoanza kutekelezwa tunageuka tena tunaona kwamba Serikali haifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali iendelee na mpango wake wa kuwaletea maendeleo Watanzania. Watanzania hawa wanapenda sana kuona kwamba nchi yao ambayo imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi, ni nchi nzuri na ina kila kitu. Kilichokuwa kinakosekana ni namna gani ambavyo tumejipanga kuweza kuzitumia rasilimali tulizonazo hapa nchini kuweza kujikomboa kiuchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imekuwa ni Serikali sikivu, tunaona namna ambavyo Serikali inaendelea kusambaza umeme kila mahali. *REA* Awamu ya Tatu inaendelea vizuri, hata katika Wilaya ya Mbogwe kazi zinaendelea na wananchi wanaona kwa macho yao na siyo tu Mbogwe ni Tanzania nzima miradi hii inaendelea kufanyiwa kazi na watu wanaona. Wakati mwingine niseme tu kwamba watu wanaamua kufanya ushereheshaji, mtu anaiona kazi lakini anaamua kugeuza na kuanza kubeza. Niiombe Serikali iendelee mbele wala isigeuke nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha niiombe Serikali kwa sababu ni Serikali yetu wote iendelee kuona utaratibu wa namna ya kuzisaidia Wilaya na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa nilimwita Mheshimiwa Hamidu Bobali lakini nafasi za *CUF* zote zimeshatumika asubuhi, kwa hiyo, sasa anaendelea Mheshimiwa Khadija Nassir akimaliza ajiandae Mheshimiwa Ole Meiseyeki.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa vile dakika nilizonazo ni chache naomba sasa niende moja kwa moja kwenye kuelezea hali halisi ya kibishara inayoendelea Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote zilizoungana na visiwa kama Tanganyika ilivyoungana na Visiwa vya Zanzibar hutumia visiwa hivyo kama *strategic center* za kibiashara kutokana na *geographical position* za visiwa. Kwa bahati mbaya sana mpaka sasa Serikali yetu haijaona umuhimu wa kutumia Zanzibar kama *center* ya kibiashara kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miezi michache iliyopita Tanzania Bara ilipatwa na *shortage* ya sukari ambayo kwa taratibu za Serikali ilizozichukua sina mashaka nazo, hatua ambazo Serikali imechukua ku-*solve* tatizo hili pia sina mashaka nazo. Mashaka na malalamiko yangu makubwa kwenye hili ni baadhi ya Watendaji wa Serikali kulichukua hili jambo na kulitekeleza kinyume na maagizo ambayo yametokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ambayo inaendelea sasa kwenye bandari yetu, Wazanzibar au wananchi wetu

hawana ruhusa hata ya kuingiza sukari kilo mbili kwa ajili ya matumizi yao binafsi. Tatizo hili limekuwa kubwa mpaka sasa wananchi wetu hawawezi kuingiza hata kilo mbili za matumizi yao ya kawaida. Kisa tu tamko lilitoka, kibali hakijatoka na utekelezaji huo umekuwa namna hiyo ambayo naielezea. Kwa masikitiko makubwa sana nathubutu kusema kwamba bado sijaona faida ya kibiashara ndani ya Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuelezea malalamiko yangu, naomba sasa nielezee juu ya Wabunge ambao wamebeba agenda ya kuibeza Zanzibar na Wazanzibari kwa ujumla. Kuna baadhi ya Wabunge humu wamebeba agenda ya kuibeza Zanzibar na Wazanzibari kwa ujumla na wamekwenda mbali mpaka kujiita kwamba wao ndiyo wababe wa Wazanzibari. Niwaambie tu, mbabe wa Wazanzibari ni Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye ndiye Rais wetu na hakuna mbabe zaidi ya huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, naomba sasa nijikite kwenye mchango wangu moja kwa moja na nitaanza kuelezea hali ya kiuchumi nchini. Ukurasa wa nane umeelezea viashiria vya kiuchumi vinaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba, 2017, uchumi ulikua kwa asilimia 6.8. Sina mashaka na maelezo haya na kwa vile hotuba hii haijaonesha ni viashiria gani ambavyo vimepima ukuaji uchumi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuangalie ripoti ya *REPOA* na takwimu ambazo imeonesha. Ripoti ya *REPOA* inaonesha kwamba mwaka 2014 asilimia 22 ya Watanzania walikuwa wanashinda na njaa wakati mwaka 2018 asilimia 27 ya Watanzania wanashinda au kulala na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hii pia imeonesha hali ya ajira nchini. Ripoti hii inaonesha kwamba vijana wa Kitanzania asilimia 43 walikuwa na imani kuwa Serikali itatengeneza ajira wakati mwaka 2018 ni vijana asilimia 31 tu ndiyo wenye imani kuwa Serikali itatengeneza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hii pia inaonesha hali ya ufukara nchini. Kwa mwaka 2014 asilimia 64 ya Watanzania hawakuweza kumudu maisha yao wakati kwa mwaka 2018 ni asilimia 76 ya Watanzania hawakuweza kumudu maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia tuangalie ripoti ya Serikali kupitia Taasisi ya *NBS* ambayo inaonesha hali ya udumavu kwa mwaka 2014 ni asilimia 34.4 ya watoto nchini walikuwa wamedumaa, wakati kwa mwaka 2018 asilimia 34.7 ya watoto nchini wamedumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hiihii pia imeonesha vifo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Khadija. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Ole Meiseyeki, ajiandae Meshimiwa Maryam Msabaha.

Mheshimiwa Meiseyeki upande wa CHADEMA.

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na pumzi na kuwa tena katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape pole viongozi wangu wote wanaopitia changamoto za kisiasa, yote ni mitihani, lakini Mwenyezi Mungu atawavusha salama. Pia nimpe pole Mheshimiwa Spika kwa neema na kwa baraka ambayo pia Mwenyezi Mungu amemjalia na kurudi Tanzania akiwa katika hali ya uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitajielekeza sana kwenye changamoto za Muungano. Nimepitia kitabu cha Waziri Mkuu ukurasa wa 11 bila kukosea, nimeona masuala ya Muungano Mheshimiwa Waziri Mkuu ameorodhesha sehemu chache sana. Ni kitu ambacho hata ukurasa huu ametoka *page* hii ya 11 ameishia hapa, hata hii *page* hapa hakufika akaendelea huku kwenye Serikali kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar bado kuna changamoto kubwa ya kero za Muungano. Nilikuwa nategemea angalau tunakuja humu kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano na sisi tumetokea upande wa pili na tumechaguliwa kwa ajili ya kuja kuwakilisha Zanzibar, tuambiwe ni kero ngapi za Muungano mpaka sasa hivi zilishapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuambiwe hata angalau ile Akaunti ya Pamoja tunaichangia kwa namna gani; Bara wanachangia shilingi ngapi na Zanzibar wanachangia shilingi ngapi ili wananchi wakapata ufahamu na wakajua sasa sisi huku labda hatuchukuliwi chetu kabisa au huku sisi hatutumiki, yakawekwa yale masuala yakawa wazi kabisa, kama ni kutangaza kwenye redio au magazeti ya Serikali ili wananchi wakajua huu Muungano ni wa namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyoungana tunatakiwa tuungane kwa maendeleo na kwa changamoto na zile sekta ambazo ni za Muungano zipewe kipaumbele. Leo tunataka tujue ni Wazanzibari wangapi ambao wameajiriwa kwenye sekta za Muungano, ni Wazanzibari wangapi ambao walikuwa wanakaimu zile nafasi na mpaka sasa hivi wamepata nyadhifa zao kamili, bado kunakuwa na kizungumkuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ikija Ofisi ya Makamu wa Rais pia ile bajeti ambayo inawasilishwa na Serikali haipelekwi kwa wakati muafaka. Sasa hizi kero za Muungano zitatatuliwa wakati gani? Leo tukihoji Akaunti ya Pamoja,

Mheshimiwa Mzee Dkt. Mipango akija hapa Zanzibar inasahaulika. Tuseme sisi Wazanzibari ndio hamtutaki au hatuna haki huku kwenye hili Bunge, mtuambie kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna wimbi la vijana, hawa vijana wengi mlikuwa mnasema ni vijana wa Zanzibar wanaenda kufanya kazi nchi za Uarabuni; Oman na sehemu zingine, lakini pia mpaka vijana wa Tanzania Bara wapo ambao wanafanya kazi Uarabuni. Sasa Serikali imejipanga vipi kusaini mkataba wa kimataifa ili kutambua hawa watumishi wanaofanya kazi nje ya nchi, hasa sehemu za Uarabuni, viwandani na majumbani ili hata zile haki zao waweze kuzidai wanapopata matatizo huko nchi ambazo wanafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie Zanzibar kuhusu masuala ya biashara. Tunatumia bandari ya pamoja lakini hii bandari imekuwa kizungumkuti. Zanzibar unakuta mtu anachukua kimzigo kidogo tu analeta Tanzania Bara, kisiwa kile kinategemea biashara, kinategemea utalii, kinategemea uvuvi, sasa anavyoleta vibiashara vyake kiasi ambacho angalau naye apate kujikimu unakuta analipa kodi mara mbili.

**TAARIFA**

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa dada yangu, Zanzibar jambo la mwanzo kuungana na Tanganyika ni suala la biashara na sasa hali ya kibiashara ya Zanzibar haiwezi ikazunguka bila kutegemea Tanzania Bara. Nimpe taarifa dada yangu aweze kwenda vizuri ili Wazanzibari tukae vizuri na tufanye kazi vizuri, suala la kibiashara na Tanzania Bara lazima liangaliwe kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo taarifa yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napokea taarifa ya kaka yangu na Wazanzibari tutasimama pale ambapo tunasimama tunakuwa kitu kimoja tunaitetea Zanzibar, Zanzibar ina Serikali yake, Zanzibar ina Baraza la Mawaziri, Zanzibar ina Baraza la Wawakilishi na sisi tumetumwa na wananchi kuja kutetea Zanzibar ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, haki za Wazanzibari tunataka zipelekwe kwa wakati muafaka. Ahsante kwa kunipa taarifa. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe na niiombe Serikali ya Muungano iangalie wafanyabiashara wa Zanzibar isiwe inawatoza kodi mara mbilimbili. Kama kodi ilishalipwa nao kama wanakuja huku wapate haki sawa kama wanavyopata haki sawa huku Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie kwenye taasisi kama hii miradi ya *TASAF* ambayo inatolewa Zanzibar, ni kaya ngapi maskini ambazo zimenufaika au hizi pesa zinaishia tu kwenye mifuko ya watu wachache ambao wana uwezo. Hiyo pia tunatakiwa tupate taarifa ya kina na wale wananchi nao wapate taarifa ya kina kama zile fedha kweli zinawafikia walengwa au ndio zinaishia kwenye mikono ya watu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Marais waliopita walithubutu kuiweka Zanzibar vizuri kulikuwa na zile kero wakazipelekapeleka mambo yakaenda. Nimshauri Mheshimiwa Rais na tumwombe naye afuate nyayo za Marais waliopita, aangalie Zanzibar. Kwa sababu hata kama mkikopa nje ni lazima mnaishirikisha Zanzibar, sasa Zanzibar nayo inanufaika vipi na hii mikopo ambayo inakopwa nje? Tuangalie kabisa masuala haya, ambalo ni fungu la Zanzibar lirudi Zanzibar, ambalo ni fungu la Tanzania Bara lirudi Tanzania Bara, hapo tutakwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ajira kwa vijana. Vijana wengi wameingia kwenye matatizo, sasa hivi vijana wanasoma hawana ajira. Serikali imejipanga vipi kuwasomesha vijana ili waweze kujiajiri wenyewe? Kwa sababu tunaona vijana wengi wanaranda na vyeti mpaka vinapauka kwenye mifuko lakini suala la ajira hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kujua Serikali ina mpango gani hasa kwenye sekta ya kilimo vijana wanapata namna ya kujiajiri, wanapata elimu na mitaji. Tumesikia kuna pesa ambazo zilikuwa zinatakiwa zitolewe, shilingi milioni 50; hizi shilingi milioni 50 vijana wa Kitanzania ambao hawana ajira watanufaika vipi na hizi pesa angalau wajiajiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana wana vipaji, Serikali inatumia vipi hivi vipaji vya hawa vijana ili wapate kujiajiri? Tumesikia Tanzania ya Viwanda, kama huyu kijana hujamuandaa bado tutakuwa na vijana wengi maskani na wengi wataishia kwenye mambo ya uhalifu. Tuangalie ni namna gani ya kuwaandaa hawa vijana waende kwenye Tanzania ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye suala la vyama vya siasa. Siasa si ugomvi, siasa siyo uhasama, sisi sote ni wanasiasa na sisi wanasiasa wote ni ndugu. Leo mimi niko CHADEMA, kuna mwingine yuko *CUF,* kuna mwingine yuko CCM, lakini vyama vya siasa visitutenganishe. Tuangalie ni namna gani kila mwanasiasa anapata fursa sawa katika Serikali hii, hasa kwenye suala la mikutano na kutangaza vyama vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama chama cha siasa mitaji yetu ipo kwa wananchi, hawa wananchi tutawatumia vipi kama sisi sera za vyama tumekatazwa kuzitangaza. Hawa wapigakura wetu wataelewa vipi kama sisi chama fulani sera yetu ni hii na sera ya chama hiki ni hii. Kwa hiyo, vyama vyote vitendewe haki, viruhusiwe kufanya mikutano bila kubagua chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Watendaji wa Serikali maana baadhi yao wanashindwa kufanya kazi zao wanamsingizia Mheshimiwa Rais...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Frank Mwakajoka, jiandae Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nianze na suala ambalo limekuwa linazungumzwa sana Bungeni hapa leo, suala linalohusu Muungano wetu kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Inaonesha kabisa kwamba CCM wanataka kuvunja Muungano kwa sababu hawathamini kabisa kazi walizofanya Baba wa Taifa pamoja na Karume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuamini, yapo matamko mabaya yanayotokea hapa kwa ajili ya kubeza Zanzibar kila siku. Watu tunasikia humu lakini hatujawahi kusikia hata siku moja kiongozi mkubwa wa Kiserikali wala Spika wa Bunge hili au Naibu Spika wamekemea jambo hili. Hili jambo ni hatari sana, watu wanalalamika ndani ya Bunge hili na sisi tumeungana kama Watanzania kwa sababu ya nchi mbili; Zanzibar pamoja na Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba suala linalohusiana na Muungano wetu kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ni vizuri tukaheshimiana ndani ya Bunge hili lakini pia tukawaheshimu wananchi wote; wa Tanzania Bara pamoja na wa Tanzania Visiwani. Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anakuja kumalizia hotuba yake tunahitaji kauli ya Serikali, inatoa onyo gani kwenye Bunge hili ili kauli za kubeza upande mwingine zisitokee tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote hapa ni Watanzania, lakini tunahitaji kuheshimiana na kukaa pamoja ili kudumisha Muungano wetu. Hatuwezi kudumisha Muungano kama tutaendelea kuona watu wengine ni bora kuliko watu wengine. Jambo hili kwa kweli si jema na halifurahishi na halipendezi, naomba kila mmoja aweze kumheshimu mwenzake. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia...

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kwamba jambo ambalo analizungumza ni sahihi, kuna Mbunge ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatumia nafasi ya Bunge hili kuikashifu Zanzibar, kuikejeli Zanzibar, kutoa maneno machafu kuhusu Zanzibar. Wazanzibari wamechoka na kauli hizi anazotoa Mbunge huyu, zimekuwa zinakera na zinaudhi Wazanzibari. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Taarifa Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea taarifa hiyo kwa sababu nahitaji zaidi Muungano. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nimeipokea taarifa hii kwa sababu nahitaji sana Muungano. Sisi vyama vya upinzani tunataka Muungano udumu na ndiyo maana tulijaribu kutoa mapendekezo ya Serikali tatu, kwamba kuwe na Serikali tatu na siyo mbili ambazo zipo sasa hivi ambazo hazieleweki zinaleta mkanganyiko; ndicho tulichokizungumza mwanzoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi taarifa mbaya za kubeza Zanzibar ndiyo hizo ukifika huko Zanzibar sasa hivi kwenye Baraza la Wawakilishi pia kumekuwa na tatizo kubwa sana lakini naamini kabisa hata Wabunge ambao wanakuwepo kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watakuwa pia wanalaumiwa na Wazanzibari wenyewe kwamba hawatekelezi shughuli zao kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ni mdogo. Hii ni taarifa ya mwisho baada ya hapo nitakuwa napokea kuhusu utaratibu tu, Mheshimiwa Kangi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kauli ambazo zinaendelea kutolewa humu ndani na kauli nyingine ambazo Mbunge aliyekuwa anachangia ameendelea kuzitoa kwamba humu ndani Wabunge wanaidharau na kuikashifu Zanzibar.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo, ndiyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hizi ambazo zinatolewa kwa jumlajumla ndizo chanzo cha

kupotosha na kusababisha Watanzania waamini kwamba kweli Zanzibar inadharauliwa katika Muungano.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Ndiyo maana hao wanaosema kwamba Zanzibar inakashifiwa humu ndani, Zanzibar inadharauliwa, hawasemi ni mtu gani Bungeni humu ambaye ameidharau Zanzibar au ambaye ameikashifu Zanzibar.

**MBUNGE FULANI:** Keissy, Keissy.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu wachangie...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kangi, Mheshimiwa Frank endelea.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, kaa chini.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, kaa chini.

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, kaa chini, Mheshimiwa Frank endelea, nenda kwenye hoja hapo.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Kanywe sumu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema mficha maradhi, kifo humuumbua. Sisi hatutaki kifo kituumbue na ndiyo maana tunazungumza, tunasema Muungano ni muhimu kuliko kitu chochote. Kama kweli taarifa anayoitoa ndugu yangu Mheshimiwa Lugola, siku zote wanavyoongea hapa kwa nini hataki kuwaambia Wabunge kwamba acheni kuzungumza maneno haya ni mabaya, mmekaa kimya humu mnashangilia mnafikiri ni jambo jema wakati wenzetu wanaumia na wananchi wa Zanzibar hawajisikii vizuri, kwa hiyo lazima tukemee jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kuzungumzia utawala bora. Katika nchi hii sasa utawala bora haupo kabisa. Huwezi kuamini katika nchi hii leo Waziri anaweza kumuagiza Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, tena kamuagiza kwa barua, lakini hawezi kutekeleza. Hii nchi imekuwa nchi ya namna gani, hakuna utawala bora kabisa yaani sasa hivi Mkuu wa Wilaya ana nguvu kuliko Waziri, Mkuu wa Mkoa ana nguvu kuliko Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mji wetu wa Tunduma kuna mgogoro ambao umekaa kwa muda mrefu sana; kuanzia Agosti, 2017 mpaka leo, Waheshimiwa Madiwani hawajakaa vikao kwa sababu ya amri ya Mkuu wa Wilaya. Wakati anakuja kuzungumza hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze, Mkuu wa Wilaya ana mamlaka gani ya kuzuia Baraza la Madiwani katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mmoja anajua ukisoma Ibara ya nane (8) kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utaona uanzishaji wa Serikali za Mitaa, ilikuwa ni kupeleka mamlaka na madaraka kwa wananchi wenyewe na ikaeleza kwamba kutakuwa na vyombo madhubuti ambavyo vitakuwa vinasimamia Serikali za Mitaa katika maeneo yao. Leo Mkuu wa Wilaya anakwenda kuzuia Baraza la Madiwani kwenye Mji wa Tunduma lisifanye kazi, Waziri ameandika barua kwamba Baraza la Madiwani liendelee kukaa, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wamegoma wamesema kwamba haitakiwi wakae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tujue sababu ni nini? Pia tunataka tujue kwa nini Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wanakuwa na mamlaka, wanatumia sheria gani? Waziri Mkuu anajua, Waziri wa TAMISEMI anajua, Waziri wa TAMISEMI ameandika barua mbili, zote akilitaka Baraza la Madiwani likae, lakini Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wanakataa. Leo mnasema kwamba utawala bora upo kwenye nchi yetu? Utawala bora hakuna kwenye nchi yetu na leo Mawaziri wengi hawaheshimiki kwa sababu Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wameshapewa madaraka makubwa kuliko Mawaziri wetu, jambo hili linatusumbua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Wakuu wa Wilaya sasa hivi wanawaweka ndani Waheshimiwa Wabunge, akiamua tu anamweka ndani. Juzi hapa Mheshimiwa Mnyeti alikuwa anamwambia Mbunge wa Kiteto kwani Mbunge ana mapembe kuliko wewe, muweke ndani, ukiwaweka ndani mimi najua kwa kuwapeleka. Hizi ni dharau kubwa na inaonesha jinsi gani nchi yetu imeshindwa kuheshimu utawala bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tena kwamba, tusifikiri tutapata uchumi kama hatutajenga demokrasia ya kweli katika nchi hii. Uchumi ni demokrasia, kama hakutakuwa na maafikiano kati ya Watanzania wote; wa Vyama vya Upinzani pamoja na Serikali iliyoko madarakani tusitegemee kwamba, tunaweza tukapata maendeleo katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni ya kwetu wote na si nchi ya mtu mmoja na si nchi ya chama kimoja, wote tuko sawa tunahitaji kupata haki sawa lakini tunashangaa leo Chama cha Mapinduzi wameonekana wao wana haki zaidi kuliko vyama vingine, wana haki zaidi kuliko mtu mwingine yeyote, kitu ambacho tunakuwa tunakosea sana. Tujenge demokrasia ya kweli katika Taifa hili, uchumi wa kweli utajengwa katika Taifa hili, lakini tukiendeleza zana za ubabe zinazoendelea katika nchi hii, tusahau kabisa uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko vigezo vingi tunvyoviona sasa hivi. Ukijaribu ukiangalia hata bajeti ya mwaka 2017/218, ukienda kwenye kilimo imetekelezwa kwa asimilia 11, ukienda kwenye madini imetekelezwa kwa asilimia sijui tatu, ukienda kwenye maji imetekelezwa kidogo. Mpaka leo karibu bajeti nzima ya Serikali haijafikia hata ya mwaka jana ya utekelezaji wa asilimia 38 ya shughuli za maendeleo. Leo hii tumekaa hapa tunasema eti nchi inakwenda vizuri au inafanya vizuri wakati hakuna kinachoendelea. Tusifiche ugonjwa kifo kitatuumbua tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusiana na umeme. Nakumbuka sana wakati tunaanzisha gesi katika Taifa hili Serikali ilizunguka nchi nzima kutangaza kwamba kukatika kwa umeme sasa hivi tutasahau na mambo mengine, Watanzania mkae mkao wa kula, anzisheni viwanda umeme unakuja. Leo hakuna anayezungumzia umeme wa gesi tena, watu mmeanza kuleta mradi wa Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Rufiji ili uweze kutekelezeka na kuisha unahitaji shilingi trilioni saba, mwaka huu 2018 tumetenga shilingi bilioni 700 tafsiri yake ni kwamba mradi huu utatekelezwa miaka kumi. Je, Mheshimiwa Rais ambaye anaanzisha mradi huu atakuwepo miaka kumi ijayo. Mradi huu inawezekana ukatekelezwa ndani ya miaka 20 wakati huo shilingi inaendelea kushuka thamani kwa maana hiyo mradi huu unaweza kuja kutekelezwa kwa shilingi trilioni labda 20 mpaka 30, huu mradi tunataka kuharibu fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushauri wetu tulikuwa tunaomba mradi wa gesi ambao umeanzishwa Mtwara hizi shilingi bilioni saba badala ya kupelekwa kule Rufiji zikapelekwa Mtwara ili gesi ile isambazwe Dar es Salam, Morogoro, Tanga na maeneo mengine ili wananchi waendele kutumia umeme ambao unatumia gesi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kengele ya pili. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Hamida na Mheshimiwa Shally Raymond wajiandae.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo ambalo limetokea ndani ya Bunge hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza mwongozo huu kwa kuzingatia matakwa ya Kikatiba ambayo yako katika Nyongeza ya Pili ya Orodha ya Masuala Muhimu ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaotaka kuomba, katika mijadala na mjadala unaendelea Bungeni limeibuka kwa nguvu suala la Muungano. Suala hili la Muungano taswira inayotaka kuchukuliwa ni kama vile Serikali yetu ya Awamu ya Tano ni Serikali ambayo haijielekezi katika mfumo huu wa kikatiba kuheshimu na kuujali Muungano wetu. Kimsingi ukiangalia chimbuko la hoja yenyewe halitokani na dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika kuhakikisha Muungano unaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira haya ambayo mijadala inayoendelea ndani ya Bunge inaweza isilete afya njema kwa Muungano wetu. Ningependa kuona ni namna gani sasa Kiti chako ili kuhakikisha kwamba jambo hili linatolewa mwongozo fasaha na kuiacha Serikali ikiendelea na msimamo wake wa kuheshimu Muungano kwa minajili ya Katiba na kushughulikia yale ambayo ni chimbuko

la mjadala huu. Nadhani sasa ni wakati muafaka mjadala huu kuongozwa vyema na kuhakikisha kwamba heshima ya Muungano wetu kadri ya Serikali inavyoheshimu Muungano wetu iendelee kubaki na mjadala huu usiendelee kuingia katika kubomoa dhamira ya Serikali ya kuheshimu Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, pande zote mbili zipo kwenye mazungumzo ya kero za Muungano na kila hoja inayozungumzwa na wananchi pande zote mbili zinajaribu kuzitatua. Tulikuwa na kero nyingi sana za Muungano zimebaki chache sana pamoja na zitakazoibuka baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maana hiyo mwongozo wangu, *issue* ya Muungano nasimamisha mjadala wake kwenye Bunge hili mpaka hapo nitakapotoa mwongozo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Kaa chini Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Si haki yangu Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa kaa chini. Mheshimiwa Mwamoto jiandae Mheshimiwa Hamida.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuchangia hoja hii kwanza kwa kuunga mkono hoja kwa ujumla. Nianze kwanza kwa

kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, lakini bila kusahau kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu ambaye kwa kweli ameonesha ujasiri mkubwa katika kupambana na gurudumu hili la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu leo itakuwa moja tu kubwa. Tanzania wakati tunawasaidia wenzetu wapigania uhuru wa Nchi za Kusini mwa Afrika tulikuwa na makambi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib, rudi kwenye kiti chako. *(Kicheko)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MBUNGE FULANI:** Muungano oyee.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Kulikuwa na makambi....

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa chini, Mheshimiwa Pauline kaa chini.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa chini, Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo yalikaliwa na wakimbizi kwa nchi yetu zaidi ya maeneo 163...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa Dar es Salam, Mwanza, Mbeya, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani, Iringa, Dodoma, Tabora, Kigoma, Morogoro, Mara, Arusha, Zanzibar na Kagera. Kwa kutunza muda siwezi kuyataja makambi yao yote lakini lengo langu ni moja kwamba Dar es Saalam katika zile Ofisi Ndogo za CCM pale Lumumba baaada ya kuzaliwa Chama cha *TANU* ilifanywa Ofisi ya wapigania uhuru ambapo Chama cha *SWAPO, FRELIMO, ANC, ZANU* na *POLISARIO* walifanya kama makazi pale, kama ofisi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi za Kamati ya Uongozi ya Afrika (*Special Unity)* sasa hivi ni ofisi ambazo zinatumiwa na Tume ya Maadili ya Uongozi, makazi ya Hayati Eduardo Mondlane Osterbay, sasa hivi inatumika kama Ubalozi wa Msumbiji; Shule ya Sekondari Makongo na Lugalo walisoma watoto wa wapigania uhuru kwa sasa ni sekondari na Uwanja wa Magunia kule Tandale bado unatumika, ilikuwa ni sehemu ya mkutano pale, walifanyia mikutano pale. Morogoro kambi za wakimbizi zilikuwepo pale, kulikuwa na Mazimbu ambako sasa hivi ni Chuo cha Sokoine, kambi za Dakawa ambako sasa hivi kuna *VETA* na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia yangu ni kwamba kule Kilolo, Kihesa Mgagao walikaa wakimbizi, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tujaribu kubadilisha matumizi, wamefanya magereza ambayo haina tija kwa sababu wafungwa wako 40. Juzi Mheshimiwa Waziri wa Michezo tulipata ugeni kutoka Afrika Kusini kwenda kutembea kwenye kambi ile, alivyosikia kwamba ni magereza alikataa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kuna sehemu ambapo Mheshimiwa Mandela na Sisulu walilala. Tulitegemea sasa kingekuwa ni kivutio kikubwa cha watalii. Kuna watoto pale wameachwa na wenzetu wa South Africa wengi tu. Kuna mambo ya kimsingi kabisa tungeweza kufanya sehemu hii kuwa kivutio kikubwa cha utali tungeweza kuingiza fedha kwenye nchi yetu bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yetu, Mheshimiwa Rais anasikia, Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake wanasikia wabadilishe matumizi kwa eneo lile ili tufanye aidha shule, chuo au *VETA*. Sasa hivi tunaenda kwenye nchi ya viwanda tunahitaji kutayarisha vijana wengi ili waweze kufanya shughuli hizo za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linawezekana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hamida Mohamed, jiandae Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. YUSSUFU SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba iliyo mbele yetu ya Waziri Mkuu...

**MWENYEKITI:** Kanuni ipi, itaje Kanuni ya utaratibu.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1).

**MWENYEKITI:** Kaa chini. Mheshimiwa Hamida.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku kaa chini.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku kaa chini. Mheshimiwa Hamida.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuwapa pole wananchi wa Mkoa wa Lindi na wana CCM wote wa Mkoa wa Lindi kwa msiba mkubwa uliotupata wa Mzee wetu Alhaji Ally Mtopa. Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anazozifanya za kuwatumikia Watanzania na kazi zake zinaonekana. Niwapongeze pia Waheshimiwa Naibu Mawaziri wake kwa kazi ambazo wanamsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo inaelezea mapitio na mwelekeo wa kazi katika kipindi cha 2018/2019. Vile vile niipongeze sana Serikali yangu kwa kazi kubwa inayoifanya katika kutekeleza mambo mbalimbali na mambo yote yaliyotekelezwa kwa kweli yameleta mafanikio makubwa katika nchi yetu na mambo yote yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika utekelezaji kwa kipindi hiki cha 2017/2018, bado tunazo changamoto mbalimbali. Nizungumzie upande wa barabara zetu. Katika bajeti hii ambayo tunategemea itaishia mwezi huu Juni, katika Mkoa wetu wa Lindi tulibahatika kupitisha bajeti ya ujenzi wa kiwango cha lami kutoka Nanganga – Luchelegwa – Nachingwea -Masasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri husika atakapofanya *windup* atueleze mpango huu wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami

umefikia wapi maana hatuoni utekelezaji na kipindi cha mwaka huu kinakwisha bado robo moja tu tutamaliza mwaka. Pia ningependa kujua, tulitenga pia bajeti ya kufanya uthamini wa barabara inayotoka Nangurukuru - Liwale - Nachingwea nayo pia atueleze imefikia wapi katika utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Lindi kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza ahadi yake ya kutuletea kivuko pale Lindi. Tumepokea kivuko *MV* Kitunda, Mheshimiwa Rais aliahidi kutoa na ameweza kutekeleza. Kwa hiyo, tunashukuru sana na tunampongeza, tunamwombea dua njema ili aweze kutekeleza mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto kubwa ya barabara inayotoka Dar es Salam – Lindi – Mtwara. Barabara hii ni mkombozi sana wa wananchi wa Mikoa hii Kusini lakini bado kuna changamoto kubwa ya barabara kuwa na mashimo mengi lakini *TANROADS* wanashindwa kufanya ukarabati kwa kukosa fedha. Naiomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa barabara hizi. Barabara ya Kusini ni mkombozi wa watu wa Kusini na kutuletea maendeleo wananchi wa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeona katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania namna ambavyo kilimo sasa kimeleta tija kubwa katika nchi yetu lakini bado tunaona Serikali imejipanga vizuri katika kuhakikisha inaendeleza kilimo katika nchi yetu. Ukiangalia zao la korosho ambalo sasa hivi limeendelezwa katika mikoa mingi nchini Tanzania lakini bado tuna Sheria ya Korosho ambapo kabla haijasafirishwa inatozwa *export levy* ambapo mapato yake asilimia 65 yanaenda katika Bodi ya Korosho na asilimia 35 inabaki katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fedha hizi Bodi ya Korosho inanunua pembejeo na kufika kwa wakati kwa

wakulima lakini pia inanunua magunia, inazalisha mbegu bora ya korosho na inafanya mambo mbalimbali ya kuendeleza zao hili la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 shilingi bilioni 88 zilipatikana na mwaka 2017/2018 zaidi ya shilingi bilioni 133 ziliweza kupatikana lakini fedha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja lakini naiomba Serikali irudishe fedha hizi katika chombo chetu cha Bodi ya Korosho ili iweze kufanya kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 64(1)(b) ambayo inasema kwamba katika mjadala hapa Bungeni, Mbunge hatazungumzia jambo ambalo halipo kwenye mjadala na tulikuwa tunazungumzia Muungano ambao uko katika ukurasa wa 11 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba unisaidie umetumia Kanuni ipi kufuta jambo ambalo lipo kwenye mjadala na ninapoongea ni Naibu Waziri Kivuli wa Muungano, unisaidie tu kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza hayo masula ya fedha...

**MWENYEKITI:** Kaa chini umeshaeleweka, nitakujibu, kaa chini. Unahoji maamuzi yangu au unahoji nini?

Waheshimiwa Wabunge, narudia tena *ruling* niliyoisema, nimesema nimeahirisha mjadala huu mpaka nitakapotoa majibu ya mwongozo. Sijasema nimefunga mjadala huu, nimesema kwa leo nimeahirisha *issue* hii mpaka nitakapotoa mwongozo. Nimetumia Kanuni ya tano (5) na *mandate* ya Kiti. Kiti kina *prerogative powers* za kufanya maamuzi.

Kama Kiti kinalalamikiwa uko utaratibu Mheshimiwa Esther, uko utaratibu Mheshimiwa Msigwa wa kuandika barua kwa mujibu wa Kanuni, unamwandikia Katibu, hunilalamikii mimi hapa. Taratibu za humu ndani hazina tofauti na mpirani, refa akisema kasema. Mimi nimeshasema hili suala nalitafakari, nitalitolea majibu, wajibu wenu ninyi ni kusikiliza anayeona Kiti kinakwenda sivyo utaratibu wa Kanuni upo, *that is how the Bunge works.*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamesimama)*

**MWENYEKITI:** Kaeni chini.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Raymond, jiandae Mheshimiwa Ndassa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Zanzibar walitoka nje ya ukumbi wa Bunge)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kipekee kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai aliyotupa sisi sote hapa. Nawashukuru sana wanawake wa Kilimanjaro walionituma kuwawakilisha huku Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri. Niseme hakika wote katika Wizara yake akiwepo Waziri wetu wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Makatibu Wakuu na Naibu Waziri wote wametutendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianzie kwenye ule ukurasa wa 14, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Imerodheshwa pale takribaini Mifuko mitano lakini tunaambiwa jumla programu na Mifuko mingine iko 31 ambayo inawezesha wananchi kwa kutoa mikopo. Hoja yangu ni kwamba, wananchi hao wanaopewa mikopo wakiwemo vijana, wanawake, wajasiriamali hawana elimu ya kukopa. Japo wanapewa hizi hela kwa mkopo lakini elimu yao ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliomba elimu kwa wananchi hawa wakiwemo wanawake wa Kilimanjaro na bahati zuri sana tuna Chuo Kikuu cha Ushirika, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu ione sasa ni wakati wa kuzungumza na chuo au na vyuo vinginevyo wakatoa elimu ya kukopa kwa wanawake au wajasiriamali wale wakati vijana wale wa chuo wanakwenda *field*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu mikopo inatolewa halafu hairejeshwi. Kuna mifuko ambayo mpaka sasa ikiwemo mfuko uliotoa mabilioni ya JK, hela zile hazikurudi na zile ni *revolving funds,* zimefika mahali zimekwama, hakuna ufuatiliaji. Niombe Kiti chako na nimuombe Mheshimiwa Spika imefika wakati sasa huku ndani iundwe Tume kufuatilia zile hela za *revolving* zimefia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nizungumzie usalama wa chakula. Bahati nzuri sana mvua zilizonyesha mwaka uliopita zilikuwa nzuri, chakula kimekuwepo, lakini uhifadhi wa chakula hiki siyo mzuri, wananchi wetu hawana maghala ya kuhifadhi chakula. Tunaambiwa kwamba ifikapo 2025 tutakuwa takribani Watanzania milioni 70 lakini tumejiandaa vipi kuzalisha chakula ambacho tunaweza kutumia na kingine tukahifadhi ili kulisha wananchi wetu? Niombe Wizara ya Kilimo iliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye mifugo. Wananchi wengi wa Tanzania ni wafugaji lakini mifugo mingi ni ile ya kiasili *(indigenous)* hakuna kuboreshwa kwa mifugo

hiyo. Mwaka jana tuliambiwa kwamba Serikali itasaidia mitamba bora na mitamba hii inaweza ikasambazwa kwa wafugaji wa hali ya chini. Naomba kujua mpaka leo tokea mwaka jana ni mitamba mingapi imetolewa kwa wafugaji hao ili tujue imeboreshwa kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ni mizuri lakini inapozagaa hovyo siyo mizuri kwa sababu inaharibu mazingira. Niipongeze pia Wizara ya Mifugo, Waziri aliyepo madarakani ameweza kudhibiti hilo na mpaka sasa hivi tumesikia migogoro kidogo sana kuhusu wafugaji. Naomba nimpongeze Waziri na Naibu Waziri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie ujenzi wa viwanda. Kwa kweli tumepewa taarifa kwamba viwanda ni vingi na vinaendelea kuwepo lakini niseme kwamba tunapokwenda kwenye viwanda tuangalie pia teknolojia inayotumika. Sasa hivi imekuwa ngumu kufufua vile viwanda kama *Machine Tools*, Kiwanda cha *Tanzania Bag* kule Moshi kwa sababu ya teknolojia iliyokuwa imetumika huko nyuma haikuweza sasa kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana vile viwanda vya Kilimanjaro vifufuliwe na pia vinapokwenda kufufuliwa na kujengwa vipya tutumie sasa teknolojia ambayo ni ya kisasa zaidi. Ni wazi kwamba viwanda vile vinatoa ajira, Kilimanjaro wengi sana walikuwa wanategemea ajira hizo, vijana wetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Ndassa, ajiandae Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nsanzugwanko, jiandae Mheshimiwa Chuachua.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kama ilivyo ada nianze kwa kuwapa hongera sana Ofisi ya Waziri Mkuu na timu yake kwa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze Serikali kupitia kwa Waziri Mkuchika kwa tangazo lake la asubuhi. Limetufariji sana kwa sababu maeneo mengi yalikuwa na shida, wenzetu wa Serikali hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mawili tu. La kwanza bahati nzuri nimeliandika kulipeleka kwa Mawaziri na watalaam ni kuhusu uraia. Nchi hii wananchi walio wengi wanaishi kwenye mipaka ya Taifa hili na katika mipaka ya Taifa hili upo Mkoa unaitwa Mkoa wa Kigoma. Sisi tumekuwa wahanga wakubwa wa ubaguzi wa waziwazi kabisa. Tumekuwa ni wahanga wa madhila na maonevu ambayo hayamithiliki kupitia wenzetu wa Idara ya Uhamiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aje atueleze hawa wananchi wa Kigoma ambao wanasumbuliwa kwa sababu ya au maumbile yao, au sura zao, au lugha yao, kwa nini kila mara wanaambiwa wao siyo raia? Tunajua iko mikoa mingi, lakini jambo hili kwa Mkoa wa Kigoma limekithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo kumetokea tukio la ajabu kabisa. Kuna mwananchi amekamatwa anaambiwa aende na wazazi wake wote wawili Uhamiaji wakati sisi tunajua kabisa ni mzaliwa wa pale pale. Haya madhila ni makubwa sana na tungeomba kwa kweli yatolewe ufafanuzi mzuri. Inawezekana pengine wenzetu wa Uhamiaji wamekosa tu weledi wa kutenda kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, litakuwa jambo la msingi sana wenzetu wa Serikali jambo hili wakilitazama na kwa kweli lipate ufumbuzi. Mbona hatusikii mambo haya kwenye

mipaka mingine ya nchi hii kama Tanga, Mbeya au Kilimanjaro ni Mkoa wa Kigoma tu kwa nini? Hili jambo linatukera sana ningeomba lipatiwe majibu ya moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nitapitia ukurasa wa 44 wa hotuba ya Waziri Mkuu ambapo anazungumzia barabara na amebainisha wazi kabisa kwamba barabara zitakazojengwa zitakuwa na urefu wa kilomita 1,760. Sasa nina ushauri tu, katika barabara zinazopangwa kujengwa, najua Serikali ni moja jambo hili ningeweza nikalizungumza kwenye sekta ya ujenzi na kama alivyosema rafiki yangu Mheshimiwa Mgimwa pale, Waziri Mkuu ndiyo Kiranja wa Mawaziri wote, nataka nimpe angalizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi hii barabara ndefu kuliko zote ambayo haijajengwa kwa miaka 20 ni barabara inayoitwa Kigoma – Kasulu – Kibondo - Nyakanazi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati umefika barabara hii sasa ipewe kipaumbele. Kwa mfano, barabara hii ya Iringa - Dodoma imekuja sasa wakati barabara ya Nyakanazi ilikuwepo haijamalizika. Barabara ya Dar es Salaam - Mtwara imekuja sasa wakati barabara hii ya Nyakanazi - Kigoma haijakamilika. Barabara ya Singida - Minjingu imekuja sasa wakati barabara ya Kigoma - Nyakanazi bado haijajengwa kwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mahitaji ya barabara ni muhimu sana katika nchi yetu, lakini barabara hii ndefu kuliko zote ambayo imesanifiwa miaka 20 iliyopita hata vipande vyake vya Kasulu - Kidahwe na Kabingo - Nyakanazi bado havijakamilika, wakandarasi wanadai fedha zao. Nimekuwa nikishangaa kupitia Wizara ya Ujenzi, wakandarasi hao walioko *site* kila wakiomba fedha zao wanalipwa kidogo kidogo na barabara hizi zimechukua muda mrefu sana takribani miaka 20 barabara haimaliziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo hapa inasikia, tunaomba barabara hii ipewe kipaumbele vinginevyo tutachukua hatua ambazo hazipendezi sana kwa sababu

hatuwezi kuona kabisa keki ya Taifa inagawiwa kwa ubaguzi wa dhahiri kabisa, kwa maana kwamba kuna maeneo mengine yanapewa kipaumbele na kujengewa barabara za lami na maeneo mengine yanaambiwa yasubiri. Tumesubiri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndassa umerudi, jiandae Mheshimiwa Chuachua.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu bado.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nsanzugwanko muda wako umekwisha, umeanza kuzungumzia masuala ya *immigration* na mambo ya mipakani, kaa chini tafadhali. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, lakini nilikuandikia *note* nikiomba kuchangia siku nyingine kwa sababu nimetoka kwenye matatizo. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chuachua.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi ya mimi kuchangia kwa muda wa dakika tano, nitazitumia vizuri. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri pamoja na wasaidizi katika Ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwa kifupi, nataka nichangie kwenye hifadhi ya jamii. Watumishi waliostaafu wa Jimboni kwangu Masasi wameniagiza niseme kwamba kutoka mwaka jana mwezi Juni mpaka leo hawajalipwa mafao yao lakini pia wananchi hawa ambao wamestaafu hawajapewa hata fedha za kuhamisha mizigo kurudi majumbani mwao. Jambo hili linahuzunisha sana kwa

sababu watu hawa wamekwishatumikia nchi hii na wameshafikia umri wa kustaafu, Serikali inapaswa kuwalipa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kidogo pia kwenye kilimo. Niishukuru Serikali kwa juhudi zake za kuimarisha sekta hii lakini pia sisi watu wa Kusini tunazo changamoto ambazo lazima tuziseme. Moja, toka tumepata tatizo la wakulima wa mbaazi kwa kutokupata bei mpaka leo Serikali haijasema kama iko tayari na imeshatafuta soko la mbaazi. Mpaka sasa hatuna majibu kwa wakulima kwa sababu mbaazi ziko mashambani tena, mwaka huu utaratibu ukoje katika kupata soko la mbaazi zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tukumbuke Serikali katika msimu wa korosho uliopita ilitoa *sulphur* bure kwa wakulima na sisi tulifanya kazi kwenye mikutano kuwashawishi wakulima wapate *sulphur* hiyo na Serikali ipeleke. Sasa tumebadilishiwa utaratibu tunaambiwa wakulima wanatakiwa wanunue *sulphur.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaiomba Serikali itoe kauli haraka ili wakulima wajue *sulphur* hiyo inapatikana vipi tena kwa kudhibiti bei ya soko la *sulphur.* Kwa sababu mpaka sasa hivi tunavyozungumza bei ya *sulphur* ni Sh.70,000, Sh.80,000 kwa mfuko ambao walikuwa wananunua kwa Sh.27,000. Kwa hiyo, Serikali ina utaratibu gani wa kudhibiti bei hii ili wakulima wetu wamudu kuinunua na ipatikane mapema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kidogo kuhusu suala la maji. Tunalo tatizo kubwa katika nchi yetu na Serikali kweli inafanya kazi ya kuhakikisha kwamba maeneo yote yanapata maji. Hata hivyo, katika Mkoa wa Mtwara, Wilaya ya Masasi na Nachingwea tunategemea chanzo cha maji cha MANAWASA. Hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo haya ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema mbaya sana kwa sababu hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja

tulimwambia kwamba, MANAWASA wana tatizo kubwa la kutokwepo chujio la kuchuja matope, kiasi kwamba katika kipindi hiki chote wanafunga maji kwa sababu maji yale yanakuja yakiwa machafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika randama tumeona mmepanga shilingi bilioni mbili kuwapa MANAWASA lakini kwa sababu mara nyingi bajeti ya MANAWASA inakuwa haitoki, tunaomba sasa Serikali kwa kipindi hiki kilichobaki bajeti hii ya shilingi hizo bilioni mbili ipelekwe kwa ajili ya kufanya usanifu wa chujio la kuchuja tope ili wananchi wetu wapate maji na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni umeme. Wabunge wengi wamezungumza, pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali lakini bado Mkoa wa Mtwara tuna tatizo la umeme, umeme unawaka kama *indicator* ya gari, unawaka unazimika, unawaka unazimika. Tumekwishaambiwa juhudi zinazofanywa na Serikali kwamba sasa hivi wanataka kufunga mashine nyingine ambayo itaongeza kiwango cha umeme. Tungependa Serikali ifanye jambo hili haraka kwa sababu linaharibu utaratibu mzima wa wananchi wa Jimbo langu pamoja na Mkoa mzima wa Mtwara kutokana na kukatikakatika umeme bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni *REA.* Nimezungumza na Waziri, nimezungumza na viongozi wa *TANESCO,* Jimbo la Halmashauri ya Mji wa Masasi vijiji vingi vimesahaulika. Tunaomba Waziri atakapokuwa anahitimisha atoe kauli ni vijiji gani sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mgumba ajiandae Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu

katika hili. Niipongeze Serikali na Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo ina mwelekeo mzuri wa bajeti yetu ya 2018/2019. Kwa sababu ya muda naomba niongelee jambo moja tu na mengine nitaongelea kwenye Wizara zinazofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano hasa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uthubutu alioufanya ambapo Marais waliopita walikuwa hawajaufanya pamoja na kazi nzuri waliyoifanya kwa kutekeleza mradi wa *Stiegler's Gorge* ambao unakwenda kutuhakikishia umeme wa uhakika zaidi ya *megawatts* 2,100 ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo siyo dogo, hili suala lilianza tangu miaka ya 60, Mwalimu Nyerere ilikuwa ni ndoto zake kulitekeleza, lakini kutokana na vikwazo mbalimbali wale wasioitakia mema Tanzania ndiyo waliokuwa wanaukwamisha mradi huu usitekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu una manufaa makubwa sana. Pamoja na uzalishaji huo wa umeme *megawatts* 2,100 lakini pia utatoa ajira kwenye uvuvi. Hili bwawa litakuwa ni sehemu ya utalii, liko bwawa karibu na mbuga yetu ya Selou lakini pia kutakuwa na heka zaidi ya 85,000 ambazo zitakuwa ni za kilimo cha umwagiliaji. Utaona ni namna gani unaona huu mradi una fursa nyingi na faida kubwa ambayo inakwenda kutekelezwa na Serikali hii ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia huu mradi utaboresha huduma za jamii. Nitoe mfano kwenye Jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki. Kupitia mradi huu, barabara ya Ubenazomozi – Ngerengere - Tununguo – Mvuha - Kisaki - *Stiegler's* Rufiji yote itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Unataka mafanikio gani zaidi ya haya? Niipongeze sana Serikali kwa kuliona hili, lakini hasa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuthubutu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine watu hawaelewi miongoni mwa sababu ya kuanzishwa *NEMC* na mambo

mengine haya ilikuwa ni kuzuia miradi kama hii ya *Stiegler's* na Kidunda kwa sababu walikuwa wanaona ni miradi ya kielelezo, inakwenda kuwakomboa Watanzania kwenye njia ya umeme pamoja na maji, wakatuwekea vikwazo chungu nzima tusiitekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kutoa mfano humu ndani Mradi wa Bwawa la Kidunda andiko lake la kwanza lilikuwa tangu mwaka 1955, andiko la pili 1962, andiko la tatu 1982 baada ya Wajapan kushinda ile tenda ya kutengeneza ule mradi ndiyo pale Wajerumani wakatuletea mradi huu wa mazingira, nani asiyejua? Leo tumepata Rais anakwenda kutekeleza yale bila kusikia lolote kwa maslahi ya Watanzania halafu tunaubeza. Niwaunge mkono, tuko nyuma yenu na kwa kusema haya naamini kabisa Serikali itapaa na Watanzania tutakwenda mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kusema haya niwaambie, haina maana Serikali imeachana na miradi ya gesi. Nawapa mfano mmoja, Rais tumemwona kama miezi miwili iliyopita aliienda kuzindua Mradi wa Umeme Kinyerezi II zaidi ya *megawatts* 168. Huu ni mradi wa gesi inatumika ile ile ya Mtwara haijasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika ni kuchanganya hii yote, mradi wa maji na mradi wa gesi ukizingatia umeme unaozalishwa kwa maji una gharama nafuu zaidi. *Megawatts* moja katika kuzalisha umeme wa gesi ni zaidi ya milioni 1.2 *USD* wakati mradi wa kuzalisha maji *megawatts* moja tunatumia zaidi ya milioni 1.0 USD maana yake ni nini? Huu mradi ambao ni wa kuzalisha kwa maji una gharama nafuu kuliko wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo Serikali haijaacha. Niwaambie suala la gesi ni la utafiti unaendelea mpaka leo, tuna neema tumeshagundua futi za ujazo zaidi ya trilioni 57…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bashungwa jiandae, Mheshimiwa Bupe halafu jiandae Mheshimiwa Ole Meiseyeki.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nianze kwa kuendelea kuwapa pole wananchi wangu wa Karagwe kwa pengo kubwa tulioachiwa na ajali ya *City Boys,* Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu waliofariki mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda mimi nina mambo mawili; nianze na suala la kahawa na katika hili niipongeze Serikali kwa kuja na mfumo wa stakabadhi ghalani, lengo la kuleta mfumo wa stakabadhi ghalani ni kumsaidia mkulima wa kahawa ili aweze kunufaika na zao la kahawa na zao hili limsaidie kumtoa kwenye umaskini. Sasa ili tuweze kutimiza hii dhamira nzuri ya Serikali mimi Serikali naishauri mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenye suala la butura; namna pekee ya kupambana na changamoto ya butura ni Serikali chini ya Vyama vya Msingi kuanzisha *SACCOS* ambazo zitakuwa zinakopesha wakulima wakati kahawa iko mashambani inasubiri kukomaa kuiva basi Serikali chini ya Vyama vya Msingi ianzishwe *SACCOS* itoe mikopo ya bei nafuu ili mkulima aweze kukopa na pale vyama vya ushirika vitakapouza kahawa yake aweze kukatwa mikopo hii ya bei nafuu. Kwa hiyo, hiyo ndio namna ambayo itatusaidia kuondokana na changamoto ya Butura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili pamoja na nia njema ya Serikali huu mfumo wa stakabadhi ghalani ili iweze kuleta weledi na uweze kumsaidia mkulima wa kahawa inabidi tujipange. Sasa bahati mbaya mfumo huu umeletwa wakati tunaingia kwenye msimu wa kahawa mwaka huu. Ushauri wangu kwa Serikali ili tuweze kujipanga vizuri maana kahawa lazima tuhakikishe iwe na ubora na ubora huu ndio itausaidia kupata bei nzuri sokoni. Serikali itumie mwaka huu kujipanga ili msimu wa mwaka unaokuja ndipo twende

kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani, tutumie mwaka huu kuhakikisha kahawa inapotoka mashambani kwenda kwenye mnada ubora unazingatiwa kuanzia shambani kuna mambo ya miundombinu ya maghala, vyama vya ushirika vina madeni sasa hatujui Serikali imejipangaje kukaa na hivi vyama vya ushirika kuhakikisha haya madeni hayahamii kwa mkulima wa kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mambo haya yanatakiwa atupate muda wa kujipanga ili tutakapohamia kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani basi mfumo umsaidie kweli kweli mkulima wa kahawa kumkwamua kutoka kwenye umasikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kuzungumzia ni mfuko wa uwezeshaji wananchi chini ya ofisi ya Waziri Mkuu. Mfuko huu ni wa muhimu sana hasa hasa kipindi cha sasa hivi cha Serikali ya Awamu ya Tano ambapo tunalenga kwenda kwenye uchumi wa kipato cha kati kupitia uchumi wa viwanda na tumekuwa tukisisitiza kwamba Serikali ijikite kwenye kusaidia Watanzania wengi katika shughuli ambazo Watanzania wengi wanajishughulisha nazo kilimo, mifugo na biashara ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu na sisi Wabunge wote humu ndani kwenye Wilaya zetu tumehamasisha watanzania Serikali hawezi kumsaidia Mtanzania mmoja mmoja tumehamasisha Watanzania wajiunge katika vikundi vya akina mama na vijana ili kupitia mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ofisi ya Waziri Mkuu Serikali iwapatie mikopo ya bei nafuu. Sasa mfuko huu una bilioni 1.6 peke yake na toka mwaka 2013 mfuko huu haujawahi kupewa hata shilingi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali hii *Mwananchi Empowerment Fund* ipeni hela ya kutosha iweze kuwasaidia wananchi kupitia vikundi vya wakina mama na vijana hasa vijijini ambapo tayari tumeshahamasisha na programu ya shilingi milioni 50 najua Serikali huko miaka ya

mbeleni itaileta lakini tukitumia mfuko huu utawasaidia wakinamama na vijana Tanzania kuendelea na biashara ili zile shilingi milioni 50 zitapokuja baadae ziwakute wako katika kuzalisha shughuli za kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipende sana kuomba Serikali ilichukue hili Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi upewe hela ya kutosha; shilingi bilioni 1.6 ni hela ndogo...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Ole Meiseyeki hayupo, Mheshimiwa Bupe, ajiandae Mheshimiwa Chumi.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na naomba nichukue dakika moja kumuombea katika kazi anazozifanya naanza kwa kusema Baba katika jina la Yesu, damu ya Yesu imfunike Dkt. John Pombe Magufuli, imfunike Majaliwa, imfunike Jenista Mhagama, ifunike Mawaziri wote, ifunike Serikali ya Tanzania ninakushukuru Baba wa Mbinguni kwa sababu Serikali ya Tanzania inafanya kazi kwa jinsi watu wanavyoitaka wote tuseme Amen. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Amen. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa kwa kuchangia katika Wizara ya Elimu. Mkoa wa Rukwa hauna Chuo cha *VETA.* Chuo cha

*VETA* kimezungumziwa muda mrefu sana lakini mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea nataka kujua tatizo ni nini? Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuleta majibu hapa atuambie kuna tatizo gani kuanzisha chuo cha *VETA* katika Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee maabara, Serikali ya John Pombe Magufuli...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** ...ilianzisha kujenga maabara katika shule za sekondari na ilikuwa na nia nzuir lakini mpaka sasa hivi maabara nyingi hazijaisha tatizo ni nini watoto wanaotaka kusoma *chemistry, science* wanashindwa kupata elimu nzuri, ninaomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi safari hii kwenye bajeti hii iweke fungu la maabara ziishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la walimu, tangu zoezi hili la kuwabadilisha walimu wa sekondari waende wakafundishe kwenye shule za msingi limeleta shida kidogo kwa sababu shule za sekondari sasa zimepungukiwa na walimu. Nilikuwa naomba Serikali ifanye haraka kuwaajiri walimu ili shule za sekondari sasa ziweze kukidhi mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la ukubwa wa Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Rukwa una majimbo matano, lakini kuna majimbo mawili ni makubwa sana nataka niongelee Jimbo la Kwela, jimbo la Mheshimiwa Malocha, jimbo lile lina kata 27 limejigawa Ufipa wa Juu na Ufipa wa Chini. Ufipa wa Juu una kata 14 na Ufipa wa Chini una kata 13. Mheshimiwa Malocha amekuwa akifanya kazi ngumu sana na kubwa, lile jimbo ni kubwa sana na ameliongelea muda mrefu kwamba tunaomba basi ligawanywe kwa sababu wananchi wanashindwa kupata huduma kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, ukianza Ufipa wa Chini ukizungukia Ufipa wa Chini kabla haujamaliza unapandisha Ufipa wa Juu unakuwa umeishiwa mpaka mafuta. Ufipa wa Juu wanaanza kulalamika kwamba Mbunge hatufikii sisi hapa watu wa Ufipa wa Juu ni kwa sababu lile jimbo limekuwa kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa na jimbo la Mheshimiwa Kandege na lenyewe lina kata 27 nilikuwa naomba kwa sababu hili linatuletea shida sana hata kwenye upande wa kisiasa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Chumi, ajiandae, Mheshimiwa Hadji Mponda, ajiandae Mwita Waitara.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na kwa sababu muda mchache napenda kuanza kwa kuunga mkono hoja na napenda kuwafahamisha Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Mchengerwa, Mheshimiwa King na Mheshimiwa Kitandula na wenzenu Simba moja, Mtibwa sifuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo kwa haraka kabisa napenda niende moja kwa moja...

**MBUNGE FULANI:** Mme-*park bus.*

**MHE. COSATO D. CHUMI:**...kwenye ukurasa wa 31 wa hotuba ya Waziri Mkuu kuhusiana na upatikanaji wa mbolea. Kitabu kimeeleza kwamba upatikanaji wa mbolea ni asilimia 64 maana yake ni kwamba asilimia 36 wananchi wetu hawapati mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tumeona changamoto nyingi za usambazaji wa mbolea. Ninapenda kuishauri Serikali kutokana na changamoto zilizojitokeza mwaka huu hebu ijaribu kuangalia ili wakulima wetu waweze kupata mbolea

sio tu kwa bei nafuu, lakini kwa wakati. Inasikitisha sana kuona mkulima wa Isalavanu, kule Itimbo, kule Kitelewasi anapata mbolea ya kupandia mwezi wa pili wakati uandaaji wa mashamba unaanza mwezi wa kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali kwa changamoto ambayo wamekutana mwaka huu kwenye usambazaji wa mbolea, hebu wazipitie na kuona kwamba kwa namna gani tutamsaidia mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama vile haitoshi tumeona kwenye ukurasa wa 27 unaozungumzia upatikanaji wa chakula tumekuwa na ziada ya chakula tani milioni 2.6. Lakini wale wanunuzi wa chakula *NFRA* wamenunua tani 26,000 tu za mahindi maana yake ni kwamba mazao yale ambayo ni ziada yameenda wapi? Yamekosa soko, sasa mwananchi huyu mkulima wa Itimbo, wa Bumilainga mbolea tunamcheleweshea lakini anafanya jitihada anazalisha ziada bado tunamzuia kuuza mazao yake. Kwa kweli tunakuwa tunawafanya wakulima kama *second citizen* katika nchi yetu.

Kwa hiyo, napenda kushauri maana yake Bunge ni kuishauri Serikali hebu iweze kuona upatikanaji wa mbolea kwa wakati, lakini pia kunapokuwa na ziada ya chakula tuwasaidie wananchi hao kupata soko tusifunge kuwazuia kwamba wasiuze nje kama ilivyotokea kwenye mazao ya mahindi tunawakatisha tamaa, muda ni mchache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili naomba sana Mheshimiwa Mama Jenista Mhagama, Kaka yangu Antony Mavunde nadhani ni mdogo wangu kuhusiana na suala zima la uchumi wa viwanda. Ni kweli tunasisitiza na Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla imekuwa mstari wa mbele tunamuona Rais amekutana na Jumuiya ya Wafanyabiashara amesikiliza kero zao, ameelekeza Mawaziri wazitatue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, rai yangu tunapoita wawekezaji na uchumi wa viwanda lazima twende sambasamba na kuangalia *walfare* ya wafanyakazi wanaofanya kazi katika viwanda hivyo, itakuwa haina

maana leo hii kama mimi mfano pale Mafinga tuna wawekezaji lakini unakuta mama anatoka Changarawe anaenda Kinyanambo C kibaruani anatembea *almost* kilometa sita mpaka tano mpaka saba; mfanyakazi huyu analazimika kuamka saa kumi alfajiri, ana-*risk* maisha yake anaenda kazini, mshahara mdogo, hakuna *NSSF*, hakuna matibabu.

Sasa mambo haya nikuombe Mheshimiwa Mavunde kwa sababu ndio unahusika moja kwa moja Kazi, Ajira na Vijana, tembelea Mafinga, toa maelekezo kwa wawekezaji ili kusudi uchumi wa viwanda uende sambasamba na kuangalia *walfare* ya wafanyakazi, vinginevyo tutaleta viwanda, lakini hali za wananchi wetu zitaendelea kuwa duni itakuwa haina maana kweli Serikali itapata kodi lakini pia lazima wananchi wetu wafurahie uchumi wa viwanda kwa wao kupata kazi ambazo watalipwa vizuri, lakini pia haki zao zitakuwa zinazingatiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia maana muda ni mchache sana naomba niende haraka kwenye *point* yangu ya mwisho kuhusiana na sekta binafsi. Nimepongeza jitihada za Mheshimiwa Rais lakini mimi naomba na kupendekeza kwa Serikali kwa mikono miwili kabisa baada ya kukutana na wafanyabiashara wale tumeona kabisa *concerns* zao na tumeona muda ulikuwa ni mchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwa Serikali na naomna Mheshimiwa Rais akiweza akutane pia na sekta kwa sekta mfano sekta mojawapo sekta ya usafirishaji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, ajiandae Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya malalamiko katika nchi hii ni mipaka na migogoro ambayo inaendelea katika vijiji vinavyopakana na hifadhi au mapori tengefu au mapori ya akiba. Naomba nianze kwa kumpongeza Waziri Mkuu kwa busara zake na kuwa msikivu zoezi hili katika bonde la Kilombero limekamilika Wilaya ya Malinyi na zoezi hili lilifanywa kwa kuwashirikisha wananchi. Pamoja na kukamilika zoezi hili yameacha kilio, imeacha kero, imeacha malalamiko kwa wananchi hawa. Naomba ieleweke zoezi hili limefanyika baada ya mabadiliko ya Sheria ya Wanyamapori ambayo yalifanyika mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hiyo ya wanyamapori kabla ya 2009 wananchi walikuwa wanaruhusu matumizi ya binadamu katika mapori tengefu likiwemo Bonde la Kilombero. Sasa ilivyobadilika sheria ile wananchi hawa kihalali kabasa vijiji karibuni 16 na vitongoji vyake kama 25 vinaishi kihalali kule katika maeneo yale. Sasa sheria imebadilika inawakataza, sasa hapo ndio umeanza mgogoro, lakini busara ambazo ametumia Waziri Mkuu ni kwamba ametuma wataalam, wajadili na wapitie mipaka ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile zoezi limekamilika kama ninavyosema bado malalamiko yako pale kwa sababu pamoja imetambulika ile mipaka, lakini mashamba ya wananchi, wananchi wa Wilaya ya Malinyi na Wilaya ya Ulanga kilio chao kikubwa mashamba walikuwa wanalima maeneo yale hasa maeneo ya *buffer zone* sasa wamezuiliwa hawawezi kulima tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini maana yake? Kwa hiyo, kuwazuia kulima maeneo yale tayari tunatengeneza mazingira magumu na tujue kwamba mpunga ambao unapatikana Ifakara au mchele unaitwa Kilombero asilimia 80 ya mchele ule unatoka Malinyi. Sasa kitendo cha kuwazuia wananchi hawa wasilime maeneo yale tayari tumetengeneza mazingira ambayo ni njaa ambayo itatokana na kukataza kulima maeneo yale.

Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu ulimtuma Waziri wako wa Maliasili na Utalii amekuja maeneo yale, ameona na mimi namshukuru Waziri Dkt. Kiwangalla ametumia busara zake, ameona hali halisi ameunda tume ya watu 21 ambayo itafanya kazi ndani ya mwezi mmoja kuona nini changamoto wananchi wale ili kama mazingira yanaruhusu basi maeneo yale waruhusiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo letu lenyewe tunaliomba wala sio kubwa sana ni katikati ya kilometa mbili mpaka kilometa tano kutoka nje ya mipaka ya kijiji, vinginevyo kama atazuia wananchi wale basi kilio kitakuwa kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili Serikali imeeleza hapa ukosefu wa pembejeo kuna changamoto mbalimbali zimesababisha na ukosefu huu. Naomba nielezee kwenye Wilaya ya Malinyi. Mwaka huu wananchi Wilaya ya Malinyi wameshindwa kulima mahindi kwa sababu ya sumu ya panya haikupatikana kwa wakati muafaka na taarifa tayari ilishatolewa kwa sababu tataizo hili limejitokeza miaka mitatu mfululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali unapofikia wakati wa kuweka hizi bajeti waangalie msimu upi ambao unatakiwa kupeleka hizi pembejeo, vinginevyo kilio hiki kitaendelea. Kwa mfano, mwaka huu watu hawatalima mahindi kwa sababu ya hizo sumu za panya hazikufika kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho Serikali mwaka 2010 waliingia mkataba wa mkopo na Serikali ya India wamekopa karibuni milioni 40 za Kimarekani toka Serikali ya India na mradi huo ulikuwa kuwezesha matrekta ya SUMA JKT, lakini mpaka ilivyofikia mwaka 2015 matrekta yale yalikuwa na matatizo ya urejeshaji wa mikopo ile na ndani ya miaka mitano ni asilimia 40 tu ya madeni 46 ndio yamerejeshwa. Sasa mwaka 2017 Serikali mmeanza mradi mwingine tena mradi mwingine wa kuunganisha matrekta pale Kibaha, matrekta aina ya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara, ajiandae Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na namshukuru Waziri Mkuu kwa sababu kimsingi anatimiza wajibu wake kama nafasi yake inavyosema. Nitaanza na eneo muhimu sana la ukurasa wa saba kwenye hotuba yake amezungumzia habari ya kudumisha amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba amani huwa hailazimishwi na utulivu wa Taifa hauwezi kulazimishwa kutumia mtutu wa bunduki. Jambo hili ili lifanyike vizuri ni lazima liwe ni zoezi shirikishi. Katika maeneo haya ndiyo maeneo ambayo sisi kama viongozi wa upande wa Upinzani tunalalamikia sana kwamba kwa sasa hali ilivyo ni kama tumesahau kwamba Rwanda nini kilitokea baada ya chokochoko nyingi; ni kama tumesahau nini kilitokea Algeria na tunazungumza kana kwamba haya mambo hayapo katika mataifa mbalimbali baada ya maoni ya Upinzani na viongozi mbalimbali kupuuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunaona kitendo cha kusema tunakuwa tunadumisha amani na utulivu katika nchi, lakini wakati huo huo viongozi ambao tunakaa katika Bunge hili tunajadiliana mambo ya kitaifa kwa upendo kabisa lakini tunawakamata kwa hila, chuki na tunawasweka ndani, tunawanyima dhamana na watu wengine kadha wa kadha wameumizwa katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nitoe wito kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye mimi namheshimu sana, kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ukiangalia picha ya yule Diwani wa Kilombero alivyokatwa mapanga kama una moyo wa nyama lazima ushtuke sana. Ukiangalia watu wanavyookotwa katika fukwe mbalimbali. Kwa hiyo, mambo

haya tungeomba kwa moyo wa dhati kabisa, kama tunalipenda Taifa letu la Tanzania ambalo tunalipenda sana ni muhimu mambo haya yachukuliwe hatua. Msione kwamba sauti za watu wanaolalamika ni kwamba ni watu ambao hawana maana, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ambayo yanaendelea tunaanza kuonesha picha mbalimbali za watu wamepigwa risasi, wengine wamepigwa visu, wengine wametupwa kwenye fukwe za bahari maana yake tunawafanya watu wetu wazoee hii hali na huko mbele hata kama hatutakuwepo, makaburi yetu yataulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuombe kama Serikali iliyoko madarakani, Chama cha Mapinduzi mchukue hatua ili Watanzania waishi kwa amani na amani ambayo inazungumzwa ionekane ikitendeka kwa maana kwamba tuheshimiane. Kama kiongozi na Mtendaji Mkuu wa Serikali ukusara wa kumi Mheshimiwa Waziri Mkuu amenukuu maneno mazuri sana, anasema; kuna uhuru wa wananchi kujiunga katika vyama vya siasa, kuna chaguzi mbalimbali zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yetu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba tunapoitisha uchaguzi, yule kiongozi ambaye wananchi walio wengi wamesema ndiyo wanamtaka ndiyo chaguo lao, huyo atangazwe aapishwe na awe kiongozi na mwakilishi wa eneo lile ili kupeleka maendeleo na isiwe vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanataka Sheria za Uchaguzi zifuatwe, wananchi hawataki polisi wengi katika vituo vya kupigia kura. Hilo tunatoa rai lishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 33 wa hotuba ya Waziri Mkuu, kwenye eneo hili amezungumzia habari ya mifugo na minada na ukurasa huo huo wa 34 amezungumzia mambo ya utalii. Naomba nitoe taarifa kwamba kule katika Jimbo la Ukonga kuna mnada mkubwa sana wa Pugu unaitwa Mnada wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mifugo alikuja katika eneo lile. Lakini mnada ule pale ukifika, jina ambalo linazungumzwa kwamba ni Mnada wa Kimataifa haufanani na hali yenyewe ya mnada ule. Pale hakuna maji ya kutosha, hakuna sehemu ya malisho, hakuna uzio, hakuna huduma ya vyoo vya kisasa, ni vurugu *match* katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungeomba kama tunataka kupata mapato mengi ya Serikali na ule ndiyo mnada ambao unatoa huduma kubwa katika Mji wa Dar es Salaam basi mnada ule uboreshwe. Lakini sasa imeibuka hoja eneo lile kuna mgogoro unaibuka kati ya mnada na wananchi wa kijiji/Kata ya *Pugu Station* Mtaa wa Banguro. Hawa watu walipewa hati ya kuwa kijiji na kufanya shughuli zao mwaka 1976 na Mwalimu Nyerere, lakini sasa wameshaishi zaidi ya robo tatu ya eneo lile lote, lakini inaonekana kwamba Wizara ya Mifugo wanasema ni eneo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunomba ili kupunguza migogoro, Serikali itumie akili ya ziada, ikae na wananchi wale, tukubaliane. Kama kuna haja ya kuhamisha mnada kutoka eneo lile kwa sababu sehemu ndogo tu chini ya robo ndiyo unatumika kwa ajili ya mnada na sehemu nyingine zaidi ya robo tatu ndiyo wananchi wanaishi basi hiyo kazi ifanyike mapema ili watu waendeshe shughuli zao. Kwanza ilitangazwa kama kijiji, wana hatimiliki lakini Wizara wanasema ni eneo lao pia. Kwa hiyo, huo nao ni mgogoro ambao naamini kwamba ukianza kujadiliwa ilileta shida katika kukwaza shughuli za kimaendeleo, lakini pia kupoteza mwngi sana wa viongozi kwenda kujadiliana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 44 na 45 inazungumza habari ya barabara. Ninapozungumza sasa maeneo mengi sana ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam na hasa Jimbo la Ukonga Mwenyekiti unafahamu, unatoka Ilala. Sasa hivi Dar es Salaam ile wakati wa mvua haipitiki na bahati mbaya ile mvua ikinyesha kwa muda mchache sana

maana yake inaonesha ama miundombinu imechakaa au kazi haikufanyika vizuri. Lakini tunazo barabara kutoka Kitunda - Kivule - Msongola ambapo mkandarasi yupo zaidi ya miezi kumi amechimba mashimo pale. Nimemwambia Waziri anayehusika, nimewaambia watu wa *TANROADS* pale. Huyu mtu amekaa miezi kumi, amesababisha kero kubwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI*,* kuna hoja inazungumzwa hapa ya *TARURA,* mimi kwa maana ya Manispaa ya Ilala, hawa watu walipokuja wamefanya kazi kubwa sana pamoja na kwamba kuna ugumu wa fedha. Kwa hiyo, nilikuwa naomba na maoni yetu ni kwamba ingewezekana hii fedha ya *TARURA* ya *TANROADS* ikawekwa asilimia 50 kwa 50 kwa sabau barabara nyingi ziko vijijini. Ili barabara zetu zitengenezwe na wakati wa mvua kuwe na mawasiliano iweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikumbushe tu kumekuwa na mambo mengi sana hapa lakini mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya TAMISEMI na Utawala. Tumepata taabu ya kujadili hii habari ya Tunduma. Ningemuomba Waziri Mkuu na Mawaziri wanaohusika kitendo cha ile Halmashauri kukaa zaidi ya miezi kadhaa kutokuwa na vikao hata bajeti ambayo imeletwa maana yake bajeti ile haikujadiliwa na Baraza la Madiwani na Mbunge na wananchi wamelalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitokea kuna uharibifu wa mali maana yake Madiwani wanajitoa, watumishi ndiyo wanapata lawama katika utendaji. Hili ni jambo ambalo halikubaliki, lifanyiwe kazi, hatua zichukuliwe. Wawakilishi wa wananchi wafanye maamuzi kwa kodi ya Watanzania wao ili waweze kujipelekea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bajeti ya Serikali, maji yamepata asilimia 25.32, afya ilipata asilimia 25, kilimo ni asilimia 18, TAMISEMI yenyewe ni asilimia 31. Katika mazingira hayo ndiyo maana Wabunge wanasema ni muhimu fedha ya maendeleo iliyotengwa mwaka wa fedha 2017/2018 ipelekwe ikamilishe Miradi ya Maendeleo vinginevyo tutakuwa

tunapoteza muda hapa. Tunajadili bajeti ya muda huu lakini bajeti iliyopita haijatekelezwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaposimama awaambie Wabunge na Watanzania mpaka sasa fedha ya maendeleo imepelekwa kiasi gani katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 48 unazungumzia habari ya elimu. Mimi nimpe ujumbe Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana katika eneo hili kwamba kwanza hatuwezi kuboresha elimu kama tunatunga maswali ya kuchagua mpaka hata maswali ya hesabu kwenye mitihani ye sekondari na kisingizio kikubwa ni kwamba hakuna muda. Haiwezekani tukapunguza uelewa kwa sababu ya kusingizia muda. Tupunguze maswali lakini wanafunzi wetu wapimwe uelewa. Kwa mfano, katika shule zetu za msingi na sekondari, tuna upungufu mkubwa sana wa matundu ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli inatakiwa Serikali ije na mkakati. Kwa sababu kwa karne hii, Taifa la Tanzania kuzungumzia habari ya matundu ya vyoo kwamba kuna upungufu mkubwa maana yake unawaambia watu kwamba watu wetu wengi, wanafunzi na walimu wanaenda kujisaidia porini na kwa hiyo, wanachafua mazingira, walete kipindupindu na magonjwa mengine ya kuhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha tuna upungufu wa matundu ya vyoo, shule za msingi 239,716; sekondari 19,122, madarasa maana yake watoto wanakaa chini, tuna upungufu wa madarasa 107,547, nyumba za walimu shule ya msingi peke yake ni upungufu wa nyumba 178,435; sekondari 69,816.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inamaanisha bado tunayo safari ndefu sana ya kuboresha elimu. Ukizingatia Sera ya Elimu ni kama kuna mkanganyiko mkubwa sana lakini ningeomba ili tuboreshe elimu mi lazima tunzingatie mambo ya msingi ya mahitaji. Upungufu wa walimu wa sayansi, vitabu, maabara na vitu vingine kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa dhati kabisa, kuna hoja imeletwa nzuri sana ya elimu bila malipo lakini jambo hili limekuwa na mkanganyiko. Tukubaliane, kwa mazingira yaliyopo Serikali haitaweza kujenga madarasa yote yaishe, huo ndiyo ukweli! Serikali haiwezi kutoa chakula kwa wanafunzi wote mashuleni kwao, lakini ni lazima tukubaliane tuwe na lugha nzuri. Tushirikishe wadau mbalimbali ili tuboreshe elimu ya Tanzania. Kumekuwa na hoja hapa ya shule za *private* na shule za sekondari. Ningeishauri Serikali iweke msimamo kuboresha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kengele ya pili. Ahsante sana, unga mkono hoja. Mheshimiwa Innocent Bilakwate, dakika kumi kwa agizo la Katibu wako.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa nguvu na afya kuwepo mahali hapa, lakini nichukue pia nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri zinazofanyika. Ndugu zangu Watanzania wanaona yale yanayofanyika. Kwa hiyo, ninampongeza Mheshimiwa Rais, anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kipindi hiki kama Watanzania tuko kwenye vita na ni vita ya kiuchumi. Vita ya kiuchumi kuna watu ambao watatu-*support,* lakini wapo watu wengine ambao watabeza, lakini kitu cha muhimu sisi tuangalie ni wapi tunakoenda na lile ambalo tumelikusudia. Hao wapiga debe tuachane nao, siku zote nilishawahi kusema hapa Bungeni, mara nyingi wapiga debe huwa sio wasafiri. Ukiwa kwenye kituo cha mabasi utaona watu wanasema twende, twende lakini mwisho wa kusafiri hawaendi. Hao wapiga debe tuachane nao tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii niongelee kwanza upande wa afya. Niipongeze Serikali yangu, Kyerwa tulikuwa hatuna kituo cha afya hata kimoja, lakini sasa hivi tuna kituo cha afya kimekamilika, kiko vizuri na niishukuru Serikali wamenipa shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuboresha kituo cha Mlongo. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali, bado tuna upungufu wa watumishi na ukilinganisha kwa mfano Wilaya yangu ya Kyerwa bado tunahitaji zaidi huduma za afya. Nina Kata 24, naomba sana Serikali kwenye mgao huu ambao mnaenda kugawa Hospitali za Wilaya 67, naomba na Wilaya yangu ya Kyerwa ipewe mgao kwa sababu tunahitaji sana huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa maji, wengine tunapopongeza wanasema tunajipendekeza lakini mambo kama yamefanyika lazima tupongeze. Kwenye Wilaya yangu ya Kyerwa nimepewa zaidi ya bilioni mbili na milioni 900. Sasa hivi tumeweza kuboresha miradi midogo kwa mfano mradi wa Kaishori, Rutunguru na Isingilo, mradi wa Mabira, hii ni miradi ambayo itawahudumia wananchi lakini kwa muda mfupi tumeweza kufanya usanifu wa mradi mkubwa ambao huu mradi utaweza kuwahudumia wananchi wa Kata 15 kati ya 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Serikali bado tuna uhitaji sana wa huduma ya maji. Kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu, niiombe sana Serikali ile shilingi 50 ambayo tumeomba iongezwe bado uhitaji wa maji kwa wananchi wetu ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Serikali ilizingatie na iweze kuliongeza. Niiombe sana Serikali, kwenye mradi wetu ambao tumeshafanyia usanifu tutakapomaliza kutangaza *tender* ninaamini Serikali yetu ni sikivu tutapatiwa pesa kwa ajili ya kukamilisha huu mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la *TARURA,* Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tunaongea sana hapa Bungeni tunasema miradi inaharibika kwenye Halmashauri, haisimamiwi vizuri. Serikali imeleta chombo kizuri ambacho ni *TARURA.* Mimi niwaeleze ukweli Waheshimiwa Wabunge, Mbunge una uwezo wa kukaa na yule Meneja wa *TARURA* mkajadiliana miradi ambayo unayo kwenye jimbo lako, lakini ninashangaa leo Wabunge ninyi ndiyo mnashauri irudishwe kwenye Halmashauri, kwa nini mlikuwa mnapiga kelele? Hili niiombe Serikali, ushauri mwingine tusiusikilize. *TARURA* wameanza vizuri, kwa muda mfupi kwenye jimbo langu wameonesha jambo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo niishauri Serikali tuongeze, badala ya asilimia 70 kwenye *TANROADs* tufanye nusu kwa nusu au kama ikishindikana tufanye asilimia 45 kwa 55 kwa sababu barabara nyingi ziko vijijini na wazalishaji wakubwa wako vijijini. Kwa hiyo, niombe sana Serikali hili ilizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la umeme. Tunahitaji umeme, kule kwetu Kyerwa bado kabisa, kwa hiyo, niombe sana waendelee kuongeza uwezo wa kuzalisha umeme ili wananchi wetu wapatiwe umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilizungumzie ni suala la kahawa. Ninaamini Serikali yetu ina nia njema kwa ajili ya kuwakomboa wakulima hao ambao wameachwa muda mrefu. Wakulima hawa walikuwa wanauza kahawa kwa butura ambayo butura wanauza 20,000 na yule anayenunua anakuja kupata zaidi ya 100,000. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali, ilisimamie hili kwa karibu kwa sababu hii na yenyewe ni kama vita. Wale waliokuwa wananunua na wao wangetamani hili la Serikali lisifanikiwe. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo niishauri Serikali kama walivyochangia Wabunge wengine, hawa wananchi walishazoea kahawa kabla haijakomaa wanaweza kuuza butura sasa kukomesha biashara ya butura,

tuanzishe *SACCOS* ambazo zitaweza kuwahudumia hao wananchi kabla kahawa haijakomaa aweze kutatua matatizo yake. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali iweze kulizingatia tuweze kuwakomba wakulima ambao wameachw amuda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nishauri kwa upande wa kahawa. Kuna madeni ambayo walikuwa wanadaiwa hawa *KDCU, KCU,* haya madeni yasije yakahusishwa na wananchi wanapouza kahawa zao. Madeni watafute namna ya kuwalipa, lakini sio wananchi wanaenda kulipa madeni, wananchi hawakusababisha haya madeni. Kwa hiyo, kama Mbunge ambaye natoka Mkoa unaolima kahawa, suala hili lisije likahusishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nishauri Serikali katika zao hili la kahawa. Kama kuna uwezekano waajiri watu kuliko haya mambo ya kuchaguana. Ndiyo maana wanachagua hata watu wengine ambao hawana uwezo, mwisho wa siku wanakuja kuharibu. Kwa kuwa, Serikali ina nia ya dhati niiombe sana Serikali wawekwe waajiriwa ambao wana uwezo kama ni wahasibu, kama ni mameneja ambao wataweza kusimamia haya mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa MWenyekiti, kitu kingine tuombe sana Serikali iwezeshe hivi vyama vya msingi kwa sababu sasa hivi hawana pesa na walikuwa hawajajiandaa ni kama wameshtukizwa. Sasa jamno ambalo wameshtukizwa leo unawaambia wanunue kahawa na huko kwenye mabenki wanadaiwa. Hii itakuwa ngumu na inaweza ikasababisha chuki kwa wananchi kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niendelee kuipongeza Serikali na niendelee kuwatia moyo. Serikali songeni mbele, kazi mnayoifanya ni kubwa, Watanzania wanaona na kwa muda mfupi kwa kweli mmeonesha mabadiliko makubwa. Watanzania wako wengi wanawaunga mkono. Hizi kelele tuachane nazo tusonge mbele. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa William Dua Nkurua dakika tano halafu Mheshimiwa Mchengerwa dakika kumi.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda ninukuu ule ukurasa wa 27 ambapo Serikali imesema; "Serikali imeamua kuweka mkazo maalum wa kuyaendeleza mazao matano ya biashara ambayo ni chai, kahawa, korosho, pamba na tumbaku. Lengo ni kuongeza mapato ya wakulima."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na wazo hili zuri la Serikali kwa sababu kama tutafanikiwa ni hakika kwamba tutakuwa tumewakomboa wananchi kwa sababu asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina hofu katika eneo hili hasa katia zao la korosho. Ili korosho izalishwe, jambo kubwa kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba pembejeo inapatikana kwa haraka na kwa wakati jambo ambalo kwa sasa nina mashaka halitafanyika kwa sababu ili korosho zipatikane mapema ni lazima mwezi wa tano wananchi waanze kupulizia *sulphur,* lakini mpaka sasa mimi kama Mbunge na wananchi hatujui ni lini *sulphur* itapatikana, itatolewa bure kama mwaka jana au itanunuliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali haijaweka wazi namna gani wananchi watapata *sulphur.* Hilo ni tatizo ambalo nina uhakika lengo la Serikali ambalo limendikwa hapa halitafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kwamba, korosho ina utaratibu wake, sisi kama wakulima wa korosho, korosho inapokwenda nje inatozwa *export levy* na ile *export levy* ina utaratibu iliwekewa, 65% ya *export levy* inakwenda kuendeleza zao la korosho na 35% inabaki kwenye Mfuko

Mkuu wa Serikali. Lakini mpaka leo ile 65% ya wananchi haijaenda. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba, korosho mwaka huu hazitakwenda vizuri kwa sababu pesa ambayo ingekwenda kueneza zao la korosho haijaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi ile ni sheria ambayo ilitungwa katika Bunge hili kwamba 65% lazima iende Bodi ya Korosho, ili ikaendeleze korosho. Kwa hiyo, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu iangalie vizuri imuambie Waziri wa Fedha apeleke pesa 65% ya hizo ambayo ni shilingi bilioni 110 iende kwa wakulima wa korosho kwa sababu ni ya kwao kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, namkumbusha Waziri wa Fedha asivunje Sheria ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea hapa inakuwa kama tunakuwa na tamaa ya hizi fedha. Na hapa nakumbuka ile hadithi ya babu yangu aliyonieleza kwamba, kulikuwa na mzee alikuwa na shida ya fedha, alipomuomba Mwenyezi Mungu akampa kuku anayetaga yai la dhahabu kwa hiyo, kila siku alikuwa anapata yai la dhahabu. Huyu mzee akaingia tamaa akaamua kumkamata yule kuku na kumkamua, ili apate mayai mengi kuku akafa na ikawa ndio mwisho wa kupata fedha, kupata mayai ya dhahabu. Sasa hii tamaa ya Serikali ya kuangalia ile pesa itauwa zao la korosho; huo ni ushauri naomba Ofisi ya Waziri Mkuu izingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni suala la maji, Serikali kweli imekusidia kuhakikisha kwamba wananchi tunapata maji safi na salama hasa katka miji mikuu na vijiji vyetu. Lakini nataka niishauri Wizara ya maji, kule Nanyumbu Serikali ilishafanya upembuzi yakinifu wa kutoa maji mto Ruvuma mpaka Mji Mkuu wa Wilaya yetu ambapo ni Mangaka. Upembuzi yakinifu ulianza 2015 mpaka leo hatujapata majibu. Sasa kwa hali hii wananchi hawajui kinachoendelea na wananchi wanataka kujua Serikali yao itawatekelezea vipi huu mradi wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, hasa Waziri wa Maji, ninakuamini sana katika utendaji wako na

nilikupeleka mpaka kwenye chanzo cha maji pale Mto Ruvuma ambako maji yatatoka kuja Mjini Mangaka. Lakini mpaka leo wananchi wanashindwa kujua kitu gani kinaendelea, naiomba Serikali ihakikishe kwamba huu mradi mkubwa wa maji ambao Serikali inataka kuuleta pale Mjini Mangaka unaufuatilia vizuri na unausimamia na hatimaye wananchi wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni umeme; umeme, kama nchi tunasema kwamba, tunatembea kwa 60% labda, vijiji veytu vinapata umeme labda 60%. Sasa hofu yangu ni kwamba hatugawi huu umeme vizuri kwa mtawanyiko ulio sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri *REA* yafuatayo, kama inataka kuutawanya umeme vijijini tutembee kwa asilimia inayofanana, tukisema Taifa tumepeleka umeme vijijini kwa 60% basi tuwe tumekaribiana, lakini kwa mfano leo Nanyumbu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mchengerwa dakika 10.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri. Lakini niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa juhudi zake kubwa za kufanikisha utawala bora wa kujenga ustawi wa maendeleo ya uchumi jamii wa Taifa letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengi mazuri yamezungumzwa na mimi kwa niaba ya Warufiji na Wandengereko wote duniani niseme tu kwamba tunaipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri iliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Rais wetu kwa kuchagua Mawaziri wa Nishati wazuri wachapa kazi ambao leo hii kuliwaka umeme eneo nusu la Rufiji, lakini hivi tunavyozungumza maeneo mengi ya Rufiji sasa yanakwenda kuwaka umeme, ikiwa ni pamoja na ahadi ya Waziri wa Nishati kwamba sasa kule Kata ya Ngarambe watapata umeme na nimeambiwa leo na kesho Kata ya Mwasenyi watawashiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengi mazuri ya kuzungumza kuhusiana na sifa za Serikali ya Awamu ya Tano, lakini kwa uchache wa muda naomba nijielekeze katika hoja ambazo nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu akisimama hapa awaeleze Watanzania. Kamati ya Katiba na Sheria ilimtaka Msajili wa Vyama vya Siasa kutatua migogoro iliyopo katika vyama vya siasa. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu akisimama kwenye Bunge lako hili Tukufu awaeleze Watanzania je, Serikali ina juhudi gani za kutatua migogoro ya vyama vya siasa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kabisa kwamba, migogoro ya vyama vya siasa inakwenda kujenga taswira potofu kuhusu kuminywa uhuru wa siasa na demokrasia. Waziri Mkuu atueleze je, migogoro hii inasababishwa na mazalia ya mambo gani yanayohitaji kupatiwa ufumbuzi? Je, ni historia ya nchi yetu? Je, ni uhuru wa Tanganyika? Je, ni Mapinduzi ya kule Zanzibar? Au ni sintofahamu ya elimu ya uraia? Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha masomo ya uzalendo na masomo ya umoja wa kitaifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kabisa kwamba, uzalendo na utaifa unajengwa kama ambavyo ilivyo kwa Masheikh, Mapadri na Maaskofu wanajengwa na kuandaliwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta mapinduzi ya kifikra unaodhamiria kuzalisha elimu ya vyama vya siasa inayotokana na mawazo duni ya udumavu yasiyoendana sambamba na mageuzi ya dira ya Serikali ya Awamu ya Tano?

Mheshimiwa Waziri Mkuu akisimama hapa basi atuelezee je, Serikali wakati tukiwa tunajielekeza katika suala zima la kuwaangalia Watanzania na kuangalia uzalendo uliopo pamoja na fikra za Watanzania, je, Serikali na ofisi yake inajipanga vipi kutoa elimu ya utaifa na kuondokana na msongo wa Taifa ili kuondokana na maporomoko ya miiko na maadili ya Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu akisimama hapa pia awaeleze Watanzania yalikuwa ni mawazo yapi ya Baba wa Taifa wakati wa kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi? Lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu awaeleze Watanzania atakaposimama hapa makutano ya mawazo ya vyama vya siasa na ni kwenye ndoto gani ya Taifa letu? Na je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kuondoa kusigana na huku kusigana kunasababishwa na ombwe la kitu gani linalosababisha kutofautiana kati ya wanasiasa, ili kuweza kujenga jamii nzuri ya Watanzania ambao kwa kweli wanailinda amani ya nchi yao na kuwa na umoja wa kitaifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu akisimama hapa basi awaeleze Watanzania Ibara ya 8 ya Katiba inatambua kwamba, ustawi wa wananchi unajengwa na Serikali yao, lakini pia Ibara ya 26 ya Katiba inatambua na inakataza kuondoa mgawanyo au kufanya makosa ambayo ameainishwa katika Katiba au makosa yaliyoainishwa katika sheria tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu akisimama hapa basi aelezee kuhusiana na mgawanyo wa pato la Taifa, yako manung'uniko mengi. Tunatambua wananchi wa Rufiji, wananchi wa Pwani, wananchi wa Kusini tunatambua kwamba, kipo kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kuendeleza Hifadhi ya Selous, lakini tunapata taarifa kwamba, kiasi kile cha fedha kimepelekwa kuendeleza Ruaha. Haya ni miongoni mwa mambo ambayo wananchi wengi wa Rufiji, Kusini na maeneo mengine wanayalalamikia, basi Mheshimiwa Waziri Mkuu ukisimama hapa ni vyema ukawaeleza wananchi wakatambua ni

namna gani na ni kwa nini mgawanyo wa pato la Taifa umekuwa ni kikwazo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaposimama hapa atambue kwamba, wananchi wa Rufiji wana imani na Serikali yao ya Awamu ya Tano, lakini pia, wamenituma nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, tarehe 02/03/2017 Rais Dkt. John Pombe Magufuli alifika Ikwiriri na akaahidi ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka Nyamwage kuelekea Utete. Mheshimiwa Waziri Mkuu tukuombe wananchi wa Rufiji sasa jambo hili mpelekee Rais wetu na atambue kwamba wananchi wa Rufiji wana imani kubwa na Serikali yao na atambue kwamba tumebakiza miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ahadi hii ya ujenzi wa barabara kiwango cha lami ilianza mwaka 2017 na Mheshimiwa Rais alisema itajengwa kabla ya mwaka 2020 basi, atambue kwamba ni kilometa 33 na kwamba tumebakiza miaka miwili tu. Na Serikali ina mpango gani sasa kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo kwa kweli, ni msingi wa wananchi wetu wa Rufiji na Pwani na maeneo mengine sisi tunampa hongera sana Rais wetu wa Awamu ya Tano kwa jitihada zake za dhati kabisa za ujenzi wa bwawa la *Stiegler's Gorge* kama ambavyo nimetanguliza kusema. Na niseme tu mwenzangu amesema kwamba *Stiegler's Gorge* ilianza miaka ya 1960, lakini mimi nataka kukataa niseme kwamba *Stiegler's Gorge* kama sisi wa Rufiji tunauita *STIGo,* ilianza miaka ya 1956 wakati wa harakati za *TANU,* harakati za uhuru wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mwalimu Nyerere alidhamiria kujenga umeme huu kuweza kuikomboa nchi yetu. Na sisi tunaunga mkono na wananchi wa Rufiji tunaunga mkono sana, tunachoomba Serikali yetu ya Awamu ya Tano kama ilivyo madini katika maeneo mengine na wananchi wa Rufiji wanaomba kunufaika na *Stiegler's Gorge.* Tuiombe

Serikali kuhakikisha kwamba mradi huu wa *Stiegler's* unakwenda kujenga barabara yetu ya kutoka Mwasenyi - Mloka kuelekea Ikwiriri, lakini pia, kutoka Mwasenyi - Mloka kuelekea Kibiti na maeneo mengine ya Morogoro yanayopakana na *Stiegler's Gorge. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni ndoto za Mwalimu Nyerere hatuna haja wala hakuna sababu ya kuzibeza. Na kwa kweli, Rais Magufuli amefanya maamuzi magumu na ni miongoni mwa Marais ambao tuliwasubiri kwa muda mrefu sana. Na sisi tunampa pongezi sana kwa jitihada hizi. Na Warufiji tuko tayari kutambua mradi huu utakwenda kuinufaisha nchi, lakini utakwenda kuinufaisha Rufiji kwa mambo mengi mazuri yanayokuja; ujenzi wa barabara, ujenzi wa madaraja, Daraja la Utete litajengwa kuiunganisha Rufiji na maeneo mengine ya Kusini. Tunampongeza sana Rais wetu, lakini pia tunamtakia kila la heri katika kutekeleza mambo haya yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kapufi, ajiandae Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Awali ya yote naomba nipongeze kiteno cha Serikali kuwarjesha watumishi. Napongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo kwa maana ya ukurasa wa saba unaozungumzia mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano kuna eneo linalozungumzia kujenga ari ya uzalendo kwa kuilinda na kuisemea nchi yetu bila woga, kudumisha amani, utulivu na mshikamano. Eneo hili bahati nzuri jana tulibahatika kupata semina ya Kamati inayoshughulikia masuala ya mauaji ya Kimbari kwa maana ya *genocide.* Tumeambiwa sisi kama Wabunge, tunayo nafasi

kubwa ya kudumisha amani, lakini ni vitendo vidogo vidogo ambavyo vikiachiwa, vitendo hivyo vikiendelea bila ustaarabu vinazaa mauaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hiyo, kama haitoshi tunaambiwa tushughulikie mapema kwa maana ya *conflict early warning system.* Tukishughulikia mapema tutaendelea kutengeneza nchi yenye amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 54 na 56 unazungumzia suala la afya. Katika eneo hili la afya naomba nijikite kwa maana ya Hospitali ya Mkoa ya Katavi. Bajeti iliyotengwa takribani shilingi bilioni 11, kwa suala zima la utoaji wa fedha na nilikuwa naomba Waziri Mkuu anisaidie katika hili, leo asubuhi nilisikia taarifa nchi ikipongezwa kwa maana idadi ya wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi wanaanza kupungua, ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukiipongeza nchi kwa hilo, kule Katavi unapoongelea ujenzi wa hospitali ya mkoa ambayo tunahitaji takribani shilingi bilioni 11 kwa kasi ya utoaji fedha, mara mmepewa shilingi milioni 500, mmebahatisha shilingi bilioni moja, maana yake tunakwenda miaka 11 ili kumaliza ujenzi wa hospitali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana. Na ninaliomba hilo kwa sababu, unafahamu Jiografia, umbali kule tuliko na bila msaada wa hilo na kwa wakati huu hospitali ya Manispaa ya Mpanda ndio inabeba dhamana ya kuwa hospitali ya mkoa, imeleemewa sana, inahudumia takribani Wilaya tatu, Majimbo matano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana hata pale tunapozungumzia kuwezesha fedha, ili kupunguza mzigo nilikuwa naomba hilo tujaribu kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kwa maana ya hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 31 mpaka 32 unazungumzia masuala ya umwagiliaji kwa ujumla wake

kwa kupitia kilimo. Tunao mradi mkubwa wa Mwamkuro, mradi huu kwa maana ya bajeti ya mwaka 2013/2014 ulitengewa milioni 294 na fedha hizo zilikuwa zimelenga kukamilisha kilometa mbili, lakini umbali wa mradi mzima ni kilometa tatu. Eneo hilo ni ukanda mzuri ambao una uzalishaji mkubwa wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nakiomba, ili thamani ya fedha iweze kuonekana kwa kiwango kile cha fedha kilichotengwa ambacho kimekwenda kukidhi kilometa mbili tu hatutaweza kuiona thamani ya fedha. Ni vizuri fedha ikatengwa ya kutosha ambayo itufikishe kwenye zile kilometa tatu zilizokusidiwa na ninalisema hilo makusudi kwa sababu kwa kupitia kilimo cha umwagiliaji na eneo lile ni zuri lina rutuba ya kutosha tutaweza kuzalisha mazao ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoke hapo, kwenye suala zima la nishati. Nafahamu jitihada za Serikali na kwa maana ya Mkoa wa Katavi tunazo mashine mbili pale zinasaidia japo umeme unakatikakatika, lakini muarobaini wa kutatua matatizo ya umeme...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Simbachawene, ajiandae Mheshimiwa Vuma.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ahotuba yake nzuri sana na niwapongeze pia Mawaziri Mheshimiwa Jenista na wasaidizi wake wanafanya kazi nzuri sana tunawaona na tunawatia moyo endeleeni hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote ile duniani inaongozwa kwa dira na kwa sisi Tanzania dira yetu ni ya 2025 na kwa sasa tunatekeleza dira ya miaka mitano na katika miaka mitano tumekuwa tukitoa hapo kila mwaka

tunatoa kipande na tunatekeleza. Kwa sasa tuna Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2018/2019, nichukue nafasi hii kupongeza sana, nimeona orodha ya miradi ya kimkakati. Niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano kwamba, miradi hii kwa kweli, iko barabarani na iko sambamba kabisa na *vision* yetu ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kokote kule na hasa kwenye nchi ambazo zimeendelea na zilizopata uhuru karibia na sisi Tanzania, nyingi sana zimepiga hatua na shabaha zao kufikiwa kwa sababu ya maamuzi ya dhati. Sisi hapa udhati wetu wa maamuzi, napata mashaka. Wakati *standard gauge* leo inajengwa wengine wanasema hiyo haina umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunajenga barabara na miundombinu inayounganisha, hapa tulikuwa hatuna barabara kwa mfano ya kutoka Iringa kupitia Dodoma kwenda mpaka Babati sasa tunaungana na Arusha; na hiyo nayo haina maana, lakini watu wanapita humo humo haina maana. Wakati wanafunzi wanalipiwa gharama kubwa sana na Serikali karibu kila mwezi shilingi bilioni 22 na ushee hilo nalo linaonekana halina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sidhani kama ni sahihi sana kwa sababu kama tutasema kila jambo tunabeza, kila jambo jema linabezwa, basi maana yake ni kwamba hatujui tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, rai yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba, hebu wakati mwingine tuzungumze kama Watanzania na pengine masuala haya ya dira yafundishwe hata kwenye shule za msingi, kwenye sekondari, kwenye vyuo vikuu yafundishwe kwa sababu hata ukimwambia Mtanzania hapa anayemaliza *degree* ya chuo kikuu kwamba hivi dira yetu sisi mpaka tunapofika mwaka 2025 tunataka tuwe tumefika wapi, unaposema suala la uchumi wa kati wengine hatuelewani, ama kwa makusudi, lakini nadhani iko haja ya kusisitiza watu kupata elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi ambazo zimepiga hatua kwa shabaha zao walizoziweka hazikuwa legelege na kuwa na mawazo ambayo yanasigana kama sisi. Wakati jambo zuri ndege zinashuka hapa, ndege tatu zimefika tunasubiri hizo mbili zije, tayari wameanza kusema ndege ni za nini? Sasa unashindwa kuelewa hivi wanajua tunakokwenda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kujenga uchumi bila kuwa na *national carrier,* uchumi wa kisasa unajengwa kwa njia za usafirishaji. Kwa hiyo, nisihi sana kwamba, si ajabu hata humu Wabunge wengine wenzetu hawajui tunakwenda wapi na ndio maana wanavuta kamba tunakotaka kuelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisihi kwamba kama tunataka kuwa Japan, kama tunataka kuwa kama China, ni lazima tuweke dira. Wenzetu Wachina juzi wameamua kuwa na Rais wao wa maisha. Uamuzi ule usifikiri ni wa kitoto ni uamuzi wa watu waliofikiri sana. Wameona kwamba Xi Jinping amekuja na ku-*address* kwa hotuba zake tatu tu. Ameeleza msingi wa *vision* yao wanayoitaka. Na sisi leo tunaye Magufuli ambaye anatupeleka kwa vitendo kwa kuangalia tunataka kuelekea wapi, lakini wako watu wanabeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Xi Jinping kwa hotuba tatu analibadilisha Taifa lenye watu wengi duniani la China, kumwamini kwamba anastahili kuwa Rais wa maisha, lakini sisi Magufuli anayetenda haya tunayoyaona makubwa tunasema hatuelewi anataka kutupeleka wapi. Kwa hiyo, niseme tu rai yangu, Mheshimiwa Waziri Mkuu nchi hii ni yetu wote ni Watanzania, lakini pale yanapofanyika mambo mazuri ni lazima wote tuunge mkono kama Watanzania tusikatishane tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnafanya kazi nzuri na kubwa sana, mnafanya kazi ya kujitolea kweli kweli lazima tuwapongeze. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza wewe binafsi kwa kazi nzuri unayofanya. Imani yangu ni kwamba

watanzania hawa ni vizuri sasa tukawaeleza tunayoona picha ya tunakokwenda. Kama... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Vuma ajiandae Mheshimiwa Maige.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, ahsante kwanza awali ya yote nipende kupongeza na niseme naunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu.

Pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutupa uhai huu, Waziri Mkuu hotuba yako ni nzuri sana. Imeeleza ni namna gani ambavyo Serikali imejipanga na kujipambanua lakini namna gani ambavyo imekuwa ikitekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwanza na yale mambo ambayo yapo kwenye Jimbo langu. Nipende kushukuru Serikali, nipende kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa hela ambazo ametupa jimbo la Kasulu Vijijini shilingi milioni 500 kwa ajili ya ukarabati wa kituo cha afya pale Nyakitonto lakini pia shilingi milioni 200 kwa ajili ya ukarabati wa kituo cha afya pale Hospitali ya Muyowozi lakini nipende kushukuru Serikali pia kupitia Waziri wa Afya kwa namna ambavyo ananipa ushirikiano pamoja na TAMISEMI kwenda kuanzia Hospitali ya Wilaya pale Muzye, pale mkandarasi atamaliza kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la viwanda nipende kumwomba Mheshimiwa Mwijage na Serikali kwa ujumla kwamba kuna mwekezaji alikuja kwetu pale *Kigoma Sugar* kwenye Jimbo langu. Mwekezaji yule alipewa ardhi ili aweze kufanya kilimo cha miwa na kuanzisha kiwanda, lakini ameshindwa kufanya hivyo na ameenda kinyume na mkataba. Sasa tunaomba Serikali iweze kumnyang’a mtu

huyu eneo lile na hatimaye waweze kuwavutia uwekezaji kwa watu wengine ili kwamba watu wengine waweze kujitokeza na kufanya kilimo cha miwa na hatimaye kiwanda cha sukari tuweze kuwanufaisha watu wa Kasulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Maliasili na Utalii, tarehe 20 Julai kama sikosei Mheshimiwa Rais alikuja Wilaya ya Kasulu, pomaja na mambo mengine ambayo alisema aliruhusu wananchi waendelee kulima sehemu ya kipande cha msitu wa Makere kusini yaani Kagerankanda na alifanya hivyo kutokana na mateso makubwa ambayo wananchi walikuwa wakiyapata kwa kupigwa na watu wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu wako watu ambao sijajua kiburi wanakitoa wapi, wanaendelea kuwanyanyasa watu ambao wanaenda kulima Kagerankanda, hii haikubaliki ni kinyume cha maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, niombe chonde chonde Mheshimiwa Kigwangalla umenipa ushirikiano katika hili, tulimalize hili wananchi waendelee kulima vizuri na hatimaye waweza kufaidi kauli ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Waziri Mkuu chapa kazi, yasema nguvu ya mamba iko kwenye maji; na maji yako wewe ni sisi tupo, tuko nyuma yako tunaona kazi kubwa ambayo wewe pamoja na Mheshimiwa Rais mnaifanya kwa ajili ya Watanzania leo haya mambo mengine makelele hayo tuachane nayo nawaambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwepo Bungeni hapa kwa muda wa miaka kama miwili na kidogo. Moja ya kitu ambacho nimegundua humu Bungeni ni kwamba tunayo macho mawili ya kibinadamu. Liko jicho ambalo ni zima lenye afya lakini liko jicho ambalo lina chongo humu ndani. Nasema hivyo kwa sababu gani, haiwezekani watu tunawambia Serikali inajenga na imeanza ujenzi wa *Standard Gauge Railway* kutoka Dar es Salaam na Mkandarasi amepatikana na ujenzi umeanza lakini watu wanabeza wanaona kama ni reli ya udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,haiwezekani tuwaambie watu kwamba tunanunua ndege na ndege zimekwishafika tatu zimeonekana, lakini watu wanazibeza wanaona kama ni *parachute* sio ndege. Tunawaambia watu kwamba hawa watu huyu kwamba hao viongozi wenu wana matatizo, wanafanya makosa wanaenda kinyume na utaratibu na wanapaswa washughulikiwe kama wahalifu wengine wao wanaona hapana wanaonewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nipende kusema kitu kimoja, ifike pahala tujitahidi sana kutenganisha kati ya kazi ya vyombo na Mheshimiwa Rais maana mtu anafanya makosa, anaenda kinyume na utaratibu, anavunja sheria halafu akianza kushughulikiwa, unakuta watu wanasema kwamba anashughulikiwa na Mheshimiwa Rais nani kasema? Nani kasema, hii ni nchi ambayo inaongozwa kwa mujibu wa sheria mtu yeyote anapokuwa amefanya makosa inapaswa ashughulikiwe kama mhalifu mwingine. Haya maneno ya watu kukimbia kwenda wapi kwenda kwa mabwana zao kutafuta sijui...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba nianze kwanza kwa kupongeza sana hatua nzuri au kazi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi na Taifa linafahamu tuna bahati sana kipindi hiki kupata Rais mwenye maamuzi, kupata Rais ambaye analitumikia Taifa kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ambayo inafanyika sasa hivi ni miradi ambayo imekuwa ni ndoto ya Watanzania ya muda mrefu na ninaamini kabisa baada ya kukamilika kwa miradi hii hakika tutakuwa Tanzania ambayo itakuwa na uchumi wa kati, uchumi ambao utakuwa unaendeshwa kwa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana sasa Waheshimiwa Mawaziri ambao hasa ndio wanamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Rais, mtusaidie pamoja na sisi wenyewe katika kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais, katika kuhakikisha tunafikia malengo ambayo tunajiwekea. Nitazungumzia mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni suala la upelekaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo. Katika ahadi tulizozitoa kwenye sekta ya afya pamoja na elimu, tulisema kwamba tutajenga vituo vya afya kila kata pamoja na zahanati kila kijiji. Baada tu ya kuwa tumewaahidi hivyo kwa mfano wananchi Jimbo langu la Msalala wameitikia vizuri sana na kama ambavyo wengi mlisikia hata hapa juzi Naibu Waziri wa TAMISEMI alitambua kazi iliyofanyika kule kwamba hivi tunavyozungumza tuna maboma zaidi ya 50 ya zahanati na vituo vya afya; mengi yana miaka miwili na zaidi, wananchi wameshafanya kazi lakini fedha za ukamilishaji hazifetwi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu Wizara zote ziko yako, wasaidie Watanzania hasa ambao ni wananchi wa kawaida waliojitikia na kuchangia nguvu zao kuinua maboma haya ili fedha za ukamilishaji ziweze kutolewa kwa wakati. Imefika wakati kwa mfano kuna sehemu ambapo wananchi tunawahimiza waanzishe miradi mingine wanasita kuchangia kwa sababu tayari kuna miradi ambayo wameshaianzisha imekamilika kwa kukamilika maboma, lakini fedha za ukamilishaji hazijetwi kwa hiyo, wanaona kwamba yanaenda kubomoka au kuharibika na nguvu zao kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe sana Serikali itoe fedha za ukamilishaji wa maboma ya zahanati na vyumba vya madarasa pale ambapo majengo hayo yameshakamilika na tayari tulishaandika andiko la kuleta taarifa rasmi Serikalini kuhusu suala hili kwa maana ya Msalala peke yake basi nilikuwa naomba Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nilitaka kutoa ushauri kwa Mawaziri tupunguze sana kugongana na wananchi pasipo sababu za msingi. Nitatoa mfano wa suala mifugo na uvuvi. *Operation* iliyofanyika juzi ya uvuvi kudhibiti makokoro ni jambo jema, lakini nilitaka kumshauri sana Mheshimiwa Waziri Mpina bahati nzuri yuko hapa kwamba sasa tujaribu kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufahamu kwamba vyazo vya asili vya samaki haviwezi vikatosheleza Watanzania milioni 50 tulionao hivi sasa. Duniani kote nchi zinazosafirisha samaki wengi au mazao ya samaki kwa wingi zimeweka nguvu kubwa kwenye *fish farming*. Eneo hili la uvuvi wa ufugaji wa samaki hatujaliwekea maanani sana.

Mheshimiwa Mweyekiti, Nchi kama *Vietnam* ambayo ni nchi ya nne kwa usafirishaji wa mazao ya samaki duniani, asilimia 70 ya samaki wanaosafirishwa nje ni wale wanaofugwa sio wale wanaovuliwa kwenye bahari kuu au kwenye maziwa na mito. Ninaamini ziwa victoria ambalo limekuwepo miaka yote limekuwa likihudumia wananchi karibia milioni nanewa miaka ya nyuma, leo hii watanzania wanaozunguka eneo hili wamefika zaidi ya milioni 20. Hauwezi ukatarajia hata ukifanya vipi mahitaji ya samaki au mahitaji ya mazao ya samaki yataendelea kuwa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, kwa mfano kwenye suala la kuku miaka nyuma tulipokuwa tukitegemea kuku kawaida wa kienyeji wa kutoka Singida ilikuwa ni tatizo. Lakini baada ya kuanzisha ufugaji wa kuku wa kisasa hawa *broilers*, leo *pressure* ya mahitaji ya kuku wa kienyeji si kubwa kama ambavyo ingeweza kuwa kama tusingeweka nguvu katika ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine ni kwenye suala la maliasili, ukiangalia tungeendelea kupambana na wananchi, tungeendelea kupambana na wananchi wanaovuna...

**MWENYEKITI:** Zima *switch* hiyo, zima *switch* hiyo, izime hiyo *switch*.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** .. Kwenye misitu ya asili tusingeweza kama tusingeweka nguvu katika...

**MWENYEKITI:** Hebu tulieni muwaachie watu maalum wanaohusika na hiyo kitu. Tulieni, tulieni tuwaache wataalam wanashughulikia tatizo hilo. Kuna fire *extinguisher* pembeni hapo.

*(Hapa palitokea hitilafu ya umeme ndani ya ukumbi wa Bunge na kusababisha moshi kutaanda ukumbini)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba unilindie muda wangu. Nitaomba uniite utakapokuwa tayari ili niendelee. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Endelea athari imekwisha, *everything is under control.*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana, naomba niwape Waheshimiwa pole Waheshimiwa Wabunge kwa tafrani hii lakini naamini sasa hali ipo shwari tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia suala la kuwasaidia Watanzania waweze kuzalisha rasilimali ambazo zinatokana na kufanya kazi. Nilikuwa nasema kwa upande wa uvuvi, pengine itakuwa ni jambo la busara sana Wizara ya Mifugo na Uvuvi kusaidia wananchi waingize nguvu au wafanye kazi ya kufanya *fish farming*. Kwa kufanya hivyo tutaweza kupunguza migogoro ya wananchi badala ya kuelekeza nguvu katika kudhibiti wananchi kuwadhibiti wasivue samaki kwenye maziwa ya asili na mito vyovyote vile *production* au uzalishaji samaki kwenye maziwa ya asili utakuwa umepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nilikuwa ninaiomba sana Serikali kwa upande wa mifugo vilevile tumeshatambua

mifugo yetu, tumeshaitia alama sasa kinachotakiwa ni kuwasaidia wakulima au wafugaji kwa maana hiyo waweze kuwa na masoko ya mifugo yao. Wafugaji tumepambana nao tumewatoa kwenye maeneo ya hifadhi. Wanauliza swali la msingi kwamba sawa tumetoka hifadhini tuende wapi? Kuna mkulima mfugaji mmoja kuna wakati alikuwa ananiuliza kwamba hivi hawa ng'ombe mnataka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na Mahakama, katika Mahakama zetu kesi zinacheleweshwa sana, anaweza mtuhumiwa kukaa rumande kwa muda mrefu sana bila ya kesi ya kusikilizwa ingawa tumeona humu katika kitabu hiki kuna idadi kubwa ya mashauri yaliyosikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha mwaka 2017/2018, ni mashauri 494,525 katika mashauri 513,329, lakini bado kuna watuhumiwa wengi wako rumande zaidi ya miaka saba na wanasubiri mashauri yao kusikilizwa. Wakati mwingine hukumu inapokuja kutolewa muda alliokaa rumande ni mkubwa kuliko atakaoutumikia baada ya hukumu. Hali hii haileti haki kwa watuhumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya watu huwa wanapotosha maamuzi yanayotolewa na Mahakama katika mitandao na huwa wanasababisha watu kukosa amani na kuleta mtafaruku katika jamii. Wanaingilia maamuzi ya Mahakama jambo ambalo ni kosa kubwa sana. Naiomba Serikali ile Sheria ya Makosa ya Kimtandao *(Cyber Crime Act)* ifanye kazi yake ili mambo haya yakomeshwe. Wanaofanya makosa haya wapo na wanajulikana. Naiomba Serikali iwachukulie hatua kali za kisheria.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikupe pole na nimwombe Mwenyezi Mungu akujalie uendelee kuwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la demokrasia na utawala bora na haki za binadamu nchini mwetu linapotea kila siku. Leo Tanzania, wananchi wanatekwa na kuuawa, wanasiasa na wanaharakati pia wanahujumiwa na Tanzania hata waandishi wa habari na vyombo vya habari hawako salama. Hali hii haileti afya kwa Taifa. Tunaiomba sana Serikali na Wizara ya Mambo ya Ndani, usalama kwa wananchi ni jambo muhimu kwa mustakabali wa amani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza kuna vijana sita Pemba wametekwa na wa watatu kati yao hadi sasa hawajulikani walipo. Vijana hawa wametekwa Pemba Jimbo la Mtambwe na hadi sasa vijana watatu hawajaonekana nao ni Thuwein Nasor Hemed (30), Khamis Abdallah Mattar (25), Khadid Khamis Hassan (30). Tunaomba Serikali itupe jibu, je vijana hawa wapo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sukari ya Zanzibar kuzuiwa kuuzwa Tanzania Bara sio haki na ni uonevu mkubwa Zanzibar na maendeleo ya Wanzanzibari, jambo hili halileti afya kwa Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kodi hasa katika Bandari ya Dar es Salaam ni tatizo na ni kero kubwa, mustakabali wa biashara kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. Tunaiomba sana Serikali kulifanyia kazi suala hili ili kuleta nafuu kwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msamiati wa kero za Muungano sasa imekuwa hadithi zisizo na tija kwani kila siku kero hizi zinaongezeka na kuzidi kudumaza maendeleo ya Zanzibar.  Kama suala hili halikupatiwa ufumbuzi linaweza kutikisa Muungano hatimaye kuvunjika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwaweka watu mahabusu kwa muda mrefu bila kuwafikisha Mahakamani

sio jambo jema. Suala la Mashekhe wa Uamsho na dhuluma wanayofanyiwa sasa imekuwa haivumiliki tena. Ni lazima Serikali kutoa jibu juu ya Mashekhe hawa. Sasa ni miaka mitano wapo ndani bila kufikishwa Mahakamani, hii sio haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uonevu uliovuka mipaka na uvumilivu unafika mwisho. Ahsante sana.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dhana ya *D by D.* Serikali ya Awamu ya Tatu na ya Nne zimetumia mamilioni ya fedha za walipa kodi kugharamia maboresho ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ugatuzi wa madaraka ni pamoja na kupeleka rasilimali watu wa kutosha na kupeleka rasilimali fedha za kutosha na kuziwezesha Serikali za Mitaa kukusanya kodi katika Halmashauri zao kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imeua dhana nzima ya *D by D* kwa kunyang'anya Serikali za Mitaa vyanzo vikubwa vya mapato nazo ni kodi za majengo na kodi za mabango. Kunyang'anywa kwa vyanzo hivi ni kupunguza uwezo wa Serikali za Mitaa kuimarisha na kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa Bunge kupitisha sheria ya kuondoa *retention* kutoka Taasisi za Umma kama *TANAPA, Immigration,* Polisi na kadhalika ni kupunguza uwezo wa Taasisi hizi kutimiza wajibu wao kwa kutumia vyanzo vya mapato. Uzoefu umeonesha fedha zikishaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali hazirudishwi kabisa au zinarudishwa kidogo kwa taasisi husika. Matokeo yake ni huduma kuzorota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie upya uamuzi wake kwa sababu Serikali za Awamu ya Tatu na ya nne ziligundua kwamba ili taasisi zifanye vizuri waachiwe kutumia mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iimarishe jukumu lake la msingi la usimamizi na ufuatiliaji, jukumu ambalo bado Serikali haifanyi vizuri. Serikali inaposhindwa jukumu la usimamizi/ufuatiliaji na tathmini, inaibua *solution* nyepesi ya kuanzisha utaratibu/taasisi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuitazama upya dhana ya *D by D* na kuimarisha Serikali za Mitaa kama ilivyokusudiwa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami namshukuru Mungu kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora, yapo malalamiko mengi kuhusu utendaji wa baadhi ya Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Wakurugenzi na kadhalika kuhusu namna wanavyotekeleza majukumu yao. Baadhi yao bado wanafanya kazi kinyume na sheria za nchi, wanatoa matamko yanayogongana na maamuzi ya viongozi wengine wa Kitaifa. Kiburi hata cha kukataa kutekeleza maagizo ya Mawaziri na ubabe wa hali ya juu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, moja, utaratibu wa kuwapata viongozi *vetting* uimarishwe. Mbili, kuwepo semina za mara kwa mara kuwakumbusha na kuwaimarisha. Tatu, kuwaondoa katika utumishi wale ambao hawataki kubadilika. Taifa liwe na benki ya watumishi badala ya utaratibu wa sasa, yaani viongozi waandaliwe mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niandike kuhusu usalama wa raia, katika siku za hivi karibuni hofu imetanda miongoni mwa wananchi kutokana na maiti zinazookotwa maeneo mbalimbali ya nchi. Wananchi wanaotekwa majumbani mwao usiku bila maelezo. Baadhi ya wananchi kupigwa risasi hadharani na matamko ya vitisho kutoka kwa baadhi ya viongozi wa wananchi. Mazoea ya matukio haya, vyombo vya dola kutotoa wajibu kutasababisha chuki hata baadaye

kisasi na hivyo kuvuruga amani ya nchi. Nashauri matukio haya yachunguzwe kwa kina na majibu ya uhakika yatolewe kwa wananchi na kwa familia za wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, elimu, ipo haja ya Taifa kujadili kwa kina kuhusu mfumo wetu wa elimu. Sasa hivi nchi inasisitiza sana mfumo wa uchumi wa viwanda. Kama elimu yetu haitaelekezwa kwenye lengo hilo tutashindwa kufikia lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri turudishe elimu ya kujitegemea kwa vijana wetu wote kuanzia shule za msingi. Pili, nashauri vyuo vya *VETA* viimarishwe na wilaya ambazo vyuo hivyo havipo utafutwe uwezekano wa haraka wa vyuo hivyo kujengwa. Vijana wafundishwe kujifunza sio kwa ajili ya kuajiriwa bali elimu iwasaidie kujipatia ajira na kuchangia katika mkakati wetu wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na nchi jirani ina mkakati wa kuboresha mipaka yetu. Hatua hiyo imewafanya wananchi kuwa na hofu. Katika mpaka wa Tarakea Wilayani Rombo, wananchi wameishi katika mpaka hata kabla ya uhuru. Taarifa walizonazo ni kwamba wakati wa kunyoosha mpaka huo wataondolewa bila fidia yoyote. Naomba Serikali kutoa tamko kuhusu jambo hili ili kuwatoa wananchi hofu na kama itawaondoa ione uwezekano wa kuwalipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji nchini ni kubwa sana. Hata hivyo, tuna maji mengi sana katika maziwa na mito yetu. Wilaya ya Rombo ni mojawapo kati ya wilaya zenye tatizo kubwa sana la maji. Ukanda wa chini katika wilaya yetu ndio unaoathirika zaidi. Hata hivyo, tunashukuru kwa miradi inayoendelea. Pamoja na hayo, tunaomba vyanzo vya maji kutoka vijito toka Rongai vinavyotiririsha maji kuingia Kenya vitumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba na tunarudia ombi hili kwamba makorongo katika mito yetu ya msimu izuiwe ili kujenga mabwawa ambayo yatatumika kuhifadhi

maji ya mvua. Matumizi ya maji ya Ziwa Chala ambayo tuliambiwa ni ya Kimataifa ili hali wenzetu wa Kenya wanayatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ajira kwa vijana sasa ni bomu kubwa katika nchi yetu. Vijana wengi wamemaliza elimu kuanzia msingi hadi vyuo vikuu. Hata hivyo, ni wazi Serikali haiwezi kuajiri vijana wote. Kama nchi ni muhimu kuliangalia tatizo hili kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mifuko mbalimbali ya kuwasaidia vijana. Vile vile kuna asilimia kumi za vijana, wanawake na walemavu katika halmashauri. Utaratibu unaotumika katika kutoa pesa hizi ni wa upendeleo na kibaguzi na halmashauri hazipeleki pesa hizo ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri ianzishwe benki maalum kwa ajili ya kuweka pesa hizi ili zitolewe kwa utaratibu na masharti maalum. Itungwe sheria ili kuwabana Wakurugenzi kutoa pesa hizi. Wakurugenzi ambao hudharau kutoa pesa hizi wachukuliwe hatua za kinidhamu. Mkakati wa kuwatafutia vijana maeneo maalum ya kilimo uimarishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa Rombo wana vikundi ambavyo kama wangepewa ardhi wako tayari kwenda sehemu yoyote katika Jamhuri ya Muugano kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba kumpongeza Waziri Mkuu na watendaji wake na naomba kuwasilisha.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo endelevu yanahitaji umoja wa Kitaifa (ushindi ni ushirikiano). Tarehe 21 Februari, 2018, Kituo cha Demokrasia Tanzania *(TCD)* tulifanya mashauriano ya pamoja kati ya Viongozi Wakuu wa Dini na Viongozi Wakuu wa Vyama vya Siasa lengo likiwa kushauriana maudhui yaliyo kwenye lengo la 16 la Malengo Endelevu ya Dunia (Amani, Haki na Ujenzi

wa Taasisi Imara). Tulikubaliana kwamba kuna umuhimu wa kuendelea na mashauriano haya kwa kushirikisha Serikali kwa kuwa mapendekezo yetu yameshafikishwa Serikalini, ni vyema mashauriano haya yakafanyika haraka iwezekanavyo kwani kuna viashiria vya wazi vya kuvunjika au kutoweka kwa amani yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naikumbusha Serikali kwamba dunia ya leo ni meza ya mazungumzo. "Meli ya amani inazama nasi wasafiri tukiwa ndani."

**MHE. LUCIA U. M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niachangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu. Kumekuwa na ongezeko kubwa la usajili wa watoto wengi wa darasa la kwanza, lakini hakuna ongezeko la Walimu, madarasa na madawati. Naomba kuishauri Serikali kuajiri Walimu wa kufundisha, hasa madarasa ya awali, darasa la kwanza na la pili, ambapo Walimu wanaofundisha madarasa hayo ni wachache na shule nyingine hakuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naishauri Serikali kuwapa moyo wananchi ambao wamejitolea kujenga madarasa, lakini wanakatishwa tamaa na viongozi wanaposhindwa kuwasaidia wanapokuwa wamejenga majengo hayo hadi kufikia kiwango fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kusimamishwa wazazi kuchangia, kumejitokeza tatizo kubwa la kupunguza mitihani ya mwaka mfano, katika Mkoa wa Njombe kila mwaka ratiba ya mitihani ya *mock* hutolewa mapema mwanzoni mwa mwaka, lakini safari hii haikutolewa ratiba hiyo. Hadi mwezi huu Aprili hakuna taarifa yoyote ya mitihani ya *mock.* Naomba suala hili lifuatiliwe ili watoto wetu waweze kujipima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji ni kubwa sana nchi nzima. Kuna maeneo ya vyanzo vizuri vya maji na mito ya kutosha, lakini bado maeneo hayo yana matatizo

makubwa ya maji. Mfano, Mkoa wa Njombe kuna vyanzo vya maji vya kutosha, pia mito ya kutosha, lakini bado kuna tatizo kubwa la maji, hasa maeneo ya Makambako, Wanging'ombe, Njombe Mjini. Naishauri Serikali kuwa na mawasiliano ya karibu na wananchi wa maeneo husika ili waweze kuweka mikakati ya kuibua njia za kupeleka maji katika maeneo yao. Pia, wawawezeshe kwa kuwapelekea wataalam na vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna tatizo kubwa la uchakavu wa mabomba ambayo yanapasuka kila siku. Mfano, hapa Dodoma maeneo ya Kisasa, mabomba yanapasuka kila siku na kusababisha upotevu wa maji. Naomba mabomba hayo yabadilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi na usalama; kumekuwa na matukio yanayohatarisha maisha ya raia. Kwanza kumekuwa na mauaji maeneo mengi ya nchi yetu, watu wamekuwa wakiuawa na kuwekwa kwenye mifuko na kutupwa baharini. Naiomba Serikali ichukue hatua haraka ya kukomesha mauaji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii katika kipindi kifupi cha takriban miaka miwili na nusu. Napenda pia, kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, napenda kumpongeza Waziri na Manaibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na wataalam wote kwa kazi nzuri yenye mafanikio makubwa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu barani Afrika ambazo uchumi wake unakua kwa kasi. Pamoja na jitihada za kukuza uchumi napendekeza kuimarisha mikakati ya kuboresha miundombinu ya bandari

zetu, reli pamoja na barabara wakati tunaendelea kwa kasi na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *SGR* na kuboresha bandari ya Dar es Salaam, Serikali iweke mkakati wa kulinda biashara ya bandari zetu kwa kuboresha reli ya *TAZARA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miradi mikubwa inayoendelea ya kuboresha bandari na reli za nchi jirani kama mradi wa *The New Port of Nacal Development Corridor Project* ya Msumbiji. Mradi huu unalenga kuifanya Msumbiji kuwa lango kuu la kibiashara za kimataifa kwa nchi za Malawi na hata Zambia, Zimbabwe na *DR Congo.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya *TAZARA* ina umuhimu wa kipekee katika kuinua uchumi, kilimo, madini, utalii, ikiwa ni pamoja na kulinda biashara ya Bandari ya Dar es Salaam, ili kuwa lango la kibiashara za kimataifa kwa nchi jirani. *TAZARA* ilijengwa kuwa na uwezo wa kuhimili treni ya spidi ya kilomita 110 kwa saa, ikiwa na uwezo mkubwa wa kusafirisha mizigo ya kilimo, mbolea, madini kwa nchi za Tanzania, Zambia, Malawi na hata *DRC* na Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuboresha pia, ijengwe bandari kavu ya Mbeya. Aidha, imebainika kuwa, Reli ya *TAZARA* inaendeshwa kwa hasara na kusababisha inatumia kodi ya wananchi badala ya kujiendesha yenyewe na kwa faida. Nashauri Serikali za Tanzania na Zambia kuweka mtaji mpya, pia kuimarisha uongozi wa *TAZARA,* ikiwa ni pamoja na kutekeleza ushauri wa kitaalam wa mfumo bora wa kuendesha reli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa miradi ikiwemo miradi ya maji. Pamoja na ujenzi wa miradi ya maji bado kuna mahitaji makubwa ya maji na huku kukiwa na tishio la tabianchi. Nashauri Serikali iweke mkakati wa kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo na matumizi ya kibinadamu. Uvunaji wa maji ya mvua umefanyika kwa mafanikio makubwa kwa nchi za Kusini mwa Afrika ambazo zinafanana kijiografia na Tanzania. Nchi hizi zimefanikiwa hata kuuza maji ya mabwawa hayo kwa nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kuboresha sekta ya afya ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya na hospitali za wilaya. Pamoja na ujenzi wa miundombinu napendekeza Serikali iweke mkakati wa kuhamasisha Watanzania wote kuwa na bima ya afya, *NHIF* au *CHF.* Kuwepo kwa bima ya afya kwa Watanzania kwa wingi wetu kutawezesha sekta ya afya kujitegemea na kuwepo kwa huduma bora za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naipongeza hotuba nzuri iliyotolewa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya, naipongeza Serikali, ila nashauri kutokana na Hospitali ya Rufaa Muhimbili iliyopo Mkoa wa Dar es Salaam kupokea wagonjwa kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani na wengi wa wagonjwa hawana ndugu Mkoa wa Dar es Salaam hivyo, naishauri Serikali ijenge eneo maalum ambalo litawasaidia ndugu waletao wagonjwa wao kuweza kukaa na kutoa huduma za dharura ambazo wauguzi hawawezi kuzifanya na itasaidia ndugu wa mgonjwa kufuatilia maendeleo ya mgonjwa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itafute eneo lingine la kuhifadhia maiti katika hospitali ya Mkoa wa Morogoro maana chumba cha kuhifadhia maiti kipo karibu na Shule ya Sekondari Morogoro, hivyo kusababisha ndugu wa wafiwa wanapokuja kuchukua maiti wao hulia na kelele hizo za vilio zinasababisha wanafunzi waliopo madarasani kukosa usikivu wa kufuatilia masomo wawapo darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kiuchumi, barabara zote za lami nchini zilizojengwa chini ya kiwango, mfano barabara ya Chalinze hadi Mlandizi, zifanyiwe ukarabati ili kuepusha ajali za barabarani. Barabara zilizojengwa pembezoni mwa milima, mfano Milima ya

Usambara katika Mkoa wa Tanga zijengewe *pavements* au uoto ambao utazuia mmomonyoko wa ardhi, hususan kipindi cha mvua ambayo uharibu barabara hizo na kutopitika kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba njia ya reli ya Dar es Salaam – Tanga ikarabatiwe ili iweze kupitika na kuweza kusaidia usafirishaji wa mizigo na abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kutafuta njia mbadala ya msongamano wa magari eneo la mizani, hususan Vigwaza Mkoa wa Pwani, ukizingatia magari ya abiria yanatembea kwa ratiba maalum hivyo, husababisha usumbufu na abiria pia, hupata usumbufu kwa kusafiri kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iboreshe viwanja vya ndege. Mfano uwanja wa ndege uliopo Mkoa wa Morogoro wakati wa usiku haufanyi kazi kutokana na ukosefu wa taa uwanjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za uzalishaji; kilimo, wakulima wahamasishwe kulima mazao ambayo yatatumika kama malighafi katika viwanda vilivyopo nchini, mfano, kilimo cha alizeti, tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda, viwanda vipya vinavyojengwa vijengwe nje, mbali na makazi ya watu. Viwanda vinavyojengwa viwe ambavyo malighafi zake zinapatikana hapa nchini ili wakulima wetu wapate soko la kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara, wafanyabiashara wakadiriwe na Mamlaka ya Mapato *(TRA),* kulingana na biashara wanayoifanya na si eneo wanalofanyia biashara. Mfano, maeneo ya Kariakoo katika Mkoa wa Dar es Salaam wafanyabiashara wanakadiriwa kutokana na eneo. Pia, wafanyabiashara wakati wanaanzisha biashara zao wapewe muda maalum *(Grace Period)* angalau wa miezi mitatu kisha ndio wafanyiwe makadirio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu; maslahi ya Walimu yaboreshwe ili wawe na utulivu wanapofundisha. Madarasa yaongezwe kuepuka msongamano wa wanafunzi katika shule zetu. Wanafunzi wapatiwe angalau mlo mmoja kwa siku wawapo shuleni.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 10 limezungumzwa suala la chaguzi ndogo za Wabunge zilizofanyika katika majimbo matano na Madiwani katika kata 59. Chaguzi hizi zilitawaliwa na vurugu, dhuluma, pamoja na ukiukwaji wa haki za binadamu. Viongozi na wanachama wa chama cha CHADEMA walikamatwa na kubambikiwa kesi, wengine waliumizwa kwa kukatwa mapanga na wengine kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano Katibu wa CHADEMA, Kata ya Hananasifu Kinondoni aitwaye Daniel aliuawa wakati wa uchaguzi mdogo wa Jimbo la Kinondoni. Hadi sasa hakuna taarifa zozote za kukamatwa kwa wauaji. Kitendo hiki kinalifanya Taifa letu kuwa siyo sehemu salama tena kama zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji ya mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Usafirishaji, Akwilina Akwilin. Pia, nchi yetu imeonesha kwamba, siyo sehemu salama tena. Mambo haya yasipodhibitiwa yanajenga chuki na visasi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali iliahidi milioni 50 kila kijiji, suala ambalo halijatekelezwa hadi sasa. Huu ni mwaka wa tatu tangu Serikali itoe ahadi, lakini jambo hili halizungumzwi tena. Siyo jambo jema Serikali kuahidi halafu ikashindwa kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya maji nchini imesimama kwa sababu ya kutopeleka fedha. Mfano Mji Mdogo wa Mlowo uliopo Jimbo la Mbozi, kuna mradi wa maji wa milioni 400 na *certificates* zilishatumwa Wizarani, lakini fedha hazijatolewa na kusababisha mradi kusimama

kwa muda mrefu sasa. Naikumbusha Serikali kupeleka fedha za mradi huu ili ukamilike na wananchi wapate huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri walioko Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuandaa hotuba hii na kuiwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu; ongezeko kubwa la wanafunzi mashuleni haliendi sambamba na kuongezeka kwa miundombinu ya madarasa, ofisi za Walimu, matundu ya vyoo na kadhaili. Serikali iweke mkakati maalum wa ujenzi wa madarasa ili watoto wote wakae madarasani katika shule za *primary* na *secondary.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali kwamba elimu ni bure na hivyo hakuna michango inayoruhusiwa mashuleni inapokelewa kwa uelewa tofauti na wazazi na hata vyakula mashuleni Serikali inatoa. Serikali itoe ufafanuzi kuhusu kauli yake kwa kuwa kwa sasa wanafunzi wengi hawapati vyakula mashuleni kwa sababu wazazi au walezi hawataki kuchangia vyakula kwa watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto mwenye njaa hafundishiki, hali hii inatishia uelewa wa wanafunzi na hivyo kushusha elimu. Walimu wengi kutopandishwa madaraja kwa wakati katika mashule ya *primary* na *secondary* katika Wilaya ya Kaliua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa kuwa na mifugo mingi, lakini pato/mchango wa sekta ya mifugo katika pato la Taifa bado ni mdogo sana. Sheria ya nchi inaelekeza maeneo ya malisho ya mifugo kutengwa, kulindwa na kutangazwa kwenye magazeti ya Serikali. Viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo *(processing plants)* ili kutoa masoko ya uhakika kwa wafugaji. Maafisa ugani (mifugo) wenye weledi na vitendea kazi ili watembelee

wafugaji mashambani na watoe elimu. Kuwepo na mashamba darasa ya mifugo katika wilaya zote na kata zinazofuga ili wafugaji wafuge kisasa kwa ubora na si kwa wingi usiokuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awaagize Wizara ya Maliasili na Utalii kurejesha vyeti vya vijiji 26 katika Wilaya ya Kaliua ambavyo vilisajiliwa Kisheria ndani ya hifadhi za misitu na baadaye Afisa wa Maliasili walifika kwenye vijiji hivyo na kupora vyeti vya usajili wa vijiji hivyo vyote. Suala hili linaathiri sana wananchi wa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu 2018 kampuni za ununuzi wa tumbaku kama vile *JTI, TLTC* na *Alliance one* wametoa maelekezo kwa vyama vya msingi kwenye vijiji hivyo 26 kwamba hawatawapa makisio ya ununuzi wa tumbaku yao (mikataba) kwa vijiji ambavyo hawana vyeti vya usajili kwa sababu hawawezi kutekeleza mpango shirikishi wa utunzaji wa misitu *(CBFM).* Hili litaumiza uchumi wa Wilaya ya Kaliua na wakulima wa tumbaku wa Kaliua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakurugenzi wa Wilaya walipewa waraka na Serikali kwa kuwatoa kazini Watendaji wa Vijiji na Kata walioajiriwa tangu mwaka 2004 wenye elimu ya darasa la saba. Ni vyema Serikali ikaliangalia agizo hili kwa jicho tofauti ili kuondoa matatizo yanayoendelea kutokea ikiwa ni pamoja na Serikali kupelekwa Mahakamani na kupoteza fedha nyingi na muda mwingi kwa kushughulika na kesi wakati tuna mambo ya msingi ya kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kaliua wanaondolewa walioajiriwa tangu miaka ya 2001. Watendaji hawa wana barua za ajira walibaki kuthibitishwa, walipelekwa mafunzo kwenye Chuo cha Hombolo na maeneo mengine, pamoja na kupewa semina mbalimbali. Watendaji hawa hawatendewi haki, wengine ni wazee lakini pia wana familia zimeathirika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kaliua na Jimbo la Kaliua tumepanga kuongeza vituo vya afya viwili katika Kata ya Usinge na Kata ya Ukumbi Siganga katika bajeti ya mwaka 2018/2019. Wananchi wanaendelea kuchangia ujenzi huo na pia Mheshimiwa Rais alipofika Kaliua alichangia shilingi milioni kumi ku-*support* Kituo cha Afya cha Usinge. Tunaiomba Serikali itenge fedha ku-*support* nguvu za wananchi katika ujenzi wa vituo vya afya viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji katika Wilaya ya Kaliua halijapatiwa ufumbuzi na hakuna mikakati ya muda mfupi kwa Serikali kuwapatia Wanakaliua maji safi na salama. Mradi wa maji mkubwa wa kutoa maji katika Mto Malagarasi ni wa muda mrefu, leo ni mwaka wa nne tangu uanze lakini bado uko kwenye hatua ya upembuzi na usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mwaka huu 2018/2019 Serikali ilete mpango mkakati wa muda mfupi wa kuwatua wanawake wa Kaliua ndoo kichwani, watoto wa kike wapate muda wa kuhudhuria masomo shuleni na si kusaka maji kwenye madimbwi.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma kushambuliwa kwa sababu ya uraia. Kumekuwa na tatizo kubwa la wananchi wa Mkoa wa Kigoma kusumbuliwa na Maafisa wa Uhamiaji juu ya kukamatwa, kusumbuliwa, kuhojiwa, kuwekwa *lock up* na hata kuombwa rushwa ili misukosuko hiyo iishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Kakonko, Jimbo la Buyungu kila basi linasimamishwa na abiria wote kuulizwa vitambulisho, kuvuliwa nguo za juu yaani shati au blauzi ili kuona chanjo iko mkono gani yaani kushoto au kulia. Hali hii isipodhibitiwa italeta kuzorota kwa amani ya maeneo ya Mkoa wa Kigoma. Mikoa mingine ya mipakani hatuoni mambo haya yakifanyika, hii ni sambamba na raia wengi wa Kigoma kuhojiwa juu ya uraia wao, mfano; Askofu Kakobe (wa Kakonko), Abdul Nondo (wa Ujiji) na wengine wengi, hii haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za wakimbizi-Mtendeli Kakonko; kumekuwepo na athari za mazingira kwenye Kambi ya Wakimbizi Mtendeli kwa ajili ya ukataji miti na kuni. Awali Serikali iliahidi kutoa gesi ya kupikia kuokoa miti inayoharibiwa na wakimbizi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji jirani na kambi kunyimwa maji. *TCRS/UNHCR* walikaa kikao na vijiji jirani na Kambi ya Mtendeli *(host community)* ili watoe maeneo ya kuchimba visima virefu kwenye maeneo ya vijiji kwa makubaliano ya kuwapa maji. Vijiji hivyo ni Asanda, Nkuba, Kewe, Kazilamihunda na Juhudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maji kupatikana (visima virefu) kwenye vijiji hivyo, maji yalipelekwa kambini bila kupewa vijiji vilivyoingia mkataba na *UNHCR/TCRS.* Huu ni uporaji wa rasilimali za wananchi kwani kambini (Mtendeli) maji yaliisha na kambi ilikuwa ihamishwe sasa wamepata maji na kuwanyima wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halikubaliki maana maji ya vijiji vyetu yakiisha wananchi watahamia wapi? Aidha, wananchi wameahidi kuharibu miundombinu ya maji hayo yanayopelekwa kambini ili wakose maji wote, yaani wananchi *(host community)* na wakimbizi. Serikali iingilie kati suala hili ili kupunguza hasira ya wananchi kwa kuchukua maji yao na kuyapeleka kambini (Mtendeli) kinyume na mkataba (*NB:* mkataba upo)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji iliyokamilika lakini haitoi maji (miradi minne). Kuna miradi ya maji chini ya *NORAD* iliyokamilika na kulipwa fedha zote mpaka *retention fee* lakini imetengenezwa chini ya kiwango hivyo haitoi maji kabisa. Miradi hiyo hewa ni:-

Nyagwijima, Kiduduye (Kata ya Mafufunzu), Katanga (Kata ya Katanga) na Muhanga (Kata ya Muhanga). Miradi hii ni kero kwa wananchi kwa sababu wanaona mabomba bila maji hata tone. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali/mfadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri; wahusika kufilisi miradi hii na wakandarasi wawajibike.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukupongeza kwa uongozi wako na pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kazi kubwa anayofanya kwa kuhakikisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi kubwa anazofanya yeye binafsi katika kuhakikisha Tanzania ya viwanda inafika na hatimaye kuleta matumaini mapya ya kiuchumi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu. Ukurasa wa 34 wa Hotuba ya Waziri Mkuu imeelezea hali ya kutatua migogoro ya mipaka kati ya vijiji na hifadhi. Lazima kama Taifa tujue idadi ya watu inaongezeka kila siku ilhali eneo la kiuchumi, yaani ardhi haiongezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwepo na hali ya wanachi hasa Jimbo langu la Singida Magharibi ambapo wamekuwa wakipoteza mali zao ikiwemo mifugo, fedha, mazao na mambo mengine yanayoathiri maisha yao kwa ujumla. Katika Jimbo langu pekee wafugaji wamepoteza zaidi ya shilingi milioni 140 kwa kulipishwa faini kwa wanyama wao kukutwa katika maeneo yanayosemekana ni ya hifadhi. Hifadhi hii ambayo inafika maeneo ya Muhintiri, Ihanja, Ighombwe, Mwaru, Mtunduru, Minyashe na Makilawa haijawahi kutangazwa kisheria mahali popote kama hifadhi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wetu wanaongezeka, wakulima na wafugaji wanakosa mahali pa kulima na

kuchungia mifugo yao kwa sababu ya mipaka ya hifadhi. Ni wakati muafaka sasa kutokana na ongezeko hili la watu, tunaiomba Wizara ya Maliasili na Utalii sasa kushirikiana na TAMISEMI kuongeza maeneo ya wananchi na kupunguza ukubwa wa hifadhi ili kuondoa migogoro ya muda mrefu isiyokwisha ambayo inagharimu wakati mwingine maisha ya wakulima na wafugaji pamoja na mali zao. Naomba sana wananchi wetu wa kata nilizozitaja watengewe maeneo maalum ya kuchungia mifugo yao badala ya kila eneo lenye malisho kuonekana ni eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapendekezo haya, naunga mkono hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ahsante.

**MHE. NURU AWADHI BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uwezo wa kuzungumza. Vile vile nimpe pole Mheshimiwa Spika, Mungu azidi kuimarisha afya yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu barabara zilizo chini ya *TARURA. TARURA* kwa kweli hadi hivi sasa hawajaeleweka kwa wananchi. *TARURA* japo inashughulikia barabara lakini bora ingewashirikisha Madiwani. Madiwani ndio wanaozijua barabara zetu zilivyo. Ikiwa *TARURA* haitawashirikisha Madiwani barabara zetu zitazidi kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu kauli ya Mheshimiwa Rais Dokta John Pombe Magufuli ya Tanzania ya viwanda. Tanzania ya kuelekea uchumi wa viwanda hiyo ni kaulimbiu nzuri lakini tujiulize, je, umeme wa kuendesha viwanda hivyo upo wa kutosha? Lazima Serikali ihakikishe tunatumia mito tuliyonayo, mfano Mto Rufiji, Kilombero na Mito mingine ambayo ina maji ya kutosha ili izalishe umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme tulionao hauwezi kukidhi kuendesha viwanda vinavyohamasishwa vianzishwe.

Kila mkoa umepewa agizo la kujenga viwada 100, je, viwanda hivyo vilijengewa umeme wa kutosha na utapatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze, Je na umeme wa kuendesha viwanda utapatikana bila tatizo?

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niishauri Serikali kuhusu ng'ombe kupigwa kuchapwa na kuwekewa namba. Jambo hili limesababisha mazao ya ng'ombe kukosa soko kwani ngozi nyingi za Tanzania zimeendelea kukosa soko. Nishauri Serikali kutafuta njia nyingine ya kutambua mifugo badala ya alama hizi kwenye ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali kuongeza juhudi za kuwawezesha wajasiriamali. Kwa mfano, walioamua kufuga nyuki wanapata shida sana ya kupata vifungashio hivyo wanauza asali zao kwa shida sana na kwa hasara. Niishauri Serikali kuwasaidia wajasiriamali hao kupunguziwa bei ya mizinga badala ya mzinga mmoja kuuzwa kwa shilingi elfu themanini, hali hiyo inasababisha ugumu kwao kumudu bei hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali inapotaka kukopesha mikopo kwa wajasiriamali isiache mbali utafutaji wa masoko ya uhakika kuliko ambavyo wajasiriamali wengi wamekuwa wakitengeneza bidhaa kisha kukosa masoko, hali ambayo imesababisha kushindwa kurejesha mikopo hiyo na hivyo kusababisha fedha hiyo kushindwa kwenda kwenye mizunguko ya ukopeshaji kwa wajasiriamali wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali juu ya ulipaji watumishi waliostaafu uwe wa haraka na umakini mkubwa kwani wastaafu wanapata shida sana kulipwa. Wapo waliostaafu tangu mwezi Julai, 2017 mpaka leo hii

hawajalipwa. Niiombe Serikali kuliangalia kwani watumishi hao wamekata tamaa na wengine kupata magonjwa ya msongo wa mawazo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya siasa nchini si nzuri kabisa. Vyama vingi vilianzishwa kwa Sheria *No.* 5 ya kuruhusu vyama vingi ndiyo maana hata chaguzi zote zinashirikisha vyama vingi, lakini katika chaguzi za marudio tumeona haki zikivunjwa na upendeleo wa wazi kwa Chama cha CCM. Kwa mfano uchaguzi wa marudio Jimbo la Siha askari polisi walikuwa wanawasindikiza CCM kukusanya maboksi ya kupigia kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki haikutendeka, Mawakala wa Vyama vya Upinzani walikuwa wanapigwa na kunyang'anywa karatasi za matokeo mbele ya askari wa Jeshi la Polisi. Hii ilisababisha hata katika Jimbo la Kinondoni baadhi ya raia kupoteza maisha kwa sababu tu ya kutokutenda haki. Hivi kulikuwa na sababu gani zilizosababisha tume kutokutoa barua za mawakala kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikutano ya hadhara. Nchi yoyote yenye kufuata sheria na inayoamini katika demokrasia ni lazima ifuate sheria maana Katiba, Ibara ya 18 inaruhusu uhuru wa kuongea na kujieleza lakini ni wazi kabisa wakati huu katika Serikali ya Awamu ya Tano, vyama vya siasa haviruhusiwi kufanya mikutano ya hadhara, hata wananchi wakitoa mawazo yao kwenye mitandao wanashtakiwa na Serikali. Maandamano ambayo ni haki ya kikatiba kupeleka meseji kwa watawala yamekatazwa. Je, Serikali hii inaweza kusema ni nchi yenye kujali haki na demokrasia kwa wananchi wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao Makuu Dodoma. Mpaka sasa juhudi kubwa bado zinahitajika kuuendeleza Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. Bado barabara nyingi hazipitiki. Kwa mfano maeneo ya Kisasa barabara ni mbovu sana. Kuna haja ya kushughulikia suala la majitaka, *system* iliyopo ilikuwa inahudumia watu wachache, sasa hivi

idadi imeongezeka, la sivyo yaliyokuwa yanatokea Dar es Salaam kwa maji machafu kufurika ovyo barabarani yatatokea hapa Dodoma na kusababisha magonjwa ya mlipuko kama kuhara, *typhoid* na kipindipindu kutokea hapa. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuongeza njia za majitaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sambamba na kuongeza shughuli za kijamii kuufanya Mji wa Dodoma kuwa kati ya miji ya vivutio kwa watalii. Kuna vivutio kama mashamba ya zabibu na miamba na mawe; mji utengenezwe uvutie watalii, hata Bunge lenyewe ni kivutio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilomo. Wananchi zaidi ya asilimia 80 ni wakulima na wengi sana walihamasika kulima mahindi, lakini zao hili limekuwa ni mwiba kwa wakulima. Kama tujuavyo mbegu za mahindi ya kisasa huwa zinaharibika haraka sana na *storage* yake ni ghali sana na wakulima wengi hawawezi nunua matenki ya kuhifadhi. Bei ya mahindi imeshuka sana inapelekea mahindi kupekechwa na wakulima kupata hasara. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wakulima hawa kupata masoko ya kuuza hata nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo, mfano Kilimanjaro, ilikuwa haina shida kuuza mahindi Kenya, lakini sasa mpaka upate kibali na vibali vyenyewe kuvipata ni shida na imejaa urasimu mkubwa. Je, Serikali hainunui tena mahindi kwa ajili ya Ghala la Taifa?

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa pili wa Hotuba ya Waziri Mkuu ameonesha kero za Muungano na jitihada za kuzitatua. Naomba kuishauri Serikali isishughulikie kero za Zanzibar peke yake, ni vema kukawa na utaratibu wa kuziangalia kero za Tanganyika na iache kuipendelea Zanzibar. Kwa mfano, katika sherehe za Mapinduzi, Dokta Shein hupigiwa mizinga ishirini na moja wakati yeye sio Amiri Jeshi wa Tanzania. Jambo hili linatukera Watanganyika na linamshusha hadhi Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jambo hili halihitaji mabadiliko ya Katiba, basi Serikali iache kumshauri Rais kuhudhuria sherehe hizo kama tunataka Dkt. Shein ndiye awe mgeni rasmi ili itifaki iweze kuzingatiwa na kama Rais wa Jamhuri atahudhuria, basi yeye ndiye awe mgeni rasmi.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Bunge kwa Mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mkuu wetu wa Nchi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi kubwa anazozifanya katika kutuletea maendeleo ya kiuchumi nchini. Kufufua zana za uchumi wa viwanda, ununuzi wa ndege za usafiri kwa ajili ya Shirika letu la Ndege la Taifa *(ATCL)*, kutekeleza kwa vitendo maamuzi ya Serikali ya kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kuja Dodoma, kutekeleza ujenzi wa reli ya kisasa ya *standard gauge,* kutekeleza ujenzi wa barabara ya juu *(flyovers)* katika maeneo ya makutano ya barabara Jijini Dar es Salaam, kutekeleza ujenzi wa mradi mkubwa wa uzalishaji umeme wa *Stiegler's Gorge,* ni mifano ya juhudi hizo za kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzaji ujuzi. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelezea umuhimu wa kukuza ujuzi wa nguvukazi tuliyonayo na kusema ni miongoni mwa ajenda muhimu za kisera. Naomba kupendekeza kwamba wataalam wastaafu wazalendo watumike katika kusambaza ujuzi na elimu kwa vijana wetu. Wapo Watanzania wengi wenye ujuzi mkubwa katika fani mbalimbali za uzalishaji uchumi na kadhalika ambao ni wastaafu ambao bado wana nguvu na uwezo mkubwa wa kushauri. Serikali iwatumie wastaafu wetu hawa pamoja na wataalam wengine ambao bado hawajastaafu, ili kuweza kupata matokeo ya haraka ya ukuzaji ujuzi na kuwajengea vijana wetu uwezo mkubwa *(capacity building).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Binafsi. Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji uchumi. Suala hili ni muhimu sana kulisimamia na kuliendeleza kwa nia ya kujenga uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo juhudi za mara kwa mara zifanyike na hatua kuchukuliwa za kuwawezesha wafanyabiashara Watanzania na wazalendo kunufaika na uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Serikali imekamilisha maandalizi ya awamu ya pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Bado uzalishaji katika kilimo ni wa kiwango cha chini ukizingatia ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo cha kumwagilia, haitumiki. Nashauri katika maandalizi hayo iwe ni pamoja na kupanga mikakati ya kulima maeneo yote yanayolimika na kutafuta masoko ya nje na ndani kwa mazao yote yatakayolimwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; Serikali imetoa fedha za kutekeleza ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya vituo vya afya na maabara ya upasuaji kwa akinamama wanaojifungua. Jumla ya vituo vya afya 100 vimepatiwa jumla ya shilingi milioni mia saba, kila moja ikiwa shilingi milioni mia nne; ni kwa kazi za umaliziaji miundombinu na shilingi milioni mia tatu zinanunulia vifaa na madawa *MSD.* Nimeomba Serikali ijumuishe Vituo vya Afya vya Mvuha, Mtamba (Kisemu) na Tawa vilivyomo kwenye Jimbo la Morogoro Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwanza kumshuku Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo. Nilichangia kwa kuongea, naomba nichangie kwa maandishi kwa eneo ambalo sikumalizia na kuweka kwa muhtasari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashauri Waziri wa Fedha aweze kupatiwa fursa tena ya kutoa msamaha wa

kodi katika eneo la miradi ya kitaifa na miradi mbalimbali ya jamii ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; marekebisho ya sheria yaje mapema Bungeni turekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nashauri Serikali iangalie namna bora ya kuweka vyanzo vya mapato vya uhakika katika Mfuko wa Mazingira. Si tozo mpya bali kutokana na ada, tozo, ushuru na leseni mbalimbali asilimia fulani ziende katika Mfumo wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala la kuwa na vyanzo vya mapato kwa ajili ya Mfuko wa UKIMWI na watu wenye mahitaji maalum. Pia halmashauri zitoe mikopo kutokana na ile asilimia 10 ya vijana na wanawake kwa wenye mahitaji maalum na wenye Virusi Vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali iangalie ushauri wa kuongeza Sh.50/= kwa kila lita ya mafuta ili iwe Sh.100/= kwa kila lita ya mafuta. Pia kuondoa kodi kwenye mitambo ya kuchimba maji, pampu za maji zenye mita na pampu za maji za sola. Hii itafanya gharama za vifaa hivyo na huduma ya uchimbaji kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Manunuzi, Serikali iboreshe kwa kutoa waraka wa kuangalia *value for money* pamoja na bei halisi. Maeneo ya kuangalia ni eneo la *TEMESA, TBA,* Taasisi ya Uchimbaji wa Mabwawa na Visima pamoja na maeneo yote tunapopata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri maeneo yote ambako Serikali inapata mapato au maduhuli zitozwe kwa njia ya kielektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu kwenye maeneo matatu muhimu. Nikianza na umuhimu wa kulinda amani, utulivu na mshikamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kuwa kuna amani nchini ilhali hakuna amani kwa sasa. Hakuna utulivu kwenye Taifa letu maana kila kukicha matukio ya maonevu yanayofanywa na vyombo vya dola ya kuvunja haki za msingi kwa raia wake. Tunashuhudia mauaji yakiendelea kwa kasi nchini, utekaji pamoja na watendaji wa Serikali kutishiwa hata kushindwa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria za nchi na weledi wa kazi yake bali wanasubiria kauli kutoka juu. Jambo hili linalirudisha Taifa letu nyuma. Taifa linakuwa la woga, wanahifadhi chuki na mawazo mbadala moyoni badala ya kuyatoa ili yasaidie kuijenga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia unyanyasaji wa dhahiri wa Vyama vya Upinzani huku Msajili wa Vyama vya Siasa anafumbia macho na zaidi anatumika kukandamiza Upinzani. Mfano kwenye Hotuba Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kabisa kuwa Vyama vya Siasa vimeruhusiwa kunadi sera zao na itikadi ili kupata wanachama, kitu ambacho ni uongo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua fika kuwa watendaji, polisi na hata Ofisi ya Usajili wa Vyama vya Siasa anaifumbia macho kauli batili inayoenda kinyume na Sheria na Kanuni za Vyama Vingi na Katiba ya nchi yetu; huku tukishuhudia Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi akiendelea na mikutano ya hadhara na kupokea wanachama huku mtendaji wa Chama cha Mapinduzi (Katibu Mwenezi), ndugu Humphrey Polepole, akiendelea kufanya mikutano ya hadhara na kuvinanga vyama vingine huku wakipandikiza chuki. Leo hii kusema kuwa wawakilishi tu ndio wafanye mikutano ilihali inafahamika fika kuwa tuna vyama ambavyo havina uwakilishi wa Wabunge, Madiwani, Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji Sasa hivi vyama vitatangaza vipi hizo sera zake na itikadi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia pia jinsi fedha za Watanzania maskini zikitumika vibaya, hasa kwa chaguzi ambazo zinarudiwa kupitia minada ya viongozi wa

wananchi kununuliwa na kusababisha si tu upotevu wa fedha bali mauaji na ulemavu kwa raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema bila aibu kuwa CCM wameshinda Majimbo yote na kata 58 huku CHADEMA wakishinda moja tu? Eti CCM wameshinda kwa kishindo ilhali anajua hujuma inayofanywa na vyombo vya dola, Tume ya Uchaguzi na Wakurugenzi ambao ni makada wa CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia jinsi Jeshi la Polisi linavyojigeuza Tume ya Uchaguzi na kubandika matokeo ya uchaguzi kinyume na taratibu, wakishuhudia watendaji wakibadili *ballot box* na kuondoka nalo mbele ya *RPC* Kinondoni na pale Magomeni. Hapa hatuwezi kuwa na uchaguzi huru na hivyo hakuna amani wala mshikamano.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marejesho ya mkopo; suala la fedha zinazotengwa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri hukopeshwa vijana na akinamama. Fedha hizo zinaporudishwa hazifuatiliwi na nyingi hutumika katika mafungu mengine katika halmashauri husika. Wabunge tumekuwa tukidai zitolewe lakini hatudai marejesho ya mikopo hiyo. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia Waziri anayehusika na Uwezeshaji wa Vijana kutoa maelekezo ya fedha zinazorudishwa na waliokopeshwa ambao ni vijana na akinamama, fedha hizi za marejesho hazisimamiwi kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi katika utekelezaji uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kazi na Ajira *(Workers Welfare Viwanda vya Mafinga).* Mafinga ina Viwanda vingi vya mazao ya misitu, lakini hali za wafanyakazi ni duni *(welfare).* Mbaya zaidi wafanyakazi wakipeleka malalamiko Ofisi ya Mkuu wa Wilaya taarifa

zinarudi kwa mwekezaji kumsemea mlalamikaji kuwa ni mtu mbaya, matokeo yake, mfanyakazi anatafutiwa visa anafukuzwa kazi na kwa lugha ya kejeli anaambiwa nenda popote. Naomba na kushauri, Mheshimiwa Waziri afanye ziara ya kushtukiza na akifika aongee na wafanyakazi, asiishie kupokea taarifa ya menejimenti au ya uongozi wa wilaya tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wanapaswa kuwathamini wafanyakazi, *OSHA* wasiishie tu kuchukua tozo bali wafanye *serious* ukaguzi, mazingira ya kufanyia kazi ni mabaya, *is completely against labour rights*. Kwa mfano, kuna kazi ya kupanga magogo, wafanyakazi hawana *gloves*, hawana mabuti, wamevaa kandambili, hawana kofia, ni mazingira hatarishi. Hawana usafiri, mtu anatembea kilometa nne hadi tano kwenda kazini *a total of eight to ten kilometers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa viwanda uendane na hali bora za wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii, hata hivyo nitoe ushauri na maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi na usalama *page* 56. Idara ya Uhamiaji na matendo ya unyanyasaji wa raia hasa wanaoishi katika mipaka ya nchi yetu na hasa wananchi wanaoishi katika Mkoa wa Kigoma. Imekuwa ni desturi hasa kwa wenzetu wa Idara ya Uhamiaji kushika watu, kunyanyasa watu eti kwa sababu ni wahamiaji haramu au uraia wao unatia mashaka. Niombe sana Ofisi ya Waziri Mkuu itoe maelekezo ya kiutawala juu ya mwenendo wa Idara ya Uhamiaji na hasa katika Mkoa wetu wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yafuatayo yazingatiwe; heshima kwa wanachi wa Kigoma na kamwe watu wasitambuliwe kwa sura zao, lugha zao na maumbile

yao. Weledi utawale na ikibidi mafunzo zaidi ya utambuzi wa nani ni raia na nani si raia yafanyike kwa uharaka. Baadhi ya wananchi wa Kigoma wanaamriwa na Idara ya Uhamiaji wapeleke vyeti vya kuzaliwa vya wazazi wao na babu zao. Mambo ambayo ni vigumu sana kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa ni kuendeleza unyanyasaji na usumbufu kwa wananchi wa Kigoma, Kasulu, Kibondo Kakonko na Uvinza. Aidha, kwa nini shida hii iwe zaidi kwa Mkoa wa Kigoma ilhali mikoa mingi ya mpakani hatusikii. Viongozi wa kisiasa, dini wanaharakati na hata wasanii mashuhuri wanatoka katika Mkoa wa Kigoma kudhaniwa na kuhisiwa siyo raia, jambo hili linatia simanzi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matukio ya hovyo ambayo viongozi mbalimbali watokao Mkoa wa Kigoma wameitwa uhamiaji kwa mahojiano na wengine hata kupelekwa kolokoloni kwa sababu tu ya kuwa wenyeji wa Kigoma. Tafadhali haki itendeke kwa wote na mtindo wa sasa wa kukomoana, vitisho na hata kuoneana ifike mwisho, watu wetu wa Kigoma wanajihisi ni raia daraja la pili. Jambo ambalo siyo sahihi, raia wetu wote wapo sawa katika nchi yetu, tusitengeneze matabaka bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakimbizi na wahamiaji haramu watambuliwe, naomba sana Serikali na hiyo Ofisi ya Waziri Mkuu ifanye kazi ya kuwatambua wakimbizi, wahamiaji haramu na wahalifu ili watofautishwe na raia wema na wakazi wa Mkoa wa Kigoma. Wakimbizi wetu wa DRC na Burundi zipo tamaduni tunazofanana, tamaduni hizo zisiwe sababu ya watu wetu kudhaniwa ni wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu vizuri juhudi za Serikali yetu, lakini Mkoa wa Kigoma kupokea wakimbizi isiwe laana, tunapokea wakimbizi kwa niaba ya Taifa lote, vitendea kazi kwa Idara ya Uhamiaji na Polisi changamoto ya vifaa vya kazi na wanafanya kazi katika Idara hizi mbili katika eneo lenye wakimbizi ni tatizo kubwa. Idadi ya Maofisa

na Maaskari iongezwe, magari ya doria yaongezwe, malipo ya motisha kwa wafanyakazi wa Idara hizi yatazamwe upya na yaongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia suala la ajira kwa wenye kiwango cha darasa la saba. Kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kuona ni lazima kiwango cha ajira kianzie kidato cha nne. Ni jambo jema kabisa ndiyo maana ya kuanzisha elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu kwenye eneo hili, naomba kuishauri Serikali ione kuna umuhimu wa kuwarudisha kazini watumishi wote waliokuwa wameajiriwa kwa kiwango hicho cha elimu huko nyuma ili wafikie kipindi chao cha kustaafu na kupunguza gharama kubwa ya kuwalipa watumishi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi hao wengi wao walioajiriwa kwenye kada za udereva, uhudumu na huduma mbalimbali katika ofisi za Serikali, kada ambazo hazihitaji utaalam mkubwa kwa *level* yao ya elimu. Najua Serikali ina nia njema ila kwa kipindi hiki cha mpito baada ya suala la elimu bure tunaamini mwamko wa kujiendeleza utakuwa mkubwa na hivyo kada hii ya elimu ya msingi itajifuta yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hifadhi ya mazingira; napenda kuipongeza Serikali kwa kuanzisha mpango wa usafi kwa ajili ya utunzaji wa mazingira. Pamoja na Serikali kuanzisha mpango huu na kuongeza idadi ya wakaguzi na kutoa elimu na uelewa kuhusu uendeshaji endelevu wa viwanda unaozingatia utunzaji bora wa mazingira. Napenda kuishauri Serikali kuona ni namna gani ya kupiga marufuku

vifungashio vya *plastic* ili kuendelea kupunguza uharibifu mkubwa wa mazingira kupitia vifungashio vya *plastic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo. Nimekuwa nikifuatilia sana kwenye mikoa mbalimbali nchini ambayo imekuwa ni wazalishaji wakubwa wa chakula. Napenda kuishauri Serikali kuhusu suala la pembejeo ambalo limekuwa na changamoto kubwa kwa upande wa upatikanaji. Kwa kuwa, maeneo mengi yana Mawakala ambao wamekuwa na urasimu mkubwa kwa namna ya upatikanaji wa pembejeo. Ushauri wangu, ni kwa nini Serikali isione umefika wakati wa kusambaza pembejeo hizi kwenye maduka na kuhakikisha inatolewa bei elekezi ili kila mkulima apate pembejeo hizi kwa wakati kwa kuwa kumekuwa na upendeleo mkubwa wa upatikanaji wa pembejeo kwa ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mazao ya biashara. Pamoja na Serikali kuweka mkazo maalum wa kuyaendeleza kwa kasi mazao ya kahawa, korosho, pamba na tumbaku, kuna zao la *apples* katika Mkoa wa Njombe ambalo kama Serikali itaweka mkazo itasaidia upatikanaji wa *apples* kwa wingi katika nchi yetu na kuacha kuagiza *apples* Afrika ya Kusini ili kuongeza kipato kwa wakazi wa Mikoa ya Kusini na kuongeza mapato na uchumi wa Taifa letu.

**MHE. HASNA S.K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Binafsi sina shaka kabisa kwamba 2020 Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Kiongozi Mkuu wa shughuli zote za Serikali. Nianze sasa kuzungumzia changamoto mbalimbali zinazoikabili Halmashauri yangu ya Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la umeme, ukurasa wa 21 tunao mradi wa *REA* awamu ya pili

kwenye Vijiji vya Kabeba, Mwakizega, Ilagala, Mkandarasi aliyekuwa akitekeleza mradi huu kasimamishwa kuendeleza mradi, wakati mradi huu ulitakiwa uwe umezinduliwa tangu Machi, 2017. Leo hii wananchi wamebaki kuziangalia nguzo na transfoma badala ya kuwasha umeme kwenye nyumba zao. Niombe Serikali ituletee Mkandarasi mwingine atakayemalizia mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, hadi tarehe ya leo hatma ya mradi wa *REA* awamu ya tatu wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini hawajui lini mradi huu utaanza rasmi, niombe Serikali kutangaza *tender* mara moja ili na mradi huu wa *REA* awamu ya tatu uanze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Uvinza inayo miradi sita (6) mikubwa ya maji. Mradi wa maji wa Nguruka, mradi wa maji wa Uvinza, mradi wa maji wa Kandaga, mradi huu wa Kandaga hadi leo Halmashauri ya Uvinza hawajui utekelezaji, kwa kuwa mradi huu unatekelezwa na Halmashauri ya Kigoma Vijijini pamoja na mradi wa maji wa Rukoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia ya kupeleka Viongozi wa Kitaifa upande mmoja wa Wilaya au upande mmoja wa Jimbo la Kigoma Kusini, mfano. Jimbo hili la Kigoma Kusini lina Kata 16 na Vijiji 61 ndani ya *square meter* za mraba 10,178 na Kanda mbili (2). Ukanda wa Reli una kata nane, Kata ya Kandaga inayopakana na Kidahwe Mbili, Kata ya Kazuramimba, Kata ya Basanza inapakana na Kasulu, Kata ya Uvinza, Kata ya Mganza, Kata ya Itabula inapakana na Urambo, Kata ya Nguruka, Kata ya Mtego wa Noti inapakana na Kibondo na Upande wa Kaliua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukanda wa Ziwa Tanganyika, Kata ya Mwakizega inapakana na Simbo. Kata ya Ilagala kwenye Gereza la Ilagala, Kata ya Sunuka, Kata ya Sigunga, Kata ya Herembe, Kata ya Igalula inayopakana na Mwesa Mkoa wa Katavi, Kata ya Bohingu kwenye Hifadhi ya Mahale, Kata ya Kalya inapakana na Mpanda. Naelezea

haya yote ili Mheshimiwa Waziri Mkuu aone umuhimu wa Viongozi wa Kitaifa wanapokuja kufanya ziara wajue kuwa ukanda huu pia una kata nane (8) na vijiji 34 na una miradi mikubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa maji mkubwa wa Kalya na wananchi wameishaanza kunywa maji na Mkandarasi anajipanga kuukabidhi mradi huu Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza. Tunao mradi wa maji Ilagala tayari maji yanatoka, tunaomba mradi wa Mwalo wa Samaki na Dagaa Muyobaozi, Kata ya Mwakizega, lakini cha kusikitisha kila kiongozi anayekuja wanaishia kumpeleka ukanda huu wa Lake Tanganyika na badala yake wote wanaishia kuwapeleka ukanda wa Reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kufanya ziara ya Wilaya ya Uvinza aje kuzindua kati ya miradi ifuatayo: Mradi wa maji Kalya, mradi wa maji Ilagala au mradi wa Mwalo wa samaki Mwakizega sambamba na mradi wa shule ya sekondari ya Mwakizega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapofanya ziara ukanda huu wa maji ndiyo ataona umuhimu wa kuligawa Jimbo, tayari utaratibu wote ulishafanyika kugawa Majimbo mawili (2) Jimbo la Uvinza na Jimbo la Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri aliyoiwasilisha kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za ofisi yake na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2018/2019. Wanachama wa CCM tumeridhika nayo kwani imelenga

nchi yetu kutoka katika uchumi mdogo na kwenda uchumi wa kati wenye kaulimbiu ya Tanzania ya Viwanda inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa wananchi katika kukuza uchumi nashauri Mikoa, Wilaya, Kata, Vijiji na Vitongoji viwe na uratibu unaoeleweka kwa wananchi na uwe wa wazi ili mwananchi azione fursa na kumrahisishia ushiriki wake kwa shughuli na miradi wanayoifanya. Fursa zilizopo zilenge kuwafikia na kuwashirikisha wananchi wa jinsi na rika zote mfano, vijana wa elimu ya juu, wanawake na wanaume mjini na vijijini pamoja na walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wenye elimu ya kawaida wasiobahatika kupata elimu mijini na vijijini, wanawake, wanaume na walemavu nao wanao mchango mkubwa kwani kufeli shule si kufeli maisha. Mwelekeo wa kuwafikia kiurahisi ni kuwa na vikundi, ushirika, *SACCOS*, *VICOBA* na kadhalika. Elimu ya ujasiriamali kwa shughuli na miradi wanayopanga kufanya ni muhimu sana kupatiwa kabla na wakiendelea kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa za masoko ndani na nje ya nchi zisimamiwe kikamilifu na kupunguza au kuondosha urasimu usio na lazima ili kuwapa moyo na kuthamini kazi wanazozifanya, kuwakutanisha na taasisi za fedha na mabenki kuweza kukopa na kuongeza mtaji kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kuwawezesha watoto wote wenye uwezo wa kuingia shule waruhusiwe bila ya malipo. Hali hii wananchi wameipokea na kuwapeleka watoto kwa wingi. Wananchi hasa wanyonge wameitumia kikamilifu fursa hii na watoto wengi walioshindwa kujiunga na shule kwa kukosa malipo sasa wameingia shule. Changamoto iliyopo ni uhaba wa majengo na Walimu. Hata hivyo naamini Serikali kupitia wadau mbalimbali na taasisi wanaungana pamoja kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa vyuo vya *VETA* kwa kujifunza kazi za amali (kujitegemea) kwa vijana wengi ambao wameshindwa kuendelea na masomo ya juu. Ukosefu wa takwimu sahihi kwa vijana wanaomaliza vyuo ama elimu ya juu na fani zao walizosomea. Nashauri mikoa, wilaya tuanzishe utaratibu wa kuwatambua wasomi wetu na fani zao walizozihitimu ili iwe rahisi kuwatumia na kuwashajihisha kujiwekea pamoja na kutafuta fursa na kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuzaliwa Tanzania unazidi kuimarika, wananchi wake wanaishi bila bugudha yoyote ili mradi havunji sheria. Kwa kuwa Muungano huu ni wa watu bila shaka zinaweza kuwepo changamoto za hapa na pale, lakini zisigeuzwe na wapinzani wetu kuwa chachu ya kuvunja Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu ni wa damu, hivyo changamoto chache zilizobaki tuzitafutie ufumbuzi ili uzidi kuimarika. Hotuba, mijadala, makongamano yaeleze kwa uwazi mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya miaka 54 ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji wa wanawake na watoto. Pamoja na jitihada kubwa inayochukuliwa na Serikali yetu ya kuweka sheria na kuridhia mikataba ya Kimataifa kupiga vita unyanyasaji wa aina zote wa wanawake na watoto, mafanikio yameanza kuonekana. Wanawake wanaweza kujitetea na kudai haki zao na kufikiwa na fursa mbalimbali bila ubaguzi, tunapongeza na kushukuru. Kwa watoto kumezuka makundi maovu yanawabaka na kuwalawiti watoto wa kike/kiume, sheria kali zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DKT. HAJDI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uzalishaji (kilimo); Serikali ilichukua mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 40 kwa kununua na kusambaza matrekta na zana zake mwaka 2010. Hadi ilipofika mwaka 2015 ni asilimia 46 tu madeni ya mauzo ya matrekta hayo yalikusanywa. Mradi huu umekumbwa na changamoto nyingi pamoja na *SUMA JKT* kukosa uzoefu katika masuala ya biashara hivyo kusababisha mradi huo kuwa na hasara kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kifupi sana kimepita katika mradi huu wa *SUMA JKT* wa matrekta kuonesha hasara, Serikali 2017 imechukua mkopo mwingine wa matrekta ya aina ya *Ursus* yanaunganishwa na kampuni ya Kibaha chini ya *NDC*. Watekelezaji wa mradi huu wa matrekta ya *Ursus* wanaonesha toka Mwanza na hawana uzoefu kabisa katika masuala ya biashara ya matrekta na zana za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe maelezo na kutuhakikishia Watanzania kwanza fedha zetu za SUMA JKT*, tractors* zitarudishwa au tayari tumeshapata hasara. Pili; nashauri Serikali kuwawezesha *NDC* wajiendeshe kibiashara katika kutekeleza mradi wa *Ursus tractors* pamoja na kutumia mikakati/mbinu zote za masoko yaani *marketing strategies* za (1) *Promotion* (2)*Price* (3) *Place* (4) *Production* vinginevyo nao *Ursus tractors project* unaweza ukaishia hasara kama ule wa SUMA JKT *(tractors project)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanyama waharibifu. Serikali iwe na mikakati ya wazi katika kuzuia wanyama waharibifu katika Vijiji vya Hunyari, Kisambu Nyangere, Mariwanda, Sarakwa, Mugeta Kyandege na Tingirima. Maeneo haya kwa muda mrefu yameathirika sana kwa wanyama kula mazao yao ya chakula na biashara toka msimu wa 2011/2012 hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia ya kifuta jasho. Tunaomba Serikali kulipa fidia ya kifuta jasho na kifuta

machozi zaidi ya shilingi milioni 360 zinadaiwa na wakulima wa Vijiji vya Nyangere, Mariwanda, Kihumbu, Sarakwa, Tingirima, Mugeta na Sarakwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msaada wa kumalizia majengo matatu ya zahanati, kuna maeneo yaliyo mbali na huduma za afya, wakazi wa vijiji husika wamejenga zahanati ili kusaidia kupata huduma za afya. Majengo matatu yameezekwa bado samani, lipu, *floor*, nyumba ya Mganga katika Vijiji vya Tiring'ati, Kambubu na Mihingo. Tunaomba Serikali kusaidia vijiji hivi ambavyo vipo mbali na huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maji katika Jimbo langu kuna uhaba mkubwa wa maji ya binadamu na mifugo na hapa ieleweke kuwa katika vyanzo vya maji katika Jimbo langu maji ya malambo na mabwawa ndio maji ya binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali kukarabati malambo ya zamani ya Kyandege, Mugeta, Tingirima, Nyang'aranga, Manchim, Wero, Mahanga, Salama A, Sarzate, Rakanaa, Mihingo, Mekomariro (Malambo mawili) na Sarakwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malambo haya yalipangwa kuchimbwa sana *budget* ya 2016/2017 hadi leo hakuna dalili, Mheshimiwa Waziri wa Maji aliahidi humu Bungeni, Bunge la Mwezi wa Pili, 2018 na kwamba Bunda imetengewa bilioni moja kwa kazi hiyo. Malambo yanatumika zaidi kwa maji ya binadamu kwa visima kukauka kila kiangazi. Suala la Malambo katika Jimbo langu yana umuhimu zaidi kuliko visima, maana visima hukauka kila kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Kitengo cha *SENEPA* wamekubali kutoa vifaa na ufundi kusaidia kukarabati malambo haya, tunaomba Serikali ikubali kusaidiana na Wizara ya Maji kukarabati malambo haya yaliyochimbwa miaka ya 60 lakini ni chanzo cha uhakika cha maji katika jimbo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukupa pole kwa kuugua pia tunamshukuru Mungu kwa uponyaji wako. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai na kutupatia Viongozi wazuri wenye nia njema ya kuleta maendeleo kwa Watanzania. Nampongeza sana Rais na Wasaidizi wake Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amekuwa ni kielelezo chenye kuleta mabadiliko ya utendaji kazi wenye kuleta tija kwa jamii na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia shughuli zote za Serikali kwa umakini na umahiri mkubwa. Nawapongeza pia Mawaziri, Manaibu, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wanaowasaidia katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, naomba kuchangia mambo yafuatayo ambayo yamekuwa ni kero au changamoto kwa jamii katika maeneo husika:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Mkoa wa Dar es Salaam. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka 2015 alipokuwa kwenye kampeni katika Mkoa wa Dar es Salaam, Jimbo la Segerea kwenye mkutano Vingunguti aliahidi kujenga barabara ya Segerea Seminari kuelekea Majumba Sita kupitia Kituo cha Polisi cha Stakishari kwa kiwango cha lami na kujenga daraja, lakini mpaka sasa hakuna dalili yoyote hata ya kukarabati ili wananchi wapite kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni mbovu watu wanapita ndani ya mto wakati wakielekea maeneo ya Ukonga kutafuta huduma mbalimbali kama *Airport*, Hospitali ya Ukonga ya Rugambwa, Mahakama ya Mwanzo Ukonga na maeneo mengine ya huduma. Eneo la Segerea *Shell Oilcom* (Kona ya Segerea Seminari) inahitaji mfereji wa

kupitisha maji ya mvua kwa haraka ili kunusuru ile barabara isikatike kwa mvua inayoendelea maana hali ni mbaya katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Afya itoe fedha za bajeti kwa wakati ili kukidhi mahitaji katika sekta ya afya kwa muda unaohitajika. Kuchelewesha kutoa fedha kwa wakati husika kunasababisha maafa na kurudisha nyuma jitihada nzuri za Serikali za kuboresha sekta ya afya. Kwa mfano, Kitengo cha Moyo Muhimbili *(Jakaya Kikwete Cardiac Institute)*, Kitengo cha Mifupa *(MOI)*, Wodi ya Wazazi wanalala wawili kitanda kimoja na hii inasababisha maambukizi kwa watoto wachanga na kusababisha vifo. Hospitali zote za Rufaa na vituo vyote vya afya, naiomba Serikali kupitia sekta hii nyeti ya afya fedha zake zipewe kipaumbele, Wizara ya Fedha itilie maanani suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Madaktari wetu wanafanya kazi nzuri sana na ya kizalendo kwa kutoa huduma kwa kiwango cha Kimataifa hasa pale *(Jakaya Kikwete Cardiac Institute)* na Kitengo cha Mifupa *(MOI)* na pia Hospitali ya Kansa *Ocean Road*, Benjamin Mkapa Dodoma na Madaktari wote na Wauguzi nawapongeza wote sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muungano wetu na changamoto. Kwanza ni suala la biashara na ajira katika Taasisi za Muungano, napenda kuishauri Serikali kuhusu masuala haya bandari tuachiwe biashara ndogondogo tupitishe bila pingamizi. Pili, ajira nazo zikitokea kuhusu Muungano tupewe japo kama Tanzania watu kumi basi tupatiwe watu wanne kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kuhamia Dodoma. Utekelezaji wa zoezi hilo unaimarika Watumishi wa Umma na Taasisi mbalimbali wamehamia Dodoma.

Miundombinu hasa barabara za ndani hasa kama *Area D'* barabara ni mbovu mno. Naishauri Serikali yangu izione barabara hizo au *TBA* nao wanahusika kuhusu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi. Naishukuru Serikali kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji ambao unatoa mikopo kupitia vikundi vya vijana, wanawake, wazee, watu wenye ulemavu na makundi mengine. Naomba Mfuko huu uimarike uzidi kusaidia mpango huu hasa kusaidia wanawake ili wajikwamue kiuchumi na kuondoa umaskini na kudhalilika kijinsia pia vijana kupata asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la vita dhidi ya dawa za kulevya. Madawa ya kulevya nchini ni tatizo. Vijana tunaowategemea ndiyo wanaoathirika hapa nchini licha ya Serikali kujitahidi juu ya suala hili bado ijitahidi kupatiwa vituo vya *Sober House* ili kuwapatia masomo na ujasiriamali waondokane na kadhia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara za vijijini na mjini. Wakala wa Barabara *TARURA*, ufanisi wao ni mdogo hawajengi barabara za kiwango wanakuwa wanafyeka tu, madaraja mabovu yakipata dhoruba za mvua yanakatika. Serikali sasa inaanza kupata hasara kubwa. Nashauri Serikali yangu Halmashauri ziwasimamie *TARURA* utendaji wao wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyojaa mashiko na mambo yote nasema ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia katika suala la kazi na wafanyakazi hasa Watendaji wa Vijiji ambao wameondolewa kazini kwa sababu ya kiwango chao cha elimu, yaani darasa la saba. Wafanyakazi hawa wamelitumikia Taifa letu wakati likiwa kwenye uhaba mkubwa wa watumishi na wengine walishindwa kujiendeleza kwa sababu ya mazingira halisi ya

maslahi yao. Kuwaondoa bila hata kupata marupurupu siyo haki kwao. Nashauri Serikali itazame upya suala hili, kwani linaleta chuki kwa Serikali yao, kama hawatarudishwa kazini, basi wapewe stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la viwanda. Viwanda 3,000 ambavyo inasemekana vipo, ni vema vikaainishwa ili Watanzania waweze kutambua vipi ni viwanda vikubwa, vya kati na viwanda vidogo. Vilevile tujulishwe viko wapi kwa ajili ya utambuzi. Nashauri pia Serikali iweke mazingira tulivu ya uwekezaji ili kupata wawekezaji wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee kuhusu suala la walemavu. Pamoja na kwamba hatua mbalimbali zimekuwa zikifanywa kuwawekea mazingira mazuri watu wenye ulemavu, bado kuna tatizo la tengeo la fedha hasa kwa ajili ya vifaa tiba vya *albino* (mafuta) pamoja na huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ifanye utafiti wa kina ili kubaini watu wenye ulemavu wasio na uwezo wa kujitibu wapatiwe matibabu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri kwa Serikali kwamba suala la kuhamisha Walimu wa Shule za Sekondari kwenda Shule za Msingi liangaliwe kwa jicho la kipekee, kwani kuna changamoto katika utekelezaji wake. Walimu hao wapewe fedha za uhamisho, wapatiwe mafunzo ya kufundisha elimu ya msingi *(child psychology),* saikolojia ya mtoto ili wakafundishe kwa ufanisi. Vinginevyo, badala ya kujenga, tutabomoa.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Nianze na suala la utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote duniani ili iwe na maendeleo, lazima ifuate sheria na taratibu ilizojiwekea kama nchi. Hivi karibuni tumeona sheria zetu zikivunjwa.

Mfano, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wamekuwa na mamlaka makubwa na bila kufuata sheria wamekuwa wakitoa amri kwa viongozi mbalimbali wakiwemo Wabunge kuwekwa ndani kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia pia, kuhusu nishati ya gesi. Miaka mitatu iliyopita wananchi waliaminishwa kuwa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam utaenda kutatua tatizo la nishati kabisa nchini, lakini katika hotuba ya Waziri Mkuu jambo hili halijazungumziwa kabisa; na kinachoendelea sasa hivi ni mradi wa *Stieglers' Gorge.* Je, ni kwa nini Serikali imeamua kubadilisha kipaumbele chake toka kwenye umeme wa gesi kwenda kwenye umeme wa maji, huku tukifahamu Serikali imeshatumia pesa nyingi za walipakodi kuwekeza kwenye mradi wa gesi asilia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huo bado haujawa *fully utilised,* kwani mpaka sasa ni 6% tu ya bomba la gesi linatumika. Naitaka Serikali iwaambie Watanzania, ni kwa nini imehamisha *focus* toka kwenye umeme wa gesi asilia kwenda kwenye umeme wa maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia, kuchangia kuhusu hali ya uchumi iliyozungumziwa ukurasa wa nane katika hotuba ya Waziri Mkuu. Hotuba inaonesha uchumi wa nchi yetu unakua kwa asilimia 6.8 kwa kiwango cha juu kuliko nchi zote za Ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka na takwimu hizo, ila tatizo langu lipo kwenye jinsi gani hali ya uchumi iko *reflected* kwa wananchi wa kawaida. Wananchi wana hali mbaya sana hata kupata milo mitatu ni tatizo. Je, huo uchumi unaokua unawanufaisha vipi wananchi, kama wananchi hawawezi hata kula milo mitatu kwa siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu

pamoja na Serikali kwa ujumla kwa hotuba nzuri iliyosheheni mambo mazuri yenye masilahi mapana kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu, mambo mengi ya msingi yamezungumzwa juu ya Sekta za Mawasiliano, Kilimo, Madini, Elimu, Miundombinu na kadhalika. Kwa leo napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi; changamoto ya ardhi imeathiri maendeleo ya wananchi wetu hususan katika Sekta ya Kilimo na katika maeneo mengi ya nchi yetu. Migogoro hii ni baina ya Vijiji na Vijiji, Kata na Kata na Wilaya na Wilaya. Kwa sehemu kubwa Watendaji wetu wa Vijiji, Kata na kushirikiana na baadhi ya Wenyeviti wa Vijiji wanakuwa ni chanzo cha changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la mgogoro wa mpaka baina ya Wilaya ya Kilindi na Kiteto, suala hili limechukua muda mrefu sasa. Binafsi nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye mwaka 2017 alifika katika eneo hili kwa kuambatana na Waziri wa Ardhi na TAMISEMI na kutoa maagizo kwa Wataalam kupitia upya mpaka huo kwa kutumia *Government Notice No. 61.* Taarifa hiyo toka mwezi Machi, 2017 ilitoka ikibainisha wazi wapi mpaka wa Wilaya hizi upo. Jambo la kushangaza, mpaka leo hakuna utekelezaji wa kuweka alama za mpaka wakati Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni mia moja kwa ajili ya utekelezaji wa agizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa maeneo ya mpakani wa Wilaya hizi bado wanaendelea kusubiri hatima ya jambo hili. Vile vile shughuli za kilimo na mifugo kwa kiasi kikubwa zimesimama kusubiri hatima ya suluhisho la mgogoro huu na mara kadhaa wananchi wa maeneo haya wameendelea kugombana kwa sababu ya wafugaji kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima. Ni matumaini yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kupitia Wizara hizi mbili (TAMISEMI na Ardhi) watakwenda na kuweka alama za kudumu ili kutoa suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kutoa mchango wangu ni suala la maji vijijini. Changamoto ya maji vijijini bado ni kubwa, pamoja na jitihada kubwa za Serikali za kutatua changamoto hii. Naipongeza Serikali kwa dhati kwa jinsi inavyohakikisha na kudhamiria kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya maji katika Vijiji na Miji yetu mingi inakosa ubora unaotakiwa. Hii inatokana na baadhi ya Watumishi wetu kwa kushirikiana na Wakandarasi kukosa uadilifu. Naishauri Serikali iweke utaratibu kwa Wizara zenye dhamana na Sekta ya Maji na TAMISEMI wahakikishe kuwa wanaunda Kitengo Maalum cha ufuatiliaji wa miradi hii ya maji, inajengwa kwa kiwango na kuzingatia thamani ya fedha *(value for money)* badala ya kusubiri hadi Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kupitia hesabu za maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke fedha zikitengwa kutekeleza mradi fulani huchukua miaka mingi eneo husika kupata tena fedha kwa mradi wa maji. Ni vema kwa sasa Serikali ikawa na mpango thabiti wa kusimamia miradi hii na kuwadhibiti wachache ambao hawana uchungu na rasimali za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa dhati kwa kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini. Uamuzi huu una dhamira ya kuhakikisha barabara zetu zinapitika katika kipindi chote cha mwaka. Dhamira hii nzuri ya Serikali inatakiwa iende sambamba kwa kuwa na chombo cha ufuatiliaji wa kazi za *TARURA* kwa kuangalia ubora wa kazi za *TARURA*. Je, ni nani msimamizi wa kazi za *TARURA*? Uwepo wa chombo hiki utasaidia dhamira nzuri ya Serikali juu ya uanzishaji wa chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali sasa ione umuhimu wa uanzishaji wa chombo kinachofanana na *TARURA* kwa kuanzisha Mamlaka ya Maji Vijijini. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa kero ya maji vijijini. Chombo hiki kitakuwa na usimamizi wa

huduma ya maji vijijini tukikumbuka sehemu kubwa ya Watanzania wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwa umahiri mkubwa. Nataka nianze mchango wangu kwa kuiasa Serikali kuwa japo upatikanaji wa mapato siyo mzuri sana, lakini hata hicho kidogo kinachopatikana basi kuwe na mgawanyo wa haki, kwani Watanzania wote ni walipakodi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikipitia bajeti zote za Awamu ya Tano. Mgawanyo wa fedha za maendeleo kwa mikoa ya Kusini, Lindi na Mtwara ni kidogo sana. Mikoa hii haina miradi mikubwa ya maendeleo. Jambo hili limekuwa ndiyo chanzo cha kudidimia uchumi wa mikoa hii, hata pale mikoa hii inapokuwa na miradi, basi miradi hiyo haipewi fedha kwa wakati. Mfano, mradi wa barabara ya Masasi – Nachingwea - Nanganga ambayo upembuzi wake ulikamilika tangu mwaka 2015, lakini hadi leo mradi huu haujapatiwa fedha, wakati miradi mingine mipya imekuwa ikipata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusisitiza hoja yangu ya mgawo wa fedha za maendeleo kwa Mikoa ya Kusini kwamba siyo wa kuridhisha, hata Kamati zako za Bunge zimekuwa hazifanyi ziara katika mikoa hiyo kwa kuwa haina miradi ya kwenda kukagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali kuhamia Dodoma ni kwa kuwa Dodoma ni katikati ya nchi yetu. Hivyo kuweka Makao Makuu hapa ni kuwezesha taasisi na wananchi kufika Makao Makuu ya nchi kiurahisi. Lengo hili halitakuwa na maana kwa wakazi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara iwapo barabara ya kuunganisha Mkoa wa Lindi hadi Morogoro haitajengwa, kwani barabara hii ni muhimu sana kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ili kufika Dodoma kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa haipeleki fedha za miradi kwenye Halmashauri zetu kwa masharti kwamba miradi hiyo ni lazima ianze kutekelezwa na Halmashauri husika. Utaratibu huu unaendelea kuziacha nyuma zile Halmashauri zenye mapato madogo ambazo hazina uwezo wa kuanzisha miradi mikubwa kama ujenzi wa Hospitali za Wilaya, majengo ya Mahakama za Wilaya na majengo ya Vituo vya Polisi vya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naishauri Serikali kuangalia upya utaratibu usio wa haki. Mfano katika Jimbo langu la Liwale, hatuna majengo hayo yote niliyotaja hapo juu na Halmashauri haina uwezo wa kujenga majengo hayo. Kama ni lazima miradi hiyo ianzie ngazi ya Halmashauri, basi Wilaya ya Liwale haitakaa ipate majengo ya Hospitali, Mahakama na Kituo cha Polisi cha Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye majibu ya Waheshimiwa Mawaziri Bungeni. Kumekuwa na tabia ya baadhi ya Mawaziri kutoa majibu mepesi kwa Waheshimiwa Wabunge bila kuzingatia hali halisi ya mazingira ya swali. Jambo hili linafanya majibu haya baada ya muda yanaonesha Waziri alilidanganya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa majibu haya ni jibu la swali langu kuhusu ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Liwale. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana alinijibu, ujenzi huo utakamilika ifikapo mwaka 2018. Cha kushangaza, hata kwenye Randama ya Bajeti ya mwaka 2018/2019 mradi huu haumo. Je kujibu vile Mheshimiwa Waziri alikusudia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie habari ya Utalii. Kumekuwepo na mradi wa kukuza Utalii Kanda ya Kusini. Cha kushangaza, mradi huu Mikoa ya Lindi na Mtwara haimo. Jambo hili haliwezi kuvumilika kwa wakazi wa mikoa hiyo, kwani ukiizungumzia Kusini juu ya utalii, huwezi kuiacha Hifadhi ya *Selous* ambayo kwa kiasi kikubwa iko Lindi. Iweje fedha zenye jina la kuendeleza Kusini zipelekwe Mbeya, Iringa

na Morogoro, ukaiacha Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani? Hii siyo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kuendelea kuitenga Mikoa ya Kusini, hata pale Mungu anapoamua kuiinua mikoa hii. Mfano upatikanaji wa gesi ambako hadi leo hakujasaidia lolote kwani hadi leo Lindi na Mtwara ndiko kuna matatizo ya upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na uandikishaji mzuri kwa wanafunzi wa darasa la kwanza, lakini kiwango hiki hakina uwiano mzuri na wahitimu wa darasa la saba. Jambo hili linaashiria kuporomoka kwa elimu yetu, sababu kubwa ni Serikali kutokuwekeza kwa upande wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikama ya Walimu wa Shule za Msingi ni mbaya sana. Mfano katika Halmashauri yangu kuna Shule za Ndapata, Kikulyungu, Norongopa. Shule hizi zina Walimu watatu kila shule. Jambo hili lipo nchi nzima. Tatizo la Walimu ni kubwa sana. Siyo hivyo tu, hata hawa Walimu wachache tulionao hatuwawekei mazingira bora ya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonesha ni asilimia 39 tu ya Walimu wanaoingia madarasani na kufundisha kwa moyo au ari. Hivyo asilimia 61 wako kazini tu, kwani wamepoteza morali ya kazi, wana migomo ya kimoyomoyo. Kwa ujumla, Walimu wamekosa mtetezi. Watumishi wengi sasa Serikalini wamepoteza morali ya kazi na kubaki na manung'uniko moyoni mwao kwani mishahara yao ni midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TARURA,* nashauri litolewe ufafanuzi, kwani haiko wazi kwamba fedha hizi za Serikali zinasimamiwa na Mamlaka gani? Kama ni Mhandisi wa Maji, Afisa Elimu, Afisa Kilimo, wote hawa wanawajibika kwa Madiwani. Kwa nini Meneja wa *TARURA* asije kwenye Baraza la Madiwani wakati barabara zinazojengwa wamiliki ni Madiwani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu; Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa na Baraza lote la Mawarizi kwa namna wanavyofanya kazi usiku na mchana kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo endelevu ni maendeleo ya watu na siyo vitu. Maendeleo ya watu huonekana katika viashiria kama vile pato la mtu mmoja mmoja, fursa ya kupata huduma muhimu kama elimu, afya, mavazi, maji safi, umeme na huduma za usafiri. Naipongeza sana Serikali kwa kuhakikisha kwamba maendeleo ya watu yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote makubwa yanayofanyika nchini yamelenga kuboresha maisha ya Watanzania. Mfano, elimu bure, maboresho mbalimbali katika Sekta ya Afya, miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege na mengine mengi yanaendelea kufanyika na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi maridadi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya ahadi za viongozi wa Kitaifa hususan Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, mpaka sasa hazijatekelezwa. Kwa namna moja au nyingine zinakatisha tamaa wananchi kwa kuona baadhi ya ahadi hazitekelezwi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu hususan barabara, katika Jimbo la Lupembe Halmashauri ya Njombe *DC* kuna barabara ya Lupembe, yaani Kibene – Lupembe – Madeke (kilometa 126) iliahidiwa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete mwaka 2010 na kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 iliahidiwa kuwa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Mwaka 2016/2017 na mwaka 2017/2018 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliipangia bajeti barabara

hii kwa ajili ya kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami kilometa 50, lakini mpaka leo hii tukiwa tunamaliza mwaka wa fedha, barabara hii haijaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana kwani ndiyo barabara pekee inayounganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro kupitia Mlimba. Pia kiuchumi barabara hii ndiyo inayoongoza kwa kuwa na magari mengi yanayosafirisha mazao mbalimbali katika Mkoa wa Njombe. Mazao yanayosafirishwa na barabara hii ni mbao, chai, mahindi, maharage, matunda mbalimbali na viazi. Hivyo tunaomba barabara hii itengenezwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali kwa kuhakikisha kwamba dawa zinapatikana katika hospitali zote. Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ni miongoni mwa Halmashauri ambazo hazina Hospitali za Wilaya. Halmashauri hii ina Vituo vya Afya vinne; Kituo cha Lupambwe, Kichiwa, Matembwe na Sovi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa ukarabati wa Vituo vya Afya, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ilikuwa ni miongoni mwa Halmashauri ambazo ziliahidiwa kupewa shilingi milioni 500. Nami kama Mbunge wa Jimbo, nilipewa taarifa na kuoneshwa orodha ya Halmashauri zilizopata shilingi milioni 500. Cha kushangaza, fedha zilipotoka hazikuletwa kwenye Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufuatilia sana, nikaambiwa tutaingiziwa kwenye mpango wa shilingi milioni 400. Fedha zilipotoka, bado Halmashauri yangu haijapata fedha hizo wakati kuna Halmashauri zimepata fedha za ukarabati kwa Vituo vya Afya viwili, nyingine vitatu. Juzi juzi tumeona baadhi ya Halmashauri zimepata vituo mpaka vitano. Halmashauri hii licha ya kuwa ina changamoto ya usafiri, vituo vyote havina hata gari la wagonjwa, lakini pia kwenye mgao wa magari tumekosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba *resources* tulizonazo hazitoshi kusambaza kwenye

Halmashauri zote, lakini angalau basi wale wenye matatizo makubwa zaidi angalau wawe wanafikiriwa. Fedha ni kidogo lakini kilichopo angalau tugawane wote. Wananchi wa Jimbo langu wanavyopata taarifa zinazoonesha Halmashauri nyingine zimepata fedha za ukarabati na miradi mingine ambayo viongozi wetu wameahidi na wao hawapelekewi hizi fedha, wanajisikia vibaya na kuona kama wanatengwa. Hivyo naiomba Serikali angalau itusaidie fedha hizi za ukarabati wa Vituo vya Afya vya Lupembe, Kichiwa na Sovi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Napongeza jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba vijijini na mijini kunakuwa na umeme. Hii itasaidia sana maendeleo ya viwanda nchini. Katika Jimbo langu kuna maeneo tayari wananchi wameitikia kaulimbiu ya Tanzania ya viwanda kwa kununua viwanda. Mfano Kijiji cha Ninga wamenunua Kiwanda cha Sembe chenye uwezo wa kuchakata tani 12 mpaka 20 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba kijiji hiki hakina umeme pamoja na ahadi za muda mrefu kwamba wataletewa umeme. Pia tuna Kijiji cha Madeke walinunua Kiwanda cha Kusindika Matunda lakini hakuna umeme. Pamoja na jitihada za Serikali kupitia mpango wa *REA,* lakini kasi yake bado ni ndogo. Hivyo tunaomba maeneo haya yapelekewe umeme haraka ili viwanda hivi vianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naipongeza Serikali hasa Waziri Mkuu kwa kufika Lupembe na kutatua baadhi ya changamoto mwaka 2017. Naomba Mwenyezi Mungu amjalie afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja iliyopo mezani.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana juhudi za Serikali kwa kazi nzuri zinazofanyika kwa ajili ya manufaa ya wananchi. Naipongeza sana Ofisi

ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri hasa katika kuwezesha wananchi kuongeza kipato kwa kupitia mikopo kwa vijana na vikundi vya wanawake, *SACCOS* na *VICOBA*. Ushauri kwa Serikali, naomba Serikali kujenga *Hostel* kwa kila sekondari ili watoto wetu waweze kukaa shuleni na kuepukana na kupata mimba kwa watoto wa kike na kuongeza kiwango cha elimu kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, naishauri Serikali ipeleke umeme kila Shule ya Msingi na Sekondari, ijenge miundombinu ya shule kama vile ujenzi wa vyoo vya shule, nyumba za Walimu pamoja na kumalizia maboma ya madarasa ambayo wananchi wameshajenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo, Serikali ipeleke mbolea na mbegu kwa wakati au kwa kufuata kalenda ya kilimo. Pia ilipe deni la Wakala ambao bado hajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali itatue tatizo la maji hasa vijijini na kuongeza Mfuko wa Maji ili bajeti ya Wizara ya Maji iwe inatosha. Pia kuanzisha Bodi ya Maji kila Wilaya; kuwe na chombo ambacho kitafuatilia utekelezaji wa miradi ambayo Serikali imeshapeleka fedha nyingi na miradi hiyo haijakamilika. Serikali imalizie maboma ya Vituo vya Afya na Zahanati ambazo bado hazijakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii kuchangia machache katika bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukizungumzia suala la amani kila siku, inawezekana sielewi amani inayozungumziwa ni ipi katika Taifa letu, kwani yameendelea kutokea matukio mbalimbali ya kutisha, watu wamekuwa wakiokotwa kwenye fukwe zetu za bahari wakiwa wamekufa; wengine wamepotea katika mazingira ya kutatanisha, wengine

wamekuwa wakitekwa na watu wasiojulikana; pia waandishi wa habari wamekuwa wakipigwa na kutekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari zilizoko mitaani zinadai kuwa Waandishi hao hufanyiwa hivyo kwa sababu ya kuandika mambo yasiyofurahisha wakubwa. Naomba kujua Serikali inachukua hatua gani kwa haya mambo yanayoendelea katika nchi yetu ambayo tunadai nchi yetu ni ya amani na utulivu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza viongozi wa dini; Maskofu kwa waraka wao waliotoa kuonesha hali ya nchi ilivyo kwa sasa. Naishauri Serikali badala ya kuubeza waraka huu tukae chini kama Taifa, tujadiliane haya kwa maslahi ya Taifa letu. Viongozi hawa wa dini wamekuwa wakituombea katika shughuli zetu za kila siku. Hivyo tusiwapuuze tu kwa sababu wamesema ukweli kuhusu hali ya nchi ilivyo, kwa sababu tusiombe tu kuombewa lakini pale wanapoona nchi haiendi vizuri wakisema, mnasema wametumwa na Wapinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba kama Taifa, kuna kila sababu ya kuzungumza kuhusu Taifa letu linavyokwenda kwa maslahi ya nchi yetu ya Tanzania, tusitengeneze Taifa la chuki na visasi. Naomba sana Serikali itutafutie hawa watu wasiojulikana ni akina nani na wako wapi? Tusiache hali hii ya wasiojulikana kuendelea kutesa na kuwa hakuna aliye salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya nchi yetu haiko salama sana. Naishauri Serikali kuhakikisha tunafanya mazungumzo na nchi tunazopakana nazo ili kukabiliana na uwekaji wa mipaka hiyo. Kamati yetu ilitembelea mpaka wa Uganda na Tanzania, hali siyo nzuri. Wananchi wa Uganda wameingia ndani ya nchi yetu kwa kuvuka alama za mipaka iliyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza *DC* wa Wilaya ya Misenyi kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama ya kuhakikisha wananchi

na mali zao ziko salama, ingawa wako baadhi ya wananchi wetu waliokufa, waliopigwa na kunyang'anywa mali zao. Naishauri Serikali kuweka barabara katika maeneo ya mipaka yetu ili kuweza kuwarahisishia Watendaji wetu kufika kwenye maeneo hayo pale yanapotokea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la barabara ni kubwa sana. Hivyo ni muhimu tukachukua hatua za haraka kuondoa kero hiyo. Wenzetu upande wa pili; Uganda, wana barabara inayopitika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo machache niliyokuwa nayo kwa leo.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu katika maeneo machache ambayo napenda kupata majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ahadi ambazo Waziri Mkuu amezitoa bado kuna mgogoro wa wananchi wa Kata ya Mngeta, Kijiji cha Ikule na Vitongoji vyake na JKT Chita ambapo Jeshi limechukua ardhi kubwa ya kilimo bila maridhiano wala muhtsari wa Kijiji na JKT Chita kumiliki eneo lote kwa kulichukulia hati Wizara ya Ardhi na kujipa uhalali pasipo wanakijiji kushirikishwa na kusababisha umaskini mkubwa kwa wananchi hasa ukizingatia wote wanategemea kilimo na hawana ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu alinitamkia/ kuwatamkia wawakilishi wa Kijiji/Kata walipofika ofisini kwake Dodoma mwaka 2016 kuwa angeagiza mazungumzo yawepo ili kupata muafaka wa suala hilo ambapo alishauri katika eneo lenye mgogoro ni vema kila mmoja akapata na kupoteza na si kundi moja kutaka kutwaa eneo lote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi niandikapo hakuna utatuzi isipokuwa ni vitisho kwa wananchi. Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na Waziri wa Ulinzi wameshindwa kusimamia utatuzi wa mgogoro huu isipokuwa ni vitisho. Hali ya

wananchi inaendelea kuwa dhaifu kwa kukosa maeneo ya kilimo na kusababisha umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni tatizo la vijiji viwili vya Idandu na Miyomboni vilivyopo Kata ya Mofu na Namwawala, Jimbo la Mlimba kutoruhusiwa kufanya uchaguzi wa vijiji hivyo tangu mwaka 2014 kwa hoja kuwa eneo hilo ni la uwekezaji na toka wakati huo hakuna aina yoyote ya uwekezaji uliofanyika. Hii inasababisha wananchi kukosa uongozi wa kusimamia au kuhamasisha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua ni lini sasa Ofisi ya Waziri Mkuu itakwenda kuyapatia ufumbuzi masuala hayo yanayoleta kero kubwa kwa wananchi wa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuchangia kuhusu *gratuity* ya Waheshimiwa Wabunge. Kukata kodi *gratuity* ya Waheshimiwa Wabunge siyo sahihi kabisa kwa kuwa kwa sasa tunakatwa kodi kwenye mishahara yetu. Nashauri wakati wa *Finance Bill* ondoeni kodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni lini agizo la Mheshimiwa Rais la kushusha riba katika taasisi za fedha litaanza ili wananchi wetu wakope na wakuze uchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, pitieni upya mgawo wa fedha za elimu bure kwani hazitoshelezi kuendeleza shule zetu.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii, ukurasa wa 23, imeonesha kuwa tayari Mheshimiwa Rais amekwishasaini Sheria ya Kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo ilitungwa na Bunge. Kufuatia kusainiwa kwa sheria hiyo inatakiwa ianze kutumika ili kuhakikisha wadau wa mifuko hiyo wanapata stahiki zao hasa pale wanapoacha kazi kwa kustaafu au kwa kuachishwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *concern* kubwa ya wadau ni *formula* ya kikokotoo kitakachotumika kwa ajili ya kulipa mafao ya kustaafu au kuacha kazi kwani katika sheria kikokotoo hakikuwekwa na Serikali ilisema kuwa *formula* itawekwa katika kanuni. Uzoefu unaonesha kuwa sheria nyingi zinazopitishwa na Bunge na kusainiwa na Mheshimiwa Rais zinachelewa kutungiwa kanuni. Hivyo basi, Serikali ijitahidi kutunga kanuni mapema ili sheria iweze kuwa *effected*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali itoe elimu kwa wadau wa mifuko hii ili ku-*raise awareness* kuhusu mabadiliko ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hotuba ya Waziri Mkuu inayohusiana na mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha za Ofisi yake na ya Bunge kwa mwaka 2018/2019, naomba nichangie kwenye huduma za jamii kipengele cha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Waziri Mkuu imeonesha kuna mafanikio makubwa ya mpango wa utoaji elimu ya awali na msingi bila malipo. Katika maelezo yake imeonesha Serikali imekuwa inapeleka fedha zote za ruzuku moja kwa moja katika shule zetu. Sisi wawakilishi wa wananchi katika maeneo yetu tunayotoka fedha hizo hazifiki kwa wakati na pia hazitoshelezi mahitaji ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano hai wa Jimbo la Manispaa ya Iringa, kuna baadhi ya shule ambazo ruzuku hii haitoshelezi mahitaji yao. Mfano wameshindwa kumlipa mlinzi wa Shule ya Msingi Azimio kwa muda wa mwaka mmoja na miezi mitatu, pia maji yamekatwa wanafunzi wa shule ya awali hawapati uji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika ongezeko la kuandikisha watoto shule za msingi naona imeshuka kutoka

2,120,667 mwaka 2017 hadi kufikia 2,078,379 mwaka 2018. Je, hili ni ongezeko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tusiweke siasa katika elimu kwa sababu elimu ni ufunguo wa maisha.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa kunipa nguvu ya kuweza kuchangia kwa maandishi angalau kutimiza azma yangu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi za dhati kwa kazi njema ifanyikayo ndani ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa miaka hii miwili na nusu chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wakishirikiana na mtendaji wao mkuu, Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa, katika lengo la kuwainua wananchi wetu kiuchumi, kuondoa umaskini na kwa jitihada ya kuanzisha na kuimarisha miundombinu yote ya kufanikisha uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu suala la ajira. Katika ukurasa wa 20, aya ya 37 ya hotuba amesema Serikali itaendelea kuimarisha ufuatiliaji wa tathmini ikiwa ni pamoja na kufanya kaguzi, kusajili, kusuluhisha na kuamua migogoro katika maeneo ya kazi. Sasa huu utaratibu uliopitishwa wa kuwaondoa watumishi wa darasa la saba ambao wamefanya kazi nzuri kuanzia Awamu ya Kwanza na jitihada zao ndio zimetufikisha hapa ndani ya Awamu ya Tano siyo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali tusizue mgogoro ambao tunalazimika wenyewe kuushughulikia kuupatia ufumbuzi. Kwanza miongoni mwao wanastaafu sasa na wataendelea kustaafu, ni bora kwa busara kuanzia sasa tuendelee na utaratibu huo unaohitajika kwa wakati huu. Hata wakati ule walikuwepo kwa uchache wao, lakini hawakuwa na wito wa kazi hizo na darasa la saba

walizichukua. Narudia tena tuwaache wamalizie muda wao wa utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu barabara, ukurasa wa 44-45. Naipongeza Serikali yangu kwa jitihada ya kujenga miundombinu ya barabara hapa nchini kwa jitihada ya kuunganisha wilaya na mikoa hata na nchi jirani. Napenda kukumbushia kwa Serikali hii sikivu kwamba mikoa ya pembezoni ilisahaulika na msukumo wa maendeleo ya barabara ulichelewa kuwafikia ndio maana maendeleo yao bado yanasuasua katika nyanja zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Daraja la Momba kujengwa na kuunganisha Chunya (Kamsamba) na Rukwa (Kilyamatundu) lakini barabara zake kuelekea Chunya na kuelekea barabara kuu ya Tunduma – Sumbawanga ni za udongo, hivi Serikali inaonaje na barabara hizo kuwa za kiwango cha lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeweza kupita Mlima Kitonga na Mlima Nyang'oro ambayo awali ilitupatia wananchi shida sana ya kupita na kuchukua muda mrefu, lakini sasa naishukuru Serikali yangu imetatua tatizo na milima hiyo inapitika na usafiri wake kwa wananchi umewarahisishia na kutekeleza majukumu yao kwa urahisi na wepesi kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali kuangalia na barabara za milima inayoteremka mabonde ya Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika kwa kuanza na hatua za awali kuelekea kiwango cha Kitonga na Nyang'oro ili wananchi wa maeneo hayo wafaidike na matunda ya Serikali yao na ikumbukwe tunapakana na nchi ya DRC – Congo na Zambia. Pia tunaomba jitihada kubwa kuongezeka kwa sasa kwani zinasuasua za Mkoa wa Rukwa kuunganishwa na Mikoa ya Katavi, Kigoma na Tabora na nchi za Zambia na DRC – Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali kutoa tamko au mwongozo wa *TARURA* kushirikiana na Mabaraza

ya Halmashauri kwani kule wanawashirikisha wananchi wa maeneo husika kufanya kazi. Pasipo kufanya hivyo kazi yao itakuwa ngumu au itawagharimu sana wakikosa ushirikiano wa awali kabla ya utekelezaji wao kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuhusu maji, ukurasa wa 52 – 53. Maji ni uhai wa viumbe wote duniani na ndiyo eneo nyeti linalohitajika kufanikisha mengine yote. Tunajitahidi kuanzisha miradi ya maji ambayo bado haijakidhi mahitaji kwa kutoa matokeo mazuri, imekuwa ni miradi ya kunufaisha hao wanaoifanya siyo walengwa (wananchi). Mradi haujatoa matokeo mhusika keshalipwa mabilioni ya pesa, siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, taasisi zetu za majeshi hawana maji na ndiyo tunawategemea kwa ulinzi na usalama, mchana na usiku ndani ya nchi na nje. Pia shule na vyuo kukosa maji ni janga la kipekee. Matatizo ya taasisi za majeshi na shule kukosa maji yamekithiri Lindi, Mtwara, Rukwa, Ruvuma kwa ujumla mikoa ya pembezoni mwa nchi yetu, tuangalieni kwa huruma, tusijutie kuwa pembezoni ni tatizo kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wakandarasi ambao hawana uwezo wa kuchimba visima na kupatikana maji kwa lengo la eneo husika wasipewe kazi na apewe muda wa kipindi maalum cha maji kupatikana na ndipo akubalike kupewa mradi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne ni afya, ukurasa wa 54. Tunashukuru jitihada ya Serikali na kujituma kwa Waziri mwenye dhamana kuhakikisha huduma ya afya inasonga mbele. Hata hivyo, jitihada hii ya kuongeza idadi ya vituo vya afya nchini tunaomba iende sambamba na ujenzi wa Hospitali za Wilaya kwani Mkoa wa Rukwa hakuna hata wilaya yenye hospitali pamoja na kuanzishwa mwaka 1974.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kushirikiana na wataalam wake kuona umuhimu wa Wabunge wa Viti Maalum kupatiwa angalau

nusu ya Mfuko wa Jimbo kwa wastani wa idadi ya majimbo yaliyomo ndani ya mkoa anaoishi. Kwani Mbunge wa Viti Maalum na Mbunge wa Jimbo hawatofautiani kwenye majukumu ingawa wa Viti Maalum anazunguka mkoa mzima na kuwajibika ndani ya majimbo yote ya Mkoa. Sio ndani ya chama changu, wananchi na Serikali hawatutenganishi wanatuhesabu Wabunge tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu huu wa kilimo zao kuu la chakula mahindi linapata pigo kubwa kutokana na kushambuliwa na viwavi (*fall army worms*). Wadudu hao wavamizi wameshambulia zao hili katika maeneo mengi ya Mikoa ya Arusha, Manyara, Tanga, Kilimanjaro, Simiyu, Mara wakati mimea iko katika hali ya kuota na palizi na cha kutisha ni kuwa dawa nyingi zimeshindwa kuwatokomeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karatu wakulima wake wengi wameathirika hadi hivi sasa wakati mahindi yako katika *stage* ya kutoa maua bado hao viwavi ni tishio kubwa. Hali hii isipodhibitiwa uzalishaji wa zao hilo utapungua sana na upungufu wa chakula utakuwepo. Naiomba Serikali ipeleke timu ya wataalam ili kupambana na wavamizi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chemchem za maji za Qangded zilizoko Mangola - Karatu ni chanzo muhimu sana cha kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima wa bonde la Eyasi (vijiji saba). Chemchem hizo zipo katika hatua ya kutoweka kutokana na kuingiliwa na shughuli za kibinadamu. Waziri Mkuu alipofanya ziara katika Wilaya ya Karatu mwishoni mwa mwaka 2016 wananchi hao walimlilia na hatimaye aliagiza chemchem hizo zipimwe mipaka yake kwa mita 100 na zihifadhiwe. Hadi wa leo chemchem hizo hazijapimwa na ziko katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa agizo lake bado halijatekelezwa na chemchem za Qangded bado zinaathirika sana. Mvua za

mwaka huu zimesababisha mafuriko ambayo yameziharibu sana chemchem hizo. Niombe Serikali ipeleke timu ya wataalam kushauri namna bora ya kuhifadhi vyanzo hivyo lakini fedha pia kwa ajili ya kukarabati miundombinu iliyoharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna migogoro ya ardhi inayosababishwa na mipaka tatanishi hasa kati ya wananchi na hifadhi za wanyama ambayo imeendelea kuwa kero. Kutokana na agizo la Serikali wataalam wameendelea kuweka alama za mipaka katika maeneo bila kuwashirikisha wananchi, malalamiko ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kumaliza mgogoro wa mpaka kati ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (*WCAA*) na Wilaya ya Karatu hususani katika maeneo ya Lositete, Endamaghang, Upper Kitete, pia mgogoro kati ya *TANAPA* na wananchi wa Bugei katika Wilaya ya Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* imeanzishwa kuwa mtengenezaji wa barabara za vijiji na mjini. Katika umri wake wa karibu mwaka mmoja bado hatujaona sana matunda. Barabara nyingi katika Wilaya ya Karatu hasa katika kipindi hiki cha mvua zimeharibika na *TARURA* wameshindwa kurudisha mawasiliano. Naomba Serikali kutenga fedha za kutosha kuwezesha *TARURA* kufanya kazi yake.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, nitoe pole kwa Mheshimiwa Spika na kumshukuru Mungu kwa ajili yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kutoa pole nyingi sana kwa viongozi wangu Wakuu wa CHADEMA akiwemo Mwenyekiti Taifa, Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu na wajumbe wa Kamati Kuu waliopata misukosuko mingi wakati wakitetea demokrasia ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze na kumtia moyo Mheshimiwa Sugu (Osmond Mbilinyi), Mbunge

wa Mbeya Mjini anayetumikia kifungo katika Gereza la Mbeya. Naamini haya yote yatapita kama upepo uvumapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma zaidi ya mara mbili hotuba ya Waziri Mkuu kuna maeneo mengi hayana ukweli na hayana uhalisia wa yanayotokea hapa nchini. Nikianza na mafanikio ya Awamu ya Tano kujenga ari ya uzalendo, kudumisha amani, utulivu na mshikamano. Jambo hili limenishangaza kwa kuwa uzalendo msingi wake mkuu ni upendo na uelewano na ndiyo maana uzalendo haujengwi kwa kampeni bali kwa mahusiano mema na hivyo huja *automatically*. Vilevile hatuwezi kuwa na mshikamano au umoja kama kuna chuki, ubabe, matumizi mabaya ya dola kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na kuwa ulinzi na usalama dhidi ya upinzani umeimarishwa sana na ndiyo sababu kila leo ni wapinzani kukamatwa na polisi au kuripoti polisi na mahakamani. Mbaya zaidi hata walipopata dhamana ile siku ya Alhamisi Kuu eti gari za magereza zikawa mabovu wakati Kisutu Mahakamani magari mengi yalikuwepo bila kazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ilipelekea viongozi hawa kuendelea kusota Segerea gerezani. Pia hata wafungwa na mahabusu waliokuwa wapelekwe Mahakama Kuu na nyinginezo walikosa kufika. Hii ni kinyume kabisa na huu ni ukiukwaji wa haki za binadamu na haki za mfungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii imerejewa tena ukurasa wa 10 pale anapozungumzia masuala ya siasa baada ya miaka 26 ya Vyama Vingi nchini kuwa ni jukumu la kila chama kunadi sera zake. Najiuliza unanadi vipi sera wakati mikutano ya hadhara imezuiwa? Huku chama tawala kikifanya kupita Mwenyekiti wake wa Chama kwa kofia ya Urais huku wengine kina Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Cheyo na kadhalika ambao ni Wenyeviti wa Vyama Taifa wakikosa fursa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua Wabunge na Madiwani kuruhusiwa kufanya mkutano ndani ya maeneo yao lakini ni wazi lengo la uanzishwaji wa vyama vingi na kazi ya vyama ni mikutano kwa ajili ya kupata wanachama. Hivyo ni ombi na rai yangu kuwa zuio hili liondolewe na kufuata Sheria ya Vyama vya Siasa ya 1992 iko wazi kwamba vyama vya siasa vitanadi sera zake sasa vitanadi vipi wakati Mheshimiwa Rais ameweka zuio?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unahamasishaje ujenzi wa demokrasia kwa wananchi wote kukiwa na ubaguzi ulio wazi? Ni jambo la ajabu sana kwamba katika awamu hii ubaguzi wa wazi wazi umetamalaki kinyume kabisa na tunu muhimu tulizoachiwa na Baba yetu wa Taifa. Tumemsikia Mheshimiwa Rais akisema hawa wamenipa kura msiwabomolee hata kama wamejenga ndani ya eneo la barabara au sehemu za vyuo na taasisi za Serikali huku wengine wakibomolewa tukiamini hawakumpa kura. Imani yangu ni kuwa unaposhinda wewe ni kiongozi wa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mshikamano kama nilivyosema unafanywa kwenye misingi ya upendo na umoja na ndiyo tunu muhimu kwa Taifa lolote vinginevyo tutakuwa tunajidanganya tukisema kuna mshikamano na amani. Niliposikia Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara wakitaka kwenda kumtembelea mjumbe mwenzao Mheshimiwa Godbless Lema gerezani Arusha na zoezi hilo likakwama na baadaye Mwenyekiti na Makamu wake kuachia nafasi zao kutokana na sababu hiyo sikuamini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila sasa naamini kwa kuwa Kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii tulipokwenda kutembelea miradi ya maendeleo tulipofika Mbeya na kufika kwa *RC* na kwa kuwa ilikuwa *weekend* tulidhani ni busara kwenda kumtembelea Mheshimiwa Sugu, lakini cha ajabu hakuna Mbunge hata mmoja wa CCM aliyeambatana nasi jambo lililonithibitishia kuwa haiyumkini lililotokea Kamati ya Viwanda na Biashara ni kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kama kweli tungekuwa na mshikamano tuliouzoea Mheshimiwa Lissu angetembelewa na Wabunge wote bila kujali itikadi katika kipindi kirefu alipolazwa Nairobi Hospital. Katika hali hii ni wazi hatuwezi kusema tuna mshikamano kama viongozi. Ni ushauri wangu kuwa ni muhimu kutembea kwenye maneno yetu bado hatujachelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa Ofisi ya Msajili ambayo kimsingi ndiye mlezi wa vyama vyote vya siasa, imekuwa ama kwa makusudi ama kwa kujua na hasa ukizingatia Jaji ni msomi na ameapa kulinda Katiba yetu, cha ajabu anakubaliana na zuio la mikutano huku chama tawala kikifanya mikutano inayoongozwa na Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Nilitegemea Mheshimiwa Jaji Mutungi angekemea hili lakini amekuwa akiandika barua vyama vya upinzani kujieleza pale ambapo wanatimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezeshwaji wa wananchi, ni ushauri wangu kuwa elimu kuhusu mikopo itolewa kwa wakopaji ili wasije kunadiwa mali zao kwa kushindwa kurejesha. Vilevile kuna tuhuma nyingi kuwa mikopo hii inatolewa kiitikadi na hivyo wasio wanachama wa chama tawala wanatengwa. Naomba kama ni kweli jambo hili liachwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKIMWI bado ni tishio na hivyo ni muhimu sana sisi kama Taifa tuwe na vyanzo maalum vya fedha kwa ajili ya UKIMWI kwa kuwa bado fedha/dawa kwa asilimia mia moja tunategemea wafadhili wa nje. Ni muda muafaka sasa ule mfuko ulioimbwa muda mrefu utaanza basi uanze.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan miradi ya ujenzi. Nashauri:-

(i) Kandarasi zitolewe kwa ushindani lakini kwa kuzingatia fursa maalum kwa makampuni ya wazalendo na

wataalam wazalendo – Wakandarasi, Wahandisi Washauri, Wabunifu na Wakadiriaji Wajenzi na kadhalika. Hii itaboresha zaidi.

(ii) Kujenga uwezo wa ndani ya nchi kwa ajili ya matengenezo (*maintanance*) ya miradi hiyo na miradi mipya.

(iii) Kuiwezesha sekta kuchangia zaidi uchumi wa nchi na kadhalika.

(iv) Miradi mikubwa yote itumike kama madarasa (vituo vya mafunzo) kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu , vyuo vya kati lakini pia kwa wahitimu wa shahada na stashahada kupitia bodi ili kuhamishia ujuzi na utaalam kwa vitendo nchini. Mifano, bomba la mafuta - Hoima, *Stiegler's Gorge* - umeme, madaraja makubwa, viwanja vya ndege vikubwa, reli – *Standard Gauge*(*SGR*), majengo makubwa na yenye mahitaji mahsusi na kadhalika.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa na inastahili pongezi kwa kufanya mambo yafuatayo katika Jimbo la Songea Mjini. Ujenzi wa barabara kilomita kumi kwa kiwango cha lami, kuboresha elimu na kuboresha huduma za afya. Pamoja na hayo Jimbo la Songea Mjini linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ukosefu wa vituo vya afya katika Kata za Ruvuma, Lilambo na Ndilimalitembo;

(ii) Ukosefu wa *ambulance* na *X-ray* katika Kituo cha Afya cha Mjimwema ambacho kinahudumia zaidi ya wagonjwa 100,000 kwa mwaka;

(iii) Ujenzi wa Mtwara *Corridor by-pass* katika eneo la Jimbo la Songea Mjini;

(iv) Upatikanaji usioridhisha wa pembejeo za kilimo kama vile mbolea na bei elekezi ambayo inabadilika kila kukicha;

(v) Soko lisilo na uhakika la mazao kama vile mahindi na mbaazi;

(vi) Ukosefu wa barabara ya uhakika (lami) inayounganisha Mji wa Songea na Jimbo la Lichinga – Msumbiji;

(vii) Ukosefu wa barabara ya lami inayounganisha Mkoa wa Ruvuma na Morogoro;

(viii) Ukosefu wa viwanda vya kusindika bidhaa za kilimo; na

(ix) Malipo ya fidia kwa wananchi waliohamishwa Songea *Airport*; wananchi wa eneo la *EPZA* Mwenge mshindo na wananchi wa eneo la Bonde la Mto Luhira.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu hasa kwangu zaidi ni ushauri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naiomba Serikali ichukue hatua ya kufuatilia miradi ya maji, kwa mtazamo wangu eneo hili lina ufisadi mkubwa sana. Miradi mingi inajengwa chini ya kiwango na wakati mwingine haikamiliki kwa wakati. Mfano, Mradi wa Maji Ntomoko, Wilayani Kondoa na Chemba ambapo licha ya Serikali kutoa trilioni mbili hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni ule wa Kijiji cha Laloda ambapo mkandarasi amelipwa zaidi ya milioni mia tano (Sh.500,000,000) na hakuna hata chembe ya maji inayotoka. Niiambie Serikali ikiwezekana kuunda Tume Maalum kuchunguza miradi mikubwa na midogo ya maji kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili, naiomba Serikali iangalie kwa kina ukubwa wa Bunge letu, uwakilishi wake na dhana ya kubana matumizi. Nchi yetu ina Halmashauri mia moja themanini na tatu (183) na Wilaya

zaidi ya 169, lakini idadi ya Wabunge ni 388. Zipo Halmashauri zina Wabunge zaidi ya mmoja na katika Wilaya yupo Mkuu wa Wilaya mmoja tu. Ushauri wangu ni kuiomba Serikali ipunguze utitiri wa majimbo na kuhakikisha kila Halmashauri inakuwa na Mbunge mmoja ili kupunguza gharama na kuhakikisha Bunge linakuwa *active* kuliko ilivyo sasa ambapo Bunge limekuwa kama mkutano wa hadhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba na hilo pia nashauri hata utaratibu wa kuwapata Wabunge wa Viti Maalum utazamwe upya. Ushauri wangu ni kwamba kila mkoa uwe na Wabunge wawili wa Viti Maalum na hii itasaidia kupunguza idadi ya Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wabunge kutoka Zanzibar ipo hoja ya kubadilisha utaratibu uliopo sasa na kufanya kila Wilaya ya Zanzibar kuwa na Mbunge mmoja anayewakilisha Bunge la Jamhuri ya Muungano na pia kuwaondoa Wabunge wanaowakilisha Baraza la Wawakilishi wanaohudumu pia Bunge la Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi sioni haja ya kuwa na Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi kuhudhuria Mikutano ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi kwa wakati mmoja. Naamini kama ushauri huu utazingatiwa Serikali na Taifa litakuwa limepunguza gharama kubwa ya uendeshaji wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ni kuhusu viwanja vya michezo. Viwanja vingi vya michezo nchini vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM). Viwanja hivi vipo katika hali mbaya, nashauri Serikali ishauriane na CCM na ikiwezekana vikodishwe kwa majeshi kama Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ambapo wanaweza kuviendeleza vikawa bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kupongeza hotuba ya Waziri Mkuu, napongeza

utendaji wake na utendaji unaofanywa na Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika mambo mbalimbali ya kuongoza nchi, tuko nyuma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa kilimo katika pato la Taifa na katika kutoa ajira nchini ni mkubwa, hauwezi kupuuzwa na mtu yeyote. Hata hivyo, namna kilimo kinavyoendelezwa hapa nchini hakileti matumaini ya kuleta maendeleo ya haraka katika uchumi wa nchi na vilevile kutoa ajira kwa asilimia 75 ya wakazi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kusema hivyo ni kwamba bado pembejeo hazipatikani kwa wakati hasa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na wakati mwingine pembejeo hazipatikani kabisa. Naomba Serikali ijue misimu ya kilimo ya kanda mbalimbali ili kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kipatikane chombo kitakachopewa wajibu wa kuratibu changamoto mbalimbali za wakulima zikiwemo pembejeo, masoko na utafiti ili kuleta tija kwa wakulima badala ya kufunga mipaka ya nchi kuuza mazao nje. Wakulima wa Rukwa wanapata hasara ya uwekezaji wao katika kilimo pale Serikali inapofunga mipaka na kufanya mazao yao kukosa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani wakulima wa mazao ya nafaka wapate hasara kwa hofu ya nchi kupata upungufu wa chakula wakati mazao ya biashara yanayolimwa na mikoa mingine inapata masoko kama kawaida. Ushauri wangu ni kwamba wakulima waendelee kulima na kuruhusiwa kuuza popote mpaka pale utaratibu muafaka utakapowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni ukosefu wa ardhi kwa wananchi wa Kata wa Nkandasi, Vijiji vya Mihindikwa, Kasu, Kisura na Malongwe ambapo ardhi yao imetwaliwa na Jeshi la JKT. Takribani ni wananchi 4,000 wa vijiji hivi wamekosa ardhi huku ardhi hiyo ikiwa imekaa bila kutumiwa na mashamba yaliyonyang'anywa wanajeshi

mmoja mmoja wanalima huku wananchi wamekaa kushangaa na bila kwenda shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limezungumziwa sana lakini hakuna aliyelisikia. Naomba Serikali ilione kwa macho mawili. Kama Mbunge wananchi wamenituma niwaletee Bungeni na mimi nimetekeleza wajibu hivyo wahusika walifanyie kazi vinginevyo watabeba dhambi ya lawama ya mateso ya ukosefu wa ardhi kwa wananchi waliofukuzwa kwenye ardhi waliopewa kihalali na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayowakabili wananchi wa Jimbo la Nkasi ni kama ifuatavyo:-

(i) Maji ni tatizo na miradi inayoendelea bado haijatoa matokeo chanya kwa wananchi;

(ii) Suala la mtandao wa simu za mkononi Kata ya Kala iliyoko mpakani mwa DRC, eneo la Ziwa Tanganyika ni kero kubwa kwa wananchi hao; na

(iii) Barabara ya Kitisi - Wampembe chini ya *TARURA* zinafunga kupitika kwa kukosa matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, jimbo langu lina takribani vijiji 60 na kila kijiji tumehamasisha wananchi kujenga madarasa matatu. Wote wameitikia kabisa na sasa tuna madarasa 180 hayajaezekwa. Naomba ombi maalum kwa mwitikio mzuri wa wananchi wapewe fedha ya kuezeka madarasa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya, jimboni kuna kata 11 ambapo kata nne wameanza kujenga vituo vya afya. Kata hizo ni Nkandasi, Kala, Ninde, na Kate, takribani zahanati 12 zimejengwa tunaomba msaada wa Serikali.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019. Serikali ya Awamu ya Tano

inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kwa dhati kujenga uchumi wa kisasa unaoongozwa na falsafa ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na sera msingi ya kuimarisha miundo msingi ya uchumi ikiwemo kujenga reli ya kisasa ya *standard gauge,* ununuzi wa ndege moja kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kuanzisha mchakato wa kujenga bwawa la kuzalisha umeme *megawatt* 2,100 ili kuunganisha nguvu za uzalishaji umeme kwa kutumia maji na ule wa kutumia nguvu za gesi asilia ili kuwezesha ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa kwa kiwango kikubwa pia kuboresha na kuboresha bandari zetu katika mwambao wa bahari ya hindi na zile za maziwa makuu ya Viktoria, Tanganyika na Nyasa. Lengo kuisaidia nchi yetu kuwa kiongozi katika kukuza biashara katika nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Serikali kwa jitihada zinazozifanya za kuboresha huduma za afya kwa Watanzania ambapo vituo vya afya na hospitali nchini zimeboreshwa kwa kuongeza vifaa tiba, madawa na wataalam na matokeo yake vifo vya akinamama na watoto vimepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naiomba Serikali iongeze nguvu katika kukiimarisha kitengo cha kukabiliana na maafa hasa baada ya nchi yetu kuanza kutishiwa na matukio na matishio makubwa ya majanga ya kiasili ambapo siku za karibuni tumeshuhudia matukio ya matetemeko ya ardhi yametikisa maeneo ya nchi yetu hasa katika kanda ya ziwa Mkoani Kagera na hata tarehe 25 Machi, 2018, Kata za Ngemo na Ushirika zilipatwa na janga la kupigwa na tetemeko la ardhi ambapo madhara katika majengo ya Taasisi za Umma na watu binafsi yaliathiriwa vibaya na watu kujeruhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo cha kuratibu na kukabiliana na maafa kiimarishwe maana kutokana na mabadiliko ya tabianchi tumeanza kuona vimbunga kutokea baharini vikianza kulikaribia bara la Afrika ikiwemo nchi yetu kuhusiana na vita dhidi ya madawa ya kulenya. Naipongeza Serikali kwa namna inavyokabiliana na janga hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naishauri Serikali kuongeza jitihada za kusambaza dawa za kutibu waathirika wa dawa za kulevya yaani *methadone* dawa hizi ziweze kupatikana katika Wilaya nchini. Naipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za kutupatia fedha shilingi milioni 800 kwa ajili ya upanuzi wa vituo vya afya viwili vya Iboya na Masumbwa ambapo ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naishukuru sana Serikali kwa jitihada zake za kuanza ujenzi wa hospitali ya Wilaya na ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe pamoja na Ofisi na Makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia suala la maji lililopo katika Jimbo langu. Katika Kata ya Kanyangereko, Vijiji vya Butahyaibega, Bulinda wakati wa kiangazi wanapata shida sana mito inakauka. Hivyo akinamama wanapata shida sana na kauli ya Serikali ni kumtua mama ndoo kichwani. Sambamba na Kata ya Bujugo, Rubafu na Maruku, shida ni hiyohiyo ya maji safi na salama. Naomba suala hili la maji litafutiwe ufumbuzi maana ni kila mwaka shida hii inajitokeza, sijui Serikali itawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu Wizara ya Mifugo na Uvuvi; je, ni lini Serikali itawapiga marufuku wafugaji kulisha mifugo yao barabarani kwa sababu inaweza kusababisha ajali kwa madereva na sehemu zingine imekwisha tokea. Hivyo, naomba lishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kuuliza, je, ni lini Serikali itakarabati barabara zilizo chini ya kiwango.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika mahali hapa nami kuchangia hoja hii muhimu iliyoko mbele yetu leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kama kiongozi wa nchi kwa namna anavyoliongoza Taifa letu katika kutuwekea misingi imara. Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu inatuonesha mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2018/2019, hotuba hii inakwenda kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuendelea kupambana katika vita dhidi ya rushwa nchini kwetu, hali ilivyo hivi sasa ni ya kuridhisha tofauti na hapo awali, kama taarifa inavyosema kuwa katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya majalada 325 yalifanyiwa uchunguzi na TAKUKURU na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ambapo 214 kati ya hayo yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ukilinganisha kwa idadi ya kesi zilizopelekwa mahakamani na kesi zilizoamuliwa na kwa idadi ya watuhumiwa waliokutwa na hatia, naweza sema bado tunahitaji kuongeza nguvu zaidi ili kuweza kufikia kiwango ambacho kitawafanya wapenda rushwa kuiogopa rushwa na kujikita zaidi katika maadili mema katika utekelezaji wa kazi za kila siku za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali adhabu katika makosa ya rushwa, watu wanapokutwa na hatia kisheria ya rushwa basi adhabu iwe kali ili iwe fundisho kwa

watu wengine. Hata hivyo, naipongeza Serikali kupitia TAKUKURU kwa kufuatilia miradi ya maendeleo na kuhakikisha fedha za umma hazipotei na kutumika ipasavyo kama zilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vita dhidi ya madawa ya kulevya imekuwa kwa kiwango cha juu sana kipindi hiki kupitia mamlaka ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulevya na tumekuwa tukishuhudia taarifa mbalimbali za kukamatwa watuhumiwa mbalimbali na baadhi ya wengine hata kujaribu kutoroka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyowahi kuchangia katika Mabunge yaliyopita, vita ya kupambambana na madawa ya kulevya siyo nyepesi, ni vita ngumu sana inayohitaji kuwawezesha kwa namna ya hali ya juu sana Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya, maana watu wanaohusika na biashara hii wana uwezo mkubwa kifedha na wana njia nyingi sana wanazoweza kuzitumia ili tu kufanikisha jambo lao. Hivyo basi ni wajibu wa Serikali kuendelea na kuongeza nguvu katika vita hii iwe endelevu na kukomesha kabisa mtandao huu hapa nchini kwetu ili kuwanusuru vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya, 2015 yaliyofanyika yameleta tija kubwa sana. Niishauri tu Serikali pale itakapoona kuna hoja ya kufanya marekebisho mengine, basi sisi Wabunge tuko tayari kushiriki kwa lengo la kuhakikisha madawa ya kulevya yanakuwa historia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha na kuongeza huduma ya watumiaji wa dawa za kulevya kwa kutumia *methadone* katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Temeke na Mwananyamala, ila naiomba Serikali kuongeza juhudi zaidi ili huduma hii iweze kufika mbali zaidi kwa waathirika wa dawa za kulevya wako kila kona ya nchi yetu kuanzia vijijini na maeneo yote ambayo

hupatikanaji wa huduma hii ni mgumu, kufanya hivyo kutasaidia sana kuokoa maisha ya vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali katika kuimarisha ulinzi na usalama katika mipaka yetu, hii inatuweka katika usalama zaidi katika kipindi hiki ambacho dunia inapita mapito mbalimbali ya kitahadhari. Vilevile naipongeza kwa kuliwezesha jeshi la polisi kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na majeshi yake mengine, bila kulisahau Jeshi la Wananchi kupitia Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie afya, kwanza niipongeze Serikali kwa kuboresha huduma mbalimbali za kiafya kwa kuanzia na utoaji wa chanjo nchi nzima. Upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba kwa kuongeza bajeti, upatikanaji wa tiba za kibingwa mfano upandikizaji wa figo, vifaa vya kuongeza usikivu katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili, upasuaji kwa kutumia tundu dogo na kufungua kifua katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* kwa kuwezesha dawa kupatikana kwa wakati na muda wa kupata huduma ya mionzi kupungua, haya na mengine mengi ni baadhi tu ya maboresho katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kila kwenye kupiga hatua hapakosi kasoro mbalimbali, kama ilivyo katika sekta ya hii ya afya kuna changamoto mbalimbali ambazo Serikali haina budi kukabiliana nazo kwa kuzidi kuipa bajeti ya kutosha Wizara ya Afya na kuhakikisha huduma muhimu zinapatikana nchi nzima na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya maji nchini imekuwa kubwa sana, Wabunge humu ndani lazima tunakabiliana na changamoto hiyo, ingawa Serikali imeendelea kuweka nguvu kubwa katika sekta ya maji, lakini bado suala la upatikanaji wa maji sehemu mbalimbali za

nchi hasa vijijini imekuwa changamoto kubwa sana. Kujenga na kupanua miradi mbalimbali ya maji vijijini itasaidia sana kukabiliana na changamoto hiyo, miradi 71 iliyokamilika bado ni idadi ndogo sana ukilinganisha na miradi inayoendelea kutekelezwa takribani miradi 366.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuweka sekta ya maji katika vipaumbele vyake kwani inawagusa watu wetu wa hali duni hasa vijijini ndiyo wanaohangaika kukesha kusaka maji. Naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali inazoendelea nazo katika mipango yake ya kuhakikisha kwa mwaka huu 2018/2019 kukamilisha miradi yake ya maji ipatayo 387 kwenye halmashauri mbalimbali nchini na pia kuanza miradi mipya ya maji vijijini, ni jambo jema lazima tulisemee kwa namna ya kupongeza na kuipa moyo Serikali kwa kuonesha inatambua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuziboresha bandari zetu nchi nzima ili kuziwezesha katika hali ya kufanya kazi kwa ufanisi, hasa bandari yetu ya Dar es Salam kuiweka katika ushindani mkubwa na kuiwezesha kupata meli nyingi kuja kushusha mizigo hapa na kuendelea kupokea watumishi kutoka nchi jirani kuitumia bandari yetu, uboreshaji huu ni katika Gati namba moja (1) mpaka saba (7) kuongeza upana wa lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli, sambamba na kuboresha mtandao wa reli bandarini pamoja na kujenga gati maalum la kuhudumia meli zinazoshusha magari, hizi ni hatua nzuri, endelevu kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya Serikali kuja na mpango wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini ni mpango mzuri sana ambao umeweka mgawanyiko wa kimajukumu ,kwani sasa wananchi wa vijiji wamepata wakala wao ambao utakuwa unashughulika na miradi ya barabara za vijijini. Tuseme tu ukweli, wananchi wa vijijini wamekuwa wakisahaulika sana kwa kutokutupiwa jicho la upendeleo, miundombinu imekuwa ni mibovu sana hasa kwa hapa

nazungumzia barabara, ambazo zimekuwa hazipitiki na ukiangalia wananchi hawa ndio wazalishaji wa mazao mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa mpango huu basi barabara nyingi za vijijini sasa zitakarabatiwa na kuwapa unafuu wananchi wetu. Hapohapo naipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (*standard gauge*) itakayokuwa na urefu wa kilometa 1,219, hadi sasa ujenzi wa kipande cha kutoka Dar es Salam hadi Morogoro kilometa 300 umeanza na unatarajia kukamilika Novemba, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna mradi mwingine mkubwa ambao umezinduliwa hivi karibuni wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi bandari ya Tanga. Bomba la mafuta hilo la kusafirishia mafuta ghafi litakuwa na urefu wa kilometa 1,445; kati ya hizo kilometa 1,115 zitajengwa nchini Tanzania. Mradi utakuwa na manufaa kwetu sisi kama nchi na wenzetu wa Uganda, hizi ni hatua za Awamu hii ya Tano kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Elimu ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, tumekuwa tukiona taarifa mbalimbali zikizungumzia sekta hii na Serikali kuchukua hatua mbalimbali pia katika kutatua changamoto ya elimu, lakini lazima Serikali ikaangalia kwa jicho pana zaidi sekta hii ya elimu ili iweze kuendana na dhana nzima ya viwanda ya Serikali hii ya Awamu ya Tano ikiongozwa na Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bila kuja na matokeo chanya yenye tija juu ya mustakabali wa elimu yetu, basi itatuwia vigumu sana kufika malengo ya Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunahitimisha hoja na tutaanza na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niseme tu mapema kwamba naunga mkono hoja, hoja ya Waziri Mkuu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hebu kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na dharura iliyojitokeza, na ukumbi kujaa moshi na kuanza kuathiri Waheshimiwa Wabunge na inawezekana moshi huu ukaathiri afya zenu na wengine msikohoe bila sababu, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi/ Kicheko)*

*(Saa 1.35 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 10 Aprili, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*